# GRAFOLOJIA NA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI: UCHANGANUZI WA RIWAYA TEULE ZA WATOTO

**ELIUD TEYIE MUSOTSI**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamifu katika Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi katika Shule ya Sanaa na Sayansi za Kijamii ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro**

**AGOSTI 2022**

## UNGAMO

Ninakiri ya kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa Chuoni humu wala katika Chuo kingine kwa minajili ya shahada yoyote.

Sahihi…..……………………………………Tarehe………………………………………

Eliud Teyie Musotsi

EDK/H/01-53095/2018

**IDHINI YA WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Tasnifu imekaguliwa kuhusu uaminifu wa kitaaluma na fahirisi yake ya kufanana sio juu ya asilimia kumi na moja (11%). Tunathibitisha kwamba tumeisoma tasnifu hii na hivyo tunapendekeza kukubalika kwa Tasnifu yenye anwani ***Grafolojia na Uchimuzi wa Maudhui katika Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: Uchanganuzi wa Riwaya Teule za Watoto*** na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi………………………………..Tarehe…………………………………………..…

Dkt. Frida A. Miruka

Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.**

Sahihi…………………………………Tarehe…………………………………………..…

Dkt. Benard O. Okal

Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika

**Chuo Kikuu cha Maseno.**

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii ni wenzo wa hakimiliki zinazolindwa na Mkataba wa Berne, sheria ya hatimiliki ya 1999 na sheria nyingine za kimataifa na za kitaifa kuhusu mali ya kielimu. Hairuhusiwi kutoleshwa tena kwa njia yoyote ikiwa kamilifu au sehemu, isipokuwa kwa dondoo fupi katika kushughulikia utafiti au masomo ya kibinafsi na hakiki ya kitaalamu bila ruhusa ya Mkuu wa Kitivo cha Masomo ya Upeo katika chuo, kwa niaba ya mwandisi na ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu mpendwa Loice Achieng Omondi, wanangu Mitchelle Amusugut Teyie na Morgan Gift Teyie.

# SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, nguvu, afya njema pamoja na kibali cha kuelimika, hali ambayo iliniwezesha kuukamilisha utafiti huu na masomo yangu ya uzamifu kwa wakati uliokadiriwa. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Frida Miruka wa Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi katika Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya na mwenzake Dkt. Benard O. Okal wa Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika wa Chuo kikuu cha Maseno. Mliniongoza vyema na kunihimiza wakati mawimbi yaliniwia mazito katika safari hii muhimu. Nawatakia kila la heri na neema ya Mwenyezi Mungu mnapoendelea kuwanoa wanafunzi na watafiti wengine katika safari hii ya usomaji. Shukrani pia ziwafikie wahadhiri wote katika Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi katika chuo kikuu cha MMUST kwa kunifundisha, kunipiga msasa na kunikosoa palipostahili. Wao ni pamoja na Mkuu wa Shule ya Sanaa na Sayansi za Kijamii Dkt. Rose Auma, Mwenyekiti wa Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi Dkt. Jairus Omuteche, wahadhiri Dkt. David Barasa, Dkt. Atichi Alati, Bwana Shadrack Opunde, Mshirikishi wa masomo ya upeo Idarani Dkt. John M'raiji, Dkt. Lucy Mandillah, Bi. Rukia Salim, Dkt. Kasili, Dkt. Mudogo, Osundwa Kassim pamoja na Mhazili Dorah. Sitasahau kuwataja wanafunzi wenzangu wa masomo ya Uzamifu wakati huo ambao tulishirikiana kwa karibu mno katika safari hii. Wao ni pamoja na Nyongesa Masika, Ayub Oyimba, Khakasa Susan, Oloo Mary na Truphena Akinyi. Ushirikiano wenu uliwezesha ushindi huu kupatikana na kwa hivyo nawatakia kila la heri katika shughuli zenu popote mlipo. Kwa wandani wangu Timothy Mumanyi na Meja Mstaafu Peter Murunga pamoja na familia zenu, ahsanteni kwa kusimama nami. Pia nawarudishia shukurani za dhati kaka zangu wapendwa Carey Francis, Dorine Namwendwa, Robert Wabuko na Vincent Khwale pamoja na familia zenu kwa msaada wenu wa hali na mali. Isitoshe, nawapa heko wazazi wangu wapendwa Mary Idewa Inzofu na Epaenitus Musotsi Inzofu kwa mapenzi, mawaidha na malezi mlionipa tangu nilipozaliwa. Mungu aendelee kuwaneemesha.

# IKISIRI

Grafolojia kama kipengele cha umitindo hudhihirika katika kazi nyingi za fasihi andishi ikiwemo fasihi ya watoto. Ingawa watunzi wa tungo za fasihi ya watoto huiingiza katika ujenzi wa kazi zao, matumizi ya baadhi ya vipengele hivyo huwatatanisha wasomaji wachanga wasiweze kufasiri au kufahamu ujumbe uliolengwa. Lengo la utafiti lilikuwa kuchunguza matumizi ya grafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto. Madhumuni maalum yalikuwa kubainisha vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto, kuchanganua dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto na kutathmini athari ya vipengele vya kigrafolojia katika ufasiri wa maudhui miongoni mwa wanafunzi. Utafiti ulijikita katika riwaya teule za Kiswahili zinazosomwa katika gredi za kwanza hadi nne katika shule za msingi za umma nchini Kenya. Mseto wa nadharia za Umitindo (Bally, 1909) na Mwitikio wa msomaji (Rosenblatt, 1939) zilitumika. Eneo la utafiti lilikuwa Kaunti Ndogo ya Mumias Magharibi inayopatikana katika Kaunti ya Kakamega. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani na ulilenga riwaya tano za Kiswahili pamoja na wanafunzi na walimu walioteuliwa kimaksudi kutoka shule za msingi za umma nchini Kenya. Riwaya za fasihi ya watoto zilizoteuliwa ni kama *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012), *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009), *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006), *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) na *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015). Utafiti ulikuwa wa kithamano na ulitumia muundo wa kimaelezo. Data ya Sekondari ilikusanywa kupitia upekuzi wa yaliyomo na uchanganuzi wa matini za riwaya zilizoteuliwa ilhali data ya nyanjani ilikusanywa kwa uchunzaji wa kushiriki madarasani pamoja na usaili usio rasmi wa wanafunzi na walimu. Vifaa vilivyotumiwa katika ukusanyaji data ni pamoja na fomu za orodha ya uchunzaji, dodoso, hati za awali, kamera, shajara, orodha ya uthibitisho, mtafiti pamoja na orodha ya maswali. Data ilichanganuliwa kithamano na kuwasilishwa kupitia ufafanuzi na maelezo. Matokeo yalibaini kuwa vipengele mbalimbali vya grafolojia hutumika katika ujenzi wa fasihi ya watoto. Hivi vinajumuisha viakifishi, herufi kubwa, picha na michoro, maandishi yenye rangi tofauti, taipografia na aina mbalimbali za fonti, maneno yaliyokolezwa, maneno yaliyolazwa, miundo mbalimbali ya aya, uwazi kati ya mistari, ukubwa wa matini / riwaya pamoja na kipengele cha umbo la matini. Vipengele hivi hutekeleza dhima anuai katika fasihi ya watoto ambazo ni: kutekeleza mawasiliano, kuimarisha uhalisia, kumpa msomaji kumbukumbu, kuendeleza ujumi, kumsisimua msomaji, kusisitiza pamoja na kufafanua msamiati. Utafiti pia ulibaini kuwa vipengele vya grafolojia huchangia katika uchimuzi wa maudhui katika riwaya za watoto za Kiswahili kwa kuimarisha ufasiri wa ujumbe uliolengwa na mwandishi. Inatarajiwa kwamba utafiti utaongeza maarifa ya uandishi, usomaji na uhakiki wa fasihi ya Kiswahili ya watoto na kuwafaidi watungaji wa mitaala, watekelezaji, waundaji sera, walimu, watunzi wa vitabu pamoja na watafiti wa baadaye. Utafiti unahitimisha kuwa vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika uandishi ni vingi na ni pamoja na faharasa ya mada, mazoezi na maswali, vielelezo na majedwali vinavyohitaji kujumuishwa miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia. Utafiti unapendekeza kuhamasishwa kwa walimu kuhusu vipengele vyote vya kigrafolojia, dhima inayotekelezwa navyo pamoja na athari ya vipengele hivyo kwa wasomaji, hususan wasomaji wachanga wa fasihi ya watoto katika Kiswahili.

## ABSTRACT

Graphology as a stylistic feature manifests itself in several literary texts including children's literature. Although most authors of children's literature use it in the construction of their works, the use of some of the graphological aspects creates ambiguity among young readers who may either fail to interpret or comprehend its use. The aim of this study was to investigate how graphology enhances thematic foregrounding in children's literature. The specific objectives were to elaborate graphological features used in children's literature, to analyse the role of graphological features in children's literature and evaluate their influence on thematic comprehension among learners. The research focused on specific Kiswahili prose texts read by young readers from grade one to four in public primary schools in Kenya. A multi model theoretical approach of Stylistics (Bally, 1909) and Readers response theory (Rosenblatt, 1939) was applied. The area of study was Mumias West Sub County of Kakamega County. This was a library based and field work research which targeted five children's novels in Kiswahili, learners and teachers selected purposively from public primary schools in Kenya. The selected Kiswahili novels were: *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta 2012), *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta 2009), *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006), *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) and *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015). This was a qualitative research whose design was basically descriptive. Secondary data was collected through document review and content analysis of selected texts while field data was collected by participatory observation and informal interview of learners and teachers. Data collection tools included observation and interview schedules, previous notes, camera, diary, check lists, the researcher as well as a questionnaire. Data was qualitatively analysed and findings presented in descriptions and explanations. The research outcome indicated that several graphological features are used in the construction of children's literature in Kiswahili. Among the features are punctuations, capital letters, pictures and drawings, the use of different colours in the wording of a text, typography and several fonts, the use of bold letters, italicization, several features of paragraphs, the use of space and spacing between words, the size of a text and the general structure of a text. These features play a critical role in childrens' literature such as effecting communication, creating realism in a text, enhancing the aesthetic role, enhancing comprehension, re-awakening the reader, emphasis as well as the enhancement of interpretation of a text through simplification of vocabulary. The research outcome confirmed that graphological features are used to foreground themes in children's novel in Kiswahili by enhancing its comprehension. It is expected that the research will add to the already existing knowledge of writing, reading and analysis of children's literature in Kiswahili and benefit curriculum developers, curriculum implementers, policy formulators, teachers, authors of texts and future researchers. The research concludes by acknowledging that there are many graphological features used in writing including the use of glossary of words in context, revision questions and answers as well as tables and graphs which previous researchers did not mention. The research recommends further sensitization of teachers on a wide range of graphological features used in writing, their roles and effects in texts as well on young readers especially in Kiswahili literary texts.

## UFAFANUZI WA DHANA

**Fasihi ya watoto:** Fasihi yoyote ambayo inawalenga watoto kama hadhira.

**Grafolojia:** Ni tawi la isimu linalochunguza mifumo ya ishara inayotumika kuwasilisha lugha kwa mfumo wa kimaandishi.

**Umitindo:** Mkabala wa uchanganuzi unaohusisha maarifa ya isimu na fasihi.

**Mtoto:** Binadamu yeyote nchini Kenya aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane.

**Riwaya asilia:** Riwaya kama ilivyochapishwa na Shirika la Uchapishaji.

**Riwaya mwigo:** Riwaya iliyoumbuliwa na mtafiti kwa mujibu wa utafiti.

**Uchimuzi:** Ni mbinu ambapo mtunzi au mwandishi anatumia mbinu za kilugha au za kimuundo kwa namna ambayo inazifanya mbinu hizo zitokeze kwa njia waziwazi na labda kuivuta makini ya msomaji.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CBC | Competency Based Curriculum |
| CNN | Cable News Network |
| KICD | Kenya Institute of Curriculum Development |
| K.S.T | Keshatajwa |
| KUR. | Kurasa |
| MSC | Mumias Sugar Company |
| NACOSTI | National Commission of Science, Technology & Innovation |
| UK. | Ukurasa |
| W.H.T | Washatajwa |

**YALIYOMO**

**UNGAMO……………………………..…………………………………………ii**

**HAKIMILIKI…………………………………………………………...….iii**

**TABARUKU…………………………………………………………………….iv**

**SHUKRANI…………………………………………………………………...v**

**IKISIRI……………………………………………………………………….vi**

**ABSTRACT………………………………………………………………….vii**

**UFAFANUZI WA DHANA……………………………………………...viii**

**ORODHA YA VIFUPISHO…………………………………………………ix**

**SURA YA KWANZA…………………………………………………………1**

**UTANGULIZI………………………………………………………………...1**

**1.0 Utangulizi…………………………………………………………………..1**

**1.1 Usuli wa mada……………………………………………………………..1**

1.1.1 Maana ya grafolojia…………………………………………………………2

1.1.2 Maana ya fasihi ya watoto…………………………………………………..4

1.1.3 Maana ya uchimuzi…………………………………………………………5

**1.2 Suala la utafiti……………………………………………………………..8**

**1.3 Madhumuni ya utafiti……………………………………………………….9**

**1.4 Maswali ya utafiti…………………………………………………………9**

**1.5 Misingi ya uteuzi wa mada…………………………………………………9**

**1.6 Nadharia ya utafiti…………………………………………………………12**

**1.7 Upeo na mipaka ya utafiti…………………………………………………13**

**1.8 Umuhimu wa utafiti……………………………………………………...14**

**1.9 Hitimisho…………………………………………………………………16**

**SURA YA PILI……………………………………………………………………….17**

**UHAKIKI WA MAANDISHI……………………………………………………….17**

**2.0 Utangulizi…………………………………………………………………………17**

**2.1 Nadharia ya utafiti……………………………………………………………….17**

2.1.1 Nadharia ya umitindo …………………………………………………………...17

2.1.2 Nadharia ya Mwitikio wa msomaji……………………………………………...26

**2.2 Dhana ya grafolojia……………………………………………………………....40**

**2.3 Dhana ya fasihi ya watoto………………………………………………………42**

2.3.1 Historia ya fasihi ya watoto……………………………………………………..44

**2.4 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto………………………………49**

**2.5 Dhima ya grafolojia katika fasihi………………………………………………….53**

2.5.1 Rangi…………………………………………………………………………….53

2.5.2 Herufi kubwa……………………………………………………………………55

2.5.3 Picha na michoro………………………………………………………………...59

2.5.4 Viakifishi………………………………………………………………………...62

2.5.5 Taipografia………………………………………………………………………63

2.5.6 Nafasi katika mistari na maneno………………………………………………...66

2.5.7 Aya………………………………………………………………………………66

2.5.8 Vipengele vingine………………………………………………………………….67

**2.6 Dhana ya uchimuzi………………………………………………………………70**

2.6.1 Grafolojia na uchimuzi wa maudhui…………………………………………….72

**2.7 Muhtasari wa riwaya teule………………………………………………………78**

2.7.1. Riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012)……………………….78

2.7.2 Riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009)…………………………79

2.7.3 Riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006)………………………...83

2.7.4 Riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003)……………………………………84

2.7.5 Riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015)…………………………….85

**2.8 Hitimisho……………………………………………………………………87**

**SURA YA TATU…………………………………………………………………….89**

**NJIA NA MBINU ZA UTAFITI………………………………………………89**

**3.0 Utangulizi…………………………………………………………………...89**

**3.1 Muundo wa Utafiti…………………………………………………………89**

**3.2 Eneo la utafiti……………………………………………………………….90**

**3.3 Kundi lengwa……………………………………………………………….91**

**3.4 Usampulishaji na sampuli………………………………………………….91**

**3.5 Ukusanyaji wa data………………………………………………………...94**

**3.5.1 Mbinu ya ukusanyaji data………………………………………………….94**

**3.5.2 Ukusanyaji wa data ya kimsingi…………………………………………...94**

**3.5.2.1 Usaili usio rasmi…………………………………………………………..94**

**3.5.2.2 Uchunzaji wa kushiriki…………………………………………………...95**

**3.5.3 Ukusanyaji wa data ya sekondari………………………………………….96**

**3.5.4 Vifaa vya ukusanyaji data………………………………………………….96**

**3.6 Uchanganuzi na uwasilishwaji wa data…………………………………...97**

**3.7 Uhalali na utegemezi………………………………………………………101**

**3.8 Maadili katika utafiti……………………………………………………...102**

**3.9 Hitimisho…………………………………………………………………...103**

**SURA YA NNE…………………………………………………………………..104**

**MATOKEO NA MJADALA…………………………………………………104**

**4.0 Utangulizi……………………………………………………………………..104**

**4.1 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto…………………………...104**

**4.1.1 Matumizi ya viakifishi………………………………………………………..104**

**4.1.2  Matumizi ya herufi kubwa…………………………………………………….118**

**4.1.3 Matumizi ya picha na michoro………………………………………………125**

**4.1.4  Matumizi ya mandishi yenye rangi  na wino tofauti…………………………143**

**4.1.5 Taipografia, nafasi kati ya mistari na aina ya fonti…………………………..145**

**4.1.6  Matumizi ya mkolezo katika matini ya fasihi ya watoto……………………152**

**4.1.7  Matumizi ya mandishi yenye mlazo katika fasihi ya watoto………………...161**

**4.1.8  Miundo mbalimbali ya aya katika matini ya fasihi ya watoto………………165**

**4.1.9  Kipengele cha kipimo au ukubwa wa riwaya katika fasihi ya watoto………171**

**4.1.10 Kipengele cha umbo la matini katika fasihi ya watoto………………………172**

**4.1.11  Matumizi ya kipengele cha faharasa katika fasihi ya watoto………………178**

**4.1.12  Matumizi ya vielelezo / majedwali katika fasihi ya watoto…………………181**

**4.1.13  Mazoezi na maswali katika fasihi ya watoto………………………………...184**

**4.2 Dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto…………………..187**

**4.2.1 Kuimarisha mawasiliano……………………………………………………..187**

**4.2.1.1 Viakifishi……………………………………………………………………187**

**4.2.1.2 Herufi kubwa………………………………………………………………..193**

**4.2.1.3 Faharasa……………………………………………………………………..199**

**4.2.1.4 Picha na michoro……………………………………………………………202**

**4.2.1.5  Rangi………………………………………………………………………..204**

**4.2.2 Kuendeleza uhalisia…………………………………………………………..205**

**4.2.2.1 Picha na michoro katika fasihi ya watoto……………………………………205**

**4.2.3 Kumsisimua msomaji…………………………………………………………...208**

**4.2.4 Kuendeleza ujumi……………………………………………………………….211**

**4.2.5 Kuweka msisitizo……………………………………………………………..212**

**4.2.5.1 Mandishi yenye rangi tofauti………………………………………………212**

**4.2.5.2 Matumizi ya mkolezo katika matini ya fasihi ya watoto……………………214**

**4.2.5.3 Nafasi ya *mlazo* katika kusisitiza……………………………………………..217**

**4.2.6 Kumwekea msomaji kumbukumbu………….……………………………..219**

**4.2.6.1 Taipografia na aina mbalimbali za fonti……………………………………220**

**4.2.6.2 Ukubwa wa riwaya katika fasihi ya watoto…………………………………224**

**4.2.6.3 Mazoezi na maswali ya ufahamu……………………………………………225**

**4.2.7 Kujenga muwala na mshikamano……………………………………………..227**

**4.2.7.1. Maumbo mbalimbali ya aya…………………………………………………228**

**4.2.7.2 Usahili wa matini………………………………………………………..231**

**4.2.7.3 Vielelezo na majedwali……………………………………………………….231**

**4.3 Muhtasari na athari ya vipengele mbalimbali vya grafolojia………………….232**

**4.3.1.1 Grafolojia na uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji……………232**

**4.4 Changamoto za utafiti……………………………………………………………248**

**4.5 Hitimisho…………………………………………………………………………..250**

**SURA YA TANO………………………………………………………………..251**

**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO…………………………251**

**5.0 Utangulizi………………………………………………………………………….251**

**5.1 Muhtasari wa tasnifu……………………………………………………………..251**

**5.1.1 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto…………………………...253**

**5.1.2 Dhima ya grafolojia katika fasihi ya watoto…………………………………..254**

**5.1.3 Athari ya grafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto…254**

**5.2 Mahitimisho……………………………………………………………………..255**

**5.3 Mapendekezo………………………………………………………………………255**

**5.3.1 Mapendekezo ya utafiti……………………………………………………255**

**5.3.2 Mapendelezo kwa ajili ya tafiti za baadaye…………………………………256**

**MAREJELEO………………………………………………………………………258**

**MAKALA…………………………………………………………………………...258**

**TASNIFU…………………………………………………………………………273**

**VITABU…………………………………………………………………………..276**

**Kiambatisho 1: Ratiba ya utafiti…………………………………………………..283**

**Kiambatisho 2: Bajeti ya utafiti…………………………………………………287**

**Kiambatisho 3: Orodha ya watafitiwa kwa ujumla………………………………...288**

**Kiambatisho 4: Orodha ya vipengele vya kuthibiti grafolojia……………………..289**

**Kiambatisho 5: Orodha ya vipengele kutokana na upekuzi wa yaliyomo………...291**

**Kiambatisho 6: Mwongozo wa usaili usio rasmi wa kuwasaili walimu……………295**

**Kiambatisho 7: Dodoso za kuwasaili wanafunzi (usaili wa kibinafsi)……………..296**

**Kiambatisho 8: Usaili usio rasmi wa mwalimu……………………………………...297**

**Kiambatisho 9:  Usaili usio rasmi wa mwanafunzi………………………………….304**

**Kiambatisho 10: Idhini ya Kurugenzi ya masomo ya upeo chuoni MMUST……..309**

**Kiambatisho 11: Idhini kutoka kwa Kamishna wa Kaunti ya Kakamega………...310**

**Kiambatisho 12: Idhini ya Mkurugenzi wa Elimu, Kaunti ya Kakamega………...311**

**Kiambatisho 13: Ombi kwa Katibu wa Kaunti ya Kakamega…………………….312**

**Kiambatisho14: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias…..313**

**Kiambatisho 15: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya St. Peters Mumias…..314**

**Kiambatisho 16: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya Mumias Central……..315**

**Kiambatisho 17: Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa na KICD…………………..316**

**Kiambatisho 18: Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa na KICD…………………..318**

**Kiambatisho 19: Vitabu vilivyoidhinishwa na KICD……………………………....319**

**Kiambatisho 20: Uchunzaji wa kushiriki, shule ya msingi ya Mumias Central…..320**

**Kiambatisho 21: Usaili usio rasmi wa mwalimu darasani………………………….321**

**Kiambatisho 22: Usaili usio rasmi wa mwalimu……………………………………322**

**Kiambatisho 23: Nikiwasili katika shule ya msingi ya Mumias Central…………..323**

**Kiambatisho 24: Usaili wa mwanafunzi darasani…………………………………..324**

**Kiambatisho 25: Usaili wa mwanafunzi darasani…………………………………..325**

**Kiambatisho 26: Uchunzaji wa kushiriki darasani…………………………………326**

**Kiambatisho 27: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi darasani………………………327**

**Kiambatisho 28: Usaili usio rasmi wa mwalimu…………………………………….328**

**Kiambatisho 29: Nikiwasili katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias………..329**

**Kiambatisho 30: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi…………………………………330**

**Kiambatisho 31: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia………………..331**

**Kiambatisho 32: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia………………..332**

**Kiambatisho 33: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia………………..333**

**Kiambatisho 34: Uchunzaji wa kushiriki……………………………………………334**

**Kiambatisho 35: Uchunzaji wa kushiriki……………………………………………335**

**Kiambatisho 36: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi…………………………………336**

**Kiambatisho 37: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi…………………………………338**

**Kiambatisho 38: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi…………………………………339**

**Kiambatisho 39: Usaili usio rasmi wa mwalimu......................................................340**

**Kiambatisho 40: Usaili usio rasmi wa mwalimu…………………………………….342**

**Kiambatisho 41: Usaili usio rasmi wa mwalimu…………………………………….344**

**Kiambatisho 42: Usaili usio rasmi wa mwalimu…………………………………….345**

**Kiambatisho 43: Riwaya mwigo ya *Usicheze na Moto* (2003)………………………347**

**Kiambatisho 44: Riwaya asilia iliyochunguzwa……………………………………..352**

**Kiambatisho 45: Mfano wa majibu ya mtafitiwa………..………………………….353**

**Kiambatisho 46: Majibu ya mtafitiwa aliyepewa msimbo wa nambari 8…………354**

**Kiambatisho 47: Ramani ya Kaunti ya Kakamega…………………………………355**

**Kiambatisho 48: Kaunti Ndogo ya Mumias Magharibi…………………………….356**

**Kiambatisho 49: Cheti / idhini ya kufanya utafiti (NACOSTI)……………………357**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inajadili vipengele vya kimsingi katika utafiti kwa kurejelea usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni na maswali ya utafiti, sababu ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti.

## 1.1 Usuli wa mada

Tafiti nyingi katika fasihi andishi kama vile ushairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya huelekea kudhibitiwa na vipengele vya kigrafolojia kama kiwango mojawapo cha uchanganuzi wa lugha katika ujenzi wake. Vipengele hivi husaidia katika kuwasilisha maudhui kwa kutegemea dhamira ya mwandishi. Hata hivyo kama anavyosema Wamitila (2008), kando na lugha, nyenzo nyingine kama vile michoro, rangi miongoni mwa vipengele vingine huchangia katika kurahisisha kufasiriwa vyema kwa fasihi kimatini.

Mawazo ya Wamitila (2008) yanaungwa mkono na watafiti wengi akiwemo Mohamed (2015) anayedokeza kwamba michoro huoanisha matini na kwa hali hiyo kuimarisha upokezi wa maudhui au ujumbe uliolengwa na mwandishi ili ufasiriwe vyema na msomaji. Akichangia kuhusu nyenzo zingine ambazo Wamitila (2008) alitaja kuwa zinachangia katika uelewekaji wa matini, Cass (1967) vilevile anakitaja kipengele cha rangi ambacho anasema kwamba pia ni cha kimsingi katika fasihi. Anashikilia kuwa kipengele hiki kina umuhimu katika fasihi, hususan fasihi ya watoto.

Cass (1967) anadokeza kuwa rangi inayotumiwa katika vitabu vya fasihi ya watoto huwa na mvuto kwa usomaji wa vitabu hivyo. Cass (k.h.t) anaendelea kusema kuwa watoto wangekuwa na uwezo wa kujichagulia vitabu, wengi wangevichagua vitabu vilivyo na mng'aro wa hali ya juu kutokana na matumizi ya rangi mbalimbali. Cass (k.h.t) aliziainisha rangi kulingana na umaarufu wake kimvuto kwa watoto. Kulingana naye, rangi nyekundu ndio ambayo huwa na mvuto mkubwa kwa watoto kuliko rangi zingine zote ikifuatiwa na rangi ya manjano, kisha rangi ya samawati na hatimaye rangi ya kijani kibichi. Kwa hivyo anashikilia kuwa mtoto huathirika na vitabu vyenye rangi ng'aavu, athari ambayo vilevile huchangia katika uteuzi wa vitabu hivyo.

Kufuatia mchango wa Cass (1967), ni dhahiri kwamba vipengele vya kigrafolojia ni vingi huku rangi ikiwa mojawapo ya vipengele hivyo ambavyo ni vya kimsingi katika ujenzi wa fasihi na hususan ya watoto. Kwa hivyo, ufasiri wa vipengele vya kigrafolojia hudhamiriwa kusaidia msomaji kuelewa ujumbe wa mwandishi awapo na uwezo wa kuufasiri ipasavyo. Hata hivyo, hali hii ni kinyume katika fasihi ya watoto ambapo wasomaji wa kiwango hicho hukosa tajriba ya kufasiri vyema ujumbe uliodhamiriwa kutokana na umri wao mdogo. Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu umechunguza vipengele vya grafolojia na uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 1.1.1 Maana ya grafolojia

Dhana ya grafolojia imeshughulikiwa na wengi. Aidha McIntosh (1961), Halliday, Mclntosh na Strevens (1964), Cass (1967), Leech na Short (1981, 2001, 2007, 2008), Kazungu (1982), Coulmas (1991, 1999), Crystal (1995), Wales (2001), Cronje (2009), Anantha (2014), Jiménez (2015), Zaheer (2016), Yaping (2017), Ufot (2017), Musotsi (2017), Toboso (2018) na wengine wameishughulikia dhana hii kwa kina. Kwa mfano,

Jiménez (2015) ametueleza kwamba tofauti na istilahi zingine za kiisimu kama vile mofolojia, sintaksia na fonetiki, istilahi grafolojia ni yenye kuzua utata na ubishi kwa kuwa ina maana yenye uluwiluwi. Anasema ya kwamba uluwiluwi huu unatokana na sababu mbili kuu: sababu ya kwanza ni ile maana inayoibuliwa na kuhusishwa na dhana hii kutokana na kuwepo kwa vipengele visivyo vya kiisimu na maana mbalimbali kutokana na kamusi, vitabu vya kiada na kazi za marejeleo kwa ujumla. Kwa mfano kamusi ya *The Oxford English Dictionary* (2013) imeifafanua dhana ya grafolojia kiisimu kwa kusema kwamba, ni utafiti kuhusu maandishi na ishara zinazochapishwa na mifumo ya uandishi.

Jiménez (2015) ameendelea kusema kwamba ni kwa sababu ya uluwiluwi ndiposa ufafanuzi ambao ulitolewa na Wales (2001) kuhusu grafolojia ulionekana kuondoa utata huo kwa kufafanua dhana hii kikamilifu. Wales (k.h.t) alishughulikia dhana hii kwa mitazamo miwili; mtazamo wa kwanza uliiangazia grafolojia kama kiwango cha kiisimu na ule mtazamo wa pili ukaiangazia grafolojia kama kiwango kisicho cha kiisimu. Alieleza kuwa ufafanuzi huo ulitokana na kujumulishwa kwa vipengele vingine katika dhana hii, kando na herufi za kialfabeti kama vile viakifishi na uwazi kati ya mistari.

Aidha, utafiti huu ulichukua mkondo wa kijumla kama alivyoeleza Wales (2001) kwa kuwa uliviangazia vipengele vya kiisimu na vingine ambavyo si vya kiisimu katika mchakato mzima wa utafiti. Ni kwa hali hii ndiposa Wales (k.h.t) aliifafanua grafolojia kwa kuiangazia kama kisawe cha grafemiki, ambao ni utafiti unaohusu elementi zinazohusiana na maandishi katika mfumo wa lugha, unaodhihirika kupitia kwa uakifishaji, ukubwa wa maandishi, matumizi ya herufi kubwa, miundo ya aya, nafasi kati ya mistari miongoni mwa vipengele vingine.

Kwa hivyo kwa mtazamo wake, Wales (2000) alipanua matumizi ya dhana ya grafolojia kwa kutaja dhahiri elementi ambazo zinahitaji kuchunguzwa katika kila kategoria ambazo zilijumulisha herufi za alfabeti, viakifishi, herufi kubwa, nafasi katika mistari pamoja na mifumo ya uandishi na uchanganuzi kitaaluma. Licha ya maoni mengi ambayo yametolewa na wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya grafolojia, utafiti huu umevichunguza vipengele vyote vya kigrafolojia ambavyo hudhihirika katika uandishi wa fasihi za Kiswahili za watoto zilizochunguzwa.

### 1.1.2 Maana ya fasihi ya watoto

Dhana ya fasihi ya watoto imeangaziwa na kushughulikiwa na watafiti na wahakiki wengi. Hunt (1994, 1996, 1999), Lynch-Brown na Tomlinson (1999), Ang (2000), Weinreich na Bartlett (2000), Murray na Kirsten (2003), Yu Chang (2007), Wamitila (2008), Junaid (2013), Mascarenhas (2015), Schneider (2016) na wengine wameijadili dhana hii kwa kina. Yu Chang (k.h.t) alishikilia ya kwamba ufafanuzi wa fasihi ya watoto lazima uviangazie vigezo vitatu vifuatavyo: hadhira lengwa kimtindo na kithamana, utumbuizo na upashwaji wa ujumbe na ufasiri.

Weinreich & Bartlett (2000) wakizungumzia hadhira lengwa walisisitiza kuwa lazima hadhira hiyo iwe watoto wenyewe huku McDowell (1973) and Hunt (1996) wakishikilia kuwa ufafanuzi mwafaka wa fasihi ya watoto lazima uhusu vitabu vinavyosomwa na watoto. Hata hivyo, kando na vitabu vinavyowalenga watoto, fasihi ya watoto pia inaweza kuhusu masimulizi yanayowalenga watoto. Kulingana na Wamitila (2008), fasihi ya watoto huwa na sifa fulani zinazoitambulisha ambazo ni pamoja na kuwepo kwa michoro mingi mizuri ya rangi za kuvutia, lugha rahisi inayoeleweka kwa watoto,

iliyosheheni fantasia, ambayo mara nyingi huwa na wahusika wakuu ambao ni watoto, na hukitwa katika motifu ya safari na msako.

Wamitila (2008) anaendelea kusema kwamba fasihi ya watoto vilevile huwa na muundo sahili, si ndefu kupindukia na inayojali saikolojia ya watoto. Hata hivyo, si lazima fasihi ya watoto idhihirike katika uandishi tu kwa kuwa pia inaweza kuhusu masimulizi ambayo yanawalenga watoto kama hadhira. Kwa mujibu wa utafiti huu, fasihi ya watoto ya Kiswahili ililenga riwaya teule zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kama anavyoeleza (Wamitila, 2008:334) ambazo zinawalenga watoto kwa kina kama hadhira.

### 1.1.3 Maana ya uchimuzi

Wataalamu mbalimbali wameishughulikia dhana ya uchimuzi. Wao ni pamoja na Leech & Short (1981), Kazungu (1982), Finch (2000), Simpson (2004), Wamitila (2008), Yuliya na Yuliya (2017) Yemets (2019) miongoni mwa wengine wengi. Kazungu (k.h.t) anaeleza utaratibu unaostahili kuzingatiwa katika kuishughulikia dhana ya uchimuzi kwa kusema kuwa uchimuzi ni nadra ushughulikiwe bila kuuambatanisha na mkengeuko kwa vile katika hali halisi, mkengeuko ni mojawapo ya masharti yanayodhibiti uchimuzi.

Hata hivyo, Kazungu (1982) anaeleza kuwa dhana ya uchimuzi inaweza kuangaziwa kwa mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule wa kimapokeo unaoyarejelea mawazo ya akina Mukarovsky, kama anavyoangaziwa katika Freeman (1970), Garvin (1958), Havrenek Kozenkova na Dubsky (1972) ambao unaangazia dhana ya uchimuzi katika muktadha wa kisanaa. Kwa hali hii, uchimuzi unahusu ukiukaji wa kaida za matumizi ya lugha kiisimu kwa lengo la kuibua matumizi ya lugha kifasihi. Kulingana na Kazungu (k.h.t) ukiukaji huu unazalisha upekee katika fasihi.

Mtazamo wa pili kulingana na Kazungu (1982), ni ule wa kisasa unaowajumuisha akina Levin (1963, 1965, 1977), Leech (196 9, 1981, 2001, 2008) na Halliday (1971) ambao unaifasiri dhana ya uchimuzi katika muktadha wa mawasiliano, ambao unakifanya kipengele fulani kujitokeza zaidi, dhidi ya vingine katika matini kwa lengo la kusisitiza. Yemets (2019) akimrejelea Leech (2007), naye anaibua mitazamo ya kithamanao na kitakwimu katika uchimuzi, huku mtazamo wa kithamano ukihusu moja kwa moja ule ukiukaji wa kaida zilizozoeleka na ilhali ule mtazamo wa kitakwimu ukihusu mchepuko.

Mawazo ya Kazungu (1982) yanashadidiwa na Simpson (2004) na Yuliya na Yuliya (2017) wanaoongezea kwa kusema kwamba uchimuzi unaweza kufikika kupitia uradidi au usambamba. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), riwaya ya Kiswahili ya kisasa ni riwaya ambayo inaelekea kukiuka sifa za jadi za riwaya katika ngazi mbali mbali kama vile ngazi ya mkakati wa kisimulizi ambapo mitindo ya kisimulizi inayotumika katika baadhi ya riwaya inakwenda kinyume na mitindo ya jadi. Kutokana na mjadala huu, Kazungu (1982) anakiri kuwa alitumia uchimuzi kumaanisha ukiukaji wa lugha ya kawaida kwa kudhamiria au kukusudia, hali ambayo inaathiri ufasihi au usanii katika lugha kimaandishi. Utafiti huu ulitumia uchimuzi kwa maana ya ukiukaji kwa dhima ya kuendeleza mchomozo katika kazi za kifasihi.

Kwa mujibu wa Ufot (2017), watafiti mbalimbali wa umitindo wamewahi kutoa maoni yao kuhusu nafasi na matumizi ya uchimuzi na miongoni mwao ni Leech (1969), Douthwaite (2000), Leech and Short (2007), Simpson (2007), Leech (2008), Jeffries na McIntyre (2010), Wales na Abrams (2011) na Harpham (2012). Akimrejelea Leech (1969), Ufot (2017) anasema kuwa uchimuzi huashiria kitu kuonekana zaidi ya kingine

kimsingi. Katika hali ya kawaida, inapofanyika hivyo, mwandishi wa matini huwa anautumia ufundi fulani kuwasilisha ujumbe wake, ambao ndio huwa maudhui ya kazi hiyo. Yaping na Yuying (2017) katika utafiti wao wamesema kwamba uchimuzi ni kipengele cha ishara katika mfumo wa lugha kifasihi ambacho kimeunganishwa na maudhui pamoja na thamana kiujumi ya kazi za kifasihi. Wamesema kuwa utafiti wao umelenga kutathmini dhima ya uchimuzi katika kazi za kifasihi hususan ufasiri wa riwaya. Kwa mujibu wao, uchimuzi katika lugha ni kipengele chenye umuhimu kwa vile kinatekeleza dhima isiyofidika kwenye mchakato wa kuwasilisha maudhui na hisia katika kazi za kifasihi.

Kwa vile muktadha ambamo fasihi ya watoto huzalishwa na kusambazwa hutawaliwa na yaliyomo na maudhui, lugha ya fasihi ya watoto inahitaji kuangaziwa kwa mapana. Stephens kwenye makala yake *Analysing Texts for Children: Linguistics and Stylistics* (1999) yanayoangaziwa katika Hunt (1999), anasema kuwa kuna uwezekano wa vitabu kuangazia maudhui yanayofanana lakini kutofautiana kwa kutegemea raslimali za kiisimu zilizotumika. Kwa mujibu wake, lugha huwawezesha wandishi kulinganisha tajriba zao, mchakato ambao ni wa kimsingi katika bunilizi za watoto. Ni kwa hali hii ndiposa grafolojia inatekeleza dhima kuu katika uchimuzaji wa maudhui katika fasihi, hususan fasihi ya watoto.

Hata ingawa mawazo haya yanayowasilishwa na wataalamu mbalimbali yameutajirisha utafiti huu, ni dhahiri kuwa yametofautiana na utafiti huu kwa kuwa yamejadili grafolojia, uchimuzi na fasihi ya watoto wa ujumla. Hivi ni kusema kuwa hakuna utafiti ambao umelenga moja kwa moja kuvibainisha vipengele vya kigrafoljia ambavyo

huchangia katika ujenzi wa kazi za fasihi za watoto za Kiswahili. Vilevile hakuna utafiti ambao umefanywa katika uchanganuzi wa vipengele vya kigrafolojia kwa lengo la kuchanganua dhima na athari inayotekelezwa na viengele hivyo katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Ni kwa ajili hii ndiposa utafiti huu umefanyika.

**1.2 Suala la utafiti**

Maudhui katika kazi ya fasihi huwasilishwa kwa kutumia mitindo na fani mbalimbali. Vipengele vya grafolojia kama vipengele vingine vya umitindo, mbali na kushirikiana katika kuwasilisha maudhui ndivyo vinavyoibainisha kazi ya kifasihi na kumtambulisha mtunzi wa kazi hiyo. Vipengele hivyo vinajumuisha uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mipangilio ya sentensi, usimulizi na mbinu za usimulizi pamoja na uakifishi hasa wa riwaya ya watoto ya Kiswahili. Licha ya kwamba watunzi wengi wa kazi za kifasihi huvishirikisha vipengele vya grafolojia katika ujenzi wa kazi zao, baadhi ya matumizi yake huwatatanisha wasomaji wachanga na hivyo kutatiza ufasiri wao wa maudhui. Aidha, mchango wa vipengele vya kigrafolojia katika ufasiri wa maudhui katika kazi ya fasihi haujafanywa kwa kina katika fasihi ya Kiswahili. Isitoshe, baadhi ya walimu na wanafunzi hawavifahamu vipengele vya kigrafolojia. Ni katika msingi huu ambapo kazi hii ilidhamiria kubainisha aina mbalimbali ya vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika ujenzi wa fasihi ya watoto katika Kiswahili, na vilevile kuchanganua dhima inayotekelezwa na vipengele hivyo kimatini, na pia kutathmini athari inayoibuliwa na vipengele hivyo katika uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

Azma ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza matumizi ya vipengele vya grafolojia katika fasihi ya watoto ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa gredi ya kwanza hadi ya nne katika shule teule za msingi za umma nchini Kenya. Lengo lilikuwa kubainisha dhima ya vipengele vya grafolojia ili kuhamasisha walengwa kuhusu umuhimu wa vipengele hivi katika ufasiri wa maudhui. Ili kufikia lengo hili, madhumuni maalumu yafuatayo yalishughulikiwa:

i) Kubainisha vipengele vya kigrafolojia katika fasihi teule ya watoto.

ii) Kuchanganua dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi teule ya watoto.

iii) Kutathmini namna matumizi ya vipengele vya kigrafolojia yanavyoathiri uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga katika fasihi teule.

## 1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni vipengele gani vya kigrafolojia vinavyobainika katika fasihi ya watoto?

ii) Je, vipengele vya kigrafolojia vina dhima gani katika fasihi ya watoto?

iii) Je, vipengele vya kigrafolojia vinavyotumiwa na watunzi mbalimbali huathiri vipi uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga?

## 1.5 Misingi ya uteuzi wa mada

Mtafiti alichochewa na sababu kadha katika uteuzi wake wa mada ya grafolojia na uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kuchanganua riwaya teule za Kiswahili. Hii ni kufuatia tathmini yake ya maumbo ya vitabu mbalimbali vya fasihi ya watoto ya Kiswahili vinavyowalenga wasomaji wachanga vinavyochapishwa

nchini Kenya. Aidha, msukumo wake ulitokana na jinsi vitabu hivyo vinavyodhihirisha upekee kimuundo kutokana na ukiukaji wa ukawaida katika ujenzi wavyo.

Baadhi ya vitabu vilivyoteuliwa kidhamirifu vilidhihirisha mvunjiko wa kiothografia, mpangilio tofauti wa aya, matumizi ya michoro, matumizi ya maandishi mengine yenye mlazo, matumizi ya herufi kubwa, maandishi yaliyokolezwa, ujongezi na hata mandishi yenye rangi tofauti katika matini miongoni mwa vipengele vingine vya viziadaisimu. Ingawa hali hii hudhihirika sana miongoni mwa vitabu vinavyowalenga wasomaji wachanga, utafiti wa kina haujafanywa kuthibitisha dhima ya mtindo huu katika usukaji wa riwaya za Kiswahili zinazowalenga wasomaji wachanga.

Aidha, uamuzi wa mtafiti wa kutafitia fasihi ya watoto ya Kiswahili ulitokana na ugunduzi kwamba fasihi ya watoto ni uwanja mpana ambao haujashughulikiwa kwa kina. Ingawa Kazungu (1982) alishughulikia grafolojia na uchimuzi katika utanzu wa ushairi, naye Toboso (2018) akashughulikia grafolojia na uchimuzi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, hakuna utafiti ambao umefanywa kubainisha aina, dhima na athari ya matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Vilevile tafiti nyingi za kifasihi zimeelekea kuzungumzia maudhui, wahusika na mbinu za lugha hasa za kifasihi. Hivyo basi, kazi hii inaibua jinsi nyingine ya kushughulikia maudhui katika fasihi, hata hivyo kwa msingi wa mbinu za lugha au mtindo wa kiisimu kama vile matumizi ya grafolojia. Basi hali hii ilimsisimua na kumchochea mtafiti katika uamuzi wake wa kuushughulikia utafiti huu.

Mtafiti aliamua kuviteua vitabu vitano vya utanzu wa riwaya ya Kiswahili kimakusudi kwa kuwa vilidhihirisha kuwa na vipengele vingi vya kigrafolojia, kando na kuteuliwa na

Taasisi ya Ukuzaji mitaala nchini *Kenya Institute of Curriculum Development* (KICD) kama vitabu vya kiada katika *Orange Book*, na hivyo basi vya kutumika katika ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya. Vitabu hivyo vilikuwa riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012), *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009), *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006), *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) na *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015). Mtafiti alivitathmini vitabu hivyo vya riwaya vya fasihi ya watoto ya Kiswahili kama vinavyoafiki kiwango cha watafitiwa waliolengwa na utafiti kufuatia tajriba yao ndogo ya usomaji, vikilinganishwa na utanzu wa tamthilia, hadithi fupi na ushairi ambavyo vingewapa changamoto watafitiwa. Pia iliweza kubainika kwamba watunzi wa riwaya hizo ni wandishi watajika katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Kuwepo kwa vipengele vingi vya kigrafolojia katika riwaya tano teule zilizotafitiwa kuliafiki mseto wa nadharia za utafiti za Umitindo na Mwitikio wa msomaji. Aidha, utafiti huu ulitumia mihimili mitano ya nadharia ya umitindo ifuatayo; kiwango cha grafolojia, uteuzi katika fasihi, sarufi na tanzu, uchimuzi na miundo ya lugha. Vilevile mihimili minne ya nadharia ya mwitikio wa msomaji ilitumika katika utafiti huu ambayo ilikuwa ni pamoja na usomaji kama tukio la kimapatano, usomaji kama tukio la kiwakati, usomaji kama tukio la kijamii kitamaduni na usomaji kama tukio linalogeuzika.

Wandishi wa riwaya tano zilizoteuliwa kimaksudi na kuchunguzwa ni wenye tajriba pana, wakiwaandikia watoto katika viwango mbalimbali huku kazi zao zikiidhinishwa na Taasisi ya Ukuzaji mitaala nchini (KICD). Kwa mfano, Ngugi (2007) ni mtafiti mtajika katika masuala ya fasihi ya watoto. Kando na kuandika makala na vitabu vingi vikiwemo

viwili vilivyotafitiwa katika utafiti huu, ana shahada ya uzamifu katika fasihi ya watoto, hali inayomfanya akidhi kuangaziwa kama mtaalam. Aidha, tajriba ya Ngugi ilimchochea mtafiti kufuata nyayo zake kwa vile pia ameazimia kubobea katika tafiti za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mtafiti aliwateua kimaksudi wanafunzi wawili wawili kutoka gredi ya kwanza (1) hadi ya nne (4) ambao hudhihirisha matokeo mema katika somo la Kiswahili kwa kusaidiwa na walimu wa somo la Kiswahili ili waweze kusailiwa. Vilevile walimu wawili wawili wanaofundisha somo la Kiswahili katika gredi ya kwanza (1) hadi ya nne (4) katika shule teule za msingi za umma nchini Kenya za Mtakatifu Petero, Mtakatifu Anna na ile ya Mumias Central katika kaunti ndogo ya Mumias Magharibi, Kaunti ya Kakamega waliteuliwa ili washirikishwe katika utafiti. Wanafunzi na walimu walioteuliwa walishirikishwa katika usaili usio wa rasmi kwa lengo la kukusanya data mwafaka ya utafiti huu.

### 1.6 Nadharia ya utafiti

Utafiti uliongozwa na mseto wa nadharia za Umitindo na Mwitikio wa msomaji. Nadharia ya umitindo iliasisiwa na Bally (1909) na kushabikiwa na waitifaki wengi wakiwemo Spitzer (1948), Leech (1969), Kitsao (1975) Wamitila (2008) miongoni mwa wengine. Kulingana na nadharia hii, umitindo ni uwanja ambao ujifunzaji wa isimu na fasihi hutukia kwa kushuhudia mwingiliano wa lugha na fasihi. Nadharia ya mwitikio wa msomaji iliasisiwa na Rosenblatt (1939) na kuungwa mkono na wengi akiwemo Iser (1978). Kulingana na nadharia hii, maana katika matini ni zao la utangamano kati ya msomaji na matini yenyewe.

### 1.6.1 Tahadhania za utafiti

Utafiti huu uliegemezwa kwenye tahadhania zifuatazo:

(i) Vipengele vya kigrafolojia hutumika katika ujenzi wa fasihi ya watoto ya Kiswahili.

(ii) Vipengele vya kigrafolojia hutekeleza dhima muhimu katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

(iii) Matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto ya Kiswahili huathiri uchimuzi wa maudhui.

## 1.7 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti ulihusu fasihi ya Kiswahili ya watoto na uliegemea katika utanzu wa riwaya. Ulishughulikia grafolojia na uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto. Madhumuni maalumu yalikuwa kubainisha vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto, kuchanganua dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto na kutathmini jinsi vipengele vya kigrafolojia vinavyoathiri uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji. Ulichunguza vipengele vya kigrafolojia katika riwaya ya fasihi ya watoto ya Kiswahili, dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto na namna vipengele vya kigrafolojia vinavyoathiri uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga. Utafiti huu uliendelezwa maktabani na ulilenga riwaya tano za fasihi ya watoto za Kiswahili ambazo zilikuwa *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012), *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009), *Harusi ya Mwansungura*, (Waihiga, 2006), *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) na *Dani na Wezi wa Toyota*, (Ngugi, 2015) na ulilenga vipengele vya kigrafolojia na vilevile ulihusu kwenda nyanjani na uliongozwa na mseto wa nadharia za Umitindo na Mwitikio wa msomaji.

## 1.8 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu utaongeza maarifa kwa tafiti zilizofanywa awali kuhusu fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha watungaji wa mitaala, walimu, watunzi wa vitabu, waundaji sera pamoja na watafiti wa baadaye kuhusu fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti huu vilevile utawanufaisha watungaji na watekelezaji wa mitaala kwa kurejelea sera ya ufunganishaji kwa lengo la kuhakikisha uimarishaji wa manufaa darasani kwa wasomaji, na pia kuongezeka kwa manufaa kwa msomaji kutokana na uboreshaji wa uwasilishwaji wa masomo. Sera ya elimu inaongozwa na katiba ambayo pia imeangazia utajiri wa utamaduni wetu. Fasihi ya watoto ya Kiswahili ni utamaduni ambao umelenga kukuza na kuendeleza utamaduni wa usomaji na utangamano wema miongoni mwa watoto wa Kenya. Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yatawachochea wandishi wa fasihi ya watoto pamoja na waundaji sera kuandika na kuweka sera mwafaka ya kuwawezesha watoto wetu kusoma fasihi yao, wakiifurahia na kujivunia.

Pia walimu watanufaika kutokana na utafiti huu. Katika jitihada za kukuza usomaji bora miongoni mwa watoto, ni walimu wanaowawekea watoto msingi mahususi. Hii si kusema kuwa wazazi hawana mchango wowote. Hata hivyo kutokana na tofauti za kiuchumi miongoni mwa wazazi, mazingira ya shule huwa mwafaka kwa usomaji wa mtoto, kwa hivyo walimu huchangia pakubwa katika uimarishaji wa usomaji wa watoto. Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yatawazindua walimu kutathmini tena mbinu mpya za kufundishia fasihi ya watoto kwa mwelekeo mseto wa kuifungamanisha fasihi na isimu (lugha) kama inavyopendekezwa na Taasisi ya Utekelezaji wa Mitaala nchini (2005). Hii ni kusema ya kwamba usomaji na uhakiki wao wa fasihi utapigwa msasa. Aidha, wazazi

watashirikishwa kwa falsafa kwamba shughuli za usomaji ni shughuli zisizo wekewa mipaka na hivyo basi wazazi wana dhima ya kuchangia katika uendelezaji wa masomo kwa kuwa ni wao wanaowanunulia watoto vitabu.

Kwa watunzi wa vitabu, matokeo ya utafiti huu yataonyesha uhusiano uliopo kati ya fasihi na isimu na jinsi isimu inavyoweza kuwa nyenzo ya kuendeleza fasihi hususan, fasihi ya watoto. Katika utunzi wao, watunzi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wamefahamu viwango mbalimbali vya kutumia vipengele tofauti tofauti vya kigrafolojia kwa dhima mbalimbali, huku umri na ufahamu wa msomaji vikipewa uzingativu unaohitajika kutegemea athari ya matumizi ya vipengele hivyo katika matini.

Watafiti wa baadaye wana fursa ya kuwapa watoto wa Kenya na kanda ya Afrika Mashariki mwelekeo unaofaa. Kwa leo (2020), watoto wa Kenya wanakulia katika mazingira tofauti ambapo wale wasio na uwezo wa kusoma hujipata wamejitenga kielimu na hata kijamii. Kwa hivyo, wanapojiimarisha katika usomaji, huenda vilevile wakajiimarisha kielimu, kiuchumi na kijamii. Litakuwa jukumu la watafiti wa baadaye kutafitia kuhusu kazi ambayo itakuwa nzuri na ya kuwavutia watoto ili watoto waweze kusoma kwa minajili ya kukuza usomaji na pia kupokea ufahamu kuhusu ulimwengu wao. Nadharia za umitindo na mwitikio wa msomaji ziliudhibiti utafiti huu na kubainisha kwamba fasihi ya watoto ni eneo pana ambalo linaweza kutafitika kitaaluma (kinadharia) katika Kiswahili. Kwa ujumla, utafiti huu utachangia katika uboreshaji wa utamaduni wa usomaji na uelewaji bora wa riwaya ya Kiswahili ya watoto nchini Kenya.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imeuwekea utafiti huu msingi mwafaka kwa kufafanua vipengele vya kimsingi vya usuli hasa grafolojia, uchimuzi pamoja fasihi ya watoto. Aidha vipengele vingine vya usuli kama vile suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi, umuhimu na upeo vimeangaziwa kidhahiri kwa lengo la kuuendeleza utafiti kwa misingi mwafaka. Sura inayofuata imejishughulisha na tahakiki za maandishi na nadharia na zinazohusiana na utafiti.

## SURA YA PILI

## UHAKIKI WA MAANDISHI

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Inawasilishwa katika sehemu nane zinazohusu nadharia ya utafiti, dhana ya grafolojia, dhana ya fasihi ya watoto, vipengele vya kigrafolojia katika fasihi, dhima ya grafolojia katika fasihi, dhana ya uchimuzi, ufupisho wa riwaya tano teule zilizochunguzwa pamoja na hitimisho. Sehemu ya kwanza inaangazia nadharia ya utafiti.

### 2.1 Nadharia ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na mseto wa nadharia za Umitindo na Mwitikio wa msomaji.

#### 2.1.1 Nadharia ya umitindo

Nadharia ya Umitindo iliasisiwa na Bally (1909) na kuenezwa na Jakobson (1958, 1961), Halliday (1971) na Leech na Short (1981, 1997, 2007). Bally katika *Precis de stylistique* (1905) anasisitiza kuhusu maelezo na uchanganuzi wa vijenzi vyote vilivyo katika ujumla wa lugha. Kulingana naye, matini ya kifasihi ni mifano mahususi ya matumizi ya lugha ingawa uchanganuzi wa matini kimtindo si dhihirisho kamili la umitindo katika matini. Huu ndio uliokuwa msingi wa nadharia ya umitindo ambao ulivichanganua vipengele vyote vya matini.

Jakobson (1961) anasema kuwa uhusiano baina ya isimu na fasihi ndio umitindo. Anaendelea kudokeza kwamba ikiwa kuna wahakiki wengine ambao wanatilia shaka umilisi wa isimu katika uimarishaji wa uwanja wa ushairi, basi hao wamepotoka.

Kulingana na Widdowson (1975), umitindo ni uwanja ambao ujifunzaji wa isimu na fasihi hutukia kwa kushuhudia mwingiliano wa lugha na fasihi. Mawazo yake yanashadidiana na mawazo ya Wamitila (2008), anayeongezea kwa kusema kwamba kutokana na umitindo, nadharia ya umitindo inaibuliwa ambayo inaweza kuchunguza mitindo ya matini za kifasihi. Wamitila (k.h.t) vilevile anataja ya kwamba kuna mkabala wa umitindo unaochunguza jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi.

Aidha, Leech na Short (1981, 1997, 2007, 2008) wanafafanua umitindo kama utafiti wa isimu kimtindo. Short (1997) anahoji kwamba umitindo ni mtazamo wa uchanganuzi wa matini ya kifasihi unaotumia maelezo ya kiisimu. Kulingana naye, mtazamo huo hunuia kueleza mbinu za uchanganuzi zilizo wazi kimaelezo ambazo zitamwezesha mtu yeyote kuifasiri matini ambayo anahitaji kutafitia kwa kuhakikisha kuwa utaratibu na vipengele vyote vya kimitindo vimeshughulikiwa. Kwa hali hii, umitindo hubadilisha mtazamo wa mtawanyiko kwa kuzingatia utaratibu unaolenga kuepuka kutegemea uwezo wa kuhisi katika uchanganuzi wa matini kwa vile unashughulikia ufasiri na misimbo iliyotumika, maana, sababu na dhima ya matini.

Kulingana na Leech na Short (1981), nadharia ya umitindo ni utafiti ambao hutathmini matumizi ya lugha, na kwamba utafiti huo hufanywa ili kueleza wazi kazi za kifasihi kithabiti na kwa ukamilifu jinsi zinavyohusiano na lugha. Katika chapisho lao la Leech na Short (2008), wao wanabaini ya  kwamba umitindo umeweza kupiga hatua kwa muda mrefu huku pia ukibadilika kwa kuyakubali na kuyashughulikia mabadiliko ya kisasa. Mchakato huu ndio ulioibua nadharia ya umitindo. Leech na Short (k.h.t) wanasema kwamba kwa muda mrefu hususan kabla ya mwaka wa 1981, uhakiki mwingi wa

umitindo ulielekezwa katika ushairi na kwamba, *Style in Fiction* (1981) ndilo lililokuwa chapisho la kwanza lililohakikiwa kimitindo kinadharia. Wanakiri kuwa wakati huo, nadharia ya umitindo haikuwa na uwezo wa kuhakiki matini kwa kuhusisha matini kifasihi na mafanikio ya mwandishi kisanaa.

Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, mabadiliko makubwa yalishuhudiwa kuhusiana na nadharia ya umitindo. Wanasema kuwa kufuatia mabadiliko hayo, vilevile kulishuhudiwa mwingiliano kati ya umitindo na taaluma zingine kama vile uchanganuzi hakiki wa usemi, huku taaluma hizo zikitumia vifaa sawa vya utafiti kama vya umitindo. Wanaendelea kudokeza kuwa nadharia ya umitindo inalenga kueleza jinsi mtu anaposoma na hali ambayo humwezesha kufasiri ujumbe uliyomo kwenye matini hadi kuibua maana akilini mwake pamoja na athari anayopokea moyoni mwake. Wanahoji kuwa dhima ya nadharia ya umitindo ni kueleza jinsi wasomaji kutokana na maneno yaliyo katika matini hunufaika kwa njia ya kuelewa matini.

Wananadharia Leech na Short (1981, 2007) wanaendelea kutueleza ya kwamba dhima kuu ya nadharia ya umitindo ni kuunganisha uhakiki wa matini na mchakato wa upokezi wa maana na msomaji kwa dhana zisizo za kifasihi ambazo zikijumuishwa, huimarisha uelewa na mwitikio wa riwaya na hadithi kwa ujumla. Wao vilevile wanamwangazia msomaji aliyedokezwa na mwandishi aliyedokezwa kifasihi katika mijadala yao. Wanahoji kwamba umitindo kimatini hulenga tathmini ya kisarufi, leksia, semantiki pamoja na elementi za kifonolojia na vipengele vya kimjadala. Kulingana nao, nadharia ya umitindo hujumulisha mseto wa matawi katika tafiti za lugha.

Wamitila (2008) anasema kwamba nadharia ya umitindo ni nadharia inayojikita katika uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa, na kwamba uchunguzi huo unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo, na kwa kuutekeleza kwa undani, unasaidia katika uelewekaji wa matini au kazi za kifasihi. Ononye (2017), anabainisha aina mbili kuu za umitindo ambazo ni umitindo wa kiisimu na umitindo wa kifasihi. Kwa mujibu wake, umitindo wa kiisimu hushughulika na upekee kiisimu wa matini ya kifasihi na isiyo ya kifasihi katika aina mbali mbali za lugha, ilhali umitindo wa kifasihi huwa tu na dhima ya kueleza kirasmi vipengele vya kifasihi katika matini na athari yavyo kiisimu inapohitajika.

Simpson (2004) ametoa mawazo yake kuhusu viwango vya lugha ambavyo hufanyiwa utafiti kimitindo. Mawazo yake yamerejelewa katika Leech na Short (2007)) ambapo anavitaja viwango vikuu tisa vya lugha vinavyotafitiwa kimitindo, ambavyo ni viwango vya kifonolojia, kifonetiki, kigrafolojia, kimofolojia, kisintaksia, kileksikolojia, kisemantiki, kipragmatiki na uchanganuzi wa usemi. Wamitila (2008) anashadidia mawazo ya Simpson kama yalivyojitokeza katika Leech na Short (k.h.t) ingawa anaendelea kudokeza kwamba uchunguzi wa matini kimitindo hauwezi kuvishughulikia viwango hivyo vyote vya kiisimu kwa pamoja kwa undani bali huteua kimoja au baadhi ya viwango hivyo na kuvichunguza. Wamitila (k.h.t) anaongezea kwa kusema kwamba maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubainisha sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi. Ni kutokana na mawazo ya Wamitila (k.h.t) ndiposa utafiti huu umeshughulikia dhima na athari ya grafolojia katika uchimuzaji wa maudhui katika matini ya riwaya teule za Kiswahili za watoto.

#### 2.1.1.1 Mihimili ya nadharia ya umitindo

Wamitila (2008) amebainisha viwango kadhaa ambavyo anasema mchanganuzi yeyote wa matini ya kifasihi kimitindo anahitaji kuviangazia kwa mapana ili aweze kuikamilisha kazi yake kwa njia ifaayo. Viwango hivyo ndivyo ambavyo hudhihirika kama mihimili ya nadharia ya umitindo, na vinajumuisha vifuatavyo:

**(i) Kiwango cha grafolojia**

Kulingana na Wamitila (2008), mhimili huu pia unajulikana kama kiwango cha kimaandishi. Wamitila (k.h.t) anahoji kwamba kulingana na mhimili huu, kazi ya fasihi kimatini haiwezi kumfikia msomaji bila ya kuwa katika maandishi mahususi. Anaendelea kudokeza kuwa uchunguzi wa matini za kazi za kifasihi aghalabu unaweza kupuuza sifa hii kwa kuchukuliwa kuwa mandishi yanayopatikana yamo katika abjadi zinazoeleweka, na pia walengwa wamezizoea.

Hata hivyo, Wamitila (2008) anasema ya kwamba matini ya kifasihi inaweza kuwa na shaksiya au sifa maalumu za kimandishi ambazo zinachimuzwa na kwa njia hii, kukifanya kiwango hiki kuwa na umuhimu mkubwa katika uchanganuzi wa matini kimitindo. Anasema kuwa sifa hii hujitokeza katika kazi nyingi za kifasihi na kwamba, ni kiwango kinachohusu uakifishaji, mpangilio wa aya au hata ukosefu wake. Linalojiri ni kwamba mhimili huu hushughulika na sura ya matini na ufundi wote uliotumika katika usukaji wa matini katika fasihi hiyo.

**(ii) Uteuzi katika fasihi au suala la lugha teule**

Kulingana na mhimili huu, uteuzi wa lugha ni uteuzi wa msamiati ambao ni kitambulishi kikuu cha matini au kazi ya fasihi yoyote. Kama anavyohoji Wamitila (2008), mwandishi anaweza kufanya uteuzi ambao hana ung'amuzi wake, kumaanisha ya kwamba

mwandishi mwenyewe anaweza kuwa na ufahamu kuhusu uteuzi alioufanya au pia asiwe na ufahamu au ung'amuzi huo. Hii, anasema kuwa inaweza kudhibitiwa na sheria ambazo ziliwekwa na wandishi wengine katika jamii. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa katika jitihada za kuandika, si lazima mwandishi azizingatie kaida za lugha zilizozoeleka kwa kuwa kuna hali ambako wandishi wanazikiuka kaida hizo. Wamitila (k.h.t) vilevile anasema kwamba suala au mhimili huu hauhusu msamiati unaotumika katika matini pekee bali vipengele vingine kama vile uteuzi wa wahusika, uteuzi wa usimulizi anaoutumia, uteuzi wa mada anayoishughulikia miongoni mwa vipengele vingine. Hii ni kusema ya kwamba mwandishi anaweza kuzikiuka kaida au uzoefu uliyopo wa lugha kwa sababu kadhaa, zikiwemo za kiujumi, kiitikadi miongoni mwa sababu zingine. Kwa hivyo linakuwa jukumu la mhakiki au mchanganuzi wa matini katika hali hii kutumia tajriba yake ili aweze kuibua sababu ya uteuzi huo na pia maana inayowasilishwa.

**(iii) Sarufi**

Wamitila (2008) anadokeza kwamba sarufi hujumuisha viwango vya kifonolojia na kisintaksia vinavyoangaziwa kama msingi wa lugha, vinavyodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Anaendelea kutueleza kuwa sifa na matumizi ya lugha huathiri pakubwa uchanganuzi wa kazi za kifasihi. Mtazamo wake unaegemea katika kuangazia mchango na dhima ya vipashio vya kisarufi katika ujenzi wa kazi za kifasihi, hali ambayo inazua miundo fulani mahususi ya kisarufi kutegemea utanzu wa fasihi inayochunguzwa au kuhakikiwa. Anatoa mfano wa muundo uliozoeleka katika utanzu wa kishairi ambapo kiima hujibu swali la nani au nini kabla ya kitenzi, huku kiarifu kikijibu swali la nini,

nacho kijalizo kikijibu swali la nani au nini baada ya kitenzi, nacho chagizo kikijibu swali la vipi, lini, wapi na kwa nini baada ya kitenzi.

Kando na kuibuliwa kwa miundo, kipengele kingine kinachojitokeza ni kiwango cha umajaribio ambacho kazi za kifasihi zitaashiria kuwa za sentensi yenye neno moja au zingine zipuuzwe kwa kutazamwa kama sentensi zenye dosari. Vilevile anataja sifa ya udhamiriaji au njia za kiisimu zinazotumiwa kuvumishia nia alionayo mtumiaji wa lugha. Mhimili huu kwa hivyo unalenga kumchochea mhakiki na mchanganuzi wa kazi za kifasihi kuwa na jicho pekuzi pamoja na ufahamu mpana katika kutekeleza kazi yake ili aweze kuibua maana mahususi ya kazi ya kifasihi kimatini.

**(iv) Muundo wa usimulizi.**

Huu ni mhimili unaoendana na msuko wa kazi ya kifasihi kimatini. Wamitila (2008) amesema ya kwamba sifa hii inahusu mambo kadhaa kama vile nani, chanzo, nini hatima na vipi. Kazi za kifasihi kimatini zinadhihirisha mfichuo mwanzoni ambao unaweza kuwa wa aina mbalimbali na kisha mwili ambao ndio sehemu kuu ya msuko inayoelezea mgogoro uliyomo katika kazi za kifasihi. Hii ni sifa muhimu katika uchanganuzi wa kazi za kifasihi kimitindo.

**(v) Uchimuzi kifasihi**

Wamitila (2008) anasema kwamba dhana hii ni muhimu mno katika fasihi kutokana na athari za nadharia ya Urasimu wa Kirusi na kwamba, ni dhana iliyo na umaarufu katika tanzu za kishairi kuliko tanzu zingine za kifasihi. Kulingana na Wamitila (k.h.t), kuchimuza kitu ni kukifanya kitu hicho kitokezee mbele na kionekana, na ni sifa ya matumizi ya lugha au muundo wa kukiuka sifa za kawaida za matumizi ya lugha kwa

kubadilisha muundo au mpangilio uliozoelewa au unaochukuliwa kama wa kawaida na kaida katika lugha. Anahoji kuwa uchimuzi unaweza kuwa uchimuzi wa ukiushi wa kimaana ambao hutumia lugha kitamathali na pia ule uchimuzi wa kisauti zinazorudiwarudiwa.

**(vi) Miundo ya lugha**

Wamitila (2008) anadokeza kwamba uchunguzi wa lugha ya matini kifasihi unapaswa kuchunguza matumizi ya jazanda ambayo anasema kwamba kimsingi, ni matumizi ya lugha ya picha na inaweza kupatikana kwa njia mbili kuu. Anabainisha jazanda za kimaelezo ambazo huangazia maelezo yanayopatikana katika matini fulani na jazanda za kiishara ambazo ni taswira zenye ujumbe wa ziada. Kwa mujibu wake, uchunguzi wa taswira ni vyema iwapo utaangazia taswira kwa upana wake. Kando na hilo, anaangazia miundo katika hali ya urefu au ufupi wa sentensi, usahili na uchangamano wa sentensi na pia uhusishi na unasibishi wa matini kifasihi.

**(vii) Mazungumzo na mbinu za uwasilishaji wa usemi na mawazo**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), uchanganuzi wa matini kifasihi kwa msingi wa nadharia hii ya umitindo hauna budi kuchunguza mazungumzo pamoja na mikakati tofauti inayotokeza kwenye mazungumzo yenyewe pamoja na mbinu zinazotumiwa kuwasilisha semi na mawazo katika matini kifasihi ambayo ni huru au halisi kimawazo au kwa usemi.

**(viii) Mtazamo na mtindo**

Wamitila (2008) amedokeza kwamba mtazamo na mtindo ni vipengele muhimu katika uchanganuzi wa umitindo wa matini kifasihi kutegemea mkabala na mchango wa mwandishi kuhusu upokezi wa yale ambayo huangaziwa.

**(ix) Lugha na itikadi**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), uchanganuzi wa kazi za kifasihi ni vyema uchunguze itikadi ya mwandishi wa kazi inayohusika. Hii ni kwa sababu mchanganuzi anahitaji kuangazia jinsi mwandishi alivyoitumia lugha kubainisha na hata kuichimuza itikadi hiyo. Kwa hali hiyo, mchanganuzi wa matini kimitindo atachunguza jinsi uteuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu na mipangilio au ruwaza zake kwa jumla unavyochangia katika kuiangazia itikadi hiyo.

**(x) Muwala na mshikamano**

Muwala hurejelea sifa za kiisimu zinazoonyesha jinsi maneno, virai, vishazi au sentensi zinavyohusiana katika matini ilhali mshikamano unahusiana na maana ya usemi kwa ujumla. Matini za kifasihi haziwezi kuwa na mshikamano bila ya kuwepo kwa sifa za kimtindo au kibalagha kwa vile lugha huwa ni jira muhimu katika ujenzi na udumishaji wa maana ya matini inayohusika. Kulingana na mawazo ya Simpson kama yanavyowasilishwa katika Leech na Short (2007), viwango hivi hudhihirisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu mno na ndivyo ambavyo huchukuliwa kama mihimili ya nadharia ya umitindo. Hata hivyo utafiti huu umechunguza vipengele mbalimbali vya kigrafolojia ambavyo watunzi hutumia katika ujenzi wa riwaya ya watoto ya Kiswahili. Hii ni kusema ya kwamba ni utafiti ambao umeangazia sura ya matini kifasihi ambayo

inahusu mpangilio wa maandishi pamoja na viziadalugha vyote katika matini ambavyo vimeteuliwa kimaksudi.

Kama wanavyoeleza Leech na Short (2007), nadharia ya umitindo inahusu matumizi ya vipengele mbalimbali vya kigrafolojia miongoni mwavyo, matumizi ya mlazo, herufi nzito, michoro, katuni na hata fonti mbalimbali za maneno. Wanashikila kuwa matumizi mema ya lugha ni ule ufundi wa mwandishi kujieleza, na kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya lugha na fasihi, na wanasisitiza kuwa grafolojia ni kipengele muhimu katika uandishi.

### 2.1.2 Nadharia ya Mwitikio wa msomaji

Nadharia ya Mwitikio wa msomaji iliasisiwa na Rosenblatt mwaka wa (1939) alipobashiri kwamba fasihi ni jumuisho la utangamano kati ya vitabu na msomaji, na kisha ikachangiwa na wahakiki wengine wengi wakiwemo Burke (2014). Kulingana na Rosenblatt (k.h.t), maana katika matini hupewa uhai na msomaji wakati ambapo msomaji huyo hutumia ujuzi wake na tajriba alionayo katika kuufasiri vyema ujumbe unaojitokeza katika matini. Kwa mujibu wa Burke (k.h.t), miongoni mwa wananadharia waliochangia pakubwa katika kuifafanua na kuipa nadharia hii umaarufu ni pamoja na akina Hirsch (1967), Holland (1968, 1975), Bressler (1973), Culler (1975), Bleich (1975), Fetterley(1978), Iser (1978), Fish (1980), Cuddon (1980), Rabinowitz (1980), Tompkins (1980), Riffaterre (1981), Jauss (1982), Booth (1983), Eco (1989) na wengine.

Mwitikio wa msomaji kama nadharia ulichochewa na swali hili: Je, matini ina maana yoyote bila msomaji na ufasiri? Swali hili lilizua msisimuko mkubwa katika miaka ya sabini kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji. Kwa mfano mwananadharia Holland

(1968) alitumia mtazamo wa uchunguzi nafsia wa Sigmund Freud uliotumika kutoa tiba ya kiakili katika kueleza mwitikio wa msomaji, huku akipendekeza ya kwamba, fasihi huwasilisha mgeuzo wa nyenzo kwa tajriba ya kisaikolojia ya msomaji. Kwa mujibu wake, matini inaweza kuwakilisha fantasia au chukizo kwa msomaji na pia inaweza kumpa starehe katika muunganisho wake na matini, hivyo basi maana iliyotokana na uchunguzi nafsia katika matini ndiyo ya kimsingi.

Naye mwananadharia Culler (1975) alitumia mpango wa kueleza mfumo wa msomaji bali sio wa mwandishi katika kuilezea nadharia ya mwitikio wa msomaji. Alimtaja msomaji kama mtu mwenye umilisi kifasihi na kwa kuwa ana umilisi huo, msomaji alihitaji mfumo wa kuelekezwa. Kulingana naye, ujenzi wa umilisi ulihusu uigaji wa kaida na mifumo ambayo msomaji anahitaji kuwa nayo ili kuelewa matini ya ziada. Fetterley (1978) aliutumia mtazamo wa kijinsia katika kuangazia uhusiano baina ya msomaji na matini. Alisema kwamba si lazima msomaji akubaliane na lugha iliyotumika katika matini. Kwa sababu ya mtazamo wake wa kifeministi, aliwarai wasomaji kupinga matini yoyote iliyokuwa na hisia na mielekeo yoyote hasi, na ambayo ililenga kuwadunisha wanawake. Hii iliathiri kazi ambazo ziliandikwa na wandishi wa kiume wa Kimarekani kama vile akina Hawthorne, Fitzgerald miongoni mwa wengine.

Wolfgang (1978) alipendekeza kuibuliwa kwa maana kutokana na kutangamana kwa msomaji na matini. Yeye aliona matini kama ukweli usio bayana uliojitokeza baina ya nguzo mbili; nguzo ya kisanaa inayohusishwa na mwandishi, na nguzo ya kiujumi inayohusishwa na msomaji. Kulingana naye, matini ilikuwa na mapengo aliyoyaita kwa

lugha ya Kijerumani *Leerstellen*, mapengo ambayo yangejazwa tu na msomaji wa matini baada ya kutangamana na matini kwa kina na kuibua maana.

Kwa mujibu wa Bleich (1978), maana ya matini imo akilini mwa msomaji na kwamba kupitia kwa mchakato wa usomaji, msomaji hujiisharaisha na matini mara kadhaa na kisha kuibua maana. Holland (1980) naye alisema kuwa uhusiano wa msomaji na matini ni jukwaa la msomaji kuleta matarajio yake yasio kifani, hofu na matamanio katika matini kupitia kwa ulinzi dhidi ya bunilizi za kimpito ili kuibua ujitambulishaji. Holland (k.h.t) aliendelea kusema kuwa ujitambulishaji hudhihirika wakati ambapo msomaji katika ukamilifu wake anaelezea hisia zake, na katika hali hiyo, kuufikia ufasiri ambao ni furaha ya mchakato wa kisaikolojia.

Hawa wananadharia walishikilia kuwa msomaji wa matini ndiye mwenye uwezo wa kueleza yale ambayo yamo katika matini, na maudhui ya matini huathiriwa na vipengele vingine ambavyo huwa nje ya matini. Licha ya kuwa wananadharia hawa waliendeleza uitikiaji wa msomaji, waliangaziwa kama wafuasi na watetezi wa nadharia ya uhakiki mpya, inayoshikilia kuwa maana hujitokeza tu katika matini na kwamba, maana hiyo inaweza kutambulika tu na mhakiki wa kifasihi mtajika, mwenye ujuzi mpana wa kuhakiki.

Fish (1980) ndiye aliyeonekana kuwaathiri wengi katika maelezo yake kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji, hususan nchini Marekani ambako wahakiki wa nadharia hii waliweza kuangaziwa kama wafuasi wa mawazo ya shule ya Fish. Fish (k.h.t) aliwazia kwamba matini ilikuwa mchakato wa kulifanya tukio bali sio kukifanya kitu. Katika kitabu chake *Is There a Text in This Class?* (1980), Fish (k.h.t) alibashiri kwamba

wasomaji wale wale wangeweza kuwa na mawazo na ufasiri sawa wa matini sawa kwa vile ni wa jamii sawa ya ufasiri. Alifafanua jamii sawa ya ufasiri kama wale wasomaji ambao walikuwa na mikakati sawa ya uandishi wa matini. Fish (1980) alimtazamia msomaji kama mtu aliyeumba upya matini, kila wakati alipoisoma. Hii ilitokana na mtazamo wake kwamba maarifa wakati mwingi hudhibitiwa na muktadha wa kijamii ambamo msomaji huishi.

Kwa hivyo mitazamo mbalimbali iliweza kuibuliwa kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji. Wengi waliyashadidia mawazo yaliyoshikiliwa na Rosenblatt kwamba maana huibuliwa tu kutokana na utangamano wa msomaji na matini. Purves na Beach (1972) walichangia katika mdahalo huo kwa kushikilia kwamba, mwitikio wa msomaji ulikuwa mtagusano wa msomaji na matini. Waitifaki wa nadharia hii huzingatia sana maana inayoibuliwa na msomaji kutoka kwenye matini, jinsi msomaji anavyoitikia ujumbe uliyomo katika matini fulani na kwa njia fulani.

Kwa hivyo hii ina maana ya kwamba, umaizi na uhitimisho wa msomaji huongozwa na msingi wa ujuzi aliyo nao, na kwamba tajriba ya msomaji huchangia katika ufasiri ambao msomaji ataufikia. Rosenblatt (1978) aliitazama matini kama chombo kilichoumbika kutokana na wino na karatasi, ambacho msomaji huitikia. Kwa mujibu wake, ni msomaji ambaye huibua maana kutoka kwenye chombo hicho chenye unyunyizio wa wino, ambacho anasema kuwa huwa kama mapatano ya msomaji na matini.

Akitoa mchango wake, Iser (1980) alisema kuwa makutanio hayo yatasalia bayana bila kujihusisha na uhalisia wa matini wala mitazamo ya msomaji. Alimtambulisha mwandishi na msomaji kisanii na kiujumi ambao kupitia kwa mapatano yao, maana ya kisanii hujadiliwa. Kwa mujibu wake, maana haiwezi kufikirika kibinafsi na msomaji au

kuzalishwa kipekee na matini bali huzalishwa kupitia kwa mchakato kamili kati ya msomaji na matini.

Jauss (1982) aliitumia dhana ya upeo wa matarajio kuelezea athari za kitamaduni ambazo zinaweza kumuathiri msomaji wa kazi yoyote kifasihi katika muktadha wa kihistoria. Kulingana naye, kazi yoyote ya matini kifasihi huwa ni muungano wa matukio ya kihistoria, na kwa hivyo ufasiri wowote kimaana wa kifasihi hutegemea pakubwa msomaji katika uhusishaji na utekelezaji kimatini. Jauss (k.h.t) aliweka msisitizo kwa mazingira ya kitamaduni ya msomaji kama yenye mchango mkubwa katika ufasiri wake wa matini kwa vile humwekea msingi sawa wa kuudhibiti ufasiri wake.

Akichangia kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji, Abdulmughni (2016) amesema ya kwamba usomaji wa kazi za kifasihi hujumuisha ustadi wa vipengele vilivyomo katika matini na ufahamu wake kimaana. Kulingana naye, katika usomaji, msomaji hujipata akiwa ametekwa nyara na vipengele vingine visivyo vya kiisimu ambavyo hujitokeza katika matini. Maana katika matini hiyo huibuliwa kutokana na mwingilianomatini na uhusiano wa msomaji pamoja na tajriba yake katika ufasiri wa matini anayoishughulikia.

Kulingana na nadharia ya mwitikio wa msomaji, usomaji ni mchakato wa mapatano ambao unawapa wasomaji fursa ya kutumia tajriba yao maishani ili kuufasiri ujumbe uliyomo katika matini. Kwa hivyo nadharia ya mwitikio wa msomaji inashikilia kuwa msomaji wa matini ndiye mwenye uwezo wa kuyafasiri yaliyomo katika matini. Kama inavyorejelewa katika Hartono (2017), nadharia hii inasisitiza ya kwamba msomaji anahitaji nafasi bora zaidi kibinafsi katika kutangamana na matini ili kuufikia ufasiri uliyo mwema.

Rosenblatt (1978) aliyaendeleza mawazo yake kuhusu nadharia hii kwa kusisitiza ya kwamba matini haiibui maana sawa kwa wasomaji wote, na kuwa kila mmoja wa wasomaji hupokezwa athari za kimsingi zinazotokana na imani, maadili, utamaduni na ujuzi wa usomaji. Utafiti huu umeongozwa na mtazamo wa Rosenblatt (1939, 1978) na waitifaki wa nadharia ya mwitikio wa msomaji ambao wanashikilia kuwa maana katika matini hufikika kufuatia mapatano na utangamano kati ya msomaji na matini.

#### 2.1.2.1 Mihimili ya nadharia ya mwitikio wa msomaji

Nadharia hii huongozwa na mihimili ifuatayao kwa mujibu wa Rosenblatt (1978):

(i) Usomaji ni tukio la kimapatano.

(ii) Usomaji ni tukio la kiwakati.

(iii) Usomaji ni tukio la kijamii na kitamaduni.

(iv) Usomaji ni tukio linalogeuzika.

**(i) Usomaji kama tukio la kimapatano**

Kulingana na Rosenblatt (1978), mhimili huu unasisitiza kuwa shughuli za usomaji wa matini zinahusu mapatano kati ya msomaji na matini, na kwamba miongoni mwa vipengele vingine vinavyohusika katika uibuliwaji wa maana ni pamoja na msingi wa mwandishi na muktadha wa kijamii na kitamaduni. Mhimili huu hushikilia kwamba msimamo wa msomaji kuhusu matini huathiri jinsi matini inavyosomwa. Kuna aina mbili ya misimamo ambayo huibuliwa kutokana na mhimili huu ambayo ni:

**(a) Msimamo changamfu**

Msimamo changamfu ni aina ya msimamo ambao hulenga au huongozwa na hoja ambazo huibuka wakati wa usomaji matini. Hii kwa hivyo inaweza kutazamwa kana

kwamba msomaji husoma kwa nia ya kupokea ufahamu ambao utamwezesha kutumia ujuzi fulani katika ulimwengu halisi. Kimsingi, Rosenblatt (1978) anasema kuwa hii hulenga tu kile ambacho kinaweza kukusanywa kutokana na usomaji wa matini ili kitumike baadaye na hujumuisha habari zitakazopatikana, suluhu ya kimantiki kwa changamoto na jinsi ya kutekeleza suluhu hiyo.

**(b) Msimamo wa kiujumi**

Rosenblatt (1978) aliibua dhana ya kiujumi kutoka kwa mzizi wa lugha ya Kigiriki wenye maana ya utambuzi kupitia kwa hisi na kipaji cha kuhisi bila kufikiria. Msimamo huu unamruhusu msomaji kuwa na tajriba ya matini anayoisoma ili mwenyewe aibuke na ufasiri. Katika kufanya hivyo, masuala ya maadili pia huangaziwa na msomaji.

**(ii) Usomaji ni tukio la kiwakati**

Kulingana na mhimili huu, usomaji wa matini ni tukio la kiwakati kama anavyosema Rosenblatt (1978). Hii ni kumaanisha ya kwamba msomaji husoma na kupata maarifa yaliyo na uwezo wa kuyapanua mawazo yake kuhusu ulimwengu. Maarifa hayo yanastahili kumwezesha msomaji kuyaweka katika utekelezaji. Kama ambavyo mhimili huu unavyoelekeza, usomaji matini kiujumi hutukia katika matarajio na kumbukumbu ambazo hujitokeza kupitia kwa kubashiri, kuidhinisha na kutoidhinisha. Kutokana na mhimili huu, msomaji anapoyasoma matini, ujuzi alionao humwezesha kujenga picha au taswira fulani akilini mwake kutoka kwenye maneno, na anapofanya hivyo, anaweza kutangamana na kubashiri matukio kutoka uhamisho wa kijamii hadi kwenye maliwazo kiujumi. Msomaji anapofanya hivyo, anapata fursa ya kuitathmini hadithi na kuchochewa kuendelea kuisoma kwa manufaa yake kwa ujumla.

**(iii) Usomaji ni tukio la kijamii na kitamaduni**

Mhimili huu unashikilia kuwa usomaji ni tukio la kijamii ambalo linawahusisha wanajamii katika mchakato mzima wa usomaji. Hii inatokana na dhima kuu ya shule ambako usomaji huimarishiwa. Kupitia kwa usomaji huu, msomaji hujifunza kutokana na matini na hutenda jinsi anavyotakikana kutenda kwa muktadha wa utamaduni wa jamii husika. Hili hufanyika kwa sababu msomaji ni zao la kijamii, na wanajamii huongozwa na maadili na mielekeo mahususi. Vilevile wandishi wa matini ni wazawa wa jamii, kwa hivyo yale wanayoyandika yanahusu jamii walimozaliwa kama alivyoeleza Rosenblatt (1978).

**(iv) Usomaji ni tukio linalogeuzika**

Rosenblatt (1978) alisema kwamba mhimili huu hushikilia kuwa usomaji ni tukio ambalo linaweza kugeuzika. Hii hutokana na manufaa yanayopatikana na usomaji. Msomaji hujiimarisha kiufahamu na hivyo basi kuyakubali maadili mema ambayo humfanya kugeuka na kuwa mwanajamii mwema.

### 2.1.3 Ufaafu wa nadharia za utafiti

Mihimili mbalimbali ya nadharia hizi ilitumika katika uchanganuzi wa data. Mihimili ya nadharia ya umitindo ambayo ilitumika katika utafiti huu ni pamoja na kiwango cha grafolojia ambacho kinahusu mandishi na sura ya matini kwa ujumla. Mhimili huu ulikuwa mwafaka kwa vile utafiti huu ulishughulikia vipengele vya kigrafolojia na ufundi unaotumika katika usukaji wa matini ya kifasihi na wandishi. Ni mhimili ambao ulichangia pakubwa katika ubainishaji wa vipengele vya kigrafolojia ambavyo vilitumika katika ujenzi wa riwaya teule zilizochanganuliwa na dhima inayotekelezwa na vipengele

vya kigrafolojia katika fasihi, hususan fasihi ya watoto. Hata hivyo, kutokana na mhimili huu, utafiti huu ulizamia katika kuvibainisha vipengele vyote vya kigrafolojia, kwa kuibua vipengele vingine ambavyo watafiti wa awali hawakuvizingatia kama vipengele mahususi vya kigrafolojia. Kati ya vile vipengele vya kigrafolojia vilivyoibuliwa ni pamoja na faharasa, mazoezi na maswali tamatini mwa matini pamoja na majedwali.

Vilevile mhimili wa uteuzi katika fasihi au suala la lugha teule ulitumika kwa vile katika usukaji wa kazi ya fasihi kimatini, kuna ukiukaji wa ukawaida uliozoeleka, sifa ambayo hujitokeza katika matini ya kifasihi. Katika tanzu za kifasihi, watunzi wengi hudhihirisha upekee wa kiasi fulani katika uteuzi wa lugha wanayoitumia ambayo ni pamoja na ukiukaji wa hali iliyozoeleka. Hali hii ya uteuzi imeshughulikiwa na mhimili huu kwa kuwa ilidhihirika kwamba baadhi ya wandishi wa fasihi ya watoto huzikiuka kaida za uandishi zilizozoeleka na kwa hali hiyo kuendeleza upekee kiutungaji. Hata hivyo, kutokana na mhimili huu, utafiti huu ulidhihirisha dhima kadhaa ya ukiukaji huo, kando na kuutambulisha upekee wa mwandishi. Kwa hivyo, mhimili huu ulichangia pakubwa katika ukamilishaji wa utafiti huu.

Pia kuna mhimili wa sarufi na tanzu ambao umedhihirika tunapokumbana na sentensi hata za neno moja katika matini. Kwa vile fasihi kimatini haiwezi kumfikia msomaji bila kupitia kwa uandishi, baadhi ya aya za riwaya zilizochunguzwa zilionekana kujengeka hata kwa maneno mawili, kwa hivyo hali hii ni sehemu mojawapo ambayo ilishughulikiwa na mhimili huu.

Aidha mhimili wa uchimuzi kifasihi pia ulitumika katika utafiti huu kwa vile uchimuzi ni mojawapo ya athari inayozalika wakati mwandishi anapovitumia vipengele vya

kigrafolojia anapotaka kuyawasilisha maudhui yake kwa njia ifaayo. Mhimili wa miundo ya lugha ndio ulikuwa wa mwisho. Kulingana na mhimili huu kama anavyoelezea Wamitila (2008), kazi nyingi za kifasihi hujengeka kwa matumizi ya jazanda. Anaendelea kueleza ya kwamba jazanda kwa kawaida ni matumizi ya picha zinazoweza kupatikana kwa njia mbili kuu ambazo ni: jazanda za kimaelezi (kutegemea maelezo) na jazanda za kiishara ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada. Baadhi ya riwaya zilizochunguzwa zilikidhi miundo hii ya lugha na kwa hivyo huu mhimili uliufaa utafiti huu. Utafiti huu umedhibitiwa na madhumuni miongoni mwayo kutathmini athari ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto ambayo imeshughulikiwa na mhimili huu.

Kwa muhtasari, uchanganuzi kimitindo bila shaka ni utafiti unaonuia kujenga daraja kati ya utafiti wa kifasihi na utafiti wa kiisimu kimatini. Utafiti huu unapoegemezwa katika matini ya kifasihi, unachangia pakubwa katika uimarishaji wa ufasiri na ufahamu na kwa hivyo kumwezesha msomaji wa kazi ya kifasihi kuwa na ujuzi na ujasiri wa kuishughulikia kazi yoyote ya kifasihi. Kama anavyosema Carter (1996), umitindo humwezesha msomaji kuwa na ujuzi wa kufasiri na kumchochea kukisia na kwa mwanafunzi, umitindo humwezesha kuhakiki na kuchanganua matini kwa namna inayostahili na hivyo basi kumnufaisha kwa njia nyingi.

Nadharia ya mwitikio wa msomaji vilevile ilitumika katika utafiti huu. Ni nadharia ambayo inashikilia kwamba fasihi ni zao la vitabu na msomaji, na kwamba maana kifasihi huibuliwa wakati msomaji anapotangamana na vitabu. Mihimili kadhaa ya nadharia hii iliunufaisha utafiti huu. Hii ilikuwa ni pamoja na mhimili wa usomaji kama

tukio la kimapatano, ambao unashikilia kwamba maana kimatini huibuliwa baada ya msomaji kutangamana na matini. Mhimili huu pia unadokeza kwamba msomaji anaweza kuathiriwa na matukio ya kimuktadha kijamii na kitamaduni anapoibua maana kutoka katika matini. Mhimili huu uliufaa utafiti huu kwa kuwa uibuliwaji wa maana kimatini ndio dhima ya mwandishi.

Mhimili wa usomaji kama tukio la kiwakati unahusu tajriba ya msomaji katika kufasiri vyema ujumbe uliowasilishwa na mwandishi akiwa anavielewa vipengele vilivyotumika katika ujenzi wa kazi ya kifasihi. Ni mhimili unaohusu uwezo wa kumbukumbu alionao msomaji katika kuibua ufasiri mwema na manufaa yatokanayo na matini hiyo. Mhimili huu umeudhibiti utafiti huu hususan katika kubashiri viwango mbalimbali vya wasomaji wa matini kiumri na ufasiri mwafaka pamoja na athari inayoibuliwa wakati vipengele fulani vinapotumika kimatini.

Vilevile mhimili wa nadharia hii wa usomaji kama tukio la kijamii kitamaduni umetumika katika muktadha wa kuiendeleza fasihi ya watoto kama utamaduni ambao unalenga kuwaimarisha wasomaji wachanga kwa ujumla; kimawazo, kijamii na hata kiuchumi. Katika kuangazia mhimili wa usomaji kama tukio linalogeuzika, mhimili huu umeunufaisha utafiti huu kwa vile kutokana na usomaji wa fasihi ya watoto, msomaji mchanga huathirika kitamaduni na katika hali hiyo, huyakuza maadili mema huku akitengana na uozo ambao huenda ameushuhudia kwa kuepuka athari za wahusika hasidi katika matini. Hii kwa hivyo ni kusema kwamba mihimili yote minne ya nadharia ya mwitikio wa msomaji imeunufaisha utafiti huu. Nadharia hizi mbili pamoja na mihimili

ambayo imetajwa na kuangaziwa zimeufaa utafiti huu kwa vile zimeendana na madhumuni na maswali ya utafiti.

Fasihi ya watoto ina misingi anuai kinadharia. Mathalani, Ngugi (2009) alizitumia nadharia tatu katika utafiti wake. Nadharia ya kwanza aliyoitumia ilikuwa utambuzi maendeleo, ilioasisiwa na Jean Piaget (1896-1980) na ikafafanuliwa zaidi na Lev Vygotsy (1896-1934). Wananadharia hawa humchukua mtoto kama mshiriki tendi katika ujenzi wa ufahamu, licha ya kuwa uriithi kibiolojia na kimazingira huathiri jinsi mtoto anavyosoma. Kwa mujibu wa Piaget (1950) akirejelewa katika Ngugi (k.h.t), mtoto hupitia awamu nne katika maendeleo na ukuaji wake kiakili, na kwamba katika kila awamu, mtoto hudhihirisha viwango mbalimbali vya manufaa anayoyaafiki kiidadi, kiubora, kimaadili na kiwakati ambavyo hudhihirisha maendeleo yake kimantiki.

Piaget (1950) alizianisha awamu hizo, huku awamu ya kwanza (1) ikiwa kuhisi (kunusa, kuonja, kuona, kusikia na kushika) ambapo kupitia kwa kuhisi, mkembe huutambua ulimwengu kihisia. Awamu ya pili (2) aliita umri wa kabla ya uchunguzi, ambayo Piaget (k.h.t) katika Ngugi (k.h.t) alisema kuwa awamu hii huwajumulisha watoto kati ya umri wa miaka miwili na saba (2-7). Ni awamu ambapo watoto huanza kuhudhuria masomo ya asasi ya chekechea, na aliihusisha awamu hii na wanyama, uhalisia na ubinafsi ambapo watoto hukuza ufahamu wa mahusiano na mazingira. Awamu ya tatu (3) aliita uchunguzi wa kudumu ambayo alisema ilijumuisha watoto kati ya umri wa miaka saba na kumi na moja (7-11). Kulingana naye, awamu hii inahusika na usomaji, ambapo mtoto anao uwezo wa kuainisha chochote anachokumbana nacho, licha ya kwamba huenda uainisho huo ukakosa umantiki. Aliita awamu ya nne (4) ya uchunguzi rasmi, ambayo

alisema kwamba inawashirikisha watoto wa miaka kumi na moja (11) na zaidi na ilidhihirika kwamba watoto wa awamu hiyo walikuwa na uwezo wa kufikiria kirasmi.

Kwa mujibu wa Huck (1979), vitabu vinaweza kuwa na mwanzo wa uigaji wa ufahamu. Hii ina maana ya kwamba fasihi inaweza kuzalisha mchakato wa ukubalifu kwa kuwapa watoto mwanga wa kuutazama ulimwengu wao kwa njia tofauti. Inapofanyika hivyo, hiyo huwa ishara kwamba mtoto anaukubali ulimwengu kwa mtazamo mpya. Katika uhitimisho wa Ngugi (2009), ilibainika wazi kwamba nadharia hii ya utambuzi kimaendeleo ni mwafaka katika kupima ufahamu wa msomaji wa kazi yoyote ya kifasihi kwa vile tunaweza kupokea habari kuhusu kichochezi kinachomfanya msomaji kuipenda kazi fulani.

Ngugi (2009) pia ameitumia nadharia ya mwitikio wa msomaji. Ni nadharia ambayo iliasisiwa na Rosenblatt mwaka wa (1939) alipoibua makisio kwamba msomaji na matini lazima watekeleze majukumu kwa pamoja ili waweze kuibua maana. Kwa mujibu wake, nadharia hii ilimfaa katika kutathmini mwitikio wa msomaji (mtoto) wa vitabu alivyovisoma. Ngugi (k.h.t) anawanukuu Purves na Beach (1972) wanaofafanua 'mwitikio' kama kuathiriana kunakoendelea kati ya msomaji na kazi za kifasihi, na wanaeleza kwamba kuathiriana huku kunaweza kuendelea, hata baada ya msomaji kumaliza kuisoma kazi hiyo. Kwa mujibu wao, mwitikio unaweza kujitokeza wazi kupitia kwa uchunzaji wa kazi zilizolengwa au hata zilizokataliwa na msomaji.

Ngugi (2009) vilevile aliweza kueleza kwamba nadharia ya mwitikio wa msomaji inayo mitazamo mbalimbali ambayo kwa ujumla wake, iliwalenga wasomaji komavu kijamii, ingawa hivi sasa, imeanza kutumika na watafiti walio na mvuto kwa wasomaji wa umri

mdogo. Ngugi (k.h.t) anamnukuu Cuddon (1991) ambaye anasisitiza kwamba nadharia hii ilipendekeza maana iibuliwe kutoka tu kwa matini bila kuihusisha na muktadha, ufahamu wa kihistoria au hisia za mwandishi wa matini.

Nadharia ya tatu ambayo Ngugi aliitumia ni ya usomaji kijamii iliyoasisiwa na Albert Bandura (1977, 1986, 1992) ambayo msingi wake ni nadharia ya Ivan Pavlov (1849-1936) ya usomaji. Ni nadharia ambayo inasisitiza umuhimu wa uchunzaji na mifano kitabia, mielekeo na mvuto wa kihisia kwa wengine. Kwa mujibu wa Bandura (k.h.t) kama anavyoelezea Ngugi (2009), watoto hujifunza mengi kitabia kupitia uchunzaji, kama vile jinsi ya kuwalinda na hata kuwaadhibu wengine. Anasema kwamba wazazi na wanajamii wengine ndio wanaoigwa kitabia. Bandura aliita hali hii usomaji kiuchunzaji.

Licha ya kwamba Ngugi (2009) ameitafitia fasihi ya watoto kwa mapana kwa kutumia nadharia tatu zilizotajwa, utafiti huu umetumia nadharia mbili ambazo ni nadharia za Umitindo na Mwitikio wa msomaji. Uamuzi wa kuzitumia hizi nadharia mbili umetokana na nia ya mtafiti ya kutathmini sura za vitabu ambavyo watoto husoma, akitumia nadharia ya umitindo, akidadavua matini, akiviainisha vipengele vya kigrafolojia na kuchanganua dhima yavyo, huku nadharia ya mwitikio wa msomaji ikimfaa mtafiti katika uchunzaji wa kushiriki na usaili usio rasmi wa wanafunzi na walimu, akilenga kufahamu athari ya vipengele vya kigrafolojia kwa wasomaji wa umri mdogo, jinsi vipengele hivyo vinavyoyachimuza maudhui au ujumbe uliyomo katika matini. Kwa hivyo, nadharia ya umitindo imemfaa mtafiti kwa kushughulikia madhumuni ya kwanza (1) na ya pili (2) katika kubainisha vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika fasihi ya watoto na dhima ya vipengele hivyo katika fasihi ya watoto. Nadharia ya mwitikio wa msomaji imemfaa mtafiti katika kushughulikia madhumuni ya tatu (3) kwa kutathmini athari ya

vipengele vya kigrafolojia katika ufasiri wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga.

**2.2 Dhana ya grafolojia**

Maana ya grafolojia ilitolewa maelezo katika sura ya kwanza ya utafiti huu. Hata hivyo, Levenston (1992) aliiangazia dhana hii kwa kina na akavibainisha viwango vya uchanganuzi wa grafolojia katika lugha. Aliongeza kwa kutaja vipengele vya taipografia na mpangilio wa kurasa kama miongoni mwa vipengele mahususi vya kigrafolojia. Lennard (2005) naye aliviainisha viwango vinane (8) ambavyo alivieleza kama vya kimsingi katika uchanganuzi wa matini kigrafolojia. Kwa mujibu wake, viwango hivyo vilijumuisha mifumo ya alfabeti ambayo hujalizwa kwenye kurasa tupu, nafasi kati ya maneno, viakifishi, maneno au vipengele vingine vilivyotofautishwa na aina ya fonti, sura, rangi, ishara au mahali pake, mpangilio wa ukurasa na ufunguzi, jinsi nambari zinavyowekwa katika kurasa, miundo ya mikusanyiko ya kurasa na hatimaye ujumla wa matini. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba wataalamu hawa wanatofautiana kuhusu idadi dhahiri ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo ni vya kimsingi katika uchanganuzi wa matini.

Kulingana na Crystal (1995), grafolojia ni dhana inayorejelea tawi la isimu linalochunguza mifumo ya ishara inayotumika kuwasilisha lugha kwa mfumo wa kimandishi. Aliendelea kudokeza kwamba mfumo huo wa kimandishi ulijumuisha othografia (mfumo wa mwendelezo wa maneno), stenografia (unukuzi kwa kutumia alama za ishara au vifupisho), teknografia (masomo ya sanaa na sayansi tekelezi kuhusiana na msambao wa kijiografia) pamoja na pedografia (maelezo ya kisayansi yanayohusu uhifadhi wa rekodi). Short (1996) aliendeleza mjadala huu kwa kusema

kuwa kuligawanisha neno katika mofu zake au kuyandika maneno bila kuzingatia nafasi za kiothografia ni kuendeleza grafolojia.

Hata hivyo, kulingana na mawazo ya Alo yanayojitokeza katika Yeibo na Akerele (2014), grafolojia ni dhana mojawapo ambayo inahusiana na viwango vya lugha kimtindo, na wanaviainisha viwango hivyo kama fonolojia (sauti na athari yake), leksia (matumizi ya maneno), sarufi (neno na miundo ya sentensi), semantiki (maana), grafolojia (othografia au mifumo ya uandishi) na pragmatiki (matumizi ya lugha). Katika uainisho huu, grafolojia inajitokeza kama kiwango cha uchanganuzi wa kiisimu ambacho hulenga sura ya matini, kiwango cha ukubwa na sura ya maneno na vipengele vingine vyovyote vya mandishi au michoro ambavyo hujenga mvuto katika matini.

Yeibo na Akerele (2014) wamesema kwamba kutokana na dhana ya grafolojia, vipengele visivyo vya kiisimu katika matini kama vile michoro na picha huweza kufasiriwa katika hali ya kuimarisha ujumbe uliobebwa pamoja na matini. Mawazo ya Eva (2015) yanashadidiana na ya Wales (2001) anaposema kwamba grafolojia ni dhana inayotumiwa kurejelea kiwango cha kiisimu katika uchanganuzi kinachojumuisha utafiti wa sanaa za mandishi, uchoraji na unakshi katika lugha. Anaendeleza maelezo yake kwa kusema kwamba dhana hii ilijitokeza mwanzoni katika tafiti za kiisimu miaka ya sitini na ilianzishwa na McIntosh (1961), aliyeitumia dhana hii katika lugha andishi, huku kiwango cha fonolojia kikitumika kurejelea hali hiyo katika lugha ya usemi. Anasema kuwa umuhimu na hadhi ya grafolojia kama kiwango cha uchanganuzi kiisimu hujitokeza hususan katika umitindo na mbinu mseto.

Adegoju (2008), Yeibo na Akerele (2014) wanairejelea dhana ya grafolojia kwa kutaja vipengele kadhaa vya kigrafolojia vikiwemo rangi, fonti, orodha, miundo ya matini miongoni mwa vingine.

## 2.3 Dhana ya fasihi ya watoto

Junaid (2013) alifafanua fasihi ya watoto kama fasihi inayohusu watoto huku akitaja vijitanzu kama vile hadithi, ushairi, ngano, vina na drama kama malighafi katika fasihi ambayo hadhira yake ni watoto. Vilevile alishangaa jinsi ulimwengu bila vitabu vya watoto ungeweza kufanana. Kulingana naye, fasihi ya watoto ni dhana inayohusu vitabu ambavyo vimeandikwa vikiwalenga watoto wanaotambulika waziwazi kama hadhira. Wanaendelea kudokeza kuwa hiyo fasihi inahitaji kudhihirisha uhalisia kwa kuzua mijadala inayoonyesha utendakazi wa fasihi hiyo na katika hali hiyo, kunazuka nadharia ya fasihi ya watoto ambayo hupatanisha uzoevu na usomaji wa vitabu.

Hunt (1994) alionekana kupanua taaluma ya fasihi ya watoto kwa kuiongezea tanzu za riwaya, hadithi, barua, bayografia, historia, fasihi simulizi, michezo pamoja na nyimbo ambazo watoto hushiriki. Hii ni kusema ya kwamba fasihi ya watoto ina uwezo wa kufanyiwa utafiti kinadharia kama inavyofanyika katika tafiti zingine kitaaluma. Lynch-Brown na Tomlinson (1999) wanaendelea kusema ya kuwa thamana ya vitabu hivyo vya fasihi ya watoto inastahili kuwa ya juu ili vitabu hivyo viwavutie watoto wenye umri mdogo hadi umri ule wa kubalehe.

Wakizungumzia maudhui katika fasihi ya watoto, Hunt (1999), Lynch-Brown na Tomlinson (1999), Ang (2000), Weinreich na Bartlett (2000), Murray na Kirsten (2003), Mascarenhas (2015), Schneider (2016) wanasema ya kwamba ni vyema maudhui ya

fasihi ya watoto yarejelee matukio ambayo watoto hukumbana nayo katika ukuaji wao, matukio ambayo yanaweza kuwa mazuri au hata ya kutisha kama vile kung'olewa kwa jino la mtoto kwa mara ya kwanza, kushiriki tafrija za watoto, kushiriki michezo ya kuiga utu uzima miongoni mwa watoto, kupokea / kupokezwa kipenzi mnyama miongoni mwa watoto miongoni mwa maudhui mengine mengi.

Watalaam Hunt (1999), Lynch-Brown na Tomlinson (1999), Ang (2000), Weinreich na Bartlett (2000), Murray na Kirsten (2003), Mascarenhas (2015), Schneider (2016) wanasema kuwa fasihi ya watoto huwanufaisha watoto kwa njia mbili kuu ambako kuna manufaa ya kibinafsi na manufaa ya kiakademia. Miongoni mwa manufaa ya kibinafsi ni pamoja na kujifurahisha, kumfikirisha, kumpa tajriba ya kiulimwengu, kumwingiza katika utamaduni, kumpa maadili pamoja na kumpa ujitambulishaji mtoto kiujumi. Lynch-Brown na Tomlinson (w.h.t) wanasema kwamba manufaa ya kiakademia kutokana na usomaji wa vitabu hivyo ni pamoja na ukuzaji wa lugha, kwa hivyo mtoto hupata uwezo wa kujijengea umilisi lugha kutokana na uzoevu wake wa usomaji pamoja na kupokea fursa ya kukuza kipawa cha mtoto cha kuandika makala ya kuvutia na pia kukuza kile kipawa cha usomaji wa makala ya fasihi anapovisoma vitabu vya thamana ambavyo huchangia katika uelewaji wa taaluma zingine pamoja na kuridhika na matukio ya kiulimwengu.

Ngugi (2017) na Purbani (2018) wakichangia kuhusu dhima ya fasihi ya watoto, wanasema ya kwamba inatekeleza dhima ya kutimiza mahitaji ya mtoto kisaikolojia. Hii ni kusema kuwa fasihi ya watoto ina nafasi nzuri zaidi na pana ya kuendeleza elimu miongoni mwa wanajamii wenye misingi tofauti. Wanahoji kuwa inaweza kuwekewa msingi shuleni kwa kuwa, bila shaka watoto wanaishi katika jamii mseto, na njia nzuri ya

kukabiliana na hali hiyo ni kupitia kwa fasihi ya watoto. Kama inavyodhihirika kutokana na mawazo ya wataalamu kadhaa, fasihi ya watoto ina dhima kuu ya kuwapa watoto burudani, kuwapa elimu na pia kuwapokeza maadili mema ya kuwawezesha kuwa watu kamili na wa kutegemewa katika jamii. Ni kwa ajili hii ndiposa Angelidou (2013) anasema ya kwamba utanzu wa fasihi ya watoto ni mada pana inayojumuisha maudhui mengi ya watoto.

Hata hivyo, Angelidou (2013) pia anasema ya kuwa kuna wataalamu wengine ambao wanaiangazia fasihi ya watoto kama shughuli za kuwapa watoto burudani tu, na kwa hali hiyo kudai ya kwamba hakuna chochote kigeni cha kutafitiwa katika fasihi hii, huku wengine wakisema ya kwamba ni taaluma yenye umuhimu mkubwa kutokana na athari ambayo fasihi ya watoto huwa nayo kwa mtoto kitabia na kisaikolojia. Petzold (2012) anasema kuwa kutokana na athari mbaya ya fasihi ya watoto kwa watoto, mara kwa mara kunashuhudiwa hali ambapo baadhi ya vitabu vilivyochapishwa vinapigwa marufuku kwenye maktaba na hata shuleni na ni hali hii inayowapelekea watu wazima kuidhibiti fasihi ya watoto kwa kuandika makala yanayowalenga watoto na hata kuwanunulia watoto vitabu na makala mengine.

Licha ya maoni yaliyowasilishwa na wataalamu mbalimbali kuhusu fasihi ya watoto, utafiti huu uliegemea katika mawazo kwamba fasihi ya watoto ni taaluma muhimu ambayo inawalenga watoto ambao ndio wanajamii wengi, na kwa hali hiyo, ni fasihi inayohitaji kushughulikiwa kwa kina kwa lengo la kuipa jamii mwelekeo unaofaa.

### 2.3.1 Historia ya fasihi ya watoto

Fasihi ya watoto ni taaluma yenye historia ndefu. Ewers (1980) akirejelewa katika Nikolajeva (1995) aliitathmini fasihi ya watoto na akaibua awamu tatu ambazo

anazitumia katika kuelezea historia na maendeleo ya fasihi ya watoto. Kwanza anasema kuwa fasihi ya watoto tangu mwanzo ilihusiana kwa karibu mno na ufundishaji shuleni, na kwamba ni fasihi iliyoshuhudia umaarufu mkubwa wakati wa kipindi cha karne ya kumi na saba. Anaendelea kudokeza kuwa wakati wa enzi hizo, jamii iliweza kutambua kuwa umri wa kitoto ulikuwa awamu muhimu mno katika kipindi cha ukuaji wa watoto kwa kuwa watoto kama wanajamii wengine, vilevile walikuwa na mahitaji yao mahususi ambayo yalihitaji kutimizwa kwa ujumla.

Ewers (1980) katika Nikolajeva (1995) anaendelea kusema ya kwamba mawazo kuhusu mtoto na mahitaji yake yakiwemo yale ya kielimu yalichangia pakubwa katika kubadilika kwa mtazamo kuhusu fasihi ya watoto, hali iliyosababisha kuchapishwa kwa vitabu vilivyosemekana kuwa mwafaka kwa kusomwa na watoto. Ewers (k.h.t) anadokeza kuwa kufuatia kubadilika kwa mtazamo kuhusu watoto, fasihi ya watoto ilianza kutazamwa kwa kuangazia ubora wa vitabu ambavyo watoto walihitaji kusoma.

Kulingana naye, hali hii vilevile iliifanya fasihi ya watoto kuanza kuangaziwa kijamii. Mtazamo huo wa fasihi ya watoto kuangaziwa kijamii ulitumia kiunzi cha pembe tatu ambacho kilijumuisha mtoto-familia-shule, ambacho kwa mawazo yake kililenga kuielezea fasihi ya watoto kipragmatiki; kutumia fasihi ya watoto katika kuwanasibisha watoto katika jamii walimoishi, kwa kuwatangamanaisha katika jamii na pia kuwapa ujuzi mwafaka wa kuwawezesha kuwa na ukamilifu.

Mtazamo wa tatu ambao Ewers (1980) katika Nikolajeva (1995) anautumia ni ule unaoingazia fasihi ya watoto kama fasihi. Hii ina maana ya kwamba baada ya fasihi ya watoto kushuhudia mabadiliko mbalimbali, fasihi ya watoto ilihitaji kushughulikiwa kitaaluma kama zinavyoshughulikiwa fasihi zingine kama vile fasihi ya vijana na fasihi

ya watu wazima. Anasema kuwa mtazamo huo wa tatu ndio alioazimia watafiti wa baadaye katika taaluma ya fasihi kuushikilia.

Aidha, Murray na Kirsten (2003) wanasema kwamba fasihi ya watoto ni vitabu vilivyoandikwa kwa madhumuni ya kusomwa na kundi mahususi la watoto ingawa wanaoviandika na kuvinunua vitabu hivyo ni watu wazima. Katika mjadala wao, wanalijibu swali la awali la nani wanaowaandikia watoto fasihi, na inabainika wazi kuwa ni kazi zinazotungwa na watu wazima ambao vilevile ndio wenye uwezo wa kuvinunua vitabu hivyo ili visomwe na watoto.

Katika kuelezea hali ilivyo sasa katika taaluma ya fasihi ya watoto, Hunt (1991) anasema kwamba fasihi ya watoto inatofautiana na taaluma zingine zote kwa vile inaonekana kuwavutia na pia kumilikiwa sio tu na wasomi wala wandishi mahususi, bali ulimwengu mzima ambao unaonekana kuichangamkia. Kwa mujibu wa Hunt (k.h.t), fasihi ya watoto inaonekana kuwa na umaarufu na ufuasi mkubwa huku ikikosa kuwabagua wanajamii wasio na ujuzi (watoto) na ambao ndio wenye uwezo wa kuichangia na kuiendeleza.

Kulingana na Mohamed (2015), katika ulimwengu wa kisasa, fasihi ya watoto ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi katika ujifunzaji lugha, na dhima ya fasihi kielimu katika masimulizi ni tukio lisilohitaji ubishi wowote. Anahoji kwamba kupitia kwa fasihi ya watoto, mtoto huimarika kiisimu, kisaikolojia, kiutambuzi na kimahusiano kwa vile hutangamana na jamii inayomkuza, huku akiimarika kiakili kwa kutangamana na watoto wa mataifa mengine kupitia kwa usomaji wake wa kina wa fasihi mbalimbali zinazowalenga watoto katika mazingira tofauti.

Mpesha (1996) alitafiti kuhusu ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto nchini Tanzania. Aliangazia kipera cha masimulizi ya hadithi za watoto nchini Tanzania. Aliutambua

mchango mkubwa unaotekelezwa na fasihi ya watoto katika jamii wa kuendeleza utangamano na vilevile kuwafungulia watoto ulimwengu mpya kupitia kwa masimulizi. Kwa mujibu wake, fasihi ya watoto si tu kumbukumbu za matukio ya kijamii bali pia ni ala ya utangamano.

Kutokana na utafiti wa Mpesha (1996), ilibainika kuwa fasihi ya watoto kihistoria ni marejeleo ya hali halisi ya matukio yanayowahusu watoto katika jamii, na kwamba inaweza kuwa kipengele muhimu katika kuwahamasisha wanajamii kupitia kwa masimulizi. Traore (2010) na Bakize (2013) vilevile walitafitia fasihi ya watoto katika eneo la Afrika Mashariki. Utafiti wao ulijikita katika nchi ya Tanzania. Walichunguza hali ya fasihi ya watoto nchini Tanzania katika muktadha wa kuifafanua na kueleza changamoto zinazowakumba watunzi na mashirika ya uchapishaji vitabu ambayo huvichapisha vitabu kwa lugha za kiasili ikiwemo Kiswahili.

Traore (2010) alitambua mojawapo ya changamoto inayoyakumba mashirika ya uchapishaji kama vile utamaduni usiobadilika na maendeleo hafifu ya usomaji ambao ulihusishwa na hali duni ya elimu barani Afrika kwa jumla. Traore (k.h.t) alidokeza kwamba kutokana na hali duni ya elimu katika nchi ya Tanzania, watunzi wengi ambao waliendeleza kazi zao kwa lugha za kiasili walikosa fursa ya kuifikia hadhira pana ya kimataifa. Hii iliifanya fasihi ya watoto isalie nyuma kimaendeleo ikilinganishwa na fasihi zingine. Hali imesalia vivyo hivyo hadi miaka ya tisini kwa sababu kabla ya miaka hiyo, fasihi ya watoto ilichukuliwa tu kama shughuli ya watunzi nchini Tanzania ya kujishughulisha na kitu kisichokuwa na thamana.

Kulingana na Traore (2010), kabla ya miaka ya tisini, uchapishaji wa vitabu vya watoto halikuwa tukio la kuangaziwa kwa kina nchini Tanzania kwa vile ni shule chache

zilizokuwa na maktaba, maktaba hizo pia zilikuwa mbalimbali na pia shule nyingi hazikuweza kununua vitabu vya kiada na ziada. Maduka ya vitabu nayo hayakutembelewa na watoto wala wazazi. Hii ni kusema kwamba kabla ya miaka ya tisini, fasihi ya watoto nchini Tanzania ilishuhudia giza kubwa. Bakize (2013) alichangia kwa kusema kwamba hali ilikuwa hivyo kwa vile wanajamii wengi waliinasibisha fasihi ya watoto na mambo ya kitoto ambayo kwa maoni yao, ilikuwa fasihi rahisi kufahamika na isiyohitaji kutafitiwa kinadharia.

Fasihi ya watoto nchini Kenya ni taaluma ambayo imeshughulikiwa na watafiti watajika wakiwemo Musau na Ngugi (1997), Muthubi (2005), Kairu (2005), Oiyo (2006), Matundura (2007), Onyango (2007), Wamitila (2008), Ngugi (2009), Kabiru na Wanjiru (2014), Mbuthia na Mutahi (2017) miongoni mwa wengine wengi. Ngugi (k.h.t) alimnukuu Osazee (1991), ambaye aliiangazia fasihi ya watoto kama kazi ya kifasihi iliyoumbwa kutokana na malighafi kutoka kwa ulimwengu wa Kiafrika. Aliendelea kusema kuwa hii ni fasihi ambayo ilikuwa imeandikwa kwa lugha na mtindo ambao uliweza kufahamika na mtoto wa Kiafrika. Alidokeza kuwa fasihi ya watoto ni lazima ionekane kana kwamba inauendeleza utamaduni wa Kiafrika na kwamba, inamwezesha mtoto wa Kiafrika kujivunia mazingira yake zaidi na pia ni fasihi iliyo na uwezo wa kumpa furaha au burudani.

Ngugi (2009) alisema kwamba kuanzia mwaka wa elfu mbili (2000) kuendelea, kumeshuhudiwa msisimko mkubwa katika fasihi ya watoto nchini Kenya kwa kuwa watafiti mbalimbali wameibuka na kutoa michango yao kuhusu fasihi hii kupitia kwa kazi zao, hii ikidhihiriha ya kwamba fasihi ya watoto ni fasihi inayokua. Ngugi (k.h.t) akishirikiana na Musau (1997), walishughulikia historia ya fasihi ya watoto ya Kiswahili

nchini Kenya, na wanatueleza ya kwamba fasihi ya wato to ya Kiswahili nchini Kenya haina historia ndefu ikilinganishwa na historia ya fasihi ya watoto katika ulimwengu wa kwanza wa Kimagharibi.

Hata hivyo, licha ya jitihada ambazo zimebainika wazi kufanywa kuhusu fasihi ya watoto nchini na pia katika eneo la Afrika Mashariki, utafiti haujafanywa kuhusu mchango unaotekelezwa na vipengele vya kigrafolojia katika kuendeleza fasihi ya watoto ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuweka wazi vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika ujenzi wa kazi za kifasihi za Kiswahili zinazowalenga watoto na dhima na athari inayotekelezwa na vipengele hivyo.

### 2.4 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto

Cer (2016) katika tathmini yake ya ufaafu wa vitabu vya wasomaji wachanga anasema kuwa ni vyema ikiwa vitabu vya watoto vitawasisimua watoto kimaisha. Anahoji kuwa ni lazima vitabu hivyo viafiki uhalisia na ufaafu wa kisanaa kwa kuwa hii fasihi ya watoto ndiyo inayowaingiza watoto ulimwenguni na kuwatangamanisha watoto na ulimwengu na matukio yote yanayodhihirika katika ulimwengu huu. Anatubainishia sehemu tatu kuu za vitabu vya fasihi ya watoto ambazo ni usanifu, muktadha na fundisho. Kulingana naye, usanifu wa kitabu unahusu vipengele kama vile thamani ya karatasi, ujalidi, jalada, taipografia na fonti, picha na michoro miongoni mwa vipengele vingine. Kinachodhihirika katika mchango wake ni kwamba baadhi ya vipengele anavyovitaja katika sehemu ya usanifu ndivyo vipengele vya kigrafolojia vinavyojitokeza katika kiwango cha lugha.

Cer (2016) anafafanua muktadha wa kitabu katika fasihi ya watoto kama jumla ya wahusika, ploti, maudhui, lugha pamoja na usimulizi, sifa zinazostahili kuangazia ujumi na usambamba katika usukaji wa fasihi ya watoto. Sehemu ya tatu ya ya kitabu katika fasihi ya watoto kulingana na Cer (k.h.t) ni fundisho ambayo inahusu athari ya ujumbe uliobebwa katika kitabu unaomlenga msomaji. Ujumbe huu unaweza kuelekeza, kukuza maadili, kuchochea hisia mbalimbali pamoja na itikadi fulani. Ni dhahiri kwamba Cer (k.h.t) katika tathmini yake ameweza kuvibainisha baadhi ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo ndio nanga ya sehemu hii ya utafiti pamoja na vile vilivyotajwa na Eva (2015). Vipengele vinavyotajwa na wataalamu hawa vinahusika na kudhihirika moja kwa moja katika fasihi ya watoto vikiunganishwa na lugha ambayo ndio msimbo unaotumika katika ufasiri wa ujumbe uliobebwa na matini. Kiwango hiki cha lugha cha kigrafolojia kiliudhibiti utafiti huu moja kwa moja kwa kuwa utafiti ulidhamiria kubainisha na kuchunguza aina mbalimbali ya vipengele vya kigrafolojia, matumizi yake na athari inayoibuliwa na kuwepo kwa vipengele hivyo katika ufasiri wa maudhui katika riwaya ya Kiswahili.

Mawazo ya Cer (2016) yanayashadidi yale ya Mohr (2006) aliyedokeza kwamba sura ya vitabu pia inajumlisha anwani na idadi ya kurasa au urefu wa kitabu miongoni mwa vipengele vingine vinavyochangia pakubwa katika kuifanya fasihi ya watoto kuwa na mvuto au hata kuvifanya vitabu hivyo kuwachukiza wasomaji. Mohr (k.h.t) alivibainisha vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto. Hata hivyo amehoji kuwa siku hizi vitabu vya fasihi ya watoto vyenye michoro au picha vimekuwa na umaarufu kutokana na hatua kubwa za kiteknolojia ya kisasa, tukio ambalo limezua uchangamfu katika taaluma ya fasihi ya watoto.

Gallagher (2018) anamshadidia Mohr (2006) kwa kusema ya kwamba katika taaluma ya fasihi ya watoto, michoro na picha ni raslimali za kimsingi hivi kwamba, hata kuna uwezekano wa kukumbana na sura nzima ambayo imeangazia raslimali hizo tele. Vilevile anakitaja kipengele kingine kando na michoro au picha cha taipografia ambacho pia kilitajwa na Cer (2016) na Mohr (2006) katika fasihi ya watoto ambacho anasema kwamba vilevile ni cha kimsingi katika matini za kifasihi.

Mawazo ya Mohr (2006) na Gallagher (2018) yanaungwa mkono na Short (2018) anapochangia kuhusu kipengele cha michoro au picha katika fasihi ya watoto. Anasema ya kwamba hivi leo watoto wamezama katika utamaduni wa kutazama, ambako michoro au picha ni tukio la kimsingi maishani na katika utangamano wao. Kutokana na hali hii, Short (k.h.t) anadokeza kuwa umbo la fasihi ya watoto lazima liangazie vipengele vya ujenzi wa vitabu hivyo na pia anataja vipengele kama vile ukubwa wa kitabu, sura ya kitabu, jalada, taipografia miongoni mwa vipengele na jinsi ambavyo vinasukwa na vipengele vingine ambavyo huvipa vitabu vya fasihi ya watoto maana. Mchango wa Short (k.h.t) ni muhimu kwa vile unabainisha wazi wazi vipengele vya kigrafolojia vinavyotafitiwa.

Alabi na Adegoju (2017) na Bakuuro, Tuurosong na Pelpuo (2018) pia wamezungumzia grafolojia na vipengele vyake. Bakuuro na wenzake (w.h.t) kwa mfano wanaanza kwa kutazamia kwamba kuna viwango vinne vya uchanganuzi kimitindo ambavyo ni grafolojia, fonolojia, mofolojia na leksikosintaksia. Katika shairi la *The Hollow Men*, wanavitaja vipengele vya mkolezo, nafasi katika mistari, uradidi na viakifishi kama mifano inayobainika katika utanzu huo ambavyo wanasema ni vipengele vya kigrafolojia.

Hata hivyo Alabi na Adegoju (2017) wanaongezea katika orodha ya vipengele vya kigrafolojia kwa kutaja matumizi ya herufi kubwa, matumizi ya mandishi yenye mlazo, matumizi ya mandishi yenye rangi tofauti na ya usimulizi, mtindo wa michoro au picha, aina na ukubwa wa fonti zilizotumika au taipografia, muundo wa aya, ukubwa wa matini, umbo la matini (sura), upigaji mstari chini ya maneno, ukawaida wa mandishi, matumizi ya herufi ndogo, udondoshaji wa maneno, matumizi ya kigothi, matumizi ya akronimu au vifupisho, muhtasari kuja chini, upembe wa mandishi, mgawanyo wa ukurasa na tahajia au taipografia.

Alabi na Adegoju (2017) wametuainishia vipengele vingi vya kigrafolojia ambavyo hutafitiwa katika umitindo kifasihi. Hata hivyo, kama anavyoeleza Anantha (2014), matumizi ya vipengele hivi pamoja na kutokea kwa hiari kwa makosa ya kiothografia katika matini hudhihirisha matumizi au hutambulisha kuwepo kwa grafolojia katika matini kutegemea uwezo wa ufundi na ujuzi wa mwandishi wa kazi ya kifasihi. Ingawa vingi vya vipengele hivi ni vya kiisimu, vilevile vinadhihirika katika fasihi mbalimbali ikiwemo fasihi ya watoto.

Vipengele vya kimitindo ambavyo vimetajwa na Alabi na mwenzake katika Adeniyi (2017) kama vinavyotafitiwa kigrafolojia ndizo elementi za kigrafolojia ambazo utafiti huu umelenga kubainisha katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Hata ingawa Alabi na mwenzake wamesema kwamba vipengele hivyo hujitokeza kifasihi, wameibua mtazamo wa kijumla kwa kuwa kuna aina mbalimbali za fasihi zinazowalenga wanajamii tofauti tofauti. Utafiti huu umeangazia kujitokeza kwa elementi hizo katika fasihi ya watoto ya Kiswahili katika utanzu wa riwaya mahususi.

## 2.5 Dhima ya grafolojia katika fasihi

Grafolojia na vipengele vyake hutekeleza dhima mbalimbali katika matini ya kifasihi. Kulingana na Ufot (2017), umitindo kimsingi ni uchanganuzi wa lugha kimatini. Hata hivyo, ili kuweza kufahamu uchanganuzi huo, mbinu mbalimbali za nadharia kiisimu zinahitajika ili kumwezesha msomaji kuibua maana na pia kumuathiri jinsi anavyojinasibisha na kazi hiyo kimatini. Kwa hivyo uelekevu wa kimitindo ni sifa bainifu inayozingatiwa katika uchanganuzi wa lugha katika taaluma mbalimbali. Anasema ya kwamba grafolojia hutekeleza dhima mbalimbali katika taaluma kadhaa ikiwemo fasihi andishi. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na:

### 2.5.1 Rangi

Mojawapo kati ya vipengele vya grafolojia vinavyotekeleza dhima muhimu katika fasihi ni rangi. Wataalamu Cer (1967), Kluck (1972), Pierson (2008), Yu (2014), Anantha (2014), Olurinola na Tayo (2015) na wengine walifanya utafiti kuhusu rangi kama kipengele mojawapo cha grafolojia katika muktadha wa fasihi ya watoto. Cer (k.h.t) alisema ya kwamba miongoni mwa rangi zote za ulimwenguni, ni rangi nyekundu iliyo na mnato wa juu mno kwa mtoto ikilinganishwa na rangi zingine zote. Utafiti wa Kluck (k.h.t) vilevile ulibaini ya kwamba rangi mbalimbali zinazotumika katika matini huwa na mchango mkubwa kwa wasomaji wa matini hizo. Katika ujumla wake, anahoji ya kuwa kuna rangi za kuchukiza na rangi za kusisimua na kwamba, rangi thabiti na za kusisimua katika fasihi ya watoto ni bora kwa kuwa huwa zinawavutia wasomaji wachanga kuliko zile rangi hafifu na zilizokwajuka, zinazowachukiza wasomaji hao wachanga.

Hata hivyo, Kluck (1972) haelezi kwa kina kile anachomaanisha anapozitaja rangi thabiti na rangi zingine za kuchukiza. Hii ni kusema ya kwamba ingekuwa vyema kama angeweka bayana rangi zinazosisimua na pia zile ambazo ni za kuchukiza. Lakini linalojitokeza ni kwamba rangi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia hutekeleza dhima ya kiujumi inapowavutia wasomaji wa kiwango cha chini kwa kuwachochea kuisoma matini zenye mvuto. Pierson (2008) vilevile alibashiri ya kwamba rangi huimarisha neno na kwamba tafiti nyingi zinadhihirisha ya kuwa msomaji wa matini atavutiwa na rangi kabla ya kuisoma matini na kuifasiri kama alivyolenga mwandishi.

Yu (2014) akitoa mchango wake kuhusu kipengele cha rangi katika uandishi, anasema ya kwamba rangi ndio msingi wa ishara za kutazamwa na hutekeleza dhima mahususi ya kuendeleza mawasiliano. Anahoji kuwa katika ustaarabu wa kirasimi, rangi ilikuwa kipengele cha kimsingi katika maisha yote na kwamba, ilihusishwa kwa karibu mno na hali za kiakili na mihemuko. Kulingana naye, nyingi za ishara za rangi zilitokana na uasili. Anasema kuwa rangi ya manjano iliashiria nguvu za maeneo yenye uhai, rutuba na mvua, isipokuwa katika dini ya Kiislam, ambapo rangi ya manjano iliashiria utukufu, huku ile ya samawati ikiashiria mbingu, nafsi na ukweli, ilhali rangi nyeusi iliashiria pande mbili huku nyeupe ikiashiria kinyume cha weusi. Hata hivyo, anasema kuwa katika tamaduni zingine, weusi ulikuwa ishara ya maafa ingawa hata kwa wengine, weupe uliashiria maafa.

Yu (2014) anaendelea kusema ya kwamba rangi nyekundu iliasharia damu ambayo ilihusishwa na uhai ingawa katika ulimwengu mwingine, wekundu uliashiria kifo. Yu (k.h.t) anadokeza kuwa, rangi katika ulimwengu wa binadamu hutekeleza dhima ya kiujumi na vilevile humpa binadamu kariha na kuchachawisha upendo wa wanafunzi ili

kuimarisha hamu yao kimaisha. Kwa hali hii, rangi hutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano kisaikolojia. Kwa mujibu wake, rangi pia inaweza kuashiria maana katika kiwango kingine akilini mwa msomaji. Hiki ni kiwango cha ishara ambacho misingi yake ni utamaduni, historia, dini, siasa na hata mahusiano ya kiisimu.

Utafiti wa Olurinola na Tayo (2015) ulihusu athari za rangi katika uhifadhi wa yaliyosomwa au kumbukumbu miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu. Uliangazia umakini, ustawishaji na utendakazi wa fahiwa. Matokeo ya utafiti huo yalibaini ya kwamba mchakato wa kuyakumbuka yaliyosomwa awali ulitegemea vipengele vingi vikiwemo kile kipengele cha rangi. Hii ni kusema ya kwamba rangi ina dhima muhimu ya kuimarisha kumbukumbu za msomaji wa matini ikiwa imeshirikishwa katika matini na pia kutekeleza dhima ya kiujumi katika fasihi.

### 2.5.2 Herufi kubwa

Treiman na Kessler (2004) walifanya utafiti kuhusu uwezo wa watoto wa kubainisha herufi kubwa na ndogo katika matini. Walichunguza mfumo wa matumizi ya herufi kubwa unaotumiwa na wasomaji wachanga walio katika shule ya chekechea hadi gredi ya kwanza (1) kuhusu maneno ambayo hayakukuwa na herufi kubwa katika tahajia ya watoto ya uandishi wa kawaida. Utafiti wao ulibainisha kuwa watoto wa umri mdogo walikuwa na uzoevu wa kubahatisha na kuandika kwa herufi kubwa huku herufi kubwa zikidhihirika mwanzoni mwa maneno mengi ambayo waliandika. Vilevile walitambua ya kwamba uzoevu wa kutumia herufi kubwa visivyo katika maandishi ya wasomaji wachanga ulitokana na kuwepo kwa herufi hiyo katika jina la kwanza la msomaji huyo mchanga.

Aidha, Soile (2008) anahoji kuwa uzoevu wa matumizi ya herufi kubwa hubadilika kutegemea aina ya lugha. Kulingana naye, wakati wa kipindi kati ya karne ya kumi na saba (17) na kumi na nane (18), lilikuwa jambo la kawaida kwa nomino zote kuanza kwa herufi kubwa katika lugha ya Kiingereza. Chukwu (2010) ameweka wazi kaida za kuzingatiwa katika matumizi ya herufi kubwa. Hata hivyo kaida hizo ni za kiisimu na zinasisitiza ya kwamba herufi kubwa itumike kutanguliza sentensi. Pia anahoji kwamba herufi kubwa vilevile itumike mwanzoni mwa maneno yanayotaja nomino za pekee kama vile Dani, Songambele, Aliya miongoni mwa zingine.

Kulingana na Chukwu (2010), usemi halisi katika dondoo pia huanza kwa herufi kubwa pamoja na majina ya vitabu au makala, dini na madhehebu na pia utangulizi wa salamu katika anwani. Kulingana na Chukwu (k.h.t), majina yanayorejea maeneo kama vile Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini yanahitaji kuanza kwa herufi kubwa kama vile yameendelezwa hapa, pamoja na lahaja za lugha kama vile Kichichifundi, Kianzwani miongoni mwa lahaja nyingine katika Kiswahili.

Hata hivyo, kaida za matumizi ya herufi kubwa zinaweza kuzingatiwa na vilevile zinaweza kukiukwa kutegemea aina ya utafiti kama wanavyoeleza Kazungu (1982), Jinemez (2017) na wengine. Ingawa wataalamu mbalimbali wakiwemo Chukwu (2010) husisitiza ya kwamba herufi kubwa zitumike kwa kuzingatia kanuni za kiisimu, utafiti huu haukuwa wa kiisimu ndiposa kumetokea matumizi ya herufi kubwa yasiyo ya kawaida. Ni kutokana na matumizi ya herufi kubwa visivyo ndiposa Wamitila (2008) aliujadili mhimili wa nadharia ya umitindo wa uteuzi katika fasihi. Alihoji kuwa mwandishi wa kazi ya kifasihi anaweza kuiendeleza kazi yake kwa kukiuka kaida za kisarufi kwa sababu kadha ili kutekeleza dhima fulani, hali ambayo huwa na athari fulani

kwa msomaji. Kutokana na maoni haya, ni bayana kwamba herufi kubwa hutumika kawaida na pia visivyo kutekeleza dhima ya kukifanya kifungu ambamo zimetumika kutokezea zaidi ya vifungu vingine, ambayo ni dhima ya kuchimuza na pia inaweza kutumika katika matini na lengo la kuweka msisitizo.

Anantha (2014) alitumia mfano huu kudhihirisha jinsi mkengeuko wa kigrafolojia unavyojitokeza katika utangazaji katika stesheni. Mfano huu unatumika kwa mawazo kwamba katika kituo cha shirika la habari, ujumbe unakuwa na mvuto iwapo umezingatia ubunifu kifasihi.

Mfano wake unatoka kwenye stesheni ya CNN (Chi & Hao, 2013):

(1) Comfort, Desig*n*, Fu*n*ction. (CNN, Time, Sep 20th)

(2) For peace of mind, stay *connected*. (CNN, Time, Sep 6th)

(3) Every perspe-tive, dime- sion, a-gle. (CNN, Time, Sep 6th)

Amesema kuwa katika utangazaji wa kawaida, herufi zilizolazwa katika mifano miwili ya kwanza huendelezwa kwa rangi nyekundu kama ilivyo ilhali ule mfano wa tatu hutumia kistariungio kudondoa herufi fulani katika maneno. Anadokeza kwamba lengo la kufanya hivyo ni kuvuta makini ya wasomaji, na hivyo basi kuchimuza CNN.

Kazungu (1982), Ouameur (2013) na Jinemez (2017) wameshughulikia mkengeuko katika fasihi. Kazungu (k.h.t) alitumia mfano huu ambamo anaonyesha kujitokeza kwa vipengele kadhaa vya grafolojia katika utanzu wa ushairi katika ubeti unaofuatia hapo chini:.

"...Hakuna: tu anaweza kushindana
na 'wakati• WAKATI UKUTA, UKIPIGANA
NAO UTAUMIA MWENYEWE. Tutagorabana
na watoto wetu bure".

Ubeti huu umenukuliwa kutoka kwa mojawapo ya mashairi aliyoyatafitia. Kazungu (1982) anaeleza kuwa ubeti huu unadhihirisha matumizi mapana ya vipengele vya kigrafolojia. Kwanza kuna viakifishi, kisha herufi kubwa, muundo wa sentensi na sura ya ubeti kama ulivyowasilishwa. Anasema kwamba umbo la ubeti huu linaashiria mchepuko katika uendelezaji wa maneno. Herufi kubwa zimetumika visivyo kuendeleza maneno katikati mwa sentensi na hivyo kukiuka kaida za kiisimu. Sura iliyoibuliwa na mfano wa ubeti aliourejelea Kazungu (k.h.t) pamoja na viakifishi inadhihirisha mkengeuko fulani.

Jimemez (2017) vilevile ameshughulikia mchepuko wa kifasihi katika ushairi. Katika makala *Foregrounding effects of the unconventional capitalization in the experimental poetry of E. E. Cummings*, Jimenez (k.h.t) ameangazia matumizi yasiyo ya kawaida ya herufi kubwa katika mashairi tisini na sita (96) ya majaribio ya Cummings. Katika uchanganuzi wa mashairi hayo, amebaini ya kwamba herufi kubwa zimetumika visivyo mwanzoni mwa neno, katikati mwa neno na hata tamatini mwa neno, hali ambayo si ya kawaida. Anasema kwamba matumizi ya herufi kubwa visivyo katika utanzu wa ushairi huwa yanalenga kutekeleza dhima ya kusisitiza vipengele fulani, kuleta athari ya udenguzu, kuzalisha maana nyingine ya maneno kisarufi pamoja na kuanzisha matukio ya rabsha katika mfano huo.

Jimenez (2017) vilevile anasema kwamba kwa kiwango kidogo, matumizi yasiyo ya kawaida ya herufi kubwa huchangia katika kuibua maana mpya ya maneno na hata shairi zima huku toni ikibainika. Hapa, inabainika kuwa jinsi vipashio hivi vya kigrafolojia vilivyotumika katika ushairi, dhima yavyo ni kuweka msisitizo, kuendeleza udenguzi, kuzalisha maana nyingine ya maneno kisarufi. Ingawa Kazungu (1982) na Jimenez (2017) walizungumzia mchepuko, utafiti wao uliegemea katika utanzu wa fasihi wa

ushairi. Ouameur (2013) alitafitia mchepuko wa kigrafolojia katika riwaya ya *Hard Times* (1995). Mchepuko huo ulidhihirisha matumizi ya herufi kubwa katikati mwa sentensi katika matini kama ilivyo hapa katika mfano huu;

> Now <u>What I Want</u> is <u>Facts</u>. Teach these boys
>
> and girls nothing but <u>Facts</u>*".(Book 1, Chap. I, p.3)*

Katika mfano huu, Ouameur (2013) anadokeza kwamba matumizi ya herufi kubwa katika maneno yaliyopigwa mstari kwenye kifungu hiki ni ukiukaji wa ukawaida. Kama wanavyoshikilia hawa watalaam, vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika katika vifungu hivi vina dhima kuu ya kuchimuza vifungu hivyo. Ni kwa msingi huu ndiposa Yeibo na mwenzake (2014) wanahoji kwamba uibuaji wa maana katika kazi yoyote ya fasihi kimatini bila kurejelea ufasiri wa violezo vya kigrafolojia huwa haujakamilika. Wanakubaliana ya kwamba mchepuko hujitokeza sana katika matini yenye matangazo ambapo makosa ya tahajia kwa kukusudia, matumizi ya fonti tofauti miongoni mwa vipengele vingine vya kigrafolojia hukithiri.

### 2.5.3 Picha na michoro

Cer (2016) anasema kuwa kuna watafiti wanaoshikilia mawazo kwamba fasihi ya watoto haikamiliki bila ya picha au michoro ambayo pia ni vipengele vya kigrafolojia. Watafiti hawa ni pamoja na Cianciolo (1970), Nodelman (1988), Kiefer (1993), Fang (1996), Leddy (2002), Nikolajeva (2005), Sever (2008) na Marantz na Marantz (2013) pamoja na wengine. Katika kujadili ufaafu wa fasihi ya watoto, wamebainisha ya kwamba picha ni kipengele muhimu katika fasihi ya watoto na ni lazima kidhihirike katika kazi hiyo.

Wataalamu hawa hata hivyo wanasema kuwa ni muhimu kuangazia jinsi matini na picha zinavyopangwa na kujitokeza katika kitabu. Wanasema ya kwamba ikiwa picha na matini

zimepangwa vyema katika hali ambayo Elster na Simons (1985) waliita hali ya utegemezi–picha, ambapo maelezo katika matini yanategemea picha au picha vilevile kutegemea maelezo moja kwa moja, utangamano huo utamwathiri msomaji vyema na hivyo basi kuimarisha ufasiri wake wa ujumbe uliolengwa na mwandishi.

Vilevile kuna watafiti wengine walio na mawazo kuwa picha katika matini ya fasihi ya watoto huathiri wasomaji visivyo, athari ambayo pia hudhihirika katika mwitikio wao wa ujumbe katika matini. Wale walio na mawazo haya wanasema ya kwamba picha si kipengele mwafaka katika fasihi ya watoto. Kundi hili linawajumulisha akina MacCann na Richard (1973), Peeck (1974), Beck (1984), Marshall (1988), Goodman (2009) na wengine. Peeck (k.h.t) kwa mfano alishikilia ya kwamba ufahamu wa hadithi huimarishwa na picha ikiwa picha hizo zinakubaliana na ujumbe ulio katika matini kwa vile ikiwa picha zitabeba dhana tofauti na matini, bila shaka zitawakanganya wasomaji wachanga.

Beck (1984) alibainisha aina mbili za umitindo katika picha; picha dhahania na picha zilizochanganuliwa na akasema kwamba picha hizi zote zina uwezo wa kuathiri ufahamu wa msomaji. Kwa mujibu wake, aina mbili hizi za picha huchochea hamu ya usomaji na vilevile hupunguza mchakato wa ufahamu. Ingawa kuna uhuru wa kuibua mawazo ya aina hii, ni vyema madai haya kuimarishwa na ushahidi wa kitafiti kinadharia. Ni kwa hali hii ndiposa Aggleton (2017) anasema kwamba wanaopinga ujumuishwaji wa picha katika fasihi ya watoto wanafanya hivyo bila ushahidi wowote wa kinadharia, na anasema kuwa hayo ni makisio tu ambayo hayana ushahidi wowote kiutafiti.

Ruthiiri (2012) akitoa mchango wake kuhusu dhima ya kipengele cha picha katika matini ya fasihi ya watoto anasema ya kwamba picha huleta mvuto kwa fasihi ya watoto.

Anahoji kuwa picha na mandishi makubwa huwa muhimu kwa kiwango fulani cha watoto kwa kuwa ndio njia ya kuendeleza uhalisia. Watoto wanapoona vitu walivyozoea kuviona katika mazingira yao, wao huweza kuafikiana na hadithi hiyo. Kwa maoni yake, picha na maandishi makubwa hutekeleza dhima ya kuleta mvuto ambayo ni dhima ya kiujumi na pia dhima ya kuimarisha uhalisia kati ya msomaji na matini.

Ruthiiri (2012) anaendelea kutueleza kuwa vilevile matumizi ya picha huwa muhimu hasa kwa watoto ambao uelewa wao wa mambo ni wa kiwango cha chini. Anamrejelea Allen (1989), anayehoji kwamba picha zinaweza kuonyesha vitu muhimu ambavyo havikuwa vimetambulika na kueleweka hapo awali katika usomaji wa hadithi. Vilevile hii ni dhima ya uhalisia kwa kuwa kupitia kwa picha, taswira fulani humjia msomaji ambaye huifasiri taswira hiyo na hali halisi katika maisha.

Kulingana na mawazo ya wataalamu walioangaziwa, picha au michoro ni vipengele vya kimsingi katika fasihi ya watoto inayotekeleza dhima ya kiujumi kutokana na mvuto, dhima kuendeleza uhalisia kwa kuwa msomaji anaitazama picha hiyo na kuiweka katika hali halisi, picha hutekeleza dhima ya kutoa muhtasari wa matini, picha hutekeleza dhima ya kuimarisha ufasiri wa ujumbe katika matini. Adam (2019) anahoji kwamba kuna ushahidi unaodhihirisha ya kwamba wasomaji wachanga wanapenda na pia huchangamkia vitabu au matini vyenye picha katika fasihi yao kuliko matini isiyo na rasilimali hizi. Picha katika matini zilizochunguzwa vilevile zimeshughulikiwa kwa wino au rangi tofauti zinazong’aa.

Picha hizo zinawakilisha mwangwi wa wahusika na matendo ambayo yamerejelewa katika maudhui. Wahusika ambao wamewakilishwa na michoro hiyo ni binadamu na wanyama. Miongoni mwa wanyama, mbinu ya kimitindo ya uhuishaji imetawala

kutokana na jinsi wanyama hao wanavyoyaendeleza matendo yao. Kwa ujumla, imebainika ya kwamba dhima ya picha katika matini ya kifasihi ni kuendeleza uhalisia, dhima ya kiujumi pamoja na kuimarisha kumbukumbu ya msomaji.

### 2.5.4 Viakifishi

Shaw (1986), Grindlay (2002), Tunicak (2003) na Opara (2013) walifanya utafiti kuhusu kipengele cha kigrafolojia cha viakifishi katika matini. Kulingana na Grindlay (k.h.t), viakifishi ni miongoni mwa elementi za kimsingi katika miundo ya lugha andishi ambavyo lazima vidhihirike katika matini. Tunicak (k.h.t) akirejelewa katika Radita (2017) anaviainisha viakifishi takriban kumi na vinane (18) ambavyo anasema kuwa, vinatumika mara kwa mara katika uandishi, miongoni mwa viakifishi vikiwemo vikomo, viulizi, alama hisi, kistariungio, kistari, mabano, koloni, semi koloni, ving'ong'o, vinyota miongoni mwa vingine ambavyo hutekeleza dhima mahususi ya kuibua maana katika matini ikiwemo ile ya kifasihi. Wanasema ya kwamba kwa mfano, ikiwa alama ya kiulizi itapachikwa mwishoni mwa sentensi, na alama hiyo isipachikwe mwishoni mwa sentensi nyingine, bila shaka sentensi moja itakuwa swali na nyingine itakuwa taarifa tu, na hivyo basi kuchochea mwitikio tofauti miongoni mwa msomaji.

Opara (2013) alitafitia viakifishi na akabaini kwamba, alama za viakifishi huimarisha mwendo wa baadhi ya usemi kifasihi ili kufunua maoni mazito ya mwandishi kwa ujumla. Alikirejelea kipengele cha mlazo, alidokeza kwamba alama hiyo huashiria mabadiliko katika mifumo ya usemi, na pia huweka msisitizo katika maudhui. Maoni yake yaliungwa mkono na Emmott na Marc (2014). Katika kuhakiki *Hallowen Party* (1972), wao walidokeza ya kwamba mlazo katika utanzu huo ulitumika kuweka msisitizo katika matini.

Wataalamu wafuatao; Alexandra, Porter, Howison, Bazzi na Darmon (2020) pia wanatoa maoni yao kuhusu dhima ya viakifishi wanaposema kwamba kwa vyovyote vile, katika usomaji, wasomaji hutambua sahihi kimitindo sio tu kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa na sarufi bali pia jinsi viakifishi vilivyotumiwa. Hii ni kwa sababu mwandamano wa viakifishi kutokana na wandishi mbalimbali huzalisha mwandamano wa kuvutia. Wanasema kwamba viakifishi ni vipengele vya kimsingi kimitindo katika uchanganuzi matini. Maoni yao yanayashadidia mawazo ya Shaw (1986) aliyedokeza kwamba viakifishi ni njia mojawapo ambayo maana katika matini hudhibitishwa kupitia kwa alama fulani. Kulingana na mchango wa wataalamu hawa, dhima ya viakifishi katika matini na hususan matini ya kifasihi ni kuibua maana na vilevile kuweka msisitizo katika baadhi ya vipengele vilivyotumiwa katika matini.

### 2.5.5 Taipografia

Kluck (1972), Fordonski (1996), Hunt (1999), Katzir, Hershko na Halamish (2013), Hojjati na Muniandy (2014) Fetić na Azizović (2014), Gallagher (2018) na Dressler (2019) wamefanya utafiti kuhusu taipografia. Kluck (k.h.t) katika utafiti wake alipendekeza kwamba maneno yanayotumika katika uandishi wa fasihi ya watoto yawe makubwa na yaliyoandikwa kwa nafasi inayoofaa ili yaweze kuyavutia macho ya msomaji mchanga.

Akizungumzia dhima inayotekelezwa na taipografia kama mojawapo ya kipengele cha kigrafolojia katika fasihi ya watoto, Hunt (1996) alisema kwamba taipografia katika fasihi ya watoto inapaswa kuwa kubwa kutegemea kiwango cha watoto. Alidokeza kuwa herufi ndogo ndogo mara nyingi haziwavutii watoto hasa wanapolazimika kukaza macho wanaposoma. Hunt (k.h.t) ni miongoni wa waasisi wa fasihi ya watoto na

anapozungumzia taipografia, utafiti huu vilevile unaathirika kwa vile pia umeangazia fonti katika matini ya fasihi ya watoto. Bila shaka, wasomaji wachanga huathirika na mandishi madogo, tajriba ambayo huenda ikawa na athari mbaya kwao.

Hojjati na mwenzake (2014) wanasema kwamba fonti ya *Times New Roman* inasomeka vyema, hivyo basi ina umaarufu katika uchapishaji wa vitabu na matini nyingi kwa ujumla ilhali ile ya *Futura Md BT 24* ni mwafaka kwa wasomaji chipukizi au wachanga ambao hawana tajriba ya usomaji. Fetić na Azizović (2014) wameshughulikia taipografia kama taaluma mahususi ya grafolojia na uamilifu wake kiujumi. Wanahoji kwamba awali, matini ilikuwa njia ya kuwasilisha ujumbe lakini kuibuka kwa ubunifu kitaipografia na ongezeko la matumizi yake, matini hivi leo yanakuwa njia ya uwasilishaji ujumbe kikamilifu. Gallagher (2018) na Dressler (2019) wanasema ya kwamba ingawa thamana ya fonti haizingatiwi sana katika mifumo ya kiakademia, inatekeleza dhima muhimu katika ukuzaji wa usomaji vyema na elimu.

Gallagher (2018) na Dressler (2019) wanaendelea kuhoji kuwa taipografia ina mchango mkubwa katika uzalishaji wa maneno. Wanaendelea kuhoji kuwa uzalishaji wa maneno wa kisasa ni matukio ya kitaipografia yanayozuka kila wakati matini inapozalishwa ingawa wandishi na wasomaji wengi huwa hawazingatii mchango na dhima ya taipografia katika utambulishaji wa matini kiujumi na pia kimaana. Wanasema kwamba taipografia ni kipengele cha kigrafolojia ambacho kando na kuimarisha matini kiujumi, vilevile kina dhima kuu katika uzalishaji wa maana katika matini. Hii ni kwa sababu taipografia hushughulikia jinsi mifumo ya herufi hutumika; jinsi herufi zinavyopangika kimtazamo licha ya hali inayozunguka uzalishaji wa herufi hizo. Mpangilio huo

humfanya mwanataipografia kuonekana kana kwamba ni mtaalamu anayezalisha maana tofauti katika matini ili msomaji naye aweze kuifasiri matini kwa njia inayotakikana.

Yadav, Chakrabarti na Bisoyi (2017) wamezungumzia aina kuu za fonti na ukubwa na udogo wa fonti katika uandishi wa matini. Kwao, mandishi ya fonti ambazo ni ndogo zaidi ya pointi kumi (fonti10) si bora katika uchapishaji. Hii inatuelekeza katika kujiuliza swali, je, uamuzi wa kutumia aina fulani ya fonti katika uandishi ni wa nani? Gutjahr na Benton (2001) wakirejelewa katika Gallagher (2018) wanaonekana kushiriki katika mdahalo huu kwa kuazimia kuchangia katika kulijibu swali hili wanapodokeza kuwa yale yote ambayo yamo katika kitabu, na mfumo wa kitabu si zalisho la mtu mmoja kwa sababu katika ulimwengu wa uchapishaji, wandishi hawaandiki vitabu bali huandika matini. Kwa mujibu wao, kitabu huzalishwa wakati matini hugeuzwa kwa kuchapishwa, wakati kinapopokea sura mpya kifasihi, sura ya kukiwezesha kitabu hicho kutambulika na kukubalika kwa wasomaji wengine.

Gutjahr na Benton (2001) wanazungumzia taipografia katika fasihi ya watoto. Kwa mujibu wao, kipengele hiki kina ukuruba na fonti kwa vile kinahusu udogo na ukubwa wa mandishi katika matini. Hata hivyo, ni vyema ifahamike kwamba utafiti huu umezichunguza riwaya teule kwa ukamilifu bila kujikita kwa mchakato unaohusu shughuli za uchapishaji na michango mbalimbali ya washikadau tofauti tofauti katika usukaji wa riwaya. Kwa hivyo inabainika kwamba taipografia na fonti hutekeleza dhima ya uzalishaiji maana na pia dhima ya kiujumi katika matini.

### 2.5.6 Nafasi katika mistari na maneno

Watafiti Madhavan, Kaur, Hairol na Mohammed (2016) walifanya utafiti kuhusu nafasi kati ya maneno katika usomaji miongoni mwa wasomaji wachanga wa umri kati ya miaka saba (7) na tisa (9) wasio na uwezo wa kusoma vizuri. Utafiti wao uliweza kubaini ya kwamba usomaji miongoni mwa wasomaji hao wachanga uliweza kuimarika wakati nafasi kati ya mistari hiyo ulivyoongezeka. Kulingana nao, usomaji ni tukio linaloathiriwa na utambuzi, na kwamba wasomaji wenye changamoto za usomaji wema hudhihirisha utambuaji na usomaji mwema ikiwa nafasi pana kati ya maneno katika mistari utaongezeka. Hii ni kusema ya kwamba nafasi kati ya mistari na maneno ina dhima muhimu ya kuimarisha usomaji wa matini.

### 2.5.7 Aya

Watafiti Wali na Madani (2020) wametafitia kipengele cha aya katika uandishi. Katika utafiti wao pia wameweza kubainisha aina tatu za aya ambazo ni aya ya masimulizi, aya ya maelezo na aya ya ufafanuzi. Aya ya masimulizi ni ile ambayo hutoa maelezo ya kijadi huku tukio la kwanza likitanguliza na hutumia lugha sahili. Ile aya ya maelezo hutoa maelezo ambayo msomaji hupokea taswira au picha fulani akilini mwake ilhali ile ya ufafanuzi hutoa maelezo yanayoandamana na mifano. Wanasema kwamba aya lazima zidhihirike katika mandishi yoyote kuashiria kuwepo kwa mshikamano na muwala miongoni mwa vipashio vya lugha. Dhima kuu ya aya katika utungo wowote uwe wa kiisimu na hata wa kifasihi ni kuendeleza mawasiliano kwa kuwa aya hudhihirisha mshikamano na muwala miongoni mwa maneno.

### 2.5.8 Vipengele vingine

Aidha, Hunt (1999) alishughulikia vipengele vingi vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto. Akizungumzia karatasi inayotumiwa kuendeleza kazi ya fasihi ya watoto, alisema ya kwamba vilevile inahitaji kuwa ngumu ili isiraruke kwa urahisi. Kipengele kingine cha kigrafolojia ambacho ni cha kimsingi katika fasihi ya watoto ni urefu wa hadithi. Hunt (k.h.t) anasema aghalabu, watoto huvutiwa na vitabu ambavyo watavisoma na kukamilisha katika kikao kimoja bila kukatisha usomaji wao. Hivyo basi, mwandishi anahitaji kutambua awali uwezo wa kuweka makini miongoni mwa watoto mbalimbali.

Adeniyi (2017) ametoa mchango wake wa dhima inayotekelezwa na kipengele cha umbo katika utanzu wa ushairi wa Brathwaite wa *Elegguas.* Katika ushairi huo, anaanza kwa kuchanganua mtandazo wake. Anatueleza ya kwamba kimuundo, ushairi huo umezungukwa na laini nyembamba za wima upande wa kushoto, na laini mbili nyembamba upande wa kulia. Kwa mujibu wake, huu ni udenguzi wa ushairi kimuundo kwa kuwa muundo, huo unaleta dhana ya kuwekewa ukuta, kuashiria kuwa hisia za mshairi zimedhibitiwa na nguvu zinazomshinda mshairi. Kimaudhui, ni ushairi wenye huzuni kwa vile uliandikwa ukiwalenga walioaga, ambao kisemantiki, matumizi ya laini hizo za wima ni ishara ya mipaka ya huzuni na masikitiko katika nafsi ya mshairi.

Kulingana na Adeniyi (2017), laini hizi ndizo zinazoashiria mipaka. Matumizi ya mipaka kuufunga ushairi huu hutoa ujumbe kuwa mshairi anaweka mipaka kati ya mauti na uhai, uhalisia na njozi. Kutokana na mchango wake, vipengele hivi vinatumika kuwasilisha ujumbe wa mvunjiko kifasihi.Katika ushairi huo, pia kuna matumizi ya vikomo

visivyofuata kanuni. Anasema kuwa kando na matumizi ya laini zilizo wima, viakifishi, makosa ya hijai, vistariungio, maneno ya mlazo, mikolezo miongoni mwa vipengele vingine vimetumika kwa njia isiyo ya kawaida. Aidha, anahoji kuwa matumizi ya viakifishi hivyo huvutia makini ya msomaji kimatini kwa vile vikomo vimewekwa baada ya sentensi zingine na pia baada ya maneno na sentensi zingine zisizokamilika.

Kwa mujibu wa Adeniyi (2017), vipengele hivi huchimuza kazi ya kifasihi kimatini. Akizungumzia matumizi ya vistariungio na mabano, anasema kuwa alama hizi hutumika kifasihi kuimarisha uchimuzi katika fasihi. Alowonle akirejelewa katika Adeniyi (k.h.t) anaendelea kueleza ya kwamba violezo vya kigrafolojia vina mchango mkubwa sana katika ufasiri wa ushairi, ambao ni kuchimuza ujumbe uliyolengwa na mshairi.

Ngugi (2017) ameangazia kipengele cha ukawaida wa mandishi na lugha katika fasihi ya watoto. Amesema kwamba ikiwa lugha iliyotumika ni ya kiwango cha juu sana, huenda mtoto akakumbwa na ugumu wa kufasiri na hivyo basi ujumbe uliolengwa kuwasilishwa kupitia kwa matini hautamfikia msomaji. Amependekeza kwamba mwandishi wa vitabu vya watoto atumie lugha kwa ustadi na kwa kuzingatia kila kiwango cha wasomaji wake. Anassema ya kwamba ni kupitia kwa lugha ndipo umaarufu wa mwandishi unakadiriwa. Anahoji kuwa ni muhimu kuzingatia umri mbalimbali wa watoto au wasomaji lengwa ili kuteua msamiati ambao utautumia katika kuiendeleza kazi yako.

Aidha, Ngugi (1997) amehoji kwamba ni vyema pia kutumia msamiati mpya ili kupanua uwezo wa kuwasiliana wa msomaji kwa kumtajirirsha kimsamiati. Msamiati huo unahitaji kuambatana na kiwango chao cha utambuzi. Maneno yanayoteuliwa na wandishi wa vitabu pamoja na mpangilio wake yanaweza kufanya kazi yake ieleweke

au isieleweke kwa watoto wa viwango tofauti. Hii ni kusema ya kwamba matumizi ya maandishi ya kawaida huwa na dhima ya kuwasilisha ujumbe kwa njia sahihi.

Aidha, Ruthiiri (2012) amevirejelea vipengele vingine vya jalada la kitabu. Ujalidi na anwani ya kitabu ni vipengele vya kimsingi katika fasihi ya watoto kama anavyodokeza. Anasema ya kwamba uhakiki wa kitabu cha watoto huanzia kwenye jalada. Kwa mujibu wake, jalada hubeba ujumbe kwa muhtasari wa hadithi iliyo katika matini au ndani ya kitabu, hivyo basi, ujumbe kwenye jalada unahitaji kuwa wenye mvuto. Hii ni kwa kuwa katika fasihi ya watoto, vielelezo kwenye jalada huweza kuwa ndicho kigezo kinachompa mtoto motisha ya kusoma kitabu fulani. Ujalidi unahusu umbile la jalada na jinsi lilivyounganishwa na kurasa zingine. Ujalidi uliofanywa vizuri ni ule ulio imara ili kitabu kiweze kudumu kwa muda mrefu.

Ruthiiri (2012) pia amezungumzia vielelezo kama vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto. Amesema kwamba mwandishi na mchoraji wa vielelezo anahitaji kuhakikisha kuwa vielelezo vimewasilishwa kwa namna ambayo watoto wanaweza kuelewa ujumbe unaowasilishwa navyo kwa haraka. Kwa mujibu wake, vielelezo katika fasihi ya watoto vina dhima muhimu kwa vile vinatekeleza majukumu yafuatayo; hutoa mwangwi wa matini au hadithi; huleta mvuto kwa msomaji, hueleza kwa muhtasari wazo kuu, husaidia kuondoa uchovu wa msomaji, humsaidia mtoto kukumbuka hadithi, na hutoa ufafanuzi zaidi kuhusu sehemu za hadithi.

Katika sehemu hii, imebainika kwamba grafolojia ni kiwango muhimu katika uchanganuzi wa fasihi kiisimu na hutekeleza dhima mahususi katika fasihi ya watoto. Hata hivyo, imedhihirika kuwa tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu grafolojia na

dhima yake zimeelekezwa katika utanzu wa ushairi huku utanzu wa riwaya ukipuuzwa. Kando na Musotsi (2017) na Toboso (2018) ambao wamejitahidi kutafiti riwaya za Kiswahili za *Mkamandume* (2013) na *Babu Alipofufuka* (2001) kwa mtawalia, utafiti kuhusu grafolojia na uchimuzi ni dhana geni katika utanzu wa riwaya. Musotsi (k.h.t) alichunguza vijenzi vya grafolojia katika riwaya ya *Mkamandume* (2013), na utafiti huo ulibainisha kwamba utanzu wa riwaya haukamiliki bila grafolojia, na kwa hivyo vipengele vya kigrafolojia hutekeleza mchango mkubwa katika ujenzi wa riwaya.

Hata hivyo, utafiti haujafanywa kuviainisha vipengele vyote vya kigrafolojia na kubainisha dhima na athari yavyo katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Kinachobainika ni kwamba grafolojia ina dhima kuu kifasihi. Aidha, grafolojia huchangia dhima nyingi kama vile kuleta mvuto, kuendeleza uhalisia, kuafiki uwasilishaji wa ujumbe (maana), kusisitiza miongoni mwa dhima zingine.

## 2.6 Dhana ya uchimuzi

Akimnukuu Chapman (1974), Kazungu (1982) alisema kuwa uchimuzi ni dhana inayotumika kuelezea mkengeuko wenye dhima ya kukiingiza kipengele kingine katika lugha kisanii na kukiimarisha ili kijitokeze kuliko vipengele vingine kwa lengo la kuweka msisitizo. Kwa hivyo kulingana naye, kuchimuza kitu ni kukifanya kitu hicho kijitokeze kwa kuonekana zaidi kuliko kingine kimaandishi. Alisema kuwa, uchimuzi huwa na dhima mahususi katika kazi za kifasihi, mojawapo ya dhima kuu ikiwa kumfurahisha msomaji na hivyo basi kuzua mtazamo wa utendaji kwa msomaji.

Kulingana na Kazungu (1982), ili uchimuzi udhihirishe umuhimu wowote kifasihi, ni vyema uangaziwe katika muktadha wa mawasiliano. Leech na Short (1981) walianisha

uchimuzi kwa vikundi vikuu viwili ambavyo vilikuwa vya kiasi na ubora. Kulingana nao, uchimuzi wa kiasi ulihusu ujitokezeaji wa mara kwa mara wa vipengele fulani vya kiisimu, ilhali ule wa ubora ulihusu ukiukaji wa kaida za kiisimu. Pia waliainisha zaidi uchimuzi wa ubora kwa kategoria nane ambazo ni kategoria ya kileksia, kifonolojia, kisarufi, kigrafolojia, kisemantiki, kilahaja, kirejista na kihistoria. Wamitila (2003) alishiriki mdahalo huu kwa kusema ya kwamba uchimuzi ni dhana ya kuichomoza kauli ikilinganishwa na kauli zingine katika matini sawa. Kwa maoni yake, ni dhahiri kuwa mchomozo huo hutambulika kwa macho katika matini na huendelezwa kwa kutumia vipengele vya kigrafolojia.

Wamitila (2003) anayashadidia mawazo ya akina Leech na Short (1981) kuwa uchimuzi unaweza kudhihirika kwa njia mbili kuu. Njia ya kwanza ni ule ukiushi ambapo kuna ukiukaji wa miundo ya kisintaksia, hali ambapo maneno fulani yanatumika kwa namna isiyo ya kawaida. Pia, kuna ule uchimuzi ambao ni ule urudiaji ambapo vipengele vya lugha vinarudiwa kwa namna inayovifanya vitokezee dhahiri. Utafiti huu ulichukua mtazamo wa ukiushi unaokiuka miundo ya kisintaksia na ulinuia kubaini athari inayotokana na matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika uchimuzaji wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Aidha mtafiti amechanganua maudhui katika riwaya tano teule huku akitathmini jinsi maudhui hayo yanavyoimarishwa kwa kuchimuzwa na vipengele mbalimbali vya kigrafolojia kimaandishi. Utafiti ulilenga kuainisha, kubaini dhima na athari inayotekelezwa na vipengele vya grafolojia katika uimarishaji wa uchimuzaji wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 2.6.1 Grafolojia na uchimuzi wa maudhui

Kulingana na Sanders (1967), maudhui mengi ambayo huangaziwa katika fasihi ya watoto huambatana na tajriba ya maisha ya watoto na shughuli za ukuaji wao. Hii ni kusema kwamba maudhui ambayo huitawala fasihi ya watoto ni matukio yenye uhalisia, licha ya kwamba ubunifu unachangia pakubwa. Anataja matukio kama vile ukuaji, ujitambulishaji, kupendana, migogoro na mengine ambayo huchangia pakubwa katika uibuliwaji wa maudhui katika fasihi ya watoto. Maudhui yanayotajwa na Sanders (1967) hujengwa kwa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo huyachimuza maudhui hayo ili yafasiriwe kama alivyokusudia mwandishi wa matini.

Kazungu katika utafiti wake wa *Deviation and Foregrounding in chosen Swahili literary Texts* (1982), aliangazia jinsi dhana hizi hudhihirika katika tanzu za riwaya, ushairi na tamthilia ya Kiswahili. Alibainisha ya kwamba dhana hizi zinazohusika na ukiukaji wa kaida zilizozoeleka kiisimu hujitokeza na kutumika kama ngazi kati ya muundo na maudhui katika matini kwa kuwa zinachangia katika kuimarisha uwezo wa msomaji kuielewa matini kwa kina ambamo zinadhihirika kutumika.

Babajide (2000) aliainisha ufaafu wa uchimuzi katika uchanganuzi wa kigrafolojia kwa kusema kwamba uchimuzi ni tukio mwafaka kigrafolojia katika matini kwa vile linahusu kuviweka vipengele vingine mbele, hali ambayo hudhihirika kupitia kwa matumizi ya mifumo kama vile herufi kubwa, mandishi yenye mlazo, vinyota pamoja na alama au ishara zote ambazo matumizi yake hukifanya kionekane zaidi ya mandishi mengine. Matumizi ya vipengele hivyo huathiri jinsi ujumbe uliolengwa na mwandishi hufasiriwa. Adegoju (2008) alisema kuwa vipengele vya kigrafolojia hutumika kama vielelezo vya

macho katika kusimba na kusimbua maana kwenye jamii ya isimu kimatini. Hii ni kusema kwamba vipengele hivi huchimuza maudhui kimatini.

Hata hivyo, nao wananadharia Leech na Short (2007) wanaainisha uchimuzi kwa makundi mawili ambayo ni: uchimuzi wa idadi ambao unahusu kadhia ya ujitokezaji wa kipengele fulani dhahiri kimatini na ule uchimuzi wa ukiukaji wa kaida za lugha. Kwa mujibu wao, uzingatiaji na matumizi ya msimbo wa lugha kwa njia ya kawaida na iliyozoeleka ndio msingi ilhali ukiukaji ndio uchimuzi kwa kuwa hii huleta ujumbe mbele ya msomaji kabla ya kuisoma matini. Halliday (1994) alielezea hali hii kama utokezo uliotiliwa hamasa kwa vile unabeba vipengele vyote vya kiisimu na visivyo vya kiisimu ambavyo hutumika na mwandishi kuzalisha maana na kuipa kazi hiyo mvuto.

Mawazo ya Leech na Short (2007) yaliathiriwa na Halliday (1994) ambaye alitangulia kuzua mawazo ya kuwepo kwa aina mbili ya uchimuzi, wakati huo akitumia dhana za usambamba na mchepuko. Kulingana Halliday (k.h.t), usambamba ulitumika kurejelea uhalalisho usiotarajiwa, huku mchepuko ukitumika kurejelea hali isiyotabirika na isiyotarajiwa. Kama anavyoeleza Halliday (1994), katika uchimuzi kuna uwezekano wa kitu kisichotarajiwa kuwa na uhalalisho au kuukosa uhalalisho huo kimuktadha. Anasema kwamba muktadha huo unaweza kuwa mwembamba kama vile mastakimu ya matini moja kwa moja au hata usiwe lakini uathiri uibuaji wa matini kimaana.

Yeibo na Akerele (2014) wameeleza jinsi mwanafasihi Chimamanda Adichie alivyovitumia vipengele vya kigrafolojia katika kazi yake ya *Graphological Foregrounding in Chimamanda Adichie's Purple Hibiscus* (2014). Kwanza, wanasema kuwa kuna uhusiano wa ufaano kati ya viwango vya lugha na dhima ya lugha, ambavyo hutumiwa na wasanii kuendeleza uhusiano baina ya mifumo ya lugha katika kuifikia

ruwaza yao. Wanahoji kuwa hali hii inatokana na uwezo wa lugha kufulikana kama chombo cha mawasiliano ambacho kinaweza kuumbwa na hata kuumbuliwa ili kutekeleza dhima fulani kimuktadha katika matini. Wanavitaja vipengele vya kiisimu kama vile urefu wa matini, muundo wa aya, matumizi ya viakifishi pamoja na topografia ya ukurasa kama alivyovitumia Adichie kuwasilisha kazi yake, na wanasema kwamba hivyo ni vipengele vya kigrafolojia.

Yeibo na Akerele (2014) wanasema ya kwamba dhima inayotekelezwa na vipengele hivyo vya kigrafolojia katika matini hiyo ni kuchimuza maudhui yaliyobebwa na matini hiyo kwa kuwa vipengele hivi vinachangia katika uimarishaji wa ufasiri wa matini na kwa hali hiyo, msomaji hupata ujumbe uliyokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi. Akichangia, Emmott (2014) anasema kwamba uchimuzi hutambulika kujitokeza kimatini katika viwango vyote vya kiisimu huku mifano ya kawaida ikiwa usambamba, ukiukaji wa ukawaida, ubunifu wa kiwango cha juu kijazanda, mvunjiko wa mwendelezo, uradidi miongoni mwa vipengele vingine vingi. Pia anasema kwamba athari ya uchimuzi huwa ni pana, ikijumuisha uainishaji wa hoja muhimu, uzalishaji wa maana kimaudhui, uibuaji wa mwitikio kihisia pamoja na uzalishaji wa athari fulani kitaswira.

Yeibo na Akerele (2014) wameshughulikia uchimuzi kama chochote katika matini ambacho kinaweza kujumulisha vipengele vya leksia au miundo, takriri, au chenye kuleta maana husishi ambacho huvuta makini ya msomaji kimatini. Kwa mujibu wao, uchimuzi ni kipengele cha kimsingi katika sanaa ya uhakiki ambacho kinawasaidia wasomaji wa sanaa kubainisha maudhui katika matini ya kifasihi.

Alowonle (2016) aliyateua mashairi matatu ya Kiafrika kimaksudi ya *Time* la Kyei, *Rain is coming* la Osundare na *Silence II* la Remi Raji ambayo anayafanyia uchanganuzi wa

kiwango cha kigrafolojia. Utafiti wake ulibainisha ya kwamba maana na ufasiri wa mashairi hayo hauwezi kukamilika bila kuyatalii kigrafolojia ili kuibua maana lengwa ya mwandishi. Aidha, anadokeza kwamba ushairi uliosukwa vyema lazima uchimuzwe kwa kutumia vipengele mbalimbali vikiwemo vya kigrafolojia. Hi ni kusema ya kwamba grafolojia ni kiolezo muhimu katika usukaji wa ushairi na kwamba, ufasiri wa maudhui yaliyomo katika ushairi unahitaji ufahamu

Ni kutokana na hali hii ndiposa wanamitindo wengi huamini ya kwamba grafolojia ina dhima kuu katika mchakato wa ufasiri wa kifasihi ambao ni kuchimuza maudhui au ujumbe uliolengwa na mwandishi. Osunnuga (2016) akitoa mchango wake, anasema ya kwamba kimitindo, grafolojia ni elementi za uchimuzi ambazo zinahusiana na uteuzi kwa kutarajia elementi za kiisimu ambazo huonekana kushinda zingine katika matini. Anasema ya kwamba kando na kuibua matumizi ya vipengele kileksia, elementi zilizochimuzwa hudhihirisha athari fulani kimaana.

Aidha, Toboso (2018) ameshughulikia grafolojia na uchimuzi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001). Anasena kwamba wandishi hutumia njia na vipengele mbalimbali vya umitindo katika matini yao kwa lengo la kuyafikia maudhui na pia kuifikia thamani ya kiujumi katika matini yao. Anadokeza kuwa uchimuzi ni mojawapo ya vipengele vinavyotumiwa na wandishi kama njia ya kuimarisha ujumi kimatini ili kuifanya matini hiyo kuwa na mvuto kiakili na kimtazamo. Anasema ya kwamba dhana hii ilitumika mara ya kwanza na Garvin mwaka wa 1964 kufasiri dhana ya shule ya Prague "*aktualisace*" kama anavyoeleza Wales (1989).

Kulingana na Simpson akirejelewa katika Toboso (2018), uchimuzi ni mfumo wa kuendeleza kiolezo kimatini, unaomotishwa na dhima ya kiujumi. Hii ina maana kwamba

uchimuzi hutekeleza jukumu la kuufikia umbo la kimatini, ambalo huwa na mvuto wa kimtazamo wa hadhira. Kwa hivyo Toboso (k.h.t) anaiona grafolojia kama seti ndogo ya uchimuzi na ni dhana inayotumika kurejelea matumizi ya vipengele mahususi vya kiothografia kama vile mlazo, herufi kubwa, viakifishi, ujongezi kama miongoni mwa elementi za viziadaisimu vinavyotumika na wandishi ili kuafikia dhima ya kiujumi katika matini kwa kuifanya iwe na mvuto wa kupendeza kando na kuwasilisha ujumbe uliolengwa kimatini.

Toboso (2018) anamrejelea Halliday (1994) anayesema kwamba uchimuzi unahusu ujitokezeaji ambao umemotishwa katika matini. Kwa hali hii, anadhihirisha kuwa baadhi ya vipengele hivi kimatini huwa sehemu yenye kuvutia au kuonekana, ili kuileta mbele kifungu au sehemu fulani, ikilinganishwa na vile vipengele vingine ambavyo husalia katika msingi wa matini. Mtazamo huu unaangazia uchimuzi kiujumi. Kwa hivyo kulingana na Toboso (k.h.t), vipengele vya umitindo hupangwa katika riwaya na wandishi tofauti ili kudhihirisha elimumwendo na uhalisia wa lugha wa kujenga sentensi ambazo huafiki muktadha mahususi. Anaendelea kusema kuwa kwa kutumia vipengele hivi, wandishi huwa na uwezo wa kuichimuza kazi yao katika jitihada za kuwasilisha ujumbe unaobebwa katika matini.

Kwa hivyo Toboso (2018), anasema ya kwamba uchimuzi ni matokeo ya umitindo kigrafolojia ambayo hutumiwa na wandishi katika kuimarisha msokotano wa kiujumi katika matini ili kuifanya matini hiyo kuwa yenye mvuto kimtazamo na kififikra na pia kurahisiwa katika ufasiri. Akimnukuu Wamitila (2008), Toboso (k.h.t) anasema kwamba ni njia ya kuifanya taarifa fulani kujitokeza kuliko nyingine katika matini sawa. Toboso (k.h.t) anaendelea kudokeza kuwa katika umitindo, uchimuzi wa kigrafolojia umetumika

tangu mwanzoni mwa karne ya ishirini. Anaendelea kusema kuwa uchimuzi umetumika na baadhi ya wandishi wa Kiswahili ingawa tafiti nyingi ni zile ambazo zimejikita katika tafiti za utanzu wa ushairi.

Toboso (2018) anahoji kuwa tafiti chache zimeweza kuelekezwa katika utanzu wa riwaya kudhihirisha ya kuwa uchimuzi katika fasihi ya Kiswahili hususan riwaya haujaangaziwa kwa kina. Katika utafiti wake, anaangazia viwango mbalimbali vya uchimuzi ikiwa ni pamoja na uchimuzi wa kigrafolojia na umuhimu wa vipengele hivyo katika matini hususan katika ufasiri wa maudhui. Anasema kuwa uchimuzi huchangia pakubwa katika kuufikisha ujumbe au maudhui na ujumi katika hiyo riwaya. Mawazo yake yanashadidiana na mitazamo ya Ngara (1982), Halliday (1994), Adegoju (2008) na Yeibo na Akerele (2014) miongoni mwa wengine ambao katika kujadili grafolojia katika uchimuzi wanavitaja vipengele mbalimbali ambavyo ni vya kigrafolojia kama vile mwendelezo, herufi kubwa, kistariungio, sura ya matini, orodha, fonti zilizotumika, upigaji mstari, mlazo, aya, rangi miongoni mwa vipengele ambavyo wanasema huzalisha athari fulani kwa msomaji, na kwamba ni njia maarufu katika uchimuzaji wa maudhui katika kazi za kifasihi.

Musotsi (2017) amebainisha kwamba vipengele vya kigrafolojia kimatini huimarisha uchimuzi wa maudhui kando na kukuza msamiati wa Kiswahili katika matini. Hii ni kutokana na kutambulika mwanzoni mwa matini kwa vipengele hivi kwa macho na kwamba, vinabeba ujumbe fulani wa kipragmatiki ambao huathiri ufasiri katika diskosi. Ufot (2017) amefanya utafiti kuhusu uchimuzi, ingawa utafiti wake umejikita katika uchimuzi kimitindo kwenye lugha ya matangazo. Ametambua kuwa lugha ya matangazo imetazamiwa kama inayodhibitiwa na nia elekezi na yenye kuathiri kihisia. Anasema

kuwa katika uwezo wake wa kushurutisha, lugha hiyo huwa imechimuzwa na udhibiti wake kiothografia, kileksimu na kisarufi. Anahoji kuwa ni katika uchanganuzi wa matangazo ambapo dhana ya umitimdo ya kuchimuza hudhihirika.

### 2.7 Muhtasari wa riwaya teule

Riwaya zilizoteuliwa na kuchunguzwa zinawasilisha masuala mbalimbali. Sehemu zifuatazo zinatoa muhtasari wa kila riwaya.

#### 2.7.1. Riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012)

Riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) iliidhinishwa na KICD ili isomwe na wanafunzi wa darasa la kwanza katika shule za msingi za umma nchini Kenya. Riwaya hii ni kitabu chenye jumla ya kurasa thelathini (30). Hadithi iliyomo inawaangazia wanyama wawili ambao ni Sungura na Simba, wanayoyadhibiti maudhui. Kibiolojia, Sungura hula majani ilhali Simba hula nyama, hali ambayo inaleta uhusiano usio wa kufaana kati ya wanyama hawa kwa kuwa Sungura anaweza kuliwa na Simba ilhali Sungura haweza kumla Simba. Hii ni kusema ya kwamba uhusiano baina ya wanyama Simba na Sungura ni wa kidhalimu, na hali hii inadhihirika kutokana na picha ya Simba katika ukurasa wa kwanza, anapoonekana kudondokwa na mate jinsi anavyomchunza Sungura.

Sungura ana nyumba ambamo anajisetiri ili aepuka hatari ya kunyofuliwa na Simba iwapo watakumbana. Hata hivyo, Simba anaonekana kukosa chakula kwa hivyo anamwandama Sungura ili apate chakula. Simba anapata nafasi ya kuingia ndani mwa nyumba ya Sungura wakati Sungura anapoondoka kwenda kujitafutia chakula. Sungura anaporejea, anahisi kwamba hali si njema kwa kuwa anapata mlango wa nyumba yake

ukiwa wazi. Jambo hili linamghadhabisha Sungura na akiwa katika hali hiyo, anauona uso wa Simba ukiwa dirishani mwa nyumba yake, jambo linalomfanya Sungura kujificha pembeni mwa mti ulio karibu na nyumba yake.

Hata hivyo, Sungura anatumia maarifa alionayo kwa kumhadaa Simba kuondoka katika nyumba yake, huku akimwelekeza aliko Ndovu, mnyama mkubwa ambaye huenda atamfaa Simba iwapo atafaulu kumwandama na kumwangamiza ili kutosheleza hitaji lake la chakula. Simba anapoondoka nyumbani mwa Sungura, Sungura anajitoma ndani ya nyumba yake na kuubana mlango huku akimpa Simba kwaheri. Kwa hakika, Sungura ametumia maarifa kuepuka kuangamizwa na Simba ambaye angali anadondokwa na mate. Mwandishi analenga kutueleza ya kwamba Sungura ni mnyama mdogo kimaumbile lakini mwenye maarifa mengi kumliko Simba, anayechukuliwa kuwa mfalme wa porini. Kwa hivyo ni vyema kutumia hekima kujiokoa au kujitoa hatarini kuliko kutumia nguvu za kimaumbile kama alizo nazo Simba.

### 2.7.2 Riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009)

*Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) ni riwaya ambayo imeandikwa kwa ushirikiano wa Bracey na Lieta (2009), na vilevile kuidhinishwa na KICD ili isomwe na wanafunzi wa darasa la pili katika shule za msingi za umma nchini Kenya. Ni kitabu chenye jumla ya kurasa arobaini na saba (47), na kimegawika katika hadithi tatu. Hadithi ya kwanza ina anwani ya ***Sababu ya Mbuni kuwa na shingo ndefu.*** Hadithi hii inaanza kwa kumrejelea Mamba ambaye mwanzoni ametajwa kama mlafi na aliye na uzoevu wa kulala ukingoni mwa mto akitarajia windo ambalo mara kwa mara ni wanyama au mifugo wanaopelekwa mtoni kunywa maji. Hata hivyo, kutokana na ulafi wake, Mamba ana uzoevu wa kula nyama ya mbuzi na ng’ombe hususan wanapopelekwa mtoni kunywa

maji. Siku moja Mamba alihisi njaa sana na wakati huo mbuzi na ng'ombe hawakuwepo ila ndege na nzi. Mamba hangeweza kuwala ndege wadogo au nzi. Basi Mamba alibuni mkakati wa kumla Mbuni, rafikiye ambaye enzi hizo hakuwa na shingo ndefu. Basi ilimlazimu Mamba kubuni mkakati mwafaka wa kumwezesha kuafiki lengo lake. Alidai ya kwamba alikuwa akiumwa na jino la mwisho upande wa kushoto mwa kinywa chake na akamsihi Mbuni aje alichunguze kwa makini huku akifahamu kwamba alipanga kumla Mbuni.

Mbuni aliukubali wito wa Mamba na alipokitia tu kichwa chake ndani ya kinywa cha Mamba, Mamba alikifunga kinywa. Hali ya sintofahamu ilizuka huku Mbuni akilazimika kukivuta kichwa chake kutoka kinywani mwa Mamba. Kila alipokivuta kichwa chake kutoka domoni mwa Mamba, shingo la Mbuni liliendelea kurefuka na hatimaye Mbuni alipofaulu kujiokoa, shingo lake lilikuwa limerefuka na likasalia ndefu hadi sasa, huku Mamba akisalia na uhitaji mkubwa wa chakula. Hadithi hii pia imeimarishwa na mifano kadhaa ya picha zinazoonyesha kusononeka kwa Mamba kutokana na njaa na vilevile jitihada za Mbuni kujiokoa kutoka kwa ulafi wa Mamba. Ujumbe unaojitokeza ni kwamba Mamba si mnyama au rafiki mwaminifu kwa wenzake na kwa hivyo, tunahitaji kujiepusha na marafiki hasidi.

Hadithi ya pili katika riwaya hii ni yenye anwani ya ***Mayai ya Mamba*.** Ni hadithi ambayo inaangazia urafiki kati ya Sungura na Mamba. Wawili hawa waliuendeleza uhusiano wao wa karibu kwa kushirikiana kwa karibu mno kwa lolote lile pamoja huku wakishiriki mvinyo. Mamba hakufahamu ya kwamba Sungura alikuwa na nia ya kumdhuluma kwa vyovyote vile. Kumbe katika ushirikiano wao, Sungura aliazimia kukula mayai ya Mamba. Baada ya Mamba kunywa tembo na kulewa chakari, Sungura

alikula mayai yote ya Mamba na kisha alimsihi Mamba amsindikize na pia kumvukisha mto ulioyatenganisha makaazi yao kwa kuwa Sungura hakuwa na ujuzi wa kuogelea. Ni katika jitihada hizo ambazo mwanawe Mamba aliweza kutambua ya kwamba mayai yao yalikuwa yameliwa na Sungura na akamwarifu babake, aliyekuwa na maruerue kuhusu kitendo hicho cha Sungura.

Mamba hakufasiri vyema ujumbe aliopewa na mwanawe kutokana na ulevi baada ya unywaji pombe na Sungura. Baadaye, Mamba aliweza kupata ufahamu wa ujumbe wa mwanawe na akaamua kumwangamiza Sungura kwa kumzamisha majini. Kwa bahati nzuri, Sungura aliweza kujiokoa kwa kuruka upande wa pili uliokuwa karibu na ukingo wa mto lakini mguu wake ukang'atwa na Mamba. Hata hivyo, Sungura alimhadaa Mamba kuwa alilokuwa amelishika lilikuwa gogo bali si mguu wake Sungura.

Mamba alikasirika na kuuachilia mguu wa Sungura, huku Sungura akitimua mbio na kujiendea zake huku akimcheka Mamba kwa upumbavu wake. Mamba alibaki akifoka kwa hasira kutokana na kuzungushwa mbuyu na Sungura. Ujumbe huu pia umeimarishwa na picha ambazo zinaonyesha matukio hayo yakitekelezwa na wahusika hawa riwayani. Inadhihirika wazi ya kwamba mnyama Sungura ni mjanja na mwenye hekima licha ya udogo wake kimaumbile na kwa kuwa anatumia ujanja huo, anamdanganya Mamba kulewa chakari na kisha kumwibia mayai yake yote.

Hadithi ya tatu katika riwaya hii ni yenye anwani ya ***Mamba na moyo wa Nyani***. Siku moja, Mamba alikuwa ukingoni mwa mto alipomwona Nyani akiwa juu ya mwembe. Mamba alimsihi Nyani ampe maembe ambayo baada ya kuyaonja, alikiri kuwa maembe hayo yalikuwa matamu na makubwa. Mamba alimuomba Nyani amtundie maembe mengine ili ampelekee mke wake. Baada ya mkewe Mamba kula maembe hayo

alioletewa na mumewe, aliyafurahia mno na akawa na uzoefu wa kula maembe. Kando na kula maembe, mkewe Mamba vilevile alipenda moyo wa nyani. Mkewe Mamba alimpa Mamba mtihani wa kumletea moyo wa Nyani ambao ulikuwa mtihani mgumu uliomfanya Mamba kuibua mkakati mwema wa kuushughulikia. Mamba alimtembelea Nyani na kumwarifu kwamba mkewe alitaka kumshukuru kwa ukarimu wake uliotokana na kumtundia maembe.

Mamba alikubali kumbeba Nyani mgongoni mwake ili wavuke mto na kufika alikokuwa mkewe. Wakiwa safarini, Mamba alimnong’onezea Nyani kwamba, mkewe vilevile alihitaji moyo wa Nyani. Pendekezo hili lilimshtua Nyani ambaye alimjibu Mamba kuwa alikuwa ameuacha moyo wake juu ya mwembe. Basi Nyani alimsihi Mamba amrejeshe ukingoni mwa mto ili apande mwembe, auchukue moyo wake kisha amkabidhi Mamba na ampelekee mkewe. Alipofika pale ukingoni, nyani aliurukia mwembe na kisha akamtusi Mamba jinsi alivyokuwa mjinga kwa vile hakufahamu ya kwamba Nyani hangeweza kuishi bila moyo. Hadithi hii vilevile imedhibitiwa na mifano mingi ya picha za Mamba na Nyani.

Ujumbe unaojitokeza katika hadithi hizi tatu ni kwamba miongoni mwa jamii ya wanyama wa porini, kuna wale wenye hekima na maarifa mengi na vilevile wengine wenye akili punguani. Sungura ni miongoni mwa wanyama wajanjahuku Mamba akijumlishwa kati ya wale wanyama wanaopumbazika na kudhibitiwa na wanyama wajanja. Mwandishi anatupa ujumbe kuwa kuna wanyama wadogo kimaumbile kama vile Sungura ambao wanatumia marifa walionayo kujiokoa kutoka hatarini na kujinufaisha dhidi ya wanyama wakubwa kama vile Mamba na Simba ambao licha ya maumbile yao, wanashawishika na kupumbazika kwa haraka.

### 2.7.3 Riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006)

*Harusi ya Mwanasungura* (2006) ni riwaya iliyoandikwa na (Waihiga, 2006). Riwaya hii ina jumla ya kurasa ishirini na mbili (22). Ni riwaya inayozungumzia urafiki kati ya wanyama Paka na Panya, ambao hapo awali walipendana kama chanda na pete. Ni kutokana na uhusiano wao wa karibu ndiposa waliishi kwa nyumba moja pamoja na familia zao, huku shughuli zao vilevile zikiendeshwa kwa pamoja. Urafiki wa wawili hawa ulipanuka na ukamhusisha Sungura na familia yake. Jamii hizi zilishiriki karamu mbalimbali. Basi siku moja, Sungura aliwatembelea Panya na Paka na kuwaarifu kuhusu arusi ya kifunguamimba wake siku ya Krismasi. Aliwaeleza kwamba mmoja wao (Paka au Panya) angeithibiti sherehe hiyo pamoja na kufungua densi na Bi. Harusi kutegemea atakavyokuwa amejitayarisha au amejiandaa.

Paka na Panya walianza maandalizi huku wakitafuta mavazi waliyoazimia kuwa yangemfaa kila mmoja siku hiyo. Duka la Shangazi ndilo lililokuwa maarufu kwa uuzaji wa mavazi ya kupendeza, na hivyo basi marafiki hao walifunga safari kuenda kulitembelea. Basi waliweza kuyanunua mavazi yao dukani humo na kisha wakarejea nyumbani. Walipowasili nyumbani, waliamua kuyafanyia mavazi hayo majaribio huku wakishangiliwa na wana wao. Hata hivyo, ilibainika kwamba Panya alikuwa na wivu, hali ambayo ilimfanya abuni mikakati kisiri ya kuharibu suti ya Paka kwa kushirikiana na mkewe na mwanawe.

Panya na mkewe waliyapata mavazi ya Panya kwenye kabati na baada ya kuyaharibu kwa kuyachanua, Panya aliyarejesha katika kabati. Siku ya Krismasi ilipofika, Paka aliamka na kulifungua kabati lake ili avae suti yake nzuri na aelekee ukumbini mwa harusi. Hakuamini macho yake kwa kuwa suti yake aliyotarajia kuvaa ilikuwa

imechanika visivyomatarajio. Alijua moja kwa moja kwamba uhaini huo ulikuwa umetekelezwa na Panya. Kwa hivyo alizua ugomvi na Panya na katika hali hiyo, Panya, mkewe na mtoto walitimua mbio huku wakiandamwa na Paka na mkewe.

Paka alipomkaribia Panya na jamii yake, wote waliokuwa wakiandamwa waliingia katika shimo lililokuwa pembeni mwa barabara na kujificha. Kwa kuwa mili ya Paka na mkewe ilikuwa imeimarika kimofolojia, walishindwa kumuandama Panya hadi shimoni humo. Basi Paka na mkewe walirudi nyumbani wakiwa na hamaki huku wakiapa kuendelea kumtafuta Panya kwa lengo la kumuadhibu kufuatia utundu wake. Hiki ndicho chanzo cha uhasama kati ya Paka na Panya, uhasama unaoshuhudiwa hadi leo. Ujumbe unaojitokeza katika riwaya hii ni kwamba ni vyema kuwatathmini marafiki zetu kwa kuwa wengine huwa na mielekeo na misukumo tofauti na tunavyotarajia kama inavyodhihirika katika hadithi hii ambamo tunapata kufahamu chanzo cha uhasama kati ya Paka na Panya.

### 2.7.4 Riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003)

*Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) ni riwaya yenye kurasa ishirini na sita (26) na ni riwaya ambayo pia imeidhinishwa na KICD ili isomwe na wanafunzi wa darasa la nne (4) katika shule za msingi za umma nchini Kenya. Riwaya hii inawarejelea watoto wanaoshiriki michezo ya kibe na ya kupika, michezo wanayoshiriki sana siku ya Jumamosi. Wanaanza na mchezo wa Kibe na kisha kushiriki ule mchezo wa kupika. Mmoja wa watoto hao Aida anaamua kujiondoa katika mchezo wa upishi kwa vile tayari alipewa tahadhari na mamake kuhusu hatari ya kucheza na moto, huku wengine wakiendelea kushiriki huo mchezo. Baada ya kuuwasha moto na kujihusisha katika mchezo wa upishi wa viazi,

watoto wengine wanaendelea kuruka kamba huku wengine wakicheza gololi wakisubiri viazi walivyokuwa wakipika viive.

Watoto hao walikuwa wameyaweka mafiga yao karibu na ghala la akina Aliya, lililokuwa limetengenezwa kwa nyasi kavu, miti na makuti na lililokuwa na nafaka. Basi upepo ulivuma ghafla na ghala hilo likashika moto huku wale watoto wakisalia katika hali ya taharuki. Ilichukua muda mfupi na lile ghala lilikuwa limeteketea kabisa huku hasara kubwa ikikadiriwa. Hata hivyo ujirani mwema ulidhihirika kufuatia juhudi za wanajamii kuuzima moto huo. Baada ya hasara hiyo, mmoja wa wasichana ambao walishiriki mchezo huo kwa jina Aliya alimwendea babake kwa lengo la kumuomba msamaha kwa kutozingatia maagizo aliyopewa kila wakati na mamake. Mwanzoni, babake Aliya alionekana mwenye hasira lakini baadaye, alimeza mate machungu na akaamua kumsamehe bintiye Aliya. Tangu siku hiyo, Aliya alichukua tahadhari kuhusu moto. Mwandishi analenga kututahadharisha dhidi ya moto na madhara ambayo yanaweza kusababishwa na mchezo wa moto hasa miongoni mwa watoto.

### 2.7.5 Riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015)

*Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) ni riwaya yenye kurasa kumi na nane (18). Ni riwaya inayomrejelea kijana wa kiume kwa jina Dani, mwenye umri wa miaka kumi ambaye anaishi katika mtaa wa Songambele na wazazi wake, mtaa uliokuwa karibu na barabara kuu. Wazazi wa Dani walipokwenda kazini, Dani alibakia pekee nyumbani kwa kuwa alikuwa likizoni baada ya shule kufungwa. Dani alitafakari njia kadhaa za kucheza na kujiburudisha akisubiri kurejea kwa wazazi wake nyumbani kutoka kazini. Njia kuu ya Songambele ilikuwa ikiyapitisha magari mengi sana.

Kwa vile magari mengi yalipita katika barabara kuu ya Songambele karibu na nyumba yao, Dani aliamua kushiriki mchezo wa kurekodi nambari na rangi ya magari yote yaliyopita katika njia hiyo. Wazazi wake waliporejea, Dani alimkabidhi babake ile karatasi ya habari kuhusu magari ambapo ilibainika ya kwamba gari aina ya Toyota ndilo lililokuwa maarufu mno miongoni mwa magari yote yaliyopita katika njia kuu.

Ilitokea kwa sadfa kwamba mojawapo ya magari aliyorekodi habari zake lilikuwa limeibwa kulingana na taarifa iliyotangazwa katika runinga siku hiyo jioni. Hii ilimlazimu bababe Dani apige simu katika kituo cha polisi kwa lengo la kubaini habari hiyo, na simu ilipopokelewa kituoni, babake Dani alimkabidhi Dani simu hiyo iliyofaulisha mawasiliano baina ya Dani na Askari Msimamizi wa kituo cha polisi. Dani alimpa huyo Askari Msimamizi takwimu alizokuwa nazo kuhusu magari yaliyotumia njia kuu ya Songambele.

Habari za mchango wa Dani kwa vyombo vya usalama zilimfurahisha Askari Msimamizi ambaye alifanya mpango wa kuzipeperusha katika gazeti lililokuwa na anwani: **Dani Asaidia Polisi Kunasa Wezi wa Toyota (**uk.13). Dani aliahidiwa kutuzwa shilingi laki moja na Meja Fanyakazi, ambaye ndiye alikuwa Askari Mkuu. Kutokana na riwaya hii, inadhihirika wazi kwamba baadhi ya michezo ambayo watoto hushiriki inaweza kuwa na manufaa kwa mtoto na vilevile kwa umma. Dani aliweza kutuzwa hela takriban laki moja kutokana na umakini wake na ushirikiano wake na vyombo vya usalama katika kukabiliana na wizi nchini.

Kutokana na ufupisho huo wa riwaya teule, inabainika kwamba miktadha ambamo fasihi ya watoto huzalishwa na kusambazwa hutawaliwa na yaliyomo na maudhui, ilhali kuwasilishwa kwa maudhui hayo hutegemea lugha na vipengele vyake. Wanyama na

binadamu pia ni wahusika wakuu katika kuyaendeleza maudhui mbalimbali yanayowasilishwa kupitia riwaya teule. Katika mifumo ya lugha, kuna uwezekano wa wasomaji wachanga katika usomaji wao kukumbana na matumizi kadhaa ya lugha huku mengine yakiwapa changamoto. Vilevile, vitabu ambavyo huenda vikawa na maudhui sawia vinaweza kutofautiana sio tu kimaudhui bali kupitia kwa rasilmali tofauti ya vipengele vya kiisimu, vikiwemo grafolojia.

## 2.8 Hitimisho

Wataalamu wengi waneangazia fasihi ya watoto na kubaini ya kwamba fasihi hii huwa na sura ambayo inawavutia wasomaji. Jiménez (2015) katika makala yake: *Introduction to Graphology* (k.h.t) anachangia katika mchakato huu anapodokeza kwamba miaka michache iliyopita, Halliday, McIntosh na Strevens waliipanua dhana ya grafolojia walipoihusisha na tahajia za maneno, uakifishaji na shughuli zingine zinazohusiana na rasilimali za grafiki katika lugha. Anaendelea kuhoji kwamba wanaisimu wengine kama vile Vachek (1973), Sampson (1985), Coulmas (1991, 1999) na Harris (1995) vilevile walishughulikia grafolojia huku wakijikita zaidi katika vipengele vya kialfabeti na historia yake. Hata hivyo, ni bayana kwamba jinsi lugha inavyojiimarisha, fasihi andishi pia hujiimarisha kwa vile inawasilishwa kupitia kwa mandishi na hivyo basi kudhihirisha mikondo ya kigrafolojia.

Kulingana na Eva (2015), sura ya matini ya fasihi ya watoto inapong'aa, huwa imeimarishwa na vipengele vingi vikwemo vipengele vya kigrafolojia. Anaendelea kusema ya kwamba grafolojia hivi leo inaweza kuangaziwa kama utafiti kuhusu grafemi na vipengele vingine husishi vinavyodhihirika kimaandishi kama vile viakifishi, aya na

hata uwazi kati ya mistari miongoni mwa mifumo mingine ya uandishi katika lugha, ambavyo ni vya kimsingi katika fasihi ya watoto. Kwa hivyo Eva (k.h.t) anachangia kwa kuvitaja baadhi ya vipengele vya kigrafolojia. Sura inayofuata inaangazia muundo wa utafiti.

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia njia na mbinu za utafiti kwa kujumuisha vipengele mahususi vilivyoangaziwa katika utafiti huu. Vipengele hivyo ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, usampulishaji na sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishwaji wa data, uhalali na utegemezi wa utafiti, maadili katika utafiti, changamoto na hitimisho.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano kwa kuwa data iliyokusanywa na kuchanganuliwa ilikuwa ya kithamano. Huu ni muundo unaotoa maelezo kuhusu kinachotafitiwa kama kinavyoonekanana bila kuhitilafiana na vigezo au bila kuwa na upendeleo wowote, na hujumulisha usoroveya na uchunzaji wa aina mbalimbali (Kothari, 2004:37). Dhima ya muundo wa kimaelezo ni kuelezea tukio au matukio kama yalivyo na sifa zinazodhihirika katika tukio au matukio hayo.

Muundo huu unajishughulisha sana na 'nini kilichofanyika' badala ya 'ni vipi kitu fulani kilivyofanyika' na kwa hivyo, unachunguza hali ya tukio katika mazingira fulani huku mtafiti akibainisha uhusiano uliopo baina ya vigezo husika na vilevile akitoa ufafanuzi sahihi wa matukio kama yalivyo wakati huo wa utafiti. Muundo wa kimaelezo hufuata mkondo au huchukua hatua mahususi ambazo ni pamoja na suala la utafiti, kuibua madhumuni ya utafiti, uamuzi kuhusu mbinu zitakazotumiwa katika ukusanyaji data, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishwaji wa matokeo.

Hatua hizi zilizingatiwa kikamilifu katika utafiti huu. Mtafiti alivibainisha vipengele mbalimbali vya kigrafolojia ambavyo hutumiwa na watunzi wa fasihi ya watoto ya Kiswahili. Alichanganua dhima yavyo katika fasihi ya watoto na pia akatathmini namna matumizi ya vipengele hivyo katika matini inavyoathiri uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga, huku madhumuni hayo yakiongozwa na maswali mahususi ya utafiti.

### 3.2 Eneo la utafiti

Kijiografia, utafiti ulifanyika katika Kaunti ndogo ya Mumias Magharibi inayopatikana katika Kaunti ya Kakamega nchini Kenya. Kaunti Ndogo ya Mumias Magharibi ina upana wa takriban kilomita mia moja sitini na tano nukta tatu (165.3) mraba na ni miongoni mwa Kaunti ndogo kumi na mbili (12) zilizounganishwa na kuunda Kaunti ya Kakamega. Kaunti ndogo ya Mumias Magharibi imegawika katika kata nne ambazo ni Musanda, Etenje, Mumias Kaskazini na Mumias ya Kati. Kaunti hii ndogo inapakana na Kaunti Nogo ya Matungu katika upande wa Kaskazini ilhali katika upande wa Mashariki, inapakana na Kaunti Ndogo ya Mumias Mashariki. Katika upande wa Kusini, Kaunti hii Ndogo ya Mumias Magharibi inapakana na Kaunti Ndogo ya Butere ilhali Magharibi mwake inapakana na Kaunti Ndogo ya Ugunja ambayo inapatikana katika Kaunti jirani ya Siaya.

Makao makuu ya Kaunti Ndogo ya Mumias Magharibi ni mji wa Mumias. Mji wa Mumias unapatikana katika eneo la $30^0$ $30^0$ longitudo Mashariki na $0^0$ $20^0$ latitudo Kaskazini (Murunga, 1998). Mji huu ni umbali wa takribani kilomita thelathini na mbili (32) kutoka mji wa Kakamega, ambao ndio makao makuu ya Kaunti ya Kakamega.

Kitaaluma, utafiti huu ulijikita katika umitindo. Umitindo aghalabu hugawika katika mawanda mapana ya umitindo kifasihi na umitindo kiisimu. Utafiti huu ulilenga umitindo kiisimu, hata hivyo kwa kuegemea katika makala ya kifasihi, hasa riwaya za watoto.

**3.3 Kundi lengwa**

Utafiti huu ulilenga wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili katika shule tatu za Msingi za umma nchini Kenya. Shule hizo zilikuwa shule ya msingi ya wavulana ya St. Peters, shule ya msingi ya wasichana ya St. Annes na shule ya msingi ya mseto ya Mumias Central. Utafiti pia ulilenga vipengele vya grafolojia katika fasihi ya watoto ya Kiswahili, hasa jumla ya riwaya tano (5) za watoto.

**3.4 Usampulishaji na sampuli**

Utafiti ulizingatia usampulishaji dhamirifu katika uteuzi wa vitabu, wasailiwa na shule teule. Vanderstoep na Johnston (2009) wanaeleza ya kwamba usampulishaji dhamirifu ni utaratibu unaomruhusu mtafiti kutumia vigezo ambavyo huwa na ujumbe toshelevu unaoendana na madhumuni ya utafiti, na kwamba vigezo hivyo huteuliwa kutokana na sababu kwamba vina sifa mwafaka kuhusiana na utafiti unaoendelezwa. Kutokana na utafiti wa awali, mtafiti alitambua kwamba vitabu kadhaa vya fasihi ya watoto vinasheheni vipengele vingi vya kigrafolojia vinavyosaidia katika uchimuzaji wa maudhui, ndiposa akaviteua vitabu vitano (5) kidhamirifu.

Kutokana na usampulishaji dhamirifu, riwaya tano za watoto za Kiswahili zilitumiwa, moja moja kwa kila gredi, Gredi 1 (1), Gredi 2 (1), Gredi 3 (1), Gredi 4 (2) isipokuwa gredi ya nne ambayo riwaya mbili zilitumiwa kwa kuwa kutokana na tajriba ya wasomaji hao, wasomaji hao wana uwezo wa kusoma na kuelewa riwaya mbili. Vitabu vifuatavyo

viliteuliwa kimaksudi; *Nyumba ya Sungura* (gredi ya kwanza ), *Hadithi ya Mamba* (gredi ya pili), *Harusi ya Mwanasungura* (gredi ya tatu ) na *Usicheze na Moto* na *Dani na wezi wa Toyota* (Gredi ya nne ).

Wasailiwa waliteuliwa kupitia mbinu ya usampulishaji dhamirifu. Kama anavyodokeza Creswell (2007:125), usampulishaji dhamirifu hutumika katika uatafiti wa kithamano. Creswell (k.h.t) anadokeza kuwa kupitia kwa mkakati wa usampulishaji dhamirifu, mtafiti huteua sampuli mahususi inayomwezesha kuyaafikia madhumuni ya utafiti wake pamoja na kujibu kikamilifu maswali ya utafiti. Kwa hivyo mtafiti aliwalenga walimu wawili wawili (2) wanaofunza somo la Kiswahili kutoka katika gredi ya kwanza hadi gredi ya nne katika shule zilizoteuliwa, na wanafunzi wawili wawili (2) wanaofanya vyema katika somo la Kiswahili katika gredi ya kwanza, gredi ya pili, gredi ya tatu na gredi ya nne katika shule zilizoteuliwa. Aidha, mtafiti alisaidiwa na walimu wa somo la Kiswahili katika gredi ya kwanza hadi gredi ya nne katika shule teule katika uteuzi wa wanafunzi ambao wameshirikishwa katika usaili usio rasmi.

Msaili aliwashirikisha wanafunzi wawili wawili wa gredi ya kwanza, gredi ya pili, gredi ya tatu na gredi ya nne katika usaili usio rasmi huku akizingatia moja kwa moja riwaya ya Kiswahili ambayo kila mojawapo ya gredi hizo hushughulikia katika somo la Kiswahili. Usaili usio rasmi wa wanafunzi ulifanyika darasani na vilevile ofisini, na kila usaili ulichukua takriban dakika thelathini. Wanafunzi wa gredi ya kwanza na gredi ya pili walionekana kutoelewa utafiti uliokuwa ukiendelezwa na kwa hivyo, msaili aliweza kuchukua muda mrefu akiwaelezea alichokuwa akitafiti katika kuendeleza usaili huo. Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti kwa wasailiwa wa gredi za tatu na ya nne. Wasailiwa au wanafunzi wa gredi ya tatu na nne walioshirikishwa katika usaili usio rasmi

walidhihirisha ufahamu wa baadhi ya vipengele vilivyokuwa vikitafitiwa huku wakijieleza kikamilifu.

Kama anavyosema Cresswell (2007:128), katika utafiti, mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa data ya kipekee ambayo ni mwafaka katika kuafiki madhumuni na pia kujibu kikamilifu maswali ya utafiti wake. Vilevile mtafiti aliwateua watafitiwa ishirini (20) kimaksudi kati ya wanafunzi hamsini (50) wa gredi ya nne mkondo wa (4C) katika shule ya Msingi ya Mumias Central. Uchaguzi wake ulitumia sampuli sahili kinasibu katika kuwafikia watafitiwa hao. Aliifikia sampuli hiyo kwa kuandika nambari moja (1) hadi ishirini (20) kwenye vijikaratasi ishirini miongoni mwa jumla ya vijikaratasi hamsini alivyoviandaa kuwakilisha wanafunzi hamsini wa humo darasani. Kwa hivyo kati ya vijikaratasi hamsini alivyovitumia, ni vijikaratasi ishirini vilivyokuwa na nambari moja hadi ishirini ilhali vijikaratasi thelathini havikuwa na mandishi au nambari zozote.

Baadaye, mtafiti alivikunja vijikaratasi hivyo, kisha akaviweka katika kasha na akalitingisha vyema lile kasha kwa lengo la kuhakikisha kuwa vijikaratasi hivyo vimechanganyika vizuri. Kisha alimpa kila mwanafunzi fursa ya kuokota kijikaratasi chochote chenye nambari yoyote kati ya vijikaratasi vyote hamsini vilivyokuwa katika bweta. Hata hivyo, wasailiwa aliowalenga ni wale ambao walikuwa na fursa ya kuokota vijikaratasi vyenye nambari moja hadi ishirini kati ya vile vijikaratasi hamsini vilivyokuwa katika bweta. Kwa hivyo wanafunzi ambao waliweza kuokota vijikaratasi vyenye nambari moja hadi ishirini ndio waliopata fursa ya kushirikishwa katika utafiti kama watafitiwa.

Watafitiwa hao ishirini walishirikishwa katika utafiti kwa kila mmoja kupewa nakala ya riwaya mwigo na riwaya asilia, wakazisoma na kuzihakiki kwa kujibu maswali

yaliyokuwa nyuma ya kila nakala. Hii ilikuwa katika jitihada za kushughulikiwa madhumuni ya tatu ya utafiti huu ambayo ililenga kupima athari ya vipengele vya kigrafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 3.5 Ukusanyaji wa data

Mchakato wa ukusanyaji data unahitaji kutambuliwa na kuelezewa kwa njia inayothibitisha matokeo. Kwa hiyo utafiti ulishirikisha ukusanyaji wa data ya aina mbili; data ya kimsingi na data ya sekondari.

#### 3.5.1 Mbinu ya ukusanyaji data

Makundi mawili ya data yaliweza kuibuliwa na mtafiti kufuatia jitihada zake za kwenda nyanjani na vilevile maktabani.

#### 3.5.2 Ukusanyaji wa data ya kimsingi

Data ya kimsingi ndiyo iliyokusanywa nyanjani na bila shaka ilidhihirika kuwa na uasilia kisifa. Data ya kimsingi ilikusanywa kupitia kwa usaili usio rasmi wa moja kwa moja wa wanafunzi na walimu na pia kupitia uchunzaji wa kushiriki darasani mwa shule tatu teule.

##### 3.5.2.1 Usaili usio rasmi

Vanderstoep na Johnston (2009) wanataja usaili usio rasmi kama mojawapo ya mbinu mwafaka za ukusanyaji data katika utafiti wa kithamano. Kulingana nao, usaili usio rasmi humpa msaili fursa ya kumwelekeza msailiwa kwa njia mwafaka za kushiriki katika utafiti ili kujibu maswali ya utafiti kwa njia iliyo bora zaidi. Hii ni pamoja na kumfafanulia msailiwa dhana ambazo huenda zikaonekana kumpa changamoto bila kuzingatia utaratibu wa maswali kama yalivyopangwa katika orodha ya usaili.

Wanafunzi wawili wawili wa gredi za kwanza hadi gredi ya nne wanaofanya vyema katika somo la Kiswahili katika shule teule walishirikishwa katika usaili huo ili kuvibainisha na pia kueleza dhima inayotekelezwa na vipengele vya kigrafolojia katika matini teule zilizotafitiwa. Mtafiti alisaidiwa katika uteuzi wa wanafunzi hao na walimu wa somo la Kiswahili katika madarasa yaliyolengwa na utafiti huu. Vilevile walimu wawili wawili wa somo la Kiswahili wanaowafunza wanafunzi wa gredi ya kwanza, gredi ya pili, gredi ya tatu na gredi ya nne katika shule teule walishirikishwa katika usaili usio rasmi. Usaili huo ulikuwa wa moja kwa moja. Usaili usio rasmi wa walimu ulifanyika katika mazingira ya nje ya ofisi kusiko na hitilafu za kelele, na vilevile ulichukuwa dakika thelathini kwa kila mwalimu. Majibu ya maswali ya usaili ya wanafunzi na walimu yalirekodiwa kwanza katika shajara na kisha yakawekwa katika fomu za usaili zilizokuwa na maswali huru.

Kwa hali hii, mtafiti aliwajibikia upekuzi wa hali ya juu na maandalizi mema na akaweza kupata data toshelevu. Hii ilifaulishwa kutokana na udhibiti mwema wa wasailiwa kwa vile jinsi wasailiwa walivyoitikia kwa kujibu maswali, ndipo msaili alivyoibua maswali mengine. Kutokana na ukosefu wa utaratibu wa usaili usio rasmi, mtafiti aliweza kuibua maswali mengi papo hapo wakati wa kuwasaili wanafunzi na walimu na akaweza kukusanya data ya kutosha.

#### 3.5.2.2 Uchunzaji wa kushiriki

Mtafiti pia alitumia uchunzaji wa kushiriki katika ukusanyaji wa data ya kimsingi kwa kutumia orodha ya maswali ya uchunzaji. Mtafiti alishiriki katika utafiti wakati wa kipindi cha somo la Kiswahili, huku akinakili maelezo mazito katika shajara kuhusu

matukio muhimu yalivyodhihirika wakati wanafunzi walipokuwa wakisoma riwaya kwa sauti na kujadili, chini ya uongozi wa walimu wa somo la Kiswahili. Pia kamera aliokuwa nayo iliweza kunasa picha na sauti za wanafunzi wakishiriki mchakato huo. Kupitia kwa njia ya usaili usio rasmi wa wasailiwa na uchunzaji wa kushiriki, mtafiti aliweza kupata data toshelevu aliyoitumia katika utafiti huu.

### 3.5.3 Ukusanyaji wa data ya sekondari

Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa utafiti mseto, mtafiti vilevile alikusanya data ya sekondari. Data ya sekondari ilikusanywa maktabani kutoka katika riwaya tano zilizoteuliwa kidhamirifu kupitia kwa mbinu ya upekuzi wa yaliyomo na pia uchanganuzi wa yaliyomo wa riwaya hizo. Mtafiti aliweza kuipekua kila mojawapo ya riwaya mara nne, akidondoa aina ya vipengele mbalimbali vya kigrafolojia vilivyodhihirika katika kila riwaya. Miongoni mwa vipengele hivyo mlijumuishwa viakifishi, picha na michoro, rangi miongoni vingine ambavyo wadishi walivitumia katika kuziendeleza riwaya hizo. Mtafiti aliweza kuibuka na orodha ya vipengele kadhaa vya kigrafolojia katika kila mojawapo ya matini ambavyo vilijumuisha data aliyoichanganua.

### 3.5.4 Vifaa vya ukusanyaji data

Vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji wa data ya kimsingi ni pamoja na orodha za uthibitishaji, dodoso, shajara, kamera, mtafiti, pamoja na orodha ya maswali. Sakti (2014) anadokeza kwamba katika utafiti wa kithamano, mtafiti ni kifaa muhimu cha utafiti kwa vile ndiye anayeupanga utafiti huo, kwa kuviteua vifaa vingine vifaavyo vya kumwezeshe kukusanya data toshelevu, akavifanyia vifaa hivyo majaribio, akakusanya data, akaichanganua data na kutoa ripoti ya matokeo ya utafiti huo. Majibu ya wasailiwa

walioweza kushirikishwa katika usaili usio rasmi kuhusu vipengele vya grafolojia yalinukuliwa kwanza katika shajara na baadaye yakahamishwa katika dodoso.

Aidha, Kamera iliweza kutumika katika kunasa shughuli za uchunzaji wa kushiriki wa mtafiti darasani na pia katika kunasa hatua za usaili usio rasmi wa wanafunzi na walimu kama ilivyoendelezwa na kutukia katika shughuli hii. Orodha ya uthibitisho ilimwezesha mtafiti kudhibitiwa katika shughuli yake ya uchunzaji wa kushiriki alipojumuika na wanafunzi wa gredi ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne madarasani katika shule tatu teule. Mtafiti aliweza kutangamana ana kwa ana na wasailiwa, huku akiongozwa na maadili ya utafiti. Orodha ya uthibitisho pia ilitumika katika ukusanyaji wa data ya sekondari katika uchanganuzi wa riwaya tano (5) teule zilizochunguzwa.

Aidha, maswali yaliyotungwa kutoka riwaya mwigo na riwaya asilia yalitumika. Mtafiti aliviondoa vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika kikawaida katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) na kuunda orodha ya maswali matano ambayo aliwapa wanafunzi wa gredi ya nne ili wayajibu baada ya kuisoma riwaya mwigo. Pia mtafiti alitumia orodha ya maswali kutoka tamatini mwa riwaya asilia au halisi na kuwapa wanafunzi ili wayajibu baada ya kuisoma riwaya asilia iliyokuwa na vipengele vingi vya kigrafolojia.

### 3.6 Uchanganuzi na uwasilishwaji wa data

Uchanganuzi kithamano unahusisha hatua kadhaa. Kothari (2004: 122) amebainisha hatua nne za kimsingi katika kuchanganuliwa kwa data ya aina hii ambazo ni uhariri na marekebisho, usimbaji, upangaji na hatimaye uchanganuzi wenyewe wa data. Mtafiti alizizingatia hatua hizi zote katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Aliaanza kwa kuchunguza kwa makini jinsi dodoso, orodha ya uthibitishaji, kamera, shajara na orodha

ya maswali yalivyotumika nyanjani na pia maktabani huku akiwasiliana na wasailiwa kwa ushauri kwa lengo la kuondoa makosa yoyote iwezekanavyo, ambayo huenda yalijitokeza katika jitihada za kukusanywa kwa data hiyo.

Kisha mtafiti alishiriki katika uhariri wa data ghafi, kwa kuipekua mara kwa mara, shughuli alioifanya kwa kina kwa lengo la kutambua na kurekebisha makosa yoyote ili kuhakikisha ya kuwa, data inayoshughulikiwa katika uchanganuzi ni sahihi na inawiana na yote yaliyokusanywa kulingana na maswali na madhumuni ya utafiti. Baadaye, mtafiti alifanya marekebisho kwa kuondoa majibu yote ambayo hayakufaa kwa mujibu wa madhumuni na maswali ya utafiti huu katika dodoso. Pia mtafiti alishiriki katika marekebisho ya kijumla yaliofanywa kwa lengo la kuondoa makosa yote katika data iliyokusanywa kwa jumla kabla ya data hiyo kuwekewa msimbo.

Uwekeaji data msimbo ni miongoni mwa hatua muhimu katika uchanganuzi wa data, kwa kuwa inachangia katika uchanganuzi kamili ambapo matokeo kadhaa yanaweza kupunguzwa na kuunda idadi ndogo ya matokeo yanayojumuisha habari muhimu inayohitajika katika uchanganuzi. Mtafiti aliuzingatia utaratibu ufaao wa hatua za kimsingi za usimbaji. Alianza kwa kuipanga data iliyokusanywa kwa makundi mahususi. Mtafiti alitumia maneno (majina mahususi ya vipengele mbalimbali vya kigrafolojia) kama msimbo, kuiwekea data msimbo kwa kuyaandika wazi wazi kama inavyodhihirika katika kiambatisho nambari nne (4).

Baadaye mtafiti aliipanga data hiyo kwa mujibu wa maswali na madhumuni ya utafiti kwa lengo la kurahisisha uchanganuzi. Kwanza aliigawa data hiyo kwa vikundi vidogo vyenye sifa zinazofanana na zile zinazotofautiana na kisha kuiwekwa data hiyo katika kategoria mahususi ili kubaini mahusiano na tofauti iliyojiri. Kisha aliianisha data hiyo

ikiongozwa na utaratibu wa mantiki na anwani ya riwaya teule kwa kila gredi kwa lengo la kuyatolea maelezo au ufafanuzi ufaao. Vipengele vya uchanganuzi katika utafiti wa kithamano kama huu mara kwa mara huwa ni maelezo. Hata hivyo, maneno yalitumika kwa kuwa yalimwezesha mtafiti kuyaweka katika kategoria ilhali katika uibuliwaji wa maana, mtafiti alitumia sentensi.

Kwa kuwa kurasa hubeba vipengele vingi vya kigrafolojia ikiwemo nafasi inayoashiria nafasi kati ya mistari katika matini, kipengele cha uchanganuzi wa yaliyomo katika utafiti huu kilikuwa ukurasa ambamo vipengele mbalimbali vya kigrafolojia vilidhihirika kutukia miongoni mwa riwaya teule zilizotafitiwa. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kupitia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Krippendorff (2004) ametaja uchanganuzi wa yaliyomo kama mojawapo ya mbinu ya uchanganuzi wa data. Mbinu hii ya uchanganuzi data ndio mwafaka katika uchanganuzi wa matini na ina nafasi kubwa katika utafiti wa kithamano. Ni mbinu inayoongezea maarifa mtazamo mpya na uwasilishwaji wa ukweli katika utafiti. Lililofichama na mbinu hii ni kwamba mtafiti ana uhuru wa kutathmini na kuyachanganua matini bila kumhusisha mwandishi au mwandalizi wa matini hiyo.

Uchanganuzi data kwa kutumia mbinu hii hudhihirika katika mikabala mitatu kama anavyoeleza Krippendorff (2004). Mkabala wa kwanza ni uchanganuzi wa yaliyomo kipragmatiki. Mkabala huu unaziainisha ishara na maneno kwa kuangazia nini kilichozisababisha ishara hizo au ni nini athari ya matumizi ya maneno au ishara hizo katika matini. Kwa mfano matumizi ya uradidi katika matini bila shaka huashiria msisitizo katika neno ambalo huwa limerudiwarudiwa. Mkabala wa pili ni ule wa

uchanganuzi wa yaliyomo kisemantiki. Mkabala huu huzianisha ishara na maneno kwa kuangazia maana ya ishara hizo na pia maana ya maneno hayo katika matini.

Mkabala wa uchanganuzi wa yaliyomo kisemantiki hudhihirika katika kategoria tatu. Kategoria ya kwanza ni uchanganuzi wa maelezo ambao unahusu muktadha ambamo vipengele vinavyochunguzwa hudhihirika. Kategoria ya pili ni ile inayohusu uchanganuzi kisifa ambao unadhihirika kupitia ishara au maneno yaliyotumika kumrejelea mhusika katika matini. Kategoria ya tatu ni uchanganuzi kimaudhui ambayo inahusu mfumo fulani wa utendakazi ambao umechukuliwa kama uamuzi wa kufuatwa na wanajamii

Mkabala wa tatu ni uchanganuzi unaoigawa data kutokana na jinsi inavyodhihirika katika matini kiidadi. Dhima ya uchanganuzi wa yaliyomo katika utafiti huu ilikuwa kuainisha ishara na vipengele vingine vya kigrafolojia na kutathmini maana inayoibuliwa na athari inayodhihirika wakati mwandishi wa matini anapoamua kuvitumia vipengele hivyo katika uendelezaji wa kazi yake. Kwa hivyo uchanganuzi wa yaliyomo katika utafiti huu ulichukua mkabala wa kisemanti kimuktadha kwa kuwa mtafiti alivibainisha wazi vipengele vya kigrafolojia vilivyodhihirika na kutambulika katika usaili usio rasmi pamoja na uchunzaji wa kushiriki na vilevile katika upekuzi wa riwaya teule tano.

Mtafiti alieleza dhima ya matumizi ya vipengele hivyo na athari inayodhihirika kwa msomaji wa matini ambamo vipengele hivyo vimetumika kimuktadha kupitia kwa maelezo. Data yote ilikusanywa na kisha ikapangwa kulingana na madhumuni matatu ya utafiti. Data iliyochanganuliwa ilifasiriwa kupitia kwa maelezo ambayo yalitumika kujibu maswali na pia kuafiki madhumumi ya utafiti huu. Vilevile matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kupitia kwa maelezo yaliyoyajibu maswali na madhumuni ya utafiti.

Maelezo hayo yaliimarishwa kwa kuongezewa vielelezo vya picha ili kuangazia kwa uwazi mifano ya grafolojia husika.

### 3.7 Uhalali na utegemezi

Kulingana na *Colorado State University Writing Centre* (2004), uhalali wa uchanganuzi wa utafiti unahusu maafikiano ya kikategoria kwa hitimisho na maono ya kijumla. Ni mchakato unaohusu ukweli wa utafiti. Utafiti ulitumia mbinu mseto katika kutathmini uhalali, na ulichukua mkakati wa kupima kwa kutumia pembe tatu ambako mtafiti alitumia vipengele mseto vya matini, wanafunzi, walimu, mbinu za utafiti pamoja na nadharia kuufikia ushahidi ulioshirikishwa kama anavyoelezea Creswell (2018).

Kwa mujibu wa Gibbs (2007) katika Creswell & Creswell (2018), utegemezi wa kithamano huashiria kwamba utaratibu ambao mtafiti ameuzingatia ni thabiti miongoni mwa watafiti tofauti. Uhalali na utegemezi wa utafiti ulihakikishwa kwa majaribio ya awali ya vifaa vyote vya utafiti na mtafiti, ili kupima ufaafu na utegemezi wavyo pamoja na matumizi ya mbinu mseto za ukusanyaji data. Vilevile mtafiti alipitia kwa makini unukuzi wote uliofanyika ili kuondoa dosari yoyote ambayo huenda ilijiri katika shughuli za utafiti. Aidha, alihakikisha kuwa hakuna ukwepaji wala utata katika ufafanuzi wa maana ya istilahi zilizotumika katika uwekeaji wa msimbo. Hili lilitendeka kwa kutoa maelezo mahususi kuhusu msimbo na katika mchakato wa kuutekeleza katika shajara. Pia mtafiti alimhusisha msaidizi wake katika utafiti huu, ambaye alipekua kwa makini mara kadhaa misimbo, kwa maafikiano ya ulinganishi wa msimbo. Utaratibu huu ulichangia katika kuafiki utaratibu wa utafiti wa kithamano.

### 3.8 Maadili katika utafiti

Mtafiti aliyazingatia maadili ya utafiti wa kiakademia. Haya aliyatekeleza kwanza, kwa kutetea utafiti wake idarani na kitivoni chuoni MMUST, shughuli iliyoidhinishwa kwa kupewa barua na Mkurugenzi wa Masomo ya Upeo chuoni MMUST. Mtafiti aliitumia barua hiyo kuomba kibali kutoka kwa tume ya kitaifa ya *National Commission of Science, Technology & Innovation* (NACOSTI) ya kumruhusu kwenda nyanjani kukusanya data. Vilevile kibali kutoka NACOSTI kilimwezesha mtafiti kuomba idhini kutoka kwa Mkuu wa Utawala wa Kaunti ya Kakamega na Mkuu wa Elimu katika Kaunti ya Kakamega, ya kumwezesha kufanya utafiti katika shule tatu teule katika eneo hilo.

Aidha, mtafiti alituma ombi kwa njia ya barua kwa walimu wakuu wa shule tatu teule ya kumwezesha kutangamana na wasailiwa, na akaundeleza utafiti wake katika shule hizo bila kuhitilafiana na shughuli za kawaida za masomo shuleni humo. Aliwaeleza wasailiwa kuhusu dhima ya utafiti huo na akaweza kukusanya data ambayo ilihusu tu mada ya utafiti. Mtafiti aliwahakikishia wasailiwa ya kwamba habari zote walizotoa zingetumika tu kwa minajili ya utafiti huo huku akikiri kuyaweka wazi matokeo ya utafiti wake kwa manufaa ya jamii. Mtafiti aliepuka kutumia njia za mkato kama vile kuwalazimisha wasailiwa kuidhinisha utafiti na hata kunukuu kazi za watafiti wengine bila kuwarejelea. Aidha, kazi mbalimbali zilizorejelewa na mtafiti zilijumuishwa katika sehemu ya marejeleo, na pia mawazo yalitoka kwa watafiti mbalimbali yalirekodiwa pamoja na wakati au mwaka mawazo hayo yalipotolewa au kupendekezwa.

### 3.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia njia na mbinu za utafiti ambazo zilizingatiwa katika kufaulisha utafiti huu. Vipengele vilivyoangaziwa ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, usampulishaji na sampulii, ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishwaji wa data, uhalali na utegemezi wa utafiti pamoja na maadili katika utafiti.

# SURA YA NNE

# MATOKEO NA MJADALA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inabainisha vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika fasihi ya watoto katika Kiswahili, dhima inayotekelezwa na vipengele hivyo na athari inayotokana na matumizi ya vipengele hivyo katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

## 4.1 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto


Vipengele kadhaa vya kigrafolojia vilidhihirika kutumika katika ujenzi wa riwaya tano (5) teule zilizochunguzwa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Vipengele hivyo vilijumuisha viakifishi, herufi kubwa, picha na michoro, maandishi yenye rangi tofauti, taipografia na aina mbalimbali za fonti na nafasi, maneno yaliyokolezwa, maneno yaliyolazwa, miundo mbalimbali ya aya, ukubwa wa matini na umbo la matini. Hata hivyo, riwaya hizo vilevile zilidhihirisha kutumia vipengele vingine kama vile vielelezo na majedwali, faharasa, maswali na mazoezi ambavyo Adeniyi (2017) hawakuviorodhesha kama miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia. Vipengele hivyo vimeainishwa na kuchanganuliwa katika sehemu inayofuata.

### 4.1.1 Matumizi ya viakifishi

Katika riwaya tano zilizochunguzwa, viakifishi ni miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia ambavyo vilionekana kuwa na umaarufu kufuatia matumizi yake mapana katika uandishi wa matini za riwaya tatu teule. Hata hivyo, matumizi ya viakifishi

yalionekana kuchukua mikabala miwili; matumizi ya viakifishi kwa njia ya kawaida iliyozoeleka na matumizi ya viakifishi kwa njia isiyo ya kawaida. Kulingana na Leech na Short (1981), dhima ya nadharia ya umitindo ni kueleza jinsi wasomaji hunufaika kutokana na maneno yaliyo katika matini kwa njia ya kuelewa matini hiyo. Hii ni kusema ya kwamba jinsi maandishi yanavyowasilishwa katika matini, ndivyo maandishi hayo yanavyostahili kusomeka na kueleweka vyema na msomaji. Hata hivyo uelewaji wa mandishi hutegemea jinsi mandishi hayo yanavyofasiriwa na msomaji kwa kuwa ufasiri mwema pia hutegemea matumizi mema ya viakifishi.

Wamitila (2008) katika kuzungumzia nadharia ya umitindo alihoji kwamba mhimili wa grafolojia ndio unaoshughulikia mandishi, na kwamba kazi ya fasihi kimatini haiwezi kumfikia msomaji bila ya kuwa katika maandishi mahususi. Anataja uakifishaji kama mojawapo ya sifa za kimsingi katika grafolojia katika umitindo. Miongoni mwa viakifishi vilivyotumika katika kuziendeleza riwaya zilizochunguzwa ni pamoja na kikomo (.), kiulizi (?), kihisishi (!) vipumuo (,), koloni (:), semi-koloni (;) deshi ( ___ ), alama za udondoshaji (…), ving'ong'o ('), *mlazo*, mnukuu (" ") na vistariungio (-). Katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* ( Bracey & Lieta 2012), viakifishi vilivyotumika ni viulizi (?), vikomo ( . ) na vituo ( , ) kama inavyodhihirika katika mfano unaofuatia ambamo viakifishi hivi vitatu vimetumika.



Simba yupo wapi?
Simba yumo ndani ya nyumba
ya Sungura.
Simba, toka kwa nyumba yangu.
Simba angalia,
Mwangalie Ndovu.
Ndovu yuko pale.
Kwaheri Simba.

Mfano 4.1.1.1 Ukurasa kutoka riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 30.

Huo ulikuwa tu miongoni mwa mifano inayoonyesha jinsi viakifishi vya kiulizi (?), kikomo (.) na kituo (,) vilivyotumiwa na waandishi katika uundaji wa kazi yao. Alama ya kikomo ( . ) imetumika mwishoni mwa sentensi **Simba yumo ndani ya nyumba ya Sungura** ( . ) Hiki kikomo kimetumika mwishoni mwa sentensi hiyo kuashiria kutamatika kwa sentensi ambayo inatoa taarifa kamili kuhusu aliko Simba. Katika sentensi **Simba** ( , ) **toka kwa nyumba yangu,** kituo ( , ) kimetumika kumpa mzungumzaji ambaye ni Sungura nafasi ya kupumua katika kuendeleza mawasiliano.

Vilevile kituo kimeweka msisitizo katika neno Simba, kinapopachikwa baada ya neno hilo kuonyesha kuwa si mnyama mwingine tu bali ni Simba.


Katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009), viakifishi vilivyotumika ni pamoja na ving'ong'o ('), viulizi (?), vikomo (.), vihisishi (!), vituo (,) mnukuu (" ") na semi koloni (;).



Basi siku moja, Mamba hakuwa na chakula.
Hakujua ale nini.
Alifikiri angeweza kumla Mbuni.
Lakini hakujua atamshikaje.
Mbuni alipotokea, Mamba alimwambia,
"Mbuni, Mbuni, njoo unisaidie."
Mbuni alienda karibu na Mamba akauliza,
"Mamba, kuna nini?"
Mamba akajibu,
"Jino langu linauma sana.
Hebu njoo uliangalie."
Mbuni alisogea karibu akamwambia Mamba,
"Fungua kinywa chako.
Hebu niliangalie jino lako.
Ni jino gani hilo?"
Mamba akasema,
"Ni hilo la mwisho upande wa kushoto.
Linauma, Oh! Oh! Oh! Oh!
Linauma."

Mfano 4.1.1.2 Ukurasa kutoka riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 5


King'ong'o (') kimedhihirika kupitia kwa mfano wa maneno **ng'ombe** (kur..2, 3), **ng'ambo** (kur.21, 22) ambayo ni maneno yenye sauti za ung'ong'o.



Mamba alipata maembe mengi.
Alianza kuyala.
Maembe yenyewe yalikuwa makubwa na matamu.
Mamba aliyapenda sana. Baada ya kuonja utamu huu alisema,
"Nitampelekea mke wangu baadhi ya maembe haya. Mke wangu anaweza kuyala maembe.
Maembe haya ni matamu; tena ni mazuri.
Mke wangu atayapenda maembe haya makubwa na matamu."

Mfano 4.1.1.3. Ukurasa kutoka katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 36.


Kiakifishi cha semi koloni (;) katika riwaya hii kimedondolewa katika sentensi **Maembe haya ni matamu; tena ni mazuri** katika mfano uliopo hapo juu. Kiakifishi hiki kimetumika kwa dhima ya kutoa maelezo zaidi kuhusu maembe, kama anavyoeleza Mamba.



Siku moja Mamba aliona
njaa sana.
Hapakuwepo na ng'ombe.
Hapakuwepo na mbuzi pia.
Hapakuwepo na wanyama
waliokwenda mtoni kunywa
Mamba alihisi njaa.
Hawezi kula nzi.
Hakuweza kuwakamata nde
Mamba hakujua afanye nini.

Mfano 4.1.1.4. Ukurasa kutoka katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 3.

Kipengele cha kigrafolojia cha viakifishi pia kimetumika katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006). Miongoni mwa viakifishi vinavyodhihirika katika riwaya hii ni mnukuu (“”), viulizi (?), vihisishi (!), semi koloni (;), vikomo (.) na vituo (,) kama inavyodhihrika katika mifano ifuatayo.



kutembea mjini Sokoni. Ziara hizo za mjini ziliwafurahisha sana watoto wao. "Mama tunataka biskuti. Tunataka peremende! Baba tununulie soda!" Waliwaambia wazazi wao kila mara walipopita karibu na maduka ya kuuzia bidhaa hizo.

Walitazama kwa mshangao majumba ya ghorofa na magari ya aina mbalimbali yaliyojaa kwenye barabara pana za mji wa Sokoni. "Tazama ile nyumba!" Angesema mtoto wa Paka. "Baba, hebu ona lile basi!" Angesema mtoto wa Panya huku akimwonyesha baba yake basi lililojaa wasafiri furi. Kwa hakika walifurahia sana safari zao mjini Sokoni.

Katika kijiji jirani kilichoitwa Maish Salama, aliishi Kaka Sungura pamoja n familia yake. Kwa miaka mingi, familia Kaka Sungura ilikuwa na urafiki mkub


2

Mfano 4.1.1.5. Ukurasa kutoka katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk.2.

Katika mfano huu, kikomo (.) kimetumika kama vile katika sentensi **Ziara hizo ziliwafurahisha sana watoto wao (.).** Kipengele hiki kimetumika kuashiria mwisho wa sentensi hiyo. Alama ya mnukuu (" ") na hisi (!) zimetumika katika kipashio hiki (**") Mama tunataka biskuti. Tunataka peremende (!) Baba tununulie soda (!) (").** Alama ya mnukuu inadhihirisha mazungumzo au taarifa halisi kama ilivyotolewa na watoto wa marafiki Paka na Panya wakiwa sokoni kuendeleza maandalizi ya harusi ya

Mwanasungura. Alama hisi inaashiria hisia za watoto. Alama ya kituo (,) inajitokeza katika mfano huo kwa mfano katika sentensi ya mwisho katika mfano wa ukurasa huo inayosema **Kwa miaka mingi** (,) **familia ya Kaka Sungura ilikuwa na urafiki mkubwa.** Alama hii imetumika kudhihirisha mpumuo au pumziko fupi katika kauli hii.

Kiulizi (?) vilevile kimetumika katika riwaya hii kupitia kwa sentensi **“ Sasa tutafanya nini ?”** katika mfano huu.



ishirini na nne Disemba, nitarudi hapa ili tuamue ni nani kati yenu atakayekuwa kiongozi wa sherehe hiyo.” Baada ya kuyasema maneno hayo, Kaka Sungura aliaga na kuondoka.

Paka na Panya waliachwa wakiwa na mawazo mengi mno. Mwaliko kama huo hawakuutarajia hata kidogo. Sungura alikuwa mzee aliyeheshimiwa sana katika eneo hilo. Pia, alikuwa na mali.

Kwa hivyo, Paka na Panya walijua kuwa sherehe hiyo ingehudhuriwa na wageni wengi mno kutoka karibu na mbali. “Sasa tutafanya nini?” Aliuliza Panya.

“Tutahitaji kuanza matayarisho.”

“Bila shaka,” alijibu Paka.


“Lakini tutatoa wapi mavazi mazuri yanayowafaa wageni wa heshima wa herehe kubwa kama hiyo?” Aliendelea uuliza Panya.

7

Mfano 4.1.1.6. Ukurasa kutoka katika **r**iwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk.7.


Alama ya kiulizi imewekwa mwishoni mwa kifungu **Sasa tutafanya nini?** kuashiria ya kwamba maelezo hayo ni swali. Ni swali ambalo Panya alimuuliza rafikiye Paka baada ya kupewa taarifa ya mwaliko wa kuhudhuria harusi ya Mwanasungura.

Viakifishi vilivyotumika katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) ni kituo (,) kikomo (.), hisi (!), mnukuu (“ ”) na kiulizi (?) kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.


“Leo tupikeni viazi,” Aliya alisema.
“Ah, kwani mnahisi njaa?” Dodo aliruka.
“La. Huu ni mchezo tu,” Aliya akamjibu.
Aida akawaambia, “Lakini mama alitukataza kuw
moto. Alisema watoto hawafai kucheza na moto.”
“Ikiwa hutaki, tuwache sisi tupike,” Aliya akamwam
Aida aliondoka. Aliwaacha. Aliienda zake.

Mfano 4.1.1.7. Riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk.5

Alama ya kunukuu imedhihirika katika sehemu ya mwanzo mwa mfano huu katika kifungu (**“) Leo tupikeni viazi (”), Aliya alisema.** Kiakifishi hiki kimetumika kuonyesha usemi halisi kama ulivyotoka kinywani mwa Aliya. Alama ya kituo (,) imetumika katika kifungu **“Ah (,) kwani mnahisi njaa (?)”** kuonyesha kipindi kifupi cha pumziko katika kauli hiyo. Vilevile katika kifungu hicho, kuna kiulizi mwishoni kinachoulizia ikiwa washiriki katika mchezo wa kupika wanahisi njaa. Kikomo (.) kinadhihirika katika sentensi **Aida aliondoka** kuonyesha ya kwamba hiyo ni sentensi yenye taarifa kamili na sentensi hiyo imehitimika. Alama hisi imetumika kama inavyojitokeza katika mifano mingi katika ukurasa huu.



Watoto wanaimba.
Wanamwimbia Dodo:

“Kibe! Bado!
Kibe! Bado!

Funga macho yako.
Baki peke yako.

Haya tujifiche watoto.
Tucheze mchezo wa kitoto.

Hesabu moja sio ziro.
Kwa sauti yako nyororo.

Hesabu hadi ishirini.
Haraka tuingie mitini.

Fungua macho yako!
Tutafute wapi tuko!


Sasa ndio tuko.
Sasa la hatuko.

Kibe! Bado!
Kibe! Bado!”

Mfano 4.1.1.8. Ukurasa kutoka katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk.2.

Kibe! Bado!, Kibe! Bado! Ni mfano mwema wa kifungu ambamo alama hisi imetumika kuonyesha hisia za watoto wanaoshiriki mchezo wa Kibe.

Viakifishi vya vituo (,), vikomo (.), mnukuu ( " "), alama hisi (!), udondoshaji (…), koloni (:), kistariungio na viulizi vilitumika katika kuiendeleza riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) kama inavyojitokeza katika mifano inayofuatia.


Vipindi vya vibonzo vilipokamilika, Dani aliinuka, akajinyoosha mwili huku akijiuliza, 'Siku ya leo itaisha kweli?' Alitazama saa, akajiambia, 'Ni saa nne tu! Na shangazi atakuja saa tisa!' Aliingia jikoni, akajitilia chai. Alirudi nayo sebuleni akaanza kuinywa. Alipomaliza kunywa chai , alirudisha kikombe jikoni akakiosha. Alirudi sebuleni tena. Alichukua kisengeretua cha runinga, akakibonyeza. Alikuwa anatafuta kipindi kingine ambacho kingemburudisha. Baada ya kufungulia chaneli zote moja baada ya nyingine, aliizima runinga huku akijiambia, 'Hakuna vipindi vya kuvutia sasa hivi.' Aliondoka taratibu na kwenda chumbani mwake.


Alipanda vidato, kimoja kimoja kana kwamba alivihesabu hadi mwisho. Alikuwa akibandika na kubandua mguu pa, pa, pa! Ile sauti ya nyayo zake ilikuwa hafifu lakini kwa sababu ya kimya ndani ya nyumba, iligonga kama kidumbaki. Aliingia chumbani mwake. Aliketi kitandani. Kisha akainuka akachukua kiti akaketi karibu na dirisha akitazama wapita-njia. Alimwona mtu aliyenunua magazeti makuukuu kutoka kwa watu pale mtaani. Mtu huyu aliwafahamisha watu kuwa amefika kununua magazeti kwa kuita kwa sauti ya juu, "Haayaa magazeeti, chupa na madebe. Mali... Maliii... Mali... Maliii..., nanunua mali zote chupa, karai kuukuu, na vyombo vya chuma! Maliii, mali maliii..." Dani

3

Mfano 4.1.1.9. Ukurasa kutoka katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.3

Katika sentensi ya kwanza katika mfano huu inayosema **Vipindi vya vibonzo vilipokamilika** (,) **Dani aliinuka, akajinyoosha mwili huku akijiuliza, 'siku ya leo itaisha kweli?'** alama ya kituo (,) imetumika baada ya neno vilipokamilika kuweka pumziko fupi katika sentensi hiyo. Alama ya kiulizi imetumika katika kifungu 'siku ya leo itaisha kweli?' kuonyesha ya kwamba kifungu hicho ni swali na hususan, swali la balagha.

Vilevile mnukuu (' ') umetumika katika mfano huo kuonyesha kuwa ni usemi halisi kama ulivyotoka kinywani mwa mzungumzaji. Kistariungio kimetumika katika mfano Alikuwa anatafuta kipindi kingine **amba-(cho)** na pia katika sentensi **Ali panda vidato, kimoja kimoja kana kwamba alivi - (hesabu).** Alama hii imetumika kuonyesha ya kuwa kuna kijisehemu cha neno hilo lililokuwa likiendelezwa ambalo halikukamilika katika mstari huo, ambalo litakamilikia katika mstari unaofuatia kwa silabi ambazo zimeonyeshwa katika mabano.


Mimi simfungulii mtu yeyote wala sitoki nje hadi mtaka-
porudi. Nitawezaje kuondoka ilhali bado nakumbuka
kisa kilichompata rafiki yangu Juma hivi juzi alipokosa
kutii ushauri wa wazazi wake!"
"Nafurahi kusikia kwamba hata wewe umejifunza
kutokana na kisa kilichompata Juma," mama alisema
huku akiondoka.
Mama Dani alikuwa amemuomba Shangazi Wumi
afike nyumbani. Alitaka Shangazi Wumi amnunulie bi
dhaa fulani kutoka duka-kuu la 'Pamoja Supermarke
Duka hili lilikuwa mbali kidogo na mtaa huo. Ma
Dani alimtaka Dani aandamane na Shangazi ili amsai
kubeba bidhaa hizo. Mama Dani alimfahamisha k
Shangazi angefika saa tisa, kwa hivyo awe tayari w
huo.
"Kumbuka kuwa Shangazi Wumi an
Mfungulie. Lakini kwanza hakikisha kuwa ni
mama alimwambia Dani huku akiingia kwenye g
Baba alitia gari moto, wakaondoka pamoja na

Mfano 4.1.1.10. Ukurasa kutoka katika **r**iwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.2.

Hii ni baadhi ya mifano ya viakifishi ambavyo wandishi wa riwaya tano teule zilizochunguzwa waliitumia katika kuendeleza kazi zao. Matumizi haya ya vipengele hivi

katika riwaya tano zilizochunguzwa yalionekana kuzingatia matumizi ya kawaida ya viakifishi na vilevile matumizi yasiyo ya kawaida. Viakifishi kama vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika maandishi vimejadiliwa na Nordquist (2016), Lauchman (2010) na Tunicak (2003). Tunicak (k.h.t) katika Radita (2017:4) alivibainisha viakifishi vinavyotumika katika mandishi ya kawaida kwa kuvitaja, kuelezea dhima yavyo na pia akavitolea mifano. Alibainisha aina kumi na nane (18) ya viakifishi kwa jumla ambavyo ni pamoja na kiulizi (?), kihisishi (!), kikomo (.), kistariungio (-), deshi ( ___ ), mabano duara ( ), mabano mraba [ ], udondoshaji (…), mshazari ( / ), kinyota (*), king'ong'o (' ), kitone cha kuonyesha ('), mlazo (*a*), mstari ( _____ ) alama za kunukuu (" "), koloni (: ), semi koloni (;), kituo (,) na koma.

Vilevile Chukwu (2010) alivitaja viakifishi kumi na vinne (14) ambavyo alivigawa katika makundi matatu. Kundi la kwanza aliliita viakifishi vya tamati na lilijumlisha kikomo, kiulizi na kihisishi. Kundi la pili aliliita viakifishi vya ndani na kundi hilo lilijumlisha koma, koloni, semi koloni, mabano, deshi, udondoshaji na kareti. Kundi la tatu kwa mujibu wa Chukwu (k.h.t), lilikuwa la viakifishi kati ya maneno, na lilijumlisha king'ong'o, kistariungio, mlazo na alama za kunukuu. Hata hivyo mtazamo wa Tunicak (k.h.t) na Chukwu (k.h.t) kuhusu vipengele hivi uliegemea katika sarufi kwa kuwa uliangazia matumizi ya viakifishi katika muktadha wa kawaida uliozoeleka kiisimu. Ingawa Radita (2017) alisema kuwa viakifishi vinatumika kuibua maana na kuweka msisitizo, utafiti huu umebaini kuwa vipengele hivi vinatekeleza dhima mbalimbali, huku kila kiakifishi kikiwa na dhima mahususi.

Wikoff (2012) vilevile katika kujadili, alisema kuwa viakifishi ni ishara zinazotumika kuwaelekeza wasomaji kusoma na pia kufasiri sentensi jinsi watu wanavyotaraji

zifasiriwe. Hata hivyo, licha ya maoni mbalimbali ya watalaam hawa kuhusu matumizi ya viakifishi, tathmini ya kina ya matumizi ya viakifishi katika matini za kifasihi inaonyesha ya kuwa viakifishi vilevile vinaweza kutumika katika matini za kifasihi huku matumizi hayo yakikiuka matumizi ya kawaida au ya kiisimu ya vipengele hivyo. Kwa mfano katika riwaya ya *Mkamandume* (2013), mwandishi ametumia maneno kama vile ul'ochacha, n'na, as'o, ak'enda (Mohamed, 466) na mengine katika ujenzi wa kazi yake.

Katika mifano hiyo, inadhihirika kuwa kuna vipashio vya kisarufi vilivyochunwa. Hata hivyo, uchunwaji huo hauathiri maana lengwa tu bali unaibua dhana nyingine ambayo inatupa mwanga kuhusu mwandishi. Kwa hivyo kando na mwandishi kujijengea upekee fulani katika ubunifu wa uendelezaji wa kazi za kifasihi kimaandishi, mwandishi pia anatudhihirishia ya kwamba vipengele hivi vinaweza kutekeleza dhima nyingine inayoweza kuleta athari tofauti kwa msomaji. Hii ni kusema kwamba maoni ya wataalamu waliorejelewa kuhusu matumizi ya viakifishi yanakubaliana na matokeo ya utafiti huu na vilevile yanakinzana na matokeo ya utafiti huu kwa kuwa kuna baadhi ya wandishi ambao wamevitumia viakifishi kinyume na kaida za kiisimu.


Kwa mfano, kipengele cha kistariungio (-) kinaweza kutumika visivyo kifasihi kama walivyojadili watalaam Tunicak (2003), Chukwu (2010) na wengine. Katika mfano **kwa nini anakichukia ki-Katija** (Mohamed 2013), kistariungio hakijatumika kuunganisha vipashio hivyo bali ufasiri wa kifasihi ni kwamba kuna dhana ya udunishaji katika matumizi ya kipengele hicho. Kwa hivyo ingawa utafiti huu ulikubaliana na mawazo ya watalaama waliotoa mawazo kuhusu mchango wa viakifishi katika uendelezaji wa maandishi, vilevile uliweza kuongezea katika matumizi ya vipengele hivyo kifasihi. Hii ni kusema ya kwamba utafiti huu ulibaini ya kwamba matumizi ya kawaida ya viakifishi

yanaweza kukiukwa, hali inayodhihirika katika fasihi. Hata hivyo ukiukwaji wa matumizi ya viakifishi unatokana na ujuzi wa mwandishi yeyote, pamoja na ubunifu na dhima ya kazi anayoishughulikia. Hali inayompa mwandishi upekee na kumbainisha kati ya wandishi wengine.

Kwa hivyo matumizi ya viakifishi miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia yanashadidiana na mhimili wa uteuzi katika fasihi kama ulivyojadiliwa na Wamitila (2008), ambao ni mojawapo wa mihimili ya nadharia ya umitindo iliyoudhibiti utafiti huu. Kulingana na mhimili huu, lugha teule ni kiunzi muhimu katika mawasiliano kimaandishi na kwamba mwandishi wa kazi za kifasihi ameruhusiwa kufanya uteuzi wa lugha ambayo ana ung'amuzi nayo au hata pengine asiwe na ung'amuzi wa lugha kuihusu kwa kukiuka kaida zilizozoeleka. Hii ni kwa sababu wakati mwingine, mwandishi anapoanza kutunga kazi yake, huwa amepokea uchochezi usioweza kuelezewa. Anapofanya hivyo, linakuwa jukumu la msomaji au mhakiki kutumia tajriba yake ili aweze kukitegue kile kitendawili kilichotegwa na mwandishi katika jitihada za kuufasiri ujumbe ambao mwandishi huwa amelenga kuuwasilisha.


### 4.1.2 Matumizi ya herufi kubwa

Katika riwaya tano zilizochunguzwa, herufi kubwa ni miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia ambavyo pia vilionekana kuwa na umaarufu mno kimatumizi kwa vile kilitumika kote katika matini zote tano teule zilizochunguzwa. Kipengele hiki kilidhihirisha kuafiki matumizi ya kawaida na pia matumizi yasiyo ya kawaida kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.





Mfano 4.1.2.1 Ukurasa huu umetolewa kutoka riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk.13

Katika mfano huu, herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa sentensi. Neno **Simba** katika sentensi **Simba yumo ndani ya nyumba ya Sungura** limeanza kwa herufi kubwa kama inavyokubalika kulingana na kaida za kiisimu.




Mfano 4.1.2.2 Ukurasa huu umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* ( Bracey &Lieta, 2009) uk. 18.

Katika mfano huo, sentensi **Wakati huo Mamba alikuwa amelala usingizi mzito,** neno wakati limeanza kwa herufi kubwa ambayo inakubalika kisarufi. Hata hivyo, neno **Mamba** vile vile limeanza kwa herufi kubwa  kuashiria dhima ya ukiukaji kwa kuwa linaitaja nomino ya kawaida.


hapo kando ya njia na bila kusita, wakaingia kwenye tundu hilo na kujificha. Paka na mkewe wakajaribu kuwafuata humo tunduni ili wawaangamize, lakini kwa vile mili yao ni mikubwa kuliko ya Panya, hawakuweza kuingia. Walirudi nyumbani wakiwa bado na hasira nyingi.


Waliapa kuwa, wataendelea kumtafuta Panya na familia yake na watakapokutana nao mahali popote pale, watawafanya kitoweo chao papo hapo.

Tangu siku hiyo, Panya akimwona Paka hutimua mbio za ajabu na kujificha ili kuokoa maisha yake.

18

Mfano 4.1.2.3 Ukurasa huu umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 18.

Katika aya ya mwisho **Tangu siku hiyo, Panya akimwona Paka hutimua mbio za ajabu na kujificha ili kuokoa maisha yake.** Sentensi hiyo imetangulizwa vyema kwa herufi kubwa mwanzoni katika neno **Tangu**. Hata hivyo maneno **Panya** na **Paka** katika sentensi hiyo yameanza kwa herufi kubwa kuashiria kuwa wanarejelewa kama majina ya wahusika na si wanyama wa kawaida kuonyesha ukiukaji katika matumizi ya herufi kubwa kwa kuwa wanyama wanaorejelewa ni nomino za kawaida.



Usicheze na moto!

Leo ni Jumamosi. Aliya, Aida, Dodo na marafiki zao wako nyumbani. Wao hawaendi shuleni. Leo ni siku ya kupumzika. Watoto hawa wako nje. Watoto hawa wanacheza mchezo wa **kibe**.

1

Mfano 4.1.2.4 Ukurasa huu umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 1.

Katika mfano huu, herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa sentensi na pia mwanzoni mwa majina **Aliya**, **Aida** na **Dodo** ambayo ni majina ya wahusika riwayani humo kuashiria ukawaida katika matumizi ya herufi hiyo. Matumizi haya ya herufi kubwa yanakubalika kisarufi kwa kuwa majina hayo yanarejelea nomino za pekee ambazo lazima zianze kwa herufi kubwa kiisimu..


yake mkononi. "Si amesema eti wezi hao walipitia barabara ya Songambele? Na ni gari la manjano?"

Dani aliketi tena akaangalia orodha yake ya magari. 'Najua kuwa nambari ya gari hilo lazima iwe kwenye orodha yangu,' Dani alijiambia tena. 'Hebu niangalie kwa makini.'

Alitazama karatasi hiyo kwa makini hasa sehemu ya rangi za magari huku akisema kimoyomoyo, 'Manjano, manjano, manjano.' Alipata rangi tano za manjano. Kisha akajiambia, 'Kati ya haya matano, nitatafuta gari aina ya Toyota.' Alianza kutafuta tena huku akiyataja magari hayo, "Subaru, Toyota, Toyota, Subaru, TOYOTA MANJANO. Ndilo hili gari waliloiba!" Dani alisema kwa sauti. "Baba, ndilo hili gari waliloiba!"

Dani alimfahamisha baba yake huku akimwonesha orodha hiyo, "Nambari zake ni KUUU 23445 U
Baba, hebu tuwapigie polisi simu. Nitawapa nambari ya gari

10

Mfano 4.1.2.5. Ukurasa huu umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.10.

Katika mfano huu, herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa sentensi na vilevile katika kutaja aina ya gari na nambari yake kama nomino nya pekee. Kimuktadha, herufi kubwa imetumika kwa njia ya kawaida kiisimu. Kutokana na mifano iliyotolewa, ni dhahiri kwamba kipengele cha herufi kubwa kinaweza kutumika kwa njia ya kawaida na vilevile kwa njia isiyo ya kawaida katika matini kama ilivyodhihirika katika riwaya zilizochunguzwa na katika fasihi ya watoto kwa ujumla.

Wataalamu Treiman na Kessler (2004) walifanya utafiti kuhusu utambuzi wa herufi kubwa miongoni mwa watoto vikembe. Walisema kwamba tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu utambuzi na matumizi ya herufi kubwa miongoni mwa watoto wadogo ziliegemea katika misingi ya kifonolojia. Utafiti wao uliegemea katika msingi usio wa kifonolojia na lengo la kubaini iwapo watoto wa umri mdogo wa gredi ya kwanza katika usomaji walikuwa na uwezo wa kuzitambua herufi kubwa katika shughuli zao. Utafiti

wao ulionyesha ya kwamba watoto wadogo wa kiwango cha gredi ya kwanza walidhihirisha uzoefu wa kuzitumia herufi kubwa mwanzoni mwa maandishi waliyoendeleza wakilinganishwa na matumizi ya herufi ndogo kimaandishi. Kwa hivyo kauli hii inaashiria ya kwamba ni kawaida kwa wanaowaandikia watoto kukiuka matumizi ya kawaida ya herufi kubwa.

Soile (2008), Chukwu (2010) na wengine vilevile walifanya utafiti kuhusu herufi kubwa na mazingira yanayodhibiti matumizi ya herufi kubwa. Hata hivyo Chukwu (k.h.t) aliweka wazi masharti yanayohitajika kuzingatiwa katika matumizi ya herufi kubwa katika matini. Masharti haya yanaweza kuangaziwa kama mihimili ya matumizi ya herufi kubwa kimaandishi kulingana na Chukwu (k.h.t). Anahoji ya kwamba ni lazima sentensi ianze kwa herufi kubwa katika lugha zozote zinazozungumzwa Duniani.

Pia anasema kwamba kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kokote ambako kitajitokeza ni lazima kiendelezwe kwa herufi kubwa pamoja na vyeo vinavyoshikiliwa na watu maarufu kama vile Profesa. Anaendelea kudokeza kwamba nomino zote za pekee zianze kuandikwa kwa herufi kubwa pamoja na herufi ya mwanzo katika salamu au anwani. Vilevile anasema ya kwamba usemi halisi lazima uanze kwa herufi kubwa. Anasema ya kwamba maneno yote yanayonuia kumwelezea Mungu, Kristo na Roho Mtakatifu pamoja na dini zote Ulimwenguni na maeneo ya Ulimwenguni kama vile Mashariki yaanze kuandikwa kwaherufi kubwa pamoja na herufi ya mwanzoni mwa anwani ya kitabu chochote au makala.

Riwaya tano zilizochunguzwa zilionyesha matumizi ya kawaida na vilevile matumizi yasio ya kawaida ya herufi kubwa. Maneno kama vile Simba, Sungura, Mamba, Mbuni, Panya, Paka na mengine ni miongoni mwa mifano ambayo kiisimu hujumlishwa katika

nomino za kawaida ambazo huanza  kwa herufi ndogo. Katika riwaya hizi, maneno hayo yameanza kwa herufi kubwa kokote yalipotumika riwayani kuashiria ukiukwaji wa matumizi ya herufi kubwa. Mtafiti Anantha (2014) aliita hali hii mkengeuko.

Leech na Short (1982) katika kujadili mhimili wa uteuzi katika fasihi wa nadharia ya umitindo walihoji kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza kuzikiuka kaida za kisarufi zilizozoeleka kwa sababu kadhaa na lengo la kutekeleza dhima fulani ambayo pia humuathiri msomaji kwa njia tofauti katika ufasiri wa maudhui yanayorejelewa kimatini. Katika kufanya hivyo, wanasema ya kwamba ndio sababu ya kuwepo matoleo mbalimbali ya kazi moja katika uandishi huku mifano inayorejelewa na iliyorejelewa awali ikitofautiana.

Kutokana na mawazo yanayoibuliwa na mhimili huu, inaonekana wazi kuwa mwandishi yeyote wa kazi za kifasihi, ikiwemo fasihi ya watoto ya Kiswahili ana uhuru na nafasi pana ya kukiuka sheria zilizoko za kisarufi katika ubunifu wake, hali inayomuibua kama mwandishi wa kipekee. Hii ni kusema ya kwamba utafiti huu unakubaliana na mawazo ya akina Chukwu (2010) na wenzake wanaozingatia matumizi ya kawaida ya herufi kubwa na vilevile unakubaliana na mawazo ya watalaam wenye mawazo kinzani kama vile akina Anantha (k.h.t) ambao wanaendeleza dhana ya mkengeuko katika matumizi ya vipashio vya kiisimu ikiwemo matumizi ya herufi kubwa katika ujenzi wa kazi bunilizi zikiwemo riwaya za watoto katika Kiswahili.

### 4.1.3 Matumizi ya picha na michoro

Mtindo wa picha na mchoro umezitawala riwaya zote tano teule zilizochunguzwa, huku picha hizo zikidhihirika kutoka kwenye sehemu ya jalada hadi ndani mwa matini, zikiwa

zimeendelezwa kwa rangi tofauti tofauti kama inavyojitokeza katika mifano mbalimbali iliyotolewa katika riwaya hizo zilizochunguzwa. Kulingana na Kluck (1972:8), picha au michoro katika fasihi ya watoto ni kipengele cha kimsingi kinachodhihirika katika ujenzi wa fasihi hiyo. Maoni yake yanashadidiwa na Wolfenbarger na Sipe (2007) wanaosema ya kwamba vitabu vyenye michoro huwakilisha upekee katika sanaa ya fasihi kimfumo kwa vile picha au mchoro unawahusisha wasomaji wachanga na watu wazima katika viwango vingi vya usomaji na ustaarabu.

Adam (2019) anadokeza kwamba kuna ushahidi unaodhihirisha ya kwamba wasomaji wachanga wanapenda sana na vilevile huchangamkia vitabu vilivyo na michoro au picha katika fasihi yao ikilinganishwa na matini isiyo na rasilimali hizi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya picha au michoro iliyozalishwa kutoka katika riwaya tano teule zilizochunguzwa.




Mfano 4.1.3.1 Hili ndilo jalada la riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012).

Katika jalada hili, kuna picha za wanyama Sungura, Simba, nyumba na mti katika mandhari maridadi, picha ambazo zimeendelezwa kwa rangi nyeupe, hudhurungi, buluu, kijani na kijani kibichi. Katika picha hii, Sungura anaonekana mwenye hofu kutokana na miondoko anayodhihirisha akielekea katika nyumba nzuri yenye paa ya rangi ya hudhurungi na kuta nyeupe na lengo la kuepuka hatari ya Simba anayemwandama. Huyo Sungura ameyakodoa macho kuashiria hofu fulani ndani mwake. Kando mwa nyumba hiyo nzuri kuna mti mkubwa huku mandhari ya mahali hapo yakionekana mazuri kutokana na rangi ya manjano ya nyasi na matawi ya miti iliyo nyuma ya nyumba. Katika jalada hilo la kuvutia, pia kuna majina ya waandishi na wachoraji wa riwaya hii na vilevile taasisi iliyokichapisha kitabu hiki. Kama anavyosema Adam (2019), bila shaka msomaji mchanga atachangamkia riwaya yenye jalada la kuvutia kama hili.




Mfano 4.1.3.2 Ukurasa huu umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk.1.

Katika picha hii, tunamwona Simba anayedondokwa mate akiwa amesimama chini ya mti mkubwa wenye matawi ya rangi ya manjano na chini yake, kuna nyasi yenye rangi ya manjano. Simba huyo anaonekana mwenye kuhisi njaa.




Mfano 4.1.3.3. Hizi picha zimetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) kur.2 na  3.

Picha ya kwanza inamwonyesha Sungura akiwa ameketi chini ya mti mkubwa akiwa ameliegemea jiwe akipumzika. Picha ya Sungura ni ya rangi ya hudhurungi huku vazi lake likiwa la rangi ya hudhurungi na mstari mweupe pembeni. Ile picha ya pili inaionyesha nyumba ya Sungura yenye ukuta mweupe, dirisha, mlango na paa yenye

rangi ya hudhurungi. Mandhari haya ni ya kuvutia kutokana na rangi ng'avu ambazo zimetumika. Picha hizi zina uwezo wa kuchochea hisia za msomaji kwa dhima ya kumhadaa kujinasibisha na riwaya zenye ufundi huu.





Mfano 4.1.3.4. Hili ndilo jalada la riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009).

Jalada hili limesukwa kwa rangi za samawati, manjano, kijani kibichi, nyeupe na hudhurungi.


Hata hivyo, kinachodhihirika zaidi ni picha ya Mamba na miondoko yake kwa miguu miwili pamoja na macho mekundu aliyoyakodoa. Jalada hili lina uwezo wa kumchochea

msomaji kutaka kujua kinachojiri katika matini kilichomfanya Mamba kudhihirisha miondoko isiyo ya kawaida katika ulimwengu wa wanyama wa pori.





Mfano 4.1.3.5. Hizi picha zimetolewa kutoka riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) kur.8 na 9.

Picha hizi zimezalishwa kutoka katika hadithi ya kwanza katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009) yenye kichwa *Sababu ya Mbuni kuwa na shingo ndefu*. Picha hizi zinaonyesha Mbuni akiwa katika shughuli za kukivuta kichwa chake kutoka kinywani mwa Mamba, huku Mamba akiwa amekibana kinywa chake.





Mfano 4.1.3.6. Hii picha imetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.10.

Katika picha hii, Mbuni amefaulu kujinasua kutoka kinywani mwa Mamba na amemwacha Mamba akiwa anahisi njaa tele.





Mfano 4.1.3.7. Hii picha imetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 11.

Katika picha hiyo, Mbuni ametimua mbio kutoka mahali alipokuwa ametekwa nyara; kinywani mwa Mamba baada ya kujinasua.





Mfano 4.1.3.8. Hii picha imetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) katika hadithi ya *Mayai ya Mamba* (Bracey & Lieta, 2009, uk.14 na uk.15).

Picha hizi zinaonyesha marafiki wawili ambao ni Mamba na Sungura wakishiriki mvinyo huku macho ya Mamba yakimuashiria kama ambaye tayari amelewa chakari kutokana na wekundu wa macho yake na vilevile kama alivyojisetiri. Macho ya Sungura yanaonekana kumakinika na kwa hivyo kutoathirika kwa vyovyote na mvinyo huo, kuashiria kuwa alikuwa hanywi chochote na kwamba alikuwa anamhadaa Mamba alewe chakari ili Sungura apate fursa ya kutekeleza uhaini fulani. Mamba alilewa na hatimaye akashikwa na usingizi akalala. Hali hiyo ilimpa Sungura nafasi ya kuiba na kula mayai yote ambayo Mamba alikuwa ameyataga.




Mfano 4.1.3.9. Hili ndilo jalada la riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006).

Hili ni jalada la riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006) ambako kuna picha za wanyama. Kundi moja la wanyama linaonekana limelala, kila wanyama wawili wawili katika vitanda viwili na kundi lingine linaonekana kuwa katika sherehe. Jalada limepambwa kwa rangi mbalimbali kama vile rangi ya samawati, rangi ya manjano, rangi nyeupe, rangi nyeusi na rangi ya hudhurungi, rangi ambazo pia zinadhihirika katika mavazi na malazi ya wanyama wanaowakilishwa na picha hizi. Bila shaka pambiko hili la jalada litamchochea msomaji mchanga kutaka kujua ujumbe uliyo katika matini ya aina hii.



Paka na Panya walichagua suti maridadi zilizowatosha kwa kipimo. Kila mmoja alijinunulia ile iliyovutia macho yake zaidi. Baada ya kutosheka, walimlipa Shangazi Twiga pesa zake na kuondoka.

Walipofika nyumbani, walizivaa tena nguo hizo ili kuwaonyesha wake na

11


Mfano 4.1.3.10. Picha hii imetolea katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk.11.

Katika picha hii, tunashuhudia marafiki wawili ambao ni Paka na Panya wakiyafanyia majaribio mavazi walioyanunua katika duka moja mjini, wakiwa katika jitihada za kujiandaa kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika harusi ya Mwanasungura. Mavazi hayo yanaonekana mazuri na ya kuvutia kutokana na mitindo yake pamoja na rangi zilizotumika katika ufundi wa kuyaunda. Rangi za madoadoa ya hudhurungi na nyeupe, suti zenye mistari myeusi na myeupe, rinda la samawati na nyeupe miongoni mwa rangi zingine za kuvutia zimetambulika.




Mfano 4.1.3.11. Picha hii imetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk.17.

Katika picha hiyo, Paka na mkewe wanawaandama Panya na familia yake kwa kasi baada ya Paka kugundua ya kwamba mavazi aliyoyanunua siku iliyotangulia katika jitihada za kujiandaa kuhudhuria harusi ya Mwanasungura, yalichanwa na Panya kwa kushirikiana na mkewe. Jambo hilo lilimdhoofisha Paka, akajawa na hamaki hivyo basi akaamua kumwandama Panya na lengo la kumuadhibu. Panya na familia yake walitoroka na kijificha katika vishimo vilivyokuwa pembeni mwa barabara.





Mfano 4.1.3.12. Hili ndilo jalada la riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003).

Katika picha hii, tunashuhudia harakati za wanajamii wakishirikiana kuuzima moto kwa njia zote. Wanajamii hao ni pamoja na wazazi wa watoto ambao kufuatia michezo yao, moto huo ulizuka na kuenea. Mavazi ambayo wanajamii hao wamevalia ni ya rangi mbalimbali za kuvutia.




Mfano 4.1.3.13. Picha hii imetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003:7)

Picha hiyo inaonyesha watoto wakishiriki mchezo wa upishi huku wakijaribu kuuasha moto. Watoto hao ni wa jinsia mseto ya kike na kiume, kuashiria uhalisia katika jamii, kutokana na rangi na mitindo ya mavazi yao. Kinachotumiwa kama sufuria yao ni mkebe uliotambulika waziwazi.





Mfano 4.1.3.14. Picha hii imetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003:18)

Picha hii inaashiria hasara ambayo imesababishwa na moto ambao ulienea wakati watoto walikuwa wakicheza mchezo wa kupika.




Mfano 4.1.3.15. Hili ndilo jalada la riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015).

Katika picha hii, tunamwona kijana mmoja akinakili ujumbe fulani katika daftari liliyo juu ya meza, na pia tunaweza kuliona gari lenye rangi nyekundu likiwa linapita barabarani. Mahali anakoishi yule kijana ni pembeni mwa barabara.





Mfano 4.1.3.16. Picha hii imetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015:14). Katika picha hii, tunashuhudia Dani akimkabidhi mamake aliyekuwa jikoni, gazeti ambalo lina ujumbe kuhusu taarifa ambayo Dani aliwasaidia polisi kunasa wezi waliokuwa wameliiba gari fulani lililotangazwa katika runinga.

Hii ni baadhi ya mifano ya picha ambazo mtafiti aliweza kuzikusanya kutoka katika riwaya tano zilizoteuliwa kimakusudi na kuchunguzwa. Aygün na Abaci (2014) wameelezea umuhimu wa picha na michoro kama vijenzi vikuu vya fasihi hususan katika fasihi ya watoto. Wanasema ya kwamba kwa ujumla, wakati picha na michoro hushirikishwa katika fasihi ya watoto, matukio mengi katika ukuaji wa watoto hudhihirika maishani mwao. Kulingana nao, ni matukio haya ambayo hujitokeza maishani mwa mtoto ambayo humpa maana maishani kwa kuwa mtoto hujifunza dhana mbalimbali, hupokea elimu na tajriba kuhusu maisha, kando na maadili na makatazo katika jamii. Wanashikilia ya kwamba ili mtoto aweze kujifahamisha na hadithi zinazosomwa na watu wazima, ni vyema ufahamu wao uimarishwe na picha na michoro. Mawazo yao yanashadidiana na yale yanayoshikiliwa na Schallert (1980), Kiefer (1993),

Mohr (2006), Cer (2016), Gallager (2018) na wengine ambao wanahoji ya kuwa fasihi ya watoto haikamiliki bila ya kuifungamanisha na picha au michoro.

Hata hivyo, kuna watafiti wengine ambao wanashikilia maoni kinzani na wanavyosema Abaci (2014) na wenzake. Kundi hili lenye maoni tofauti linajumuisha Peeck (1974), Beck (1984) Elster na Simons (1985), Marshall (1988), Goodman (2009) na wenzake. Kulingana nao, matumizi ya mandishi na picha au michoro katika matini huhitilafiana na ufasiri vyema wa ujumbe na msomaji kwa kuzua uhamaji wa ufasiri wa moja kwa moja.

Licha ya mawazo kinzani yanayoendelezwa na hawa watafiti, utafiti huu ulibaini ya kwamba matini njema ya kifasihi ni ile iliyowasilishwa kwa madhumuni ya kufasiriwa vyema na msomaji lengwa. Uwasilishwaji huo hata hivyo huathiriwa na ujuzi wa mwandishi wa kuweza kubuni kazi nzuri akidhihirisha matumizi mema ya vipengele mbalimbali vya kiufundi kimaandishi kutegemea kiwango cha wasomaji wanaolengwa. Kulingana na kiwango cha wasomaji wachanga wa gredi ya kwanza, gredi ya pili, gredi ya tatu na gredi ya nne zilizotafitiwa katika shule za msingi za umma nchini, picha au michoro ni viunzi vikuu vya fasihi ya wasomaji hao.

Kipengele hiki cha picha na michoro kinaafiki moja kwa moja mhimili wa kiwango cha grafolojia katika nadharia ya umitindo. Ni kipengele ambacho kinahusiana moja kwa moja na sura ya matini ambacho vilevile kinahusiana na uimarishaji wa ufasiri wa matini kifasihi. Kwa hivyo ni vyema kwa washikadau wote katika taaluma ya fasihi ya watoto na hususan, ya Kiswahili kuhakikisha ya kwamba wanashirikisha picha au michoro katika ujenzi wa matini zao kwa kuwa vipengele hizi vina dhima kuu na huwa na athari kubwa kwa msomaji.

### 4.1.4 Matumizi ya mandishi yenye rangi na wino tofauti

Baadhi ya wandishi wa riwaya tano teule zilizochunguzwa waliweza kuiendeleza kazi yao kwa kutumia rangi tofauti tofauti na ile ya kawaida kimaandishi. Katika uandishi wa kawaida, rangi nyeusi ndio hutumika kuandika katika karatasi ambayo kawaida huwa yenye rangi nyeupe. Matumizi ya mandishi yenye rangi tofauti na ya kawaida ilidhihirika katika riwaya zilizochunguzwa. Hali hiyo ilishuhudiwa sio tu katika ujaladishaji wa riwaya zilizochunguzwa bali pia katika picha na matini zenyewe katika riwaya teule.

Katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009), maneno kama vile: Hadithi Sisimka, Hadithi za mamba na sasa sema (uk.i), Mafunzo, Umoja, Wingi (uk.46) na Maswali (uk.47) yaliendelezwa kwa rangi nyekundu na samawati kama ilivyojitokeza katika mwendelezo wa mifano hii. Katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006), maneno: Harusi ya Mwanasungura, Gichohi Waihiga (uk.i), Walipendana kama chanda na pete (uk.1), furi (uk.2), tafrija (uk.3), ukarimu, sebuleni (uk.4), kifunguamimba (uk.5), mwaliko (uk.7), walirauka (uk.8), wageni waalikwa, tafrija (uk.12), aliduwaa, ukazuka (uk.16), maneno yaliyofafanuliwa katika jedwali lenye anwani sherehe (uk.19-20), zoezi (uk.21) vilevile yameendelezwa kwa wino wekundu uliotumiwa kuitaja mifano hii.

Riwaya ya *Usicheze na Moto* (2003) ina maneno Usicheze na moto (uk.i) na tena Usicheze na moto (uk.1) yakiwa yameandikwa kwa rangi za manjano na samawati mtawalia. Katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) maneno kama vile Dani na Wezi wa Toyota, sasa sema (uk.i), vibonzo (uk.2), sebuleni, kisengeretua, magazeti makuukuu (uk.3), shingo upande (uk.7), vipuri, wakaliteka nyara (uk.9), takribani (uk.13) na kachero (uk.15) yameandikwa kwa wino mwekundu. Vilevile katika riwaya hii, taarifa ya walinda usalama kuhusu wizi unaorejelewa riwayani imeandikwa kwa ukurasa wenye

rangi ya manjano huku msaada alioutoa Dani katika jitihada za kuwanasa wezi hao nao ukiandikwa kwa ukurasa wenye rangi ya samawati. Vilevile maneno magumu yaliyoorodheshwa katika ukurasa wenye rangi ya samawati katika (uk.17) yametajwa kwa rangi nzito ya samawati.

Kwa hivyo, rangi zilizotumika katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012) ni nyeupe, nyekundu, manjano, kijani kibichi, nyeusi, samawati na hudhurungi. Katika *Hadithi za Mamba* (2009), rangi za samawati, nyeusi, nyekundu, manjano, kijani kibichi na hudhurungi zimetumika. Riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006) imesukwa kwa matumizi ya rangi za samawati, manjano, nyekundu, nyeusi, nyeupe na hudhurungi. Katika *Usicheze na Moto* (2003), rangi ambazo zimedhihirika ni manjano, kijani kibichi, nyeusi, hudhurungi, samawati nyeupe na waridi. Katika *Dani na Wezi wa Toyota* (2015), rangi nyekundu, samawati, waridi, nyeusi, kijani kibichi, nyeupe na manjano zimetumika. Kipengele cha rangi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia kimezungumziwa na watalaam wengi wakiwemo Cass (1967), Kluck (1972), Ruthiiri (2012), Yu 92014), Olurino na Tayo (2015). Kulingana na mchango wao, rangi ni kiunzi muhimu katika kazi za fasihi andishi hususan fasihi inayowalenga watoto. Yu (k.h.t) amesema ya kwamba rangi ndio msingi wa ishara zinazotazamwa ambazo hutegemewa sana katika mawasiliano.


Utafiti huu vilevile unashadidia mawazo ya watalaam waliotajwa kwamba, rangi ni miongoni mwa vipengele vinavyotekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano katika matini kwa kuwa kutegemea msingi wa msomaji kiitikadi, yeye huifasiri dhima mbalimbali ya rangi iliyotumika katika ujenzi wa matini, kabla ya kuyasoma makala. Hii ni kusema kwamba rangi ni kipengele cha kigrafolojia. Kipengele hiki kinaafiki mhimili

wa uchimuzi wa nadharia ya umitindo. Leech na Short (1982) waliujadili mhimili huu walipokuwa wakielezea mtindo na ubora katika uchimuzi wa matini. Walisema ya kwamba kuna vigezo mbalimbali ambavyo mwandishi wa matini anaweza kuvitumia katika kuiendeleza kazi yake ambavyo kando na kudhibitiwa na kiwango cha kisemantiki, vilevile huhusiana na viwango vingine vya kiisimu kama vile sinkaksia na fonolojia vinavyoibua ukamilifu wa lugha. Wanaendelea kusema ya kwamba kwa kuwa fasihi katika ukawaida wake inahusiana na uandishi, kiwango cha grafolojia ni mwafaka kwa vile lugha ni msimbo, msimbo huo ni lazima uendeleze ubunifu wa watumiaji ambao wana utamaduni unaojulikana waziwazi kuhusu kila shughuli yao, baadhi ya shughuli hizo zikiweza kurejelewa kwa ishara fulani.

Rangi ni mojawapo za ishara za kibinadamu. Kipengele cha rangi katika ukawaida wake kinatumika kuashiria na katika uashiriaji huo, maana lengwa hudhihirika na kuwasilishwa kimatini, hali ambayo huwa imechimuzwa. Rangi zimeainishwa na watalaamu waliotajwa huku zingine zikijitokeza kama zenye kuwasisimua wasomaji na zingine zikiwa rangi zenye kuweza kuwaogofya wasomaji.


### 4.1.5 Taipografia, nafasi kati ya mistari na aina ya fonti

Fonti mbalimbali zilidhihirika kutumika katika ujenzi wa riwaya tano teule zilizochunguzwa kama ilivyo katika mifano inayofuatia.





Mfano 4.1.5.1 umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012:28).

Katika mfano huu, aina ya fonti iliyotumika ni *Sans- Serif Futura Md BT* yenye ukubwa wa pika ishirini na nne na nafasi kati ya mistari wa milimita tano huku uwazi kati ya maneno ukiwa milimita tatu. Vilevile kuna nafasi inayodhohirika kati ya alama ya kiakifishi na neno linalofuatia ambao ni wa milimita tatu.


Huyu ni Mamba.
Mamba huishi mtoni.
Hupenda kulala ukingoni mwa mto.
Anapenda kulala juani.

Mamba ni mnyama mlafi sana.
Anapenda kula nyama nyingi.
Huwala mbuzi na ng'ombe.
Waendapo mtoni kunywa maj
Mamba huwashika na kuwal

Mfano 4.1.5.2. umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009:2). Aina ya fonti iliyotumika katika mfano huu ni *Sans- Serif Futura Md BT* ya pika ishirini na nne yenye nafasii kati ya mistari wa milimita tano na nafasi kati ya maneno wa milimita tatu.



na Panya hawakupata usingizi vizuri. Waliota mbalimbali kuhusiana na harusi hiyo.


Kila mmoja alijiona akiwa mbele ya halaiki kubwa ya wageni waalikwa huku akiongoza sherehe ya harusi.

Katika ndoto hizo, walijiona wakiongoza tafrija za jioni huku wakishangiliwa kwa nderemo na vifijo

12

Mfano 4.1.5.3. umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 12.

Aina ya fonti hii ni *Sans- Serif Futura Md BT* pika ishirini na nne. Nafasi kati ya mistari ni milimita tano na nafasi kati ya maneno ni wa milimita tatu.




Wakati wanasubiri viazi viwe tayari, watoto walicheza michezo mingine. Wengine wao waliruka kamba. Wengine wanacheza gololi.
Wengine wanacheza mchezo wa kubahatisha shilingi imefichwa mkono upi. Watoto wote walifurahia michezo hii yao.

8

Mfano 4.1.5.4. umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 8.

Aina ya fonti iliyotumika katika mfano huu ni *Sans- Serif Times New Roman* pika kumi na mbili. Nafasi kati ya mistari ni milimita nane na uwazi kati ya maneno ni milimita mbili. Vilevile kuna nafasi kati ya neno na alama ya kiakifishi ambao ni milimita tatu.



… pamoja na jina la mtaa unamoishi," askari alimwomba Dani.

Dani alimpa askari habari zote na maelezo zaidi kuhusu jinsi alivyopata nambari hizo za magari. Baada ya shughuli hiyo, aliizima simu akamrudishia baba yake. Aliketi akaendelea kuitazama orodha yake.

Mama alimwuliza, "Je, Dani, ulipata wapi orodha ya nambari hizo?"

"Mliponiacha hapa, nilibuni mchezo wangu wa kuandika nambari za magari yaliyopita barabara hii," alisema Dani. "Hii hapa," alimkabidhi mama yake orodha hiyo.

11

Mfano 4.1.5.5. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 11.

Aina ya fonti iliyotumika katika mfano huu ni *Sans- Serif Times New Roman* pika kumi na mbili. Nafasi kati ya mistari unaodhihirika katika mfano huu ni milimita nane ilhali ile nafasi kati ya maneno ni milimita mbili.

Hii ni baadhi ya mifano ya fonti mbalimbali na nafasi kati ya mistari na maneno iliyotumika katika riwaya teule zilizochunguzwa. Kwa hivyo inadhihirika kuwa fonti zilizotumika katika ujenzi wa riwaya zilizochunguzwa ni *Sans- Serif Futura Md BT* yenye ukubwa wa pika ishirini na nne na nafasi kati ya mistari wa milimita tano na nafasi

kati ya maneno ukiwa milimita tatu katika riwaya za *Nyumba ya Sungura* (2012), *Hadithi za Mamba* (2009) na *Harusi ya Mwanasungura* (2006) na *Sans- Serif Times New Roman* pika kumi na mbili ya nafasi kati ya mistari wa milimita nane na uwazi kati ya maneno wa milimita mbili katika riwaya za *Usicheze na Moto* (2003) na *Dani na Wezi wa Toyota* (2015). Yadav, Chakrabarti na Bisoyi (2014) wamezungumzia taipografia kama mtindo katika ufundi ambapo wamejadili aina mbalimbali za taipografia na matini ambamo taipografia hizo hutumika. Wanasema kuwa uamuzi wa aina ya fonti itakayotumika katika maandalizi na uchapishaji wa matini hutegemea hadhira inayolengwa kusoma matini hayo. Wanapendekeza fonti ya *Sans- Serif* yenye pika kubwa kwa wasomaji wachanga kama ilivyotumika katika uchapishaji wa riwaya zilizochunguzwa. Matokeo haya basi yanalingana na maoni ya Yadav, Chakrabarti na Bisoyi kwamba matini zinazolenga wasomaji wachanga yatumie pika kubwa ya fonti ya *Sans- Serif*.


Kipengele hiki cha fonti kimefungamana n a mhimili wa nadharia ya umitindo wa kiwango cha grafolojia unaozungumzia usukaji wa matini kimaandishi kama anavyoeleza Wamitila (2008). Kulingana naye, ufundi wowote wa matini andishi ni lazima uzingatie taipografia kwa kuwa kutokana na taipografia, matini inaweza kuandikwa, kusomeka na kufasiriwa vyema kutegemea kiwango cha wasomaji wanaolengwa na mwandishi. Ni kwa hali hii ndiposa aina mbalimbali ya vipengele vya taipografia vilitumika, huku uwazi mpana ukishuhudiwa miongoni mwa riwaya zilizowalenga masomaji chipukizi wa gredi ya kwanza, ya pili na ya tatu katika shule za msingi za umma.

Matokeo haya yanawiana na mawazo yaliyopendekezwa na Yadav na wenzake (2014) na Azizović Fetić (2014) miongoni mwa wataalamu waliotafiti kuhusu taipografia kwa

kuwa fonti ya *Sans- Serif Futura Md BT* yenye ukubwa wa pika ishirini na nne na nafasi kati ya mistari ya milimita tano na nafasi kati ya maneno ikiwa milimita tatu ilitumika katika uchapishaji wa riwaya zilizowalenga wasomaji wachanga mno, wasio na tajriba yoyote ya usomaji huku *Sans- Serif Times New Roman* pika kumi na mbili ya nafasi kati ya mistari wa milimita nane na uwazi kati ya maneno wa milimita mbili ikitumika kwa wasomaji ambao wako na tajriba ya usomaji.


### 4.1.6 Matumizi ya mkolezo katika matini ya fasihi ya watoto

Data aina ya mkolezo pia iliweza kukusanywa. Katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009) ambayo ina hadithi tatu, anwani tatu za hadithi hizo zimekolezwa kama inavyodhihirika kupitia kwa mifano inayofuatia.





Mfano 4.1.6.1 umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.1.

Anwani iliyokolezwa ni **Sababu ya Mbuni kuwa na shingo ndefu.**





Mfano 4.1.6.2 umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.12. Anwani ya hadithi iliyokolezwa ni **Mayai ya Mamba.**




Mfano 4.1.6.3 umetolewa katika katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.32.

Anwani ya hadithi iliyokolezwa ni **Mamba na moyo wa Nyani** (uk.32).

Katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006), mkolezo umejitokeza katika faharasa katika neno **Sherehe** kama inavyoonekana hapa na vilevile neno hilo pia limeendelezwa kwa rangi nyekundu..


Sherehe

1. walipendana kama chanda na pete : Waliper


2 furi : Hali ya kujaa s

3. tafrija : Shughu kufura fulani;


ukarimu : Moyo kumpo

sebuleni : Katik

Mfano 4.1.6.4. umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 19.





Mfano 4.1.6.5. umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 21. Neno lililokolezwa ni **Zoezi** kama inavyodhihirika hapo na pia limeendelezwa kwa rangi nyekundu.





Mfano 4.1.6.6. umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (2003) uk.1.

Maneno yaliyokolezwa ni **Usicheze na moto!.**





Mfano 4.1.6.7. umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003 uk. 25).

Maneno ambayo yamekolezwa ni **Kamusi yangu.**




Mfano 4.1.6.8. umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 26 pia una neno **Maswali** ambalo limekolezwa.



Dani Asaidia Polisi Kunasa Wezi wa Toyota.

Mtoto wa miaka kumi amewasaidia polisi kuwanasa we
walioiba gari aina ya *Toyota Corolla NZE* hapo jana. Mto
uyu, Dani Makini, ni mwanafunzi wa darasa la tano kat
hule ya Msingi ya Hekima. Dani alijibunia mchezo
andika nambari za magari jana alipokuwa ameac
umbani peke yake. Aliubuni mchezo huu baada ya k
ovu kwa kukosa la kufanya nyumbani. Kwa hivyo alit
ya kujiburudisha. Mchezo ulihusu kuandika ai
ari, nambari zake na rangi ya kila gari lililopita ba
ongambele kati ya saa tano na saa tisa.

Wakati huo huo, majambazi hao walikuwa wakite
ndo cha wizi wa Toyota kwa kuliteka nyara g
shuhudia walisema kuwa wezi hao walitorokea b
ngambele.

huyu alipata habari za wizi huo jana jio

Mfano 4.1.6.9. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.13. Maneno yaliyokolezwa ni **Dani Asaidia Polisi Kunasa Wezi wa Toyota.**

Mkolezo ni kipengele chenye umuhimu katika uandishi kama wanavyoeleza watalaamu Macaya na Perea (2014), Yehudah na Alkalai (2017) na wengine. Wataalamu hawa wamejadili jinsi mkolezo unavyotumika katika maandishi na uchapishaji wa makala kutekeleza dhima mahususi na pia athari anayokuwa nayo msomaji wa matini ambamo mkolezo huwa umetumika. Kipengele cha mkolezo kama kiunzi cha mandishi kinaafiki


mhimili wa uchimuzi kifasihi katika nadharia ya umitindo. Imedhihirika kuwa waandishi wanatunga kazi zao, ni maneno machache tuu ambayo hukolezwa, kuashiria uchimuzi.

Leech na Short (1982) walizungumzia uchimuzi kwa kumrejelea Halliday na shule ya mawazo ya Prague. Walisema kuwa wakati mwingine mwandishi hukiuka kaida za uandishi kwa kukusudia kwa lengo la kukifanya kifungu au neno fulani lionekane zaidi ya mengine katika matini. Walidai kuwa hilo ni tukio la kiakili ambalo humuathiri msomaji katika ufasiri wa ujume uliyomo katika matini, na kwamba uchimuzi unaweza kuwa wa ubora au wa idadi. Uchimuzi unaojitokeza katika mkolezo huu ni wa ubora.

Mhimili wa uchimuzi unajadili jinsi maneno mengine katika matini yanavyoyavutia macho ya msomaji moja kwa moja na kuyafanya maneno hayo kuonekana zaidi ya mengine. Mkolezo unapotumika katika mandishi, bila shaka neno au maneno ambayo huwa yamekolezwa huonekana kwanza zaidi ya yale mengine katika matini. Hali hiyo humwathiri msomaji katika kuufasiri ujumbe ambao huwa umelengwa kuwasilishwa na mwandishi. Wamitila (2008) anaielezea hali hii kama sifa ya matumizi ya lugha ambayo vile vile inategemea kiwango cha ubunifu wa mwandishi. Kwa kukoleza maneno mengine katika matini zilizochunguzwa, waandishi walilenga kuwasiliana na wasomaji kwa njia isiyo ya kawaida.

### 4.1.7 Matumizi ya mandishi yenye mlazo katika fasihi ya watoto

Kipengele cha mlazo kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia kilitumika kwa mapana katika ujenzi wa riwaya. Hata hivyo, ni mojawapo tu ya riwaya teule iliyochunguzwa iliyoshuhudia matumizi mapana ya *mlazo* ambayo ilikuwa ni riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) kama inavyodhihirika katika mifano kadhaa inayofuatia.



heri niziandike nambari za kila gari na aina ya gari na rangi yake. Nitaweza kufahamu magari wanayopenda Wakenya.' Alitabasamu. 'Sasa nimepata mchezo mzuri wa kunisaidia kupitisha wakati kabla Shangazi Wumi hajaja.' Dani alianza kufikiria kama mwanatakwimu.

Alichukua kalamu, karatasi na rula kutoka mezani. Alichora mistari mitatu kuanzia juu hadi chini. Katika kila mstari aliandika: *Aina ya Gari, Rangi na Nambari za Gari.*

Alipomaliza, aliitazama karatasi hiyo kisha akasem
'Sasa niko tayari kuanza mchezo wangu.'


Dani alijiweka tayari karibu na dirisha mahali amba
angeweza kuona vizuri nambari zote za magari. Kila
lililopita, aliandika aina yake:... Toyota, Subaru, Su
na kadhalika. Alifanya kazi hii kwa makini.

Wakati mmoja alijiambia, 'Na hawa Wakenya
apenda magari meupe. Mimi nitanunua gari je

5

Mfano 4.1.7.1 umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 5

Maneno yaliyolazwa kama inavyodhihirika ni *Aina ya Gari, Rangi na Nambari za Gari.*


Dani Asaidia Polisi Kunasa Wezi wa Toyota.


oto wa miaka kumi amewasaidia polisi kuwanasa wezi oiba gari aina ya *Toyota Corolla NZE* hapo jana. Mtoto , Dani Makini, ni mwanafunzi wa darasa la tano katika e ya Msingi ya Hekima. Dani alijibunia mchezo wa dika nambari za magari jana alipokuwa ameachwa bani peke yake. Aliubuni mchezo huu baada ya kuhisi u kwa kukosa la kufanya nyumbani. Kwa hivyo alitafuta a kujiburudisha. Mchezo ulihusu kuandika aina ya , nambari zake na rangi ya kila gari lililopita barabara gambele kati ya saa tano na saa tisa.

kati huo huo, majambazi hao walikuwa wakitekeleza cha wizi wa Toyota kwa kuliteka nyara gari hilo uhudia walisema kuwa wezi hao walitorokea barabar mbele.

habari za wizi huo jana jioni kupi

Mfano 4.1.7.2. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 13.

Maneno yaliyolazwa ni *Toyota Corolla NZE* ambayo pia yameendelezwa hivyo katika uk.13.



Maswali
. Kwa nini Dani akaachwa nyumbani peke yake?
Je, Dani ni kijana wa miaka mingapi?
Je, Dani aliishi mtaa gani?
Dani alikuwa anamngojea nani aje saa tisa?
aada ya kuona vibonzo alienda wapi?
ani aliamua kufanya nini ili kupoteza wakati?
hezo huo ulisaidia polisi kwa njia gani?
i hao walikuwa wanatorokea nchi gani?
aweza kuzitambua nchi hizi ukizipanga
herufi hizi? - *gadanu, niatanza*.
zo gani tunapata kutoka kwa hadithi hii?

Mfano 4.1.7.3. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.16

Maneno yaliyolazwa ni – *gadanu, niatanza*. Wataalamu mbalimbali wamezungumzia kipengele cha *mlazo* katika uandishi. Farkas (1983) alijadili kwa kina kuhusu alama ya kudondoa na ya *mlazo* katika uandishi, huku akikiri kuwa alama hizi zinatekeleza dhima muhimu katika uandishi, ambayo vile vile huathiri ufasiri wa maudhui yanayowasilishwa kimatini. Wandishi wa riwaya zilizochunguzwa pia waliutumia ufundi huu katika uenendelezaji wa kazi zao kupitia kwa mifano iliyotolewa. Kulingana na mhimili wa

kiwango cha kigrafolojia wa nadharia ya umitindo, maandishi hutekeleza dhima ya kuwasilisha ujumbe na kilicho muhimu ni jinsi ujumbe unavyowasilishwa.

Wamitila (2008) katika kuzungumzia mhimili wa kiwango cha kigrafolojia wa nadharia ya umitindo, anasema kuwa mhimili huu unahusiana na uandishi kwa ujumla. Anadai kuwa kupitia kwa maandishi yaliyolazwa, mwandishi huchochea hisia fulani za msomaji kisaikolojia ambazo msomaji anazizingatia katika jitihada zake za kuufasiri ujumbe uliolengwa na mandishi yaliyolazwa. Hata hivyo, anasema kuwa hii pia ni sehemu ya ufundi kimandishi ambao hutumiwa na wandishi wakiwemo wa fasihi ya watoto ya Kiswahili kama ilivyodhihirika. Kwa hivyo *mlazo* katika matini zilizochunguzwa ulitumika kushika makini ya msomaji na pia kudhihirisha ujuzi wa ufundi wa matini.


### 4.1.8 Miundo mbalimbali ya aya katika matini ya fasihi ya watoto

Data ya miundo mbalimbali ya aya iliyotumika katika ujenzi wa matini zilizofanyiwa uchunguzi iliangaziwa. Hata hivyo, baadhi ya riwaya zilionekana kuzingatia miundo ya kawaida ya aya, huku zingine zikionekana kukiuka ukawaida huo kama inavyodhihirika kupitia kwa mifano inayofuatia.

**Simba. Simba. Njoo hapa.**


**Mfano 4.1.8.1**. umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 14.

Mfano huo umechukua nafasi ya aya kama ilivyo katika matini, lakini kiisimu, huu ni mfano wa sentensi. Hata hivyo, huu ni ukiukaji wa muundo wa aya katika uandishi uliyozoeleka.




Mfano 4.1.8.2. umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 3.

Hii ni aya ambayo imeundwa kwa sentensi moja sahili. Wali na Madani (2020) wanazungumzia umuhimu wa aya katika uandishi. Wanataja kuwa urefu wa aya unategemea mwandishi na wanatoa mwanga kwamba aya inaweza kuwa na sentensi moja au hata ukurasa mzima, lakini kilicho muhimu ni kuwepo kwa mshikamamo na muwala katika aya hiyo.




Huyu ni Mamba.
Mamba huishi mtoni.
Hupenda kulala ukingoni mwa mto.
Anapenda kulala juani.

Mamba ni mnyama mlafi sana.
Anapenda kula nyama nyingi.
Huwala mbuzi na ng'ombe.
Waendapo mtoni kunywa maji,
Mamba huwashika na kuwala.

2

Mfano 4.1.8.3.umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 2. Mfano ulioyo hapo juu una aya mbili kama inavyoonekana waziwazi. Aya hii imechukua umbo la beti mbili katika utanzu wa ushairi aina ya tarbia ambalo huwa na mishororo minne katika kila ubeti ambalo ni dhihirisho la ukiukaji wa muundo wa uandishi wa kawaida wa riwaya. Hii ni kwa kuwa ya hizi mbili zimetumia lugha ya mkato, kando na kusheheni idadi ya sentensi nne katika kila aya, kuashiria usambamba. Ufundi huu hudhihirika zaidi katika tanzu za kishairi kifasihi na ni ufundi wa kawaida katika utanzu wa riwaya. Huu nin ukiukaji katika uandishi wa kawaida.



Hapo zamani za kale, Paka na Panya walikuwa marafiki wakubwa. Walipendana kama chanda na pete. Hata waliishi katika nyumba moja wakiwa na familia zao. Kijiji walimoishi kiliitwa Chanjara, na kilikuwa karibu na mji wa Sokoni.

Mara kwa mara wakiandamana n
wake na watoto wao, walikwend

1

Mfano 4.1.8.4. umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006, uk. 1).

Katika mifano ya aya hizi, aya ya kwanza haijajongezwa lakini katika mfano wa aya ya pili, ujongezi umedhihirika kuashiria ukiukaji wa kiisimu.



peke yake. Kila siku mama na baba ... kuondoka kwenda kazini, mama alimtahadharisha Dani kwa kumwambia, "Funga lango vizuri, kisha uufunge mlango wa nyumba. Kwa vyovyote vile, usimfungulie mtu yeyote atakayebisha isipokuwa mimi au baba yako. Pia usitoke nje ovyoovyo."

Mama alifahamu kuwa wakati kama huu wa likizo, wezi hutembea kila mahali wakitaka kuiba.

Dani alimwambia mama, "Ah, mama wee, ısiwe na vasiwasi hata idogo.

1

Mfano 4.1.8.5. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi na Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 1.

Katika riwaya hii, kuna aya ambayo imeundwa kwa sentensi moja ambayo ni: **Mama alifahamu kuwa wakati kama huu wa likizo, wezi hutembea kila mahali wakitaka kuiba.**

Hii ni baadhi ya mifano ya aya iliyotolewa kutoka katika riwaya zilizochunguzwa. Wataalamu kadhaa wakiwemo Wali na Madani (2020) wamezungumzia kipengele cha aya katika uandishi. Wamedai ya kwamba kwa kuwa maandishi ni mojawapo ya nyenzo

ambamo mawasiliano hutekelezwa katika jamii, mrundiko wa maandishi pasipo na utaratibu wowote hauendelezi mawasiliano. Wanasema kwamba ni vyema ikiwa maandishi yatavishirikisha vipengele vingine vya uandishi vikiwemo aya zenye miundo iliyokubalika ili maandishi hayo yaweze kuwasilisha ujumbe bila kuzua utata wowote. Wanasema ya kuwa maandishi ni kama binadamu ambaye anahitaji umoja na ushirikiano wa kina ili mawasiliano yakamilike.

Miundo mbalimbali ya aya imedhihirika katika matini zilizochunguzwa, huku kukishuhudiwa aya kama vile ya maneno manne, aya ya sentensi moja na pia aya ya sentensi kadhaa. Castillo na Mongui (2011) wamefafanua aya kama mkusanyiko wa sentensi zenye uhusiano fulani kimaudhui. Kulingana nao, kujitokeza kwa aya yenye maneno manne na nyingine iliyojengeka kwa sentensi moja ni dhihirisho la ukiukaji kwa kuwa wanabainisha aina tatu ya aya ambazo ni aya za kimaelezo, aya za mfichuo na aya fuatilizi ambazo vijenzi vyake ni vikubwa kuliko maneno manne na sentensi moja. Linalojitokeza ni kwamba aina hizi za aya zilitumika katika ujenzi wa riwaya tano teule kwa vile viwango lengwa vya wasomaji vilitofautiana. Hii ni kusema ya kwamba aya ya maneno machache iliwalenga wasomaji chipukizi kama vile wa gredi ya kwanza na ya pili ilhali ile aya iliyojengeka kwa sentensi ambatani na labda changamani iliwalenga wasomaji wa gredi ya tatu na gredi ya nne kwa kuwa tayari walikuwa na ufahamu na usomaji.

Hata hivyo kipengele hiki cha aya kinashadidiana na mhimili wa muwala na mshikamano katika nadharia ya umitindo. Akitoa maelezo kuhusu mhimili huu wa nadharia ya umitindo, Wamitila (2008) alisema kuwa muwala unahusu sifa za kiisimu zinazoonyesha jinsi maneno, virai, vishazi au sentensi zinavyohusiana katika matini huku mshikamano

ukihusiana na maana ya usemi. Simpson katika Leech na Short (2007) alisema kuwa viwango hivi hudhihirisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu na ndio msingi wa nadharia ya umitindo. Kipengele cha aya kinahusu viwango vya kifonolojia na sintaksia ambapo sentensi zinaunganishwa na kuunda vipashio vingine vikubwa kuliko sentensi. Alisema kuwa muwala na mshikamano humwezesha msomaji kupata vyema ujumbe ulionuiwa kuwasilishwa na mwandishi.

### 4.1.9 Kipengele cha kipimo au ukubwa wa riwaya katika fasihi ya watoto

Ukubwa wa riwaya ni kipengele mahususi cha kigrafolojia na pia cha uandishi kwa jumla kutegemea wasomaji waliolengwa na mwandishi. Riwaya teule ambazo zilichunguzwa na kuzalisha data ya kipengele cha kipimo cha ukubwa wa riwaya zilidhihirisha kujengeka kwa kati ya kurasa kumi na nane na kurasa arobaini na saba. Riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012) ina kurasa thelathini (30), riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009) ina jumla ya kurasa arobaini na saba, riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006) ina kurasa ishirini na mbili, riwaya ya *Usicheze na Moto* (2003) ina kurasa ishirini na sita ilhali riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) ina kurasa kumi na nane. Riwaya hizi zina kurasa chache zikilinganishwa na riwaya za watu wazima kama vile riwaya ya *Mkamandume* (2013) yenye kurasa mia tano (500) na vilevile riwaya ya *Mbali na Nyumbani* (2012) yenye kurasa mia tano na moja (501), labda kwa kutaja tu baadhi ya riwaya kubwa katika utanzu wa fasihi andishi ya Kiswahili.


Cass (1967), Ewers (1980), Nikolajeva (1995) na wengine wamechangia pakubwa kuhusiana na dhana na taaluma ya fasihi ya watoto. Katika mijadala yao, wameweza kuainisha bayana sifa ya fasihi ya watoto. Mojawapo ya sifa inayodhihirika katika

mijadala hiyo ni sifa ya ufupi wa matini. Ingawa wataalamu hawa hawajaijadili sifa hii moja kwa moja, wameeleza kuwa kazi nzuri iliyoandikiwa watoto ni ile ambayo inaweza kusomwa kwa kipindi kifupi. Ingawa sifa ya kipindi kifupi inaweza kuleta utata, cha msingi ni ule muda ambao mtoto anajitolea kusoma kwa kumakinikia anachokisoma.

Wanasaikolojia, akiwemo Pan (2012) wamedhihirisha ya kwamba watoto wana uwezo wa kusoma kwa makini kwa muda wa dakika chache, na baada ya muda huo kuathirika na yale wanayoyasoma. Ni kwa sababu hii ambapo riwaya zilizochunguzwa zilionekana kujengeka kwa kurasa chache ili wasomaji waliolengwa waweze kuzisoma na kuufasiri vyema ujumbe uliomo bila ya changamoto nyingi. Kwa hivyo utafiti huu unakubaliana na kipimo cha ukubwa wa riwaya kama ilivyodhihirika katika mifano. Pia unaafiki mhimili wa nadharia ya umitindo wa kiwango cha grafolojia unaohusika moja kwa moja na uandishi kwa jumla. Lililo muhimu ni kwamba bora huo uandishi uweze kubeba ujumbe ambao wasomaji wanaolengwa wana uwezo wa kuufasiri ipasavyo ili mawasiliano yawe yameendelezwa kwa njia iliyotarajiwa.


### 4.1.10 Kipengele cha umbo la matini katika fasihi ya watoto

Vipengele vya umbo la matini vilivyodhirika ni msamiati mwepesi na sentensi sahili katika riwaya za *Nyumba ya Sungura* (2012), *Hadithi za Mamba* (2009), *Harusi ya Mwanasungura* (2006) na *Usicheze na Moto* (2003) isipokuwa katika riwaya moja ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015). Riwaya nne zilizotajwa awali zilisukwa kwa umbo sahili kimsamiati na kisentensi kama inavyojitokeza katika mifano inayofuatia.





Mfano 4.1.10.1. umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 16.

Msamiati uliotumika katika mfano huu unaoiwakilisha riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012) ni mwepesi na pia sentensi zinazodhihirika ni sahili.




Mfano 4.1.10.2. umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 18.


Msamiati uliotumika katika mfano huo ni mwepesi na vilevile sentensi zinazodhihirika katika riwaya hii nzima ni sentensi sahili.



Hapo zamani za kale, Paka na Panya walikuwa marafiki wakubwa. Walipendana kama chanda na pete. Hata waliishi katika nyumba moja wakiwa na familia zao. Kijiji walimoishi kiliitwa Chanjara, na kilikuwa karibu na mji wa Sokoni.

Mfano 4.1.10.3. umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006) uk. 1.


Msamiati uliotumika katika mfano huu ni mwepesi na vilevile sentensi zinazodhihirika ni sahili.


Upepo mkali ulivuma. Ulielekea upande wa chakula
kilichokuwa kikipikwa. Upepo huo ulisababisha cheche za
moto wa kuni kuruka. Cheche zile ziliruka mpaka kwenye
ghala. Ghala lilianza kushika moto. Watoto hawakuuona
kamwe moto ulioanza.

1

Mfano 4.1.10.4. umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 11.

Katika mfano huo, msamiati mwepesi na vilevile sentensi sahili zinaonekana kama zilivyotumika riwayani.



aina ya Toyota umezidi. Natumai utaendelea na mchezo wako wa kumakinika na huenda siku moja utakuwa kachero. Labda wewe ndiwe utakayekomesha wizi wa magari hapa nchini," mamake alimweleza.

"Kweli mama?" Dani alimwuliza mamake kwa furaha.

"Kweli mwanangu," mamake alimjibu. "Kupigana na uovu huu ni jukumu la kila mtu... Nenda sasa ukanywe chai ukisubiri siku ya tuzo yako."

"Ahsante sana mama, wizi wa Toyota utakomeshwa!" Dani aliondoka na kwenda kujiunga na babake kupata kiamsha kinywa.

Mfano 4.1.10.5. umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015).


Ni katika mfano huu ambapo msamiati mwepesi na sentensi changamano zimetumika moja kwa moja. Katika riwaya tano teule zilizochunguzwa, nne zilidhihirisha miundo sahili huku riwaya moja ikidhihirisha uchangamano. Ilibainika kuwa riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012) ilizingatia umbo sahili kwa kuwa iliwalenga wasomaji chipukizi; wasomaji wa gredi ya kwanza huku ile riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) ikidhihirisha uchangamano kwa kuwa iliwalenga wasomaji ambao walikuwa wameanza kukuza tajriba ya usomaj. Iliwalenga wasomaji wa gredi ya nne.

Leech na Short (1981) wakishughulikia nadharia ya umitindo wamejadili kuhusu mhimili wa grafolojia kama mojawapo ya viwango vinavyotafitiwa kimitindo katika uandishi.

Uchanganuzi wa riwaya tano teule zilizotafitiwa ulibaini kuwa riwaya hizo ziliafiki kaida za umitindo kwa viwango vya wasomaji waliolengwa na matini.

### 4.1.11 Matumizi ya kipengele cha faharasa katika fasihi ya watoto


Faharasa ni miongoni mwa vipengele ambavyo watalaam Kazungu (1982) na wengine hawakuvitaja na kuvijumlisha katika grafolojia licha ya vipengele hivi kutumika kwa mapana katika riwaya teule zilizochunguzwa kama inavyodhihirika katika mifano ya data ifuatayo.




Mfano 4.1.11.1. mfano huu wa faharasa umetolewa katika katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 19.

Katika mfano huu, msamiati ambao mwandishi aliufasiri kama mzito au mgumu kwa mwanafunzi wa kiwango cha daraja ya pili ambayo imependekezwa aisome riwaya hii

umefafanuliwa kimuktadha kulingana na mwandish. Hata hivyo, huenda kukawa na maneno mengine ambayo ni mazito kufasiriwa ipasvyo na msomaji lakini mwandishi aliyateua hayo na akayaorodhesha katika faharasa. Maneno sita ambayo yameorodheshwa na kufafanuliwa na mwandishi yana uwezo wa kumpa msomaji au mwanafunzi wa gredi ya pili changamoto.



**Kamusi yangu**


| | |
|---|---|
| **bahatisha:** | jaribu kupata kitu bila ya kujua matokeo yake |
| **balaa:** | baa, madhara, hasara |
| **dhihaka:** | mzaha, utani, mchezo |
| **ghala:** | mahali panapowekwa nafaka au kuhifadhia mazao ya shambani, stoo |
| **iva:** | kuwa tayari |
| **kibe:** | mchezo wa watoto wa kujificha na kutafutana |
| **kuwatii:** | fuata unachoambiwa kama vile amri au maagizo |
| **mafiga:** | mawe matatu yenye kutumiwa kama jiko |
| **majivu:** | vumbi la kitu kilichoteketezwa na moto |
| **makusudi:** | kwa kupanga au kuwa na nia ya kufanya jambo |
| **mkasa:** | jambo au tukio lililomfika mtu, msiba |
| **mwangalifu:** | mtu anayefanya mambo kwa uangalifu au makini |
| **vuma:** | enda haraka au kwa kasi |

25

Mfano 4.1.11.2 kutoka kwa riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003: 25).

Mwandishi wa riwaya hii ameamua kuitenga sehemu hii katika matini ya riwaya yake na kuielezea kama **Kamusi Yangu** huku akiwa ameyaorodhesha maneno ambayo kulingana

na tajriba yake, yanaweza kumtatiza msomaji wa gredi ya nne katika shule za msingi za Umma nchini.


**Maneno magumu**

| | |
|---|---|
| vibonzo: | katuni; mifano ya picha za viumbe kama watu au wanyama vinavyochekesha |
| sebuleni: | eneo la kupokea wageni ndani ya nyumba |
| magazeti makuukuu: | magazeti yaliyochakaa; magazeti yaliyozeeka |
| shingo upande: | bila hiari; bila kupenda kufanya jambo |
| vipuri: | vitu vya kurekebishia kitu hasa mashine |
| teka nyara: | kamata kwa nguvu |
| takribani: | karibu |
| kachero: | jasusi; polisi anayechunguza uhalifu na kuwakamata wahalifu |
| kisengeretua: | kifaa cha kufungua, kufunga au kubadilisha chaneli za vyombo vya umeme kama vile runinga, au redio kwa mbali; rimoti |

Mfano 4.1.11.3. mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 17.

Katika mfano huu, mwandishi wa riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) aliamua kuitenga sehemu ya **Maneno magumu** katika riwaya yake ambako maneno


ambayo yangempa msomaji wa gredi ya nne changamoto katika jitihada za kufasiri vyema maudhui yanayorejelewa na mwandishi.

Kufuatia matumizi mapana ya kipengele hiki cha faharasa miongoni mwa riwaya tano teule zilizochunguzwa, ni dhahiri kuwa ni kijenzi cha kimsingi katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Ingawa kipengele hiki hakikuorodheshwa wala kutajwa na wataalamu mbalimbali wa awali kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia, utafiti huu uliweza kubaini kuwa faharasa ni mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia, na kwamba ni cha kimsingi katika uandishi wa fasihi ya watoto, kwa kuwa kinatekeleza dhima muhimu katika uimarishaji wa upokezi wa maudhui kwa vile kinarahisisha ufasiri wa yaliyomo miongoni mwa wasomaji wachanga.

Viera (2017) ameshughulikia faharasa katika mtazamo wa ufahamu kimsamiati katika muktadha wa uzalishaji matini kimaandishi. Anasema kwamba kipengele hiki kinajitokeza katika uandishi wa matini yanayowalenga wasomaji wasio wa lugha ya kwanza inayotumika katika uandishi. Kwa kuwa kipengele hiki kinatumika katika mandishi ya msamiati kimuktadha, kinahusiana moja kwa moja na mhimili wa uchimuzi kifasihi wa nadharia ya umitindo kama ulivyoshughulikiwa na Wamitila (2008). Mhimili huu wa nadharia ya umitindo unashughulikia utambuaji wa msamiati kimatini miongoni mwa msamiati uliotumika katika matini, hali inayolifanya neno au maneno mengine kutambulika zaidi ya mengine katika matini.

### 4.1.12 Matumizi ya vielelezo / majedwali katika fasihi ya watoto

Vielelezo au majedwali ni miongoni mwa vipengele vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya teule zilizochunguzwa kama inavyoonyeshwa katika mifano inayofuatia.



Mimi Sisi
Wewe Nyinyi
Yeye Wao

| | | |
|---|---|---|
| Hapa | Hapo | Pale |
| Huyu | Huyo | Yule |


Ndani Nyumba Angalia
Habari Asubuhi Wapi?

| | | | |
|---|---|---|---|
| Yangu | Yako | Yake | Yetu |

Habari ya asubuhi, Simba.
Mimi nipo hapa.
Ndovu yupo pale.

Mfano 4.1.12.1. mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 29.

Jedwali hili linaonyesha nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu katika umoja na wingi. Pia limetumika kuonyesha ukaribu na umbali miongoni mwa vipashio vingine vya kisarufi.



| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Embe | Maembe |
| Mwembe | Miembe |
| Mti | Miti |
| Moyo | Mioyo |
| Nzi | Nzi |
| Mamba | Mamba |
| Nyani | Nyani |
| Ng'ambo | Ng'ambo |
| Ukingo | Kingo |
| Jino | Meno |
| Yai | Mayai |


Mfano 4.1.12.2. mfano huu umetolea katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 46.

Jedwali hili linaonyesha umoja na wingi wa msamiati uliotumiwa na mwandishi katika ujenzi wa riwaya. Vipengele hivi viwili vilidhihirika katika ujenzi wa baadhi ya riwaya zilizochunguzwa na kuchanganuliwa. Ingawa wataalamu wengi wakiwemo Alabi na Adegoju katika Adeniyi (2017) na wengine hawakutaja vielelezo na majedwali miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia, matokeo ya utafiti huu vilevile yalibaini kuwa vipengele hivi ni vya kimsingi katika ujenzi wa matini na ufasiri wa maudhui, hivyo basi vinahitaji kujumuishwa miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia, na kwamba vinachangia pakubwa katika uchimuzi wa maudhui. Hii ni kusema ya kwamba vielelezo na majedwali

ni vijalizo vya uandishi wa matini ya fasihi ya watoto na kuwa vinadhihirika kigrafolojia licha ya kuwa havijaorodhoshwa miongoni mwa vipengele hivyo.

### 4.1.13 Mazoezi na maswali katika fasihi ya watoto

Vipengele hivi pia vilidhihirika katika ujenzi wa riwaya zilizochunguzwa kupitia kwa mifano inayofuatia.




Zoezi

1. Hadithi hii inahusu wanyama kadhaa. Taja wanne.
2. Panya na Paka walikuwa wakienda kutembea katika mji fulani? Mji huo uliitwaje?
3. Ni kwa nini Kaka Sungura alikuja kuwatembelea Paka na Panya siku kadhaa kabla ya sikukuu ya Krismasi?
4. Paka na Panya walipopanda basi la kuelekea mjini waliwakuta wanyama wengine kadhaa. Taja watatu.
5. Walipofika mjini, walinunua mavazi ya aina gani?
6. Waliyanunua katika duka gani?
7. Ni kwa nini Paka na Panya walicheza

Mfano 4.1.13.1. mfano kutoka riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 21.

Ni mkusanyiko wa jumla ya maswali saba ambayo mwandishi anayarejelea tamatini mwa riwaya yake.



**Maswali**

1. Kwa nini watoto hawakwenda shule?
2. Aida aliwaambia wenzake kitu gani amba aliwakataza?
3. Taja michezo mitano waliocheza watoto?
4. Eleza faida ya kuwa na majirani wema?
5. Je, watoto walilichoma ghala kwa makus
6. Aliya alijifunza nini kuhusu moto?

133

Mfano 4.1.13.2. mfano kutoka riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 26.

Mwandishi ameorodhesha jumla ya maswali sita kutoka riwayani humo yanayohusiana moja kwa moja na hadithi iliyowasilishwa kimandishi. Vilevile vipengele vya mazoezi na maswali ni miongoni mwa vipengele ambavyo watalaam waliorejelewa hawakuvitaja au kuvijumuisha miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa hivi pia ni vipengele vyenye umuhimu katika ujenzi wa matini,

hususan za wasomaji wachanga kwa kuwa vinawachochea wasomaji hao katika kukuza vipawa vyao katika kufasiri vyema ujumbe katika matini pamoja na kuwapa kumbukizi. Hii ni kusema ya kuwa utafiti huu unapendekeza ya kwamba vipengele hivi vijumuishwe katika orodha ya vipengele vya kigrafolojia. Leech na Short (1982) katika kuijadili nadharia ya umitindo wanasema ya kuwa grafolojia ni taaluma inayohusu matumizi ya matini katika kuwasilisha ujumbe. Ujumbe uliolengwa na mwandishi unaweza tu kumfikia msomaji vyema kupitia kwa nyenzo mbalimbali ambazo nyingi zinahusiana na jinsi mwandishi huyo anavyoisuka lugha yake kimaandishi.

Kulingana na mwananadharia wa mwitikio wa msomaji Culler (1975), msomaji ni mtu mwenye umilisi kifasihi na kwa hivyo yeye hutumia umilisi huo ili kuelewa matini. Kutokana na mhimili wa nadharia ya mwitikio wa msomaji wa usomaji kama tukio la kiwakati, msomaji huyo hutumia mikakati mbalimbali katika jitihada zake za kuupokea ujumbe uliyo katika matini. Kwa hali hiyo, mazoezi na maswali ambayo yamejitokeza tamatini mwa riwaya zilizotafitiwa ni baadhi ya mikakati ambayo inachangia pakubwa katika uchimuzaji wa maudhui ambayo mwandishi hulenga kuwasilisha.

Kutokana na matokeo haya, utafiti umehitimisha kuwa kuna vipengele kochokocho vya kigrafolojia ambavyo hutumika katika fasihi ya watoto. Vipengele hivi ni viakifishi, herufi kubwa, picha na michoro, rangi, taipografia, mkolezo, mlazo, miundo mbalimbali ya aya, kipimo cha ukubwa na umbo la matini. Utafiti pia ulibaini kuwa kuna vipengele vinavyotumika katika ujenzi wa fasihi ya watoto katika Kiswahili ingawa havijaorodheshwa na wataalamu. Utafiti kwa hivyo unapendekeza kuwa vipengele hivi viongezwe katika orodha iliyopo ya vipengele vya kigrafolojia. Vipengele hivi ni faharasa ya maneno kimuktadha, vielelezo, majedwali, mazoezi na maswali kwa kuwa

vinachangia pakubwa katika ufundi wa ujenzi na pia ufasiri wa fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 4.2 Dhima ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto

Madhumuni ya pili ya utafiti yalichanganua dhima ya vipengele vya grafolojia katika fasihi ya watoto. Utafiti umebaini kuwa grafolojia na rasilimali zake hutekeleza dhima mbalimbali mahususi kifasihi. Miongoni mwa dhima hizo ni kuimarisha mawasiliano, kujenga uhalisia, kumsisimua msomaji, kuendeleza dhima ya kiujumi, kuweka msisitizo, kuendeleza kumbukumbu na kuweka mshikamano na muwala katika vipashio mbalimbali vya kisarufi.

#### 4.2.1 Kuimarisha mawasiliano

Grafolojia na raslimali zake hutekeleza dhima muhimu ya kuendeleza mawasiliano katika matini ya kifasihi. Uimarishaji huo wa mawasiliano hutukia kupitia kwa vipengele vifuatavyo vya kigrafolojia.

##### 4.2.1.1 Viakifishi

Viakifishi ni vipengele vya kimsingi katika uandishi wowote na alama za uakifishaji hutumika katika kuweka wazi ujumbe wa mwandishi. Hii ni kusema ya kwamba viakifishi hutekeleza dhima ya kisemantiki na kisintakisia katika matini. Hata hivyo, viakifishi vinaweza kutumika kikawaida na vilevile vitumike visivyo kawaida kama inavyodhihirika kifasihi. Zahra (2013) anawataja baadhi wa wanafasihi wa kishairi kama vile Cummings, Blake na Pound ambao anasema kuwa wamewahi kuvitumia viakifishi vyema kwa njia isiyo ya kawaida kuwasilisha maana mbalimbali katika tanzu zao za

kishairi. Hata hivyo, anasema kuwa katika matumizi yoyote ya viakifishi, kinachowasilishwa ni maana ambayo mwandishi huwa amenuia kuiwasilisha. Maoni yake yanaungwa mkono na Shaw (1986), Trask (1997), MacCasill (2012) ambao anawarejelea, wanaosema kuwa viakifishi hutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano kimandishi kwa kuhakikisha ya kwamba mandishi hayo yana maudhui au ujumbe ambao mwandishi alilenga kuyawasilisha kimatini.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa viakifishi mbalimbali hutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano mema kimandishi hususan katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Katika mfano nambari 4.1.1.1, kiakifishi aina ya kiulizi (?) kimetumika mwishoni mwa sentensi **Simba yuko wapi (?)** kuonyesha ya kwamba hilo ni swali ambalo dhima yake ni kuchochea mwitikio wa kujibiwa. Anayeuliza kuhusu aliko Simba ni Sungura, na ana nia ya kujua aliko Simba ili achukue tahadhari asije akamkaribia Simba kwa kujitia hatarini, kwa kuwa anaweza akaangamizwa kwa kufanywa kitoweo cha Simba.

Katika mfano 4.1.1.2, kituo (,) kimetumika katika sentensi ya kwanza **Basi siku moja (,) Mamba hakuwa na chakula** ili kubua dhima ya kuendeleza kuweka mtuo na kumpa msimulizi fursa ya kupokea pumziko fupi katika jitihada za kuendeleza maelezo yake. Kikomo (.) kimetumika katika sentensi ya pili **Hakujua ale nini (.)** kuonyesha mwisho wa sentensi au kudhihirisha mwisho wa taarifa. Mnukuu **(“ ”)** umetumika katika kifungu **“Mbuni, Mbuni, njoo unisaidie.”** kuonyesha usemi halisi kama ulivyotoka katika kinywa cha Mamba.

Kiulizi **(?)** kimetumika katika kifungu **Ni jino gani hilo?”** kuonyesha jitihada za Mbuni kufahamu jino mahususi ambalo lilikuwa likimpa Mamba maumivu. Kihisishi (!) kimedhihirika kutumika katika kifungu **Linauma, Oh! Oh! Oh! Oh!** kuonyesha hisia za


uchungu zilizokuwa zikimkabili Mamba kutokana na jino lililokuwa likimsababishia maumivu. Katika mfano 4.1.1.9, alama ya udondoshaji imetumika katika mfano wa Mali..Maliii.., Mali… kuonyesha ya kwamba, anayetangaziwa anafahamu dhima inayotokana na tangazo kuhusu aina ya mali inayochuuzwa na anayetangaza kwa hivyo hahihitaji kuelezwa tena kuwa ni mali ya aina gani. Katika mfano 4.1.1.10, alama hisi inajitokeza mwishoni mwa sentensi **Nitawezaje kuondoka ilhali bado nakumbuka kisa kilichompata rafiki yangu Juma hivi juzi alipokosa kutii ushauri wa wazazi wake!"** Kauli hiyo inatupa dhima ya Dani ambaye ndiye mzungumzaji kama alivyo na hisia nzito kuhusu kisa kilichomtendekea rafikiyake ambaye ni Juma.

Kama vile wataalamu mbalimbali walivyovishughulikia viakifishi na kubaini dhima yavyo kigrafolojia, dhima ya kuendeleza mawasiliano vyema ni ya kimsingi. Wataalamu Shaw (1986), Grindlay (2002), Tunicak (2003), Grindlay (2002), Opara (2013), Bakuuro na wenzake (2018), Alabi na Adegoju (2017) na wengine wamevitaja viakifishi miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia ambavyo hutafitiwa katika umitindo kifasihi. Hata hivyo, Grindlay (k.h.t) amebaini wazi kuwa kuna uhaba katika tafiti za kina zinazohusu viakifishi, hali inayomchochea kukata kauli ya kuwa tafiti zinazohusu uakifishaji ni eneo lililopuuzwa.

Hali hiyo ndiyo iliyomchochea kuvifanyia utafiti viakifishi akavibainisha viakifisha pamoja na kuelezea dhima kuu ya uimarishaji wa mawasiliano. Wataalamu hawa wanashikilia mawazo kwamba ingawa hivi ni vipengele vya kiisimu, ni elementi za kimsingi katika uandishi wowote ukiwemo ule wa kifasihi. Mawazo ya wataalamu hawa yanashadidiana na matokeo ya utafiti yaliyobaini kuwa viakifishi vinaweza kutumika

kikawaida na pia kutumika kwa njia isiyo ya kawaida kama ilivyodhihirishwa na mifano mbalimbali ambayo imerejelewa kutoka katika riwaya zilizotafitiwa.

Vilevile matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa mandishi yoyote hayawezi kumfikia msomaji vyema na pia kudhihirisha maana pasipo na matumizi mema ya viakifishi, iwe katika uzingativu wa kaida za kiisimu au katika ukiukwaji wa kaida hizo. Vilevile matokeo yametambua kwamba viakifishi vinaimarisha mwendo wa matukio kimaandishi na kwa njia hiyo kufafanua maoni ya mwandishi kwa ujumla, kauli ambayo pia inawiana na maoni ya watalaam mbalimbali waliorejelewa. Wandishi wa riwaya tano zilizochunguzwa walionekana kudhihirisha upekee jinsi walivyovitumia viakifishi mbalimbali katika kazi zao, huku wengine wakiafikiana na wengine kukiuka matumizi ya viakifishi kwa njia iliyozoeleka.



Vipindi vya vibonzo vilipokamilika, Dani aliinuka, akajinyoosha mwili huku akijiuliza, 'Siku ya leo itaisha kweli?' Alitazama saa, akajiambia, 'Ni saa nne tu! Na shangazi atakuja saa tisa!' Aliingia jikoni, akajitilia chai. Alirudi nayo sebuleni akaanza kuinywa. Alipomaliza kunywa chai , alirudisha kikombe jikoni akakiosha. Alirudi sebuleni tena. Alichukua kisengeretua cha runinga, akakibonyeza. Alikuwa anatafuta kipindi kingine ambacho kingemburudisha. Baada ya kufungulia chaneli zote moja baada ya nyingine, aliizima runinga huku akijiambia, 'Hakuna vipindi vya kuvutia sasa hivi.' Aliondoka taratibu na kwenda chumbani mwake.

Alipanda vidato, kimoja kimoja kana kwamba alivihesabu hadi mwisho. Alikuwa akibandika na kubandua mguu pa, pa, pa! Ile sauti ya nyayo zake ilikuwa hafifu lakini kwa sababu ya kimya ndani ya nyumba, iligonga kama kidumbaki. Aliingia chumbani mwake. Aliketi kitandani. Kisha akainuka akachukua kiti akaketi karibu na dirisha akitazama wapita-njia. Alimwona mtu aliyenunua magazeti makuukuu kutoka kwa watu pale mtaani. Mtu huyu aliwafahamisha watu kuwa amefika kununua magazeti kwa kuita kwa sauti ya juu, "Haayaa magazeeti, chupa na madebe. Mali... Maliii... Mali... Maliii..., nanunua mali zote chupa, karai kuukuu, na vyombo vya chuma! Maliii, mali maliii..." Dani

3

Mfano kutoka riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota*, (Ngugi, 2005) uk.3

Viakifishi kadhaa vimedhihirika kutumika katika mfano huu. Kuna matumizi ya alama ya koma (,) pia kuna matumizi ya alama za kunukuu (''), matumizi ya alama ya kiulizi (?), alama hisi (!), kituo (.), kistariungio (-) na alama ya udondoshaji (…). Matumizi ya viakifishi hivi yanaonekana waziwazi katika mfano huu. Vipengele hivi vimetumika kiisimu kuwasilisha ujumbe mahususi kuhusu shughuli aliyoifanya Dani siku hiyo akiwa pekee nyumbani. Kwanza alianza kwa kutazama vipindi vya vibonzo, baada ya vipindi hivyo, alikuwa na uchovu kisha akajinyoosha. Baadaye aliendа jikoni akachukua chai akanywa akiwa sebuleni na alipobaini kuwa hakukuwa na kipindi kizuri katika runinga,

alijielekeza katika chumba chake cha kulala. Aliketi kwenye kitanda huku akiwatazama wapitanjia.

Dani alimwona mtu aliyekuwa na uzoevu wa kununua magazeti makuukuu pale mtaani pamoja na chupa, madebe na karai. Ujumbe huo unafululiza na kuibua maana mahususi kutokana na matumizi mema ya viakifishi kwa kuwa kama vipengele hivyo havingetumika vyema, haya yangekuwa maneno tu yasiyo na maana. Hii ni kusema ya kwamba viakifishi vinatekeleza dhima kuu ya kuhakikisha kuwa ujumbe unamfikia msomaji wa matini kwa njia iliyo mwafaka.


Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na maoni ya wataalamu waliotajwa na kutoa mawazo yao kuhusu dhima ya viakifishi katika uandishi na fasihi ya watoto kwa ujumla isipokuwa katika matumizi ya kistariungio. Katika sentensi **Alipanda vidato, kimoja kimoja kana kwamba alivi** - (**hesabu**) matumizi ya kistariungio yanatofautiana na wanavyosema wataalamu wengi akiwemo Stephano (2015) ambaye ametoa maelezo kuhusu matumizi ya kistariungio. Akitathmini matumizi ya nadharia tumizi ya uakifishaji, Stephano (k.h.t) anaeleza jinsi wandishi wengine wanavyokiuka matumizi mema ya viakifishi. Kwa mujibu wake, kistariungio kinastahili kutumika tu kuunga silabi moja katika kipande ambacho huwa kinaendelezwa. Katika mfano tulioutaja, kistariungio kimetumika kuunga kipande **(hesabu)** kwa kipande **(alivi-)** kuashiria ukiukwaji kwa kuwa kimetumika kuunganisha silabi tatu katika kipande cha neno lililokuwa likiendelezwa. Hata hivyo, kilicho muhimu ni ujmbe unaowasilishwa na kipengele hicho katika kumwezesha msomaji kuibuka na ufasiri ufaao.

Kwa hivyo kando na matumizi mengine ya viakifishi kwa njia iliyozoeleka, ni mfano huu mmoja uliokinzana na mawazo ya wataalamu lakini kwa kuwa wandishi wa kazi za

kifasihi hudhihirisha upekee katika ujenzi wa kazi zao, ukiukwaji ni tukio la kawaida katika kazi za matini za kifasihi. Mhimili wa kiwango cha grafolojia wa nadharia ya umitindo umezungumzia hali hii ambayo kazi za kifasihi zinapuuza kaida za matumizi kiisimu katika usukaji wa kazi hizo na kumpa mwandishi wa kazi za kifasihi uhuru na upekee fulani katika usukaji wa kazi yake. Hii ni kusema ya kwamba katika mchakato wa utungaji na uandishi wa kazi za kifasihi, hakuna utaratibu mwafaka ambao wandishi wanahitajika kuuzingatia bali cha kimsingi ni jinsi kazi hiyo inavyotafsiriwa na kufasiriwa na wasomaji. Kwa hali hiyo, viakifishi vinatekeleza dhima ya kuendeleza mawasiliano mema kimandishi kwa kuwa bila viakifishi mandishi yoyote, yakiwemo ya kifasihi hayatafasiriwa vyema na hivyo basi yataleta utata.

#### 4.2.1.2 Herufi kubwa


Herufi kubwa vilevile imetumika kutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano katika matini. Katika mfano 4.1.1.1, neno la tamati mwa sentensi hiyo **Sungura** limeanza kwa herufi kubwa kuendeleza dhima ya ukiukaji kiisimu kwa kuwa linataja nomino ya kawaida. Yeibo na mwenzake (2014) katika kujadili dhima ya matumizi ya herufi kubwa, wamedokeza ya kwamba kipengele cha herufi kubwa hutumika kwa lengo la kukifanya kifungu ambamo herufi kubwa imetumika kutokezea zaidi ya maneno mengine. Matokeo ya utafiti miongoni mwa riwaya teule zilizochunguzwa yamebaini kuwa herufi kubwa imeshuhudia matumizi ya kawaida na vilevile matumizi yasio ya kawaida. Aidha riwaya ya *Usicheze na Moto* (2003) ndiyo iliyozingatia matumizi ya kawaida ya herufi kubwa kama ilivyobainika katika mfano ulio hapo chini.




Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk.1


Katika mfano huo, maneno yaliyotumika yamezingatia ukawaida wa matumizi ya herufi kubwa. Yale ambayo yanataja nomino za pekee kama majina ya wahusika **Aliya**, **Aida** na **Dodo** yameanza kwa herufi kubwa na yale ambayo si nomino za pekee yametumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi ambayo ni matumizi ya kawaida ya herufi kubwa.

Katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012), herufi kubwa imetumika visivyo kupitia kwa mfano ulio hapo chini.





Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk.3.

Katika mfano huo, neno **Sungura** lililo mwishoni mwa sentensi hiyo linaloitaja nomino ya kawaida limeandikwa kwa kutangulizwa kwa herufi kubwa kuashiria ukiukaji wa matumizi ya herufi kubwa katika matumizi ya kawaida. Kwa kufanya hivyo, mwandishi amelipatia neno hilo upekee fulani. Riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009) vilevile ina mifano ya maneno ambamo herufi kubwa imetumika visivyo kama ilivyodhihirika katika mfano ulio hapo chini. Katika mfano huo, neno Mamba limeendelezwa likiwa limeanza kwa herufi kubwa katikati na tamatini mwa sentensi kuashiria ukiukaji wa matumizi ya herufi kubwa kiisimu kwa kuwa neno hilo haliwakilishi nomino ya pekee kisarufi.




Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* ( Bracey &Lieta, 2009) uk. 18.



hapo kando ya njia na bila kusita, wakaingia kwenye tundu hilo na kujificha. Paka na mkewe wakajaribu kuwafuata humo tunduni ili wawaangamize, lakini kwa vile mili yao ni mikubwa kuliko ya Panya, hawakuweza kuingia. Walirudi nyumbani wakiwa bado na hasira nyingi.


Waliapa kuwa, wataendelea kumtafuta Panya na familia yake na watakapokutana nao mahali popote pale, watawafanya kitoweo chao papo hapo.

Tangu siku hiyo, Panya akimwona Paka hutimua mbio za ajabu na kujificha ili kuokoa maisha yake.

18

Mfano kutoka katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* ( Waihiga, 2006) uk.18.

Katika mfano ulio hapo juu, maneno **Paka** na **Panya** yaliyo katika aya ya mwisho, ambayo yanarejelea nomino za kawaida yameandikwa kwa kutangulizwa kwa herufi kubwa kuashiria ukiukaji wa matumizi ya herufi kubwa. Kwa kuyaendeleza maneno hayo huku yakiwa yametangulizwa kwa herufi kubwa, mwandishi anaendeleza ukiukaji wa kiisimu.


yake mkononi. "Si amesema eti wezi hao walipitia barabara ya Songambele? Na ni gari la manjano?"

Dani aliketi tena akaangalia orodha yake ya magari. 'Najua kuwa nambari ya gari hilo lazima iwe kwenye orodha yangu,' Dani alijiambia tena. 'Hebu niangalie kwa makini.'

Alitazama karatasi hiyo kwa makini hasa sehemu ya rangi za magari huku akisema kimoyomoyo, 'Manjano, manjano, manjano.' Alipata rangi tano za manjano. Kisha akajiambia, 'Kati ya haya matano, nitatafuta gari aina ya Toyota.' Alianza kutafuta tena huku akiyataja magari hayo, "Subaru, Toyota, Toyota, Subaru, TOYOTA MANJANO. Ndilo hili gari waliloiba!" Dani alisema kwa sauti. "Baba, ndilo hili gari waliloiba!"

Dani alimfahamisha baba yake huku akimwonesha orodha hiyo, "Nambari zake ni KUUU 23445 U. Baba, hebu tuwapigie polisi simu. Nitawapa nambari ya gari

10

Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.10.


Katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015), herufi kubwa imetumika kama inavyodhihirika katika mfano ulio hapo juu. Katika mfano huo, maneno **TOYOTA MANJANO** na nambari yake **KUUU 23445U** yameendelezwa kwa herufi kubwa vilevile kudhihirisha ukiukaji wa kaida za kiisimu za matumizi ya herufi kubwa. Kulingana na mfano huo, mwandishi alizitumia herufi kubwa kusisitiza ya kwamba halikuwa gari lingine lililoibiwa bali aina ya gari la **TOYOTA** ambalo rangi yalo ilikuwa **MANJANO** bali si nyekundu wala rangi nyingine ile, na vile vile nambari ya usajili haikuwa nyingine tu bali **KUUU 23445 U**. Kulingana na Chukwu (2010), dhima ya kutumia herufi kubwa visivyo ni kulichimuza neno ambamo herufi hiyo imetumika na vilevile kuweka msisitizo katika neno hilo. Kwa hivyo kulingana na matokeo ya utafiti huu, matumizi yasiyo ya

kawaida ya herufi kubwa katika riwaya teule yalilenga kuchimuza maudhui au ujumbe uliobebwa na mandishi hayo na vilevile kuweka msisitizo katika maneno hayo, hali inayobainisha dhima ya herufi kubwa.

Khan na Khan (2015) katika Adeniyi (2017) wanasema kuwa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia huwa na dhima mahususi kimtindo katika matini ambayo ni kuimarisha vyema ufasiri na uelewa wa matini kando na kuleta upatanishi katika matini. Matokeo ya utafiti yameshadidia maoni ya wataalamu mbalimbali waliorejelewa kuhusu dhima inayotekelezwa na herufi kubwa kimandishi ambayo ni kuimarisha mawasiliano au ujumbe uliolengwa na mwandishi kama ilivyodhihirika katika mifano iliyoangaziwa kutoka riwaya teule kadhaa.

#### 4.2.1.3 Faharasa

Kipengele cha faharasa kilidhihirika katika baadhi ya riwaya zilizochunguzwa kama ilivyo katika mfano unaoangaziwa katika ukurasa unaofuata



**Maneno magumu**

| | |
|---|---|
| vibonzo: | katuni; mifano ya picha za viumbe kama watu au wanyama vinavyochekesha |
| sebuleni: | eneo la kupokea wageni ndani ya nyumba |
| magazeti makuukuu: | magazeti yaliyochakaa; magazeti yaliyozeeka |
| shingo upande: | bila hiari; bila kupenda kufanya jambo |
| vipuri: | vitu vya kurekebishia kitu hasa mashine |
| teka nyara: | kamata kwa nguvu |
| takribani: | karibu |
| kachero: | jasusi; polisi anayechunguza uhalifu na kuwakamata wahalifu |
| kisengeretua: | kifaa cha kufungua, kufunga au kubadilisha chaneli za vyombo vya umeme kama vile runinga, au redio kwa mbali; rimoti |

Mfano kutoka katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 17.

Ingawa watafiti Alabi (2007), Adegoju (2008) Alowonle (2016) miongoni mwa wengine hawakukitaja faharasa kama kipengele mojawapo kinachojumuishwa miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia, utafiti huu umebaini ya kwamba faharasa ni kipengele muhimu katika uandishi kwa kuwa kinaafiki maelezo wanayotoa Khan na Khan (2010) na wengine katika Adeniyi (2017) kuhusu grafolojia. Wao wanaeleza ya kuwa grafolojia ni umitindo mahususi unaomwezesha msomaji kumakinikia usomaji matini kwa lengo la kumwezesha kupokea kwa ukamilifu ujumbe ulio katika matini.

Kulingana na kauli hii, ni dhahiri kuwa kupitia kwa faharasa katika matini, msamiati ambao huwa umetumika na mwandishi kimuktadha katika utunzi wa kazi yake

unafafanuliwa na inapofanyika hivyo, msomaji huwa amepata fursa nzuri ya kuyafasiri maudhui yaliyolengwa na mwandishi wa matini hayo vyema kwa kuwa huwa anauelewa msamiati uliyotumika vyema.

Kwa hivyo dhima ya faharasa katika matini huwa ni kuimarisha upokezi wa ujumbe au maudhui kwa kuwa msomaji huelekezwa jinsi msamiati ulivyotumika kimuktadha katika matini. Kutokana na uelekezi na ufafanuzi wa msamiati huo kimuktadha, mwandishi kupitia kwa faharasa huhakikisha ya kwamba dhana na istilahi au maneno yaliyotumika yamefasiriwa vyema na mawasiliano yaliyokusudiwa na mwandishi yamemfikia msomaji vyema. Kwa hali hiyo, msomaji anakuwa na fursa nzuri ya kuufasiri ujumbe, kwa hivyo, ni dhahiri kuwa matumizi ya faharasa katika matini ni njia mojawapo ambayo mwandishi hutumia katika kuimarisha upokezi wa ujumbe kwa msomaji.

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa faharasa ni kipengele chenye manufaa mengi katika fasihi ya watoto kwa vile kikiwepo katika matini, msomaji hupata kufahamu ujumbe ulio katika matini kimuktadha na vile vile hupokea tajriba kuhusu matumizi mema ya msamiati ambao awali huenda hakuufahamu, hivyo basi, faharasa ni kipengele cha kimsingi katika utunzi au ujenzi wa tanzu za riwaya za watoto kwa kuwa kinaimarisha ufasiri mwema wa ujumbe uliyomo katika matini na hivyo basi kuchimuza maudhui.

Kwa hivyo matokeo hayo yanawiana na maoni anayoshikilia Nordquist (2019), anayesema kuwa matini huandikwa ili kuimarisha mawasiliano. Hata hivyo anahoji kuwa kutokana na tofauti za viwango vya wasomaji, faharasa huwekwa baada ya mahitimisho katika vitabu ili kutoa ufafanuzi wa baadhi ya msamiati ambao unaweza kuwa umewapiga chenga wasomaji wengine. Nordquist (k.h.t) anaendelea kusema kwamba iwapo maelezo hayo yatadhihirika kila mara msamiati fulani unatumika, hatua hiyo

inaweza kuwaudhi wasomaji wa kiwango cha juu cha ufahamu. Hii ni kusema ya kuwa matumizi ya faharasa huwalenga wasomaji chipukizi, na utafiti unapendekeza kuwa kipengele hiki kiongezwe katika orodha ya idadi au miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

#### 4.2.1.4 Picha na michoro

Picha na michoro husaidia kuimarisha ufasiri wa maudhui katika matini na hivyo kuimarisha mawasiliano baina ya mwandishi na msomaji wa matini. Hii ni kusema ya kwamba picha na michoro huimarisha uchimuzi wa maudhui katika matini.




Mfano kutoka katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) kur.14 & 15

Mfano huo ulio hapo juu umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009) na hadithi yenyewe ni *Mayai ya Mamba*. Ni hadithi inayozungumzia jinsi Sungura alivyoiba mayai ya Mamba. Ni dhahiri kuwa Sungura ni miongoni mwa wanyama wajanja sana huku Mamba akiwa miongoni mwa wanyama wakali mno. Kwa hivyo Sungura anaitumia pombe kama chambo cha kumhadaa Mamba katika kuyalegeza makali yake. Mamba anaibugia pombe hiyo kwa pupa kiasi cha kulewa chakari huku Sungura akisalia makini kwa kuuweka tu ule mrija katika kinywa chake. Sungura alinuia kuiba mayai ya Mamba, tukio ambalo alilipangia kwa kumchochea Mamba alewe na apoteze fahiwa zake na akafaulu katika kulitimiza azma yake.

Ciancilio (1970) na wenzake vilevile waliibua mawazo juu ya kutathmini jinsi picha na matini zinavyopangika katika kazi ya kifasihi. Hata hivyo, walisisitiza ya kwamba ni muhimu kuangazia jinsi matini na picha zinavyopangwa katika kitabu. Wanasema kuwa ikiwa picha na matini zimepangwa vyema katika hali ambayo Elster na Simons (1985) waliita hali ya utegemezi – picha, ambapo maelezo katika matini yanategemea picha au picha ikawa inategemea maelezo moja kwa moja, utangamano huo utamwathiri msomaji vyema na hivyo basi kuimarisha ufasiri wake.

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa picha na michoro kimatini huimarisha mawasiliano na yanawiana na mawazo ya watalaam waliorejelewa akiwemo Amelsvoort (2013) aliyefanya utafiti kuhusu dhima ya picha na michoro katika matini za kufunzia lugha ngeni, hususan ya Kiingereza katika chuo Kikuu cha Kanagawa nchini Japani. Anakata kauli kuwa picha hubeba ujumbe mwingi kuliko matini na kwamba zina mchango mkubwa kuhusu upokezi wa msamiati na ufasiri wa ujumbe ambavyo ni vigezo vikubwa katika uimarishaji wa mawasiliano.

Hii ni kusema kuwa matumizi ya picha na michoro katika matini husaidia pakubwa katika kuimarisha ufasiri wa maudhui yaliyobebwa na matini. Vipengele hivi vina dhima kuu hususan katika fasihi ya watoto ambao hawana tajriba pana kwa kuwa kwa kuzitazama hizo picha na kuzifungamanisha na matini, wasomaji wachanga wanakuwa na fursa bora ya kuufasiri ujumbe uliolengwa kuwasilishwa na mwandishi.

#### 4.2.1.5 Rangi

Kando na vipengele vya kigrafolojia ambavyo vimetajwa na kushughulikiwa kama vyenye dhima ya kuimarisha mawasiliano, vilevile rangi hutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano. Parikh (2022) anasema kuwa rangi kila wakati huwasilisha maana mbili ambazo ni maana nyumbuvu na maana kimuktadha. Anasema kuwa maana kimuktadha inahusu moja kwa moja ile maana inayoibuliwa katika muktadha wa jamii anamoishi mwanajamii na inathibitiwa na nguvu za kihistoria. Kulingana naye, rangi nyeusi inaashiria kifo na maombolezi, rangi ya manjano inahusishwa na uwoga, rangi nyekundu inahusishwa na dhambi, rangi nyeupe inahusishwa na upole, rangi ya kijani inahusishwa na wivu, rangi ya zambarau inahusishwa na ufahari, rangi ya samawati inahusishwa na matumizi ya lugha yasiyofaa ilhali rangi ya hudhurungi inahusishwa kwa karibu mno na hisia mbaya. Hata hivyo, anapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kwa lengo la kuafikia ufasiri wa kijumla unaokubalika kuhusu aina mbalimbali za rangi.

Ingawa picha na michoro imejadiliwa kwa kina kama mojawapo ya vipengele vinavyoimarisha mawasiliano, picha na michoro huwa na mvuto wa juu ikiwa zitawasilishwa kwa rangi ng'avu. Pierson (2008) alifanya utafiti kuhusu athari ya mawasiliano kupitia kwa uchunzaji. Ni katika kazi hiyo ambapo anajadili dhima ya rangi

katika mawasiliano. Anadokeza kuwa rangi ni lugha ya kimataifa inayovuka mipaka ya tamaduni mbalimbali na kupitisha ujumbe fulani mahsusi. Kwa mujibu wake, matumizi ya mseto wa rangi mbalimbali hutekeleza dhima ya kuongeza na kuimarisha maana katika mawasiliano ya kuchunza kwa kuwasilisha ujumbe wakati huo huo. Anawarejelea Eiseman (2000), Evans (2006), Cheiskin (1947) na wengine wanaoshikilia kuwa uwezo na nafasi inayoshikiliwa na rangi katika hatua zozote za mawasiliano katika nyanja zote haziwezi kulinganishwa na kingine kutegemea matumizi mema ya rangi zinazoshirikishwa. Hii ni kusema kuwa kipengele cha rangi hakiwezi kupuuzwa katika usukaji wa matini za kifasihi na kwamba rangi inatekeleza dhina mahususi katika uimarishaji wa mawasiliano.

### 4.2.2 Kuendeleza uhalisia

Dhima ya uendelezaji wa uhalisia aghalabu huimarishwa kutokana na matumizi ya picha na michoro kama tunavyofafanua katika vijisehemu vifuatavyo:

#### 4.2.2.1 Picha na michoro katika fasihi ya watoto

Mifano kadhaa ya picha ilidhihirika katika riwaya teule tano zilizochunguzwa kupitia kwa mifano nambari **4.1.3.1**. hadi mfano nambari **4.1.3.8**. Dhima ya picha za aina hii katika matini ya fasihi ya watoto ni kuendeleza uhalisia. Mifano hii inawakilisha picha ambazo wandishi wa riwaya tano teule walizitumia katika ujenzi wa kazi zao. Matumizi haya ya picha yanashadidia mawazo ya watafiti mbalimbali kuhusu fasihi ya watoto. Cer (2016) anahoji kuwa kuna baadhi ya wataalamu wanaoshikilia mawazo kwamba fasihi ya watoto haikamiliki bila ya picha na kundi hilo la wataalamu linajumlisha Ciancilio (1970), Nodelman (1988), Kiefer (1993), Fang (1996), Leddy (2002), Nikolajeva (2005),

Marantz na Marantz (2013) na wengine. Katika kujadili ufaafu wa fasihi ya watoto, wamebainisha kwamba picha ni kiunzi muhimu katika fasihi ya watoto na ni lazima kidhihirike katika kazi hiyo ya fasihi ya watoto kwa lengo la kumwezesha mtoto kuunganisha mawazo yake na vitu anavyokumbana navyo katik ukuaji wake.




Hili ni Jalada la riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012).

Uhalisia unadhihirika kupitia ujumbe unaowasilishwa na hili jalada. Katika jalada hili, kuna wanyama wawili na nyumba nzuri. Wanyama hao ni Simba na Sungura. Sungura anaonekana mwenye hofu na wasiwasi, ishara inayoonekana kutokana na uso wake na jinsi alivyoyakodoa macho, kando na miondoko anayodhihirisha. Simba anaonekana mwenye furaha na nia ya kumnasa Sungura. Hii ni kwa kuwa licha ya hawa wote kuwa wanyama, ni kawaida kwa Simba kuwala wanyama wengine kama vile Sungura na kwa hali hiyo, ni kawaida kwa wanyama kama vile Sungura kuchukua hatua ya dharaura ili

kujiokoa kutokana na makali ya Simba. Kwa hivyo Sungura ametimuka na kuelekea katika ile nyumba ili ajiokoe kutokana na makali ya Simba.




Mifano hii imetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) kur.2 na 3.

Picha hizi mbili zinamwonyesha Sungura akiwa ametulia chini ya mti uliozingirwa na mandhari mazuri na nyingine inaionyesha nyumba yake. Ni nyumba nzuri yenye ukuta wa rangi ya kupendeza na mlango na dirisha nzuri inayofanana na paa. Paa la nyumba hiyo na mlango na dirisha zimerembeshwa kwa rangi ya hudhurungi. Hata vazi la Sungura linafanana na rangi za nyumba yake. Ufundi huu unaleta ujumi na bila shaka

unaweza kumsisimua msomaji mchanga kwa kuwa atazilinganisha picha hizo na mazingira alimo na kuufikia ufasiri ufaao. Ciancilio (1970) na wenzake wanasema kwamba picha hujenga mnato kati ya msomaji mchanga na matini, huku dhima kuu ya picha ikiwa ni kumwezesha msomaji huyo mchanga kujifunza dhana kwa kutambua mazingira yanayomzunguka. Cianciolo (1970) kwa mfano alidokeza kuwa vitabu vilivyo na picha huleta tukio la kihisia kifasihi kwa kuvifanya vitabu hivyo vieleweke vyema pamoja na kumfanya msomaji kujivunia sanaa na ufundi wa mwandishi katika fasihi hiyo.

Akanwa (2017) anasema kuwa picha katika fasihi ya watoto zinalenga kumwezesha msomaji huyo mchanga kushika makini yake kando na kuongeza thamana ya kiujumi katika matini hiyo. Hii ni kusema kwamba kifasihi, picha na michoro huimarisha uelewa wa maudhui ambayo huwa yameangaziwa katika matini. Akitoa mchango wake, Greene (2001) pia anasema kuwa dhima ya picha au michoro katika matini ni kuendeleza ujumi katika kazi za kifasihi. Anashikilia kuwa ni muhimu kufahamu ya kwamba suala la kiujumi lina ukuruba na falsafa na kuwa linahusu utambuzi, hisi, ubunifu na jinsi matukio haya yanavyohusiana na ufahamu, uelewa na kuhisi kuhusu ulimwengu, hali ambayo inamwezesha msomaji kuvutiwa na matini yenye picha, inayomuunganisha na sanaa.

### 4.2.3 Kumsisimua msomaji

Schallert (1980) alisema kwamba picha katika matini inaweza kutumika badala ya maelezo mengi ambayo huchukua muda na nafasi kubwa katika matini. Vilevile alisema kwamba picha huipa kazi ya fasihi mvuto wa juu hivyo basi kuchochea hamu ya msomaji

ya kuisoma kazi hiyo kwa ukamilifu huku akiwa na furaha. Utafiti huu kwa hivyo ulibaini kuwa fasihi ya watoto haitakuwa kamilifu bila yab matumizi ya picha na michoro katika kuiendeleza. Fang (1996) katika kuangazia dhima ya picha katika fasihi, alisema kuwa picha hutanguliza hali ya ujumbe unaopatikana katika matini na pia hufafanua wahusika katika kazi hiyo, hususan hadithi fupi ambazo fursa ya ukuzaji wa wahusika huwa haipo.

Kama wanavyoeleza Nikolajeva na Scott (2001) katika Helmly (2010), picha au michoro katika matini ni njia tofauti za kutoa maelezo kuhusu matukio kwa vile matukio hayo hufafanuliwa kupitia kwa matini huku vilevile yakielezwa kupitia michoro. Kulingana na kauli hii, ni dhahiri kwamba matini iliyoandamana na mchoro au picha hurahisisha ufasiri wa msomaji. Kauli hii inaungwa mkono na Ruthiiri (2012) anayedokeza kwamba picha katika matini ya fasihi ya watoto huifanya kazi hiyo kuwa na uhalisia hususan watoto wanapokuwa na fursa ya kushuhudia matukio ambayo wameyazoea katika hali halisi yakirejelewa katika matini.

Kluck (1972:8) anahoji kuwa picha katika fasihi ya watoto hupanua hadithi inayorejelewa kwa kuibua mawazo ambayo huwa hayajatajwa moja kwa moja katika matini. Mawazo ya Kluck (k.h.t) yanashadidiwa na Wolfenbarger na Sipe (2007) wanaosema kwamba vitabu vyenye michoro huwakilisha upekee katika sanaa ya fasihi kimfumo kwa vile vinawahusisha wasomaji wachanga na watu wazima katika viwango vingi vya usomaji na ustaarabu.

Greene (2001:38) anaonekana kuunga mkono mawazo ya Ciancilio (1970) na wenzake kuhusu dhima ya picha au michoro katika matini. Kulingana naye, dhima ya picha au michoro katika matini ni kuendeleza ujumi katika kazi za kifasihi. Anasema kuwa ni

muhimu kufahamu ya kwamba suala la kiujumi lina ukuruba na falsafa na linahusu utambuzi, hisi, ubunifu na jinsi yanahusiana na ufahamu, uelewa na kuhisi kuhusu ulimwengu, hali ambayo inamwezesha msomaji kuvutiwa na matini yenye picha, inayomuunganisha na sanaa. Kufuatia mchango wa wataalamu hawa, ni dhahiri kwamba picha na michoro katika fasihi ni kiunzi muhimu hususan katika fasihi ya watoto kwa vile ndizo raslimali za kimsingi katika kuwapa watoto msingi kielimu.

Kwa hali hii, picha na michoro ni mwangwi ambao unampa msomaji ufahamu, na vilevile kumpa raha katika pekua pekua zake kimatini, hali ambayo huchimuza ujumbe uliyomo katika matini. Katika riwaya zilizochunguzwa, picha zilidhihirika kupangika kwa njia ya kumfanya msomaji wa matini kudhibitiwa vyema na vipengele hivi. Kwa mfano katika riwaya hizi teule, kila baada ya maandishi katika ukurasa, mwandishi aliweza kupachika picha ilhali pale ambapo picha iliutanguliza ukurasa, mandishi yalifuata baada tu ya picha hiyo. Katika kurasa zingine, wandishi walizitumia picha na mandishi kwa usambamba miongoni mwa riwaya hizi kama vile katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006).

Mpangilio huu wa picha katika riwaya ulionekana mwafaka kwa kuwa ulimwelekeza au kumdhibiti msomaji katika ufasiri wa ujumbe ambao mwandishi alilenga kuuwasilsha. Hii ndio hali ambayo Elster na Simons (1985) waliita utegemezi - picha, utegemezi ambapo maelezo katika matini yanategemea picha, au picha katika matini inategemea maelezo kimandishi. Walisema kwamba mpangilio wa aina hiyo humfanya msomaji kuathirika moja kwa moja na rasilimali za picha katika matini. Kwa hivyo raslimali za picha katika riwaya tano teule ziliendeleza dhima ya kumsisimua msomaji katika hadithi ambazo wandishi walizirejelea.

#### 4.2.4 Kuendeleza ujumi

Ujumi ulidhihirika kupitia kwa utangamano baina ya wanyama kama vile kati ya Mamba na Mbuni, Sungura na Mamba, Mamba na Nyani katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009). Katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006), ushirikiano baina ya wanyama Paka, Panya na Sungura unaangaziwa. Mwishowe wanyama hawa waliweza kukosana na huo ukawa msingi wa visasili kama vile **Sababu ya Mbuni kuwa na Shingo Ndefu**, **Chanzo cha Uhasama kati ya Paka na Panya** miongoni mwa visasili vingine.

Beck (1984) alibainisha aina mbili za umitindo katika picha ambao aliuta picha dhahania na picha zilizochanganuliwa, na akasema kwamba zote zina uwezo wa kuendeleza ujumi katika matini. Kwa mujibu wake, aina mbili hizi za picha huchochea hamu ya usomaji na vilevile hupunguza mchakato wa ufahamu. Ingawa kuna uhuru wa kuibua mawazo ya aina hii, ni vyema madai haya kuimarishwa kwa ushahidi wa kitafiti kinadharia. Ni kwa hali hii ndiposa Aggleton (2017) anasema kwamba wanaopinga ujumuishwaji wa picha katika fasihi ya watoto wanafanya hivyo bila ushahidi wowote wa kinadharia, na vilevile akasema kuwa hayo ni makisio tu ambayo hayana ushahidi wowote kiutafiti.

Adam (2019) anahoji kwamba kuna ushahidi unaodhihirisha kwamba wasomaji wachanga wanapenda na huchangamkia vitabu vyenye picha katika fasihi yao kuliko matini isiyo na raslimali hizi. Picha katika matini zilizochunguzwa vilevile zimeshughulikiwa kwa wino au rangi tofauti zinazong'aa. Picha hizo zinawakilisha mwangwi wa wahusika na matendo ambayo yamerejelewa katika maudhui riwayani.

Utafiti huu kwa hivyo ulibaini kuwa fasihi ya watoto haikamiliki bila picha na kama wanavyoeleza Nikolajeva na Scott (2001) katika Helmly (2010), mwingiliano baina ya

picha na matini ni tukio lisiloweza kutenganishwa kwa urahisi katika fasihi ya watoto. Kwa hivyo Marantz na Marantz (2013) wamekubaliana na wanavyosema Fang (1996), Mohamed (2015) na wengine kwamba picha katika fasihi ya watoto ni kipengele muhimu na kwamba fasihi ya watoto haikamiliki bila kuwepo kwa picha kwa kuwa ubora wa picha ni mwingi ukilinganishwa na ukosefu wa picha katika matini ya fasihi ya watoto kama walivyopendekeza watafiti wengine.

Kufuatia mchango wa wataalamu hawa, ni dhahiri kwamba picha au michoro katika fasihi ya watoto ni kiunzi muhimu hususan katika fasihi ya watoto kwa vile ndizo rasilimali za kimsingi katika kumpa watoto elimu. Picha au michoro kwa hivyo ni mwangwi ambao unampa ufahamu msomaji, na vilevile kumpa raha katika pekua pekua zake kimatini hali ambayo huchimuza ujumbe uliyomo katika matini

#### 4.2.5 Kuweka msisitizo

Vipengele vya grafolojia vilevile vimetumika kusisitiza maneno mengine katika matini ya fasihi ya watoto.

##### 4.2.5.1 Mandishi yenye rangi tofauti

Rangi ni kipengele cha kimsingi katika uandishi wowote ukiwemo wa matini za kifasihi. Maneno kadhaa katika riwaya tano teule zilizochunguzwa pia yaliendelezwa kwa rangi tofauti na ile iliyotumika katika uandishi wa riwaya hizo kwa ujumla. Katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009), maneno kama vile Mafunzo, Umoja, Wingi (uk.46) na Maswali (uk.47) yaliendelezwa kwa rangi nyekundu. Katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (2006), maneno kama vile Walipendana kama chanda na pete (uk.1), furi (uk.2), tafrija (uk.3), ukarimu, sebuleni miongoni mwa mengine yaliendelezwa kwa rangi

nyekundu. Riwaya ya *Usicheze na Moto* (2003) ina maneno kama vile Usicheze na moto (uk. 1) yakiwa yameandikwa kwa rangi ya samawati. Katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) maneno kama vile sebuleni, kisengeretua, magazeti makuukuu (uk.3) yameandikwa kwa rangi nyekundu.

Kwa hivyo rangi mbalimbali zimetumika katika riwaya tano teule kwa dhima ya kuyawekea maneno hayo msisitizo. Wandishi waliusisitiza msamiati ulioonekana kuwa mzito kwa wasomaji wachanga na pia kuuelezea katika sehemu ya faharasa au kamusi kama ilivyodhihirika miongoni mwa riwaya zilizochunguzwa kama njia mojawapo ya kuwaimarisha wasomaji kimsamiati na kwa hali hiyo, kuboresha ufasiri wa ujumbe uliyolengwa kupitishwa kwa wasomaji lengwa.


Hata hivyo, Leech na Short (1981) wakijadili kuhusu nadharia ya umitindo, walihoji kuwa mandishi kama haya yanahitaji kushughulikiwa katika mhimili wa kiwango cha kigrafolojia kwa kuwa mhimili huu unajishughulisha na sura ya matini kwa mapana kutokana na mapambo ya rangi tofauti katika matini. Kipengele hiki kina mchango mahususi katika ujenzi wa fasihi ya watoto. Pierson (2008:13) alisema kwamba rangi ni kipengele muhimu katika uchapishaji wa makala na kwamba, rangi husisitiza neno lililochapishwa kwa rangi tofauti na ile ya usimulizi.

Kulingana naye, tafiti nyingi zimedhihirisha kuwa msomaji atavutiwa na rangi kabla ya kuisoma kazi hiyo wala kuifasiri. Anauendeleza mjadala huu kwa kusema kwamba kando na kusisitiza msamiati huo katika matini, rangi hiyo pia hutekeleza dhima ya kuleta mvuto kwa kipengele fulani katika matini. Kwa hivyo kulingana na mawazo ya Pierson (2008), dhima kuu inayotekelezwa na maandishi ya rangi tofauti tofauti katika matini ni kuusisitiza msamiati huo.

Matokeo ya utafiti yanashabihiana na mawazo ya watalaam kuhusu kipengele cha rangi katika uandishi. Kutokana na mchango wa watalaam hao, maneno ambayo yamedhihirisha kuendelezwa kwa rangi tofauti na ile ya usimulizi (nyeusi) katika riwaya zilizochunguzwa yamesisitizwa. Msamiati huo huo uliosisitizwa vilevile umetolewa ufafanuzi katika sehemu ya faharasa na pia tamatini mwa riwaya hizo. Kulingana na mtafiti, msisitizo huo unalenga kupanua ufahamu wa msomaji kimsamiati kwa kumfahamisha na kumwelekeza jinsi ya kuyatumia maneno mageni kimuktadha kama wanavyoeleza Cass (1967), Pierson (2008), Ruthiiri (2012), Yu (2014) na wengine.


#### 4.2.5.2 Matumizi ya mkolezo katika matini ya fasihi ya watoto

Mkolezo ulitumika katika ujenzi wa riwaya tano zilizochunguzwa kama inavyodhihirika katika mifano nambari **4.1.6.1** hadi **4.1.6.9.** Katika mifano hiyo, maneno yalikolezwa kwa kutumia wino wenye uzito katika kuyaendeleza. Hii ni kusema ya kwamba mkolezo ulitumika kwa dhima ya kusisitiza maneno fulani miongoni mwa mengine yaliyotumika katika matini katika baadhi ya riwaya zilizochunguzwa kama ilivyo katika mifano miwili iliyo hapa chini.




Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.1.

Maneno yaliyokolezwa ni anwani **Sababu ya Mbuni kuwa na shingo ndefu.**



Mfano kutoka riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk.12.


Maneno yaliyokolezwa ni **Mayai ya Mamba.**

Hata hivyo Anantha (2014) anadokeza kwamba mkolezo hutumiwa kimatini kusisitiza neno bila kuhitilafiana na maana ya neno au maneno yaliyokolezwa kimaana. Maoni ya Anantha (k.h.t) yanashadidiana na ya Manuel & Maria (2014), Macaya & Perea (2014) na wengine ambao kufuatia tafiti zao, waliafikiana kwamba mkolezo katika matini ya kifasihi hutumika kuweka msisitizo kwa neno au maneno yaliyokolezwa kwa kulifanya au kuyafanya maneno hayo kutambulika kwanza kabla ya yale mengine katika mchakato wa utambuzi wa neno kimatini. Wao wametaja jinsi mkolezo katika matini unavyomvutia msomaji kuliko maneno ya kawaida ambayo hayajakolezwa hivyo basi kinadharia, uandishi wa aina hii ni ufundi kwa mujibu wa nadharia ya umitindo.

Leech na Short (1981) wameujadili umitindo huu katika nadharia ya umitindo, ambao wanasema kuwa hutekeleza dhima ya kulifanya au kuyafanya maneno mengine yatokezee zaidi ya yale mengine kimatini. Macaya na Perea (2014) wanaendelea kusema ya kwamba kando na kusisitiza, mkolezo huwa na dhima ya kiujumi katika kazi ya kifasihi. Hii ni kusema kwamba katika kazi za kifasihi, mkolezo unapotumika kimatini, urembo fulani hudhihirika katika fasihi za aina hiyo kama ilivyoshuhudiwa katika riwaya teule zilizochunguzwa. Kwa hivyo katika utafiti huu, mkolezo umetumika kuchimuza msamiati, kusisitiza pamoja na kuimarisha kazi za kifasihi kiujumi.

#### 4.2.5.3 Nafasi ya *mlazo* katika kusisitiza

Kipengele cha *mlazo* kilitumika katika ujenzi na hata uendelezaji wa riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) kama ilivyorejelewa katika mifano nambari **4.1.7.1, 4.1.7.2** na **4.1.7.3.**



heri niziandike nambari za kila gari na aina ya gari na rangi yake. Nitaweza kufahamu magari wanayopenda Wakenya.' Alitabasamu. 'Sasa nimepata mchezo mzuri wa kunisaidia kupitisha wakati kabla Shangazi Wumi hajaja.' Dani alianza kufikiria kama mwanatakwimu.

Alichukua kalamu, karatasi na rula kutoka mezani. Alichora mistari mitatu kuanzia juu hadi chini. Katika kila mstari aliandika: *Aina ya Gari, Rangi na Nambari za Gari.*

Alipomaliza, aliitazama karatasi hiyo kisha akasem
'Sasa niko tayari kuanza mchezo wangu.'


Dani alijiweka tayari karibu na dirisha mahali amba
angeweza kuona vizuri nambari zote za magari. Kila
lililopita, aliandika aina yake:... Toyota, Subaru, Su
na kadhalika. Alifanya kazi hii kwa makini.

Wakati mmoja alijiambia, 'Na hawa Wakenya
apenda magari meupe. Mimi nitanunua gari je

5

Mfano kutoka katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk. 5.

Maneno yaliyolazwa kama inavyodhihirika ni *Aina ya Gari, Rangi na Nambari za Gari.*


Maswali
. Kwa nini Dani akaachwa nyumbani peke yake?
Je, Dani ni kijana wa miaka mingapi?
Je, Dani aliishi mtaa gani?
Dani alikuwa anamngojea nani aje saa tisa?
aada ya kuona vibonzo alienda wapi?
ani aliamua kufanya nini ili kupoteza wakati?
hezo huo ulisaidia polisi kwa njia gani?
i hao walikuwa wanatorokea nchi gani?
aweza kuzitambua nchi hizi ukizipanga
herufi hizi? - *gadanu, niatanza.*
zo gani tunapata kutoka kwa hadithi hii?

Mfano kutoka katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) uk.16.

Maneno yaliyolazwa ni – *gadanu, niatanza.*

Ni maneno macheche tu kama inavyodhihirika katika mifano hiyo yaliyolazwa. Dhima ya wandishi kutumia mandishi yenye mlazo ni kuweka msisitizo katika maneno hayo ili kuyafanya yaonekane zaidi ya mengine. Mlazo pia hutumika katika matini kutambua dhana mpya katika matini kikawaida. Jinsi msomaji apatapo fursa ya kulitambua neno lipya katika matini, ndipo msomaji huyo anapokuwa na fursa njema ya kuufasiri ujumbe uliobebwa na matini vyema. Kwa mujibu wa Macaya na Perea (2014), mlazo katika matini huashiria dhima mahususi katika neno hilo lililolazwa.

Farkas (1983) vilevile anahoji ya kwamba dhima ya kutumia mlazo katika matini ni kuweka msisitizo kwa kuwa mwandishi anahisi ya kuwa msomaji huenda asiwe na

ufahamu kuhusu msamiati ambamo mlazo umetumika, na kwa hali hiyo kumjuza kuwa atauelezea msamiati huo, labda katika sehemu ya faharasa. Hata hivyo, Chukwu (2010) anadokeza ya kwamba, mlazo ni kipengele cha kimsingi katika uandishi kilicho na dhima mahususi kifasihi hivyo basi matumizi yake kimatini yasipuuziliwe mbali.

Emmott na Marc (2014) pia wanasema ya kwamba mlazo hutumika katika matini kuweka msisitizo. Maoni yao yanaungwa mkono na Baazizi (2015:12) anayedokeza kwamba mlazo katika mazungumzo na pia katika mandishi huwa na dhima ya kuweka msisitizo au pia kuonyesha kwamba mandishi yaliyolazwa ni anwani au mada, kutambulisha maneno ya lugha tofauti na ile ya usimulizi pamoja na kutaja majina ya meli, ndege, treni na magari. Mawazo ya Baazizi (k.h.t) yanayashadidia yale ya Waldhorn na Zeiger katika Chukwu (2010) ambao pia wanasema kwamba dhima inayotekelezwa na mlazo katika matini ni kuweka msisitizo katika mandishi.


Kwa kufanya hivyo, msomaji huimarika kimakini anapokumbana na mandishi yaliyolazwa kama ilivyodhihirika katika mifano iliyorejelewa hapo juu. Kwa hivyo maneno yaliyolazwa yamesisitizwa kufuatia huko kulazwa. Matokeo haya yanashadidiana na mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu matumizi ya mandishi ya mlazo. Jinsi Wamitila (2008) alivyoeleza, maneno ambayo huwa yamelazwa hutokezea na kuonekana zaidi katika matini, yakilinganishwa na matini zima. Kwa hivyo kulingana na mtafiti, mandishi yoyote yaliyolazwa kifasihi hutambulika zaidi yakilinganishwa na yale ya kawaida na kwa hali hiyo huwa yamesisitizwa.

### 4.2.6 Kumwekea msomaji kumbukumbu

Kulingana na matokeo ya utafiti, dhima hii imetekelezwa na vipengele anuai vya kigrafolojia.


#### 4.2.6.1 Taipografia na aina mbalimbali za fonti

Kitaipografia, aina mbili za fonti zilidhihirika katika riwaya tano zilizochunguzwa. Aidha fonti hizo zilikuwa *Sans- Serif Futura Md BT* yenye ukubwa wa pika ishirini na nne na *Times New Roman* yenye pika kumi na mbili zinazoonekana kupitia kwa mifano mbalimbali iliyorejelewa.




Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 28.

Katika mfano huu, aina ya fonti iliyotumika ni *Sans- Serif Futura Md BT* yenye ukubwa wa pika ishirini na nne na nafasi kati ya mistari wa milimita tano huku uwazi kati ya maneno ukiwa milimita tatu. Vilevile kuna nafasi inaoyodhihirika kati ya alama ya kiakifishi na neno linalofuatia ambao ni wa milimita tatu.



Wakati wanasubiri viazi viwe tayari, watoto walicheza michezo mingine. Wengine wao waliruka kamba. Wengine wanacheza gololi.
Wengine wanacheza mchezo wa kubahatisha shilingi imefichwa mkono upi. Watoto wote walifurahia michezo hii yao.

8

Mfano kutoka riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) uk. 8.

Aina ya fonti ni iliyotumika katika mfano huu ni *Sans - Serif Times New Roman* pika kumi na mbili. Nafasi kati ya mistari ni milimita nane ilhali nafasi kati ya maneno ni milimita mbili. Vilevile kuna nafasi ya uwazi kati ya neno na alama ya kiakifishi, ambao ni milimita tatu.

Kluck (1972) alipendekeza kuwa maneno yanayotumika katika uandishi wa fasihi ya watoto yawe makubwa na yaliyoandikwa kwa nafasi inayofaa ili kuyavutia makini ya msomaji mchanga kwa lengo la kumwezesha kuufasiri vyeme ujumbe uliolengwa.

Fordonski (1996), Hojjati na Muniandy (2014) miongoni mwa watafiti wanaoshadidia kuwa fonti zinazotumiwa katika uandishi huwa na dhima fulani mahususi. Hojjati na mwenzake (w.h.t) wanasema kwamba fonti ya *Times New Roman* inasomeka vyema hivyo basi ndiyo yenye umaarufu katika uchapishaji wa vitabu na matini nyingi kwa ujumla ilhali ile ya *Futura Md BT 24* ni mwafaka kwa wasomaji chipukizi au wachanga ambao hawana tajriba ya usomaji.

Hojjati na Muniandy (2014) wamesema kwamba matini ni elementi za kimsingi katika uwasilishaji wa ujumbe kati ya tamaduni na pia katika usomaji. Yadav, Chakrabarti na Bisoyi (2017) wamezungumzia aina kuu za fonti na ukubwa na udogo wa fonti katika uandishi wa matini. Kwao, mandishi ya fonti ambazo ni ndogo zaidi ya pointi kumi (fonti10) si bora katika uchapishaji. Hii inatuelekeza katika kujiuliza swali je, uamuzi wa kutumia aina fulani ya fonti katika uandishi ni wa nani? Gutjahr na Benton (2001) wakirejelewa katika Gallagher (2018) wanaonekana kushiriki katika mdahalo huu kwa kuazimia kuchangia katika kulijibu swali hili wanapodokeza kuwa yale yote ambayo yamo katika kitabu, na mfumo wa kitabu si zalisho la mtu mmoja kwa sababu katika ulimwengu wa uchapishaji, wandishi hawaandiki vitabu bali huandika matini.

Kwa mujibu wao, kitabu huzalishwa wakati matini hugeuzwa kwa kuchapishwa, wakati kinapopokea sura mpya kifasihi, sura ya kukiwezesha kutambulika na kukubalika kwa wasomaji wengine. Gutjahr na Benton (2001) wanazungumzia taipografia katika fasihi ya watoto. Kwa mujibu wao, kipengele hiki kina ukuruba na fonti kwa vile kinahusu udogo na ukubwa wa mandishi katika matini. Hata hivyo, ni vyema ifahamike kwamba utafiti huu umezichunguza riwaya teule kwa ukamilifu. Kinadharia, Leech na Short (1981) wamesema kwamba juhudi za nadharia ya umitindo ni kuunganisha uhakiki wa matini na

mchakato wa upokezi wa msomaji kwa dhana zisizo za kifasihi ambazo zikijumuishwa, zina uwezo wa kuimarisha uelewa wa mwitikio kwa riwaya na hadithi kwa ujumla. Hii ni kusema kwamba fonti mbalimbali hutumika kwa lengo la kumwezesha msomaji kusoma hayo matini bila ugumu wowote ili vile vile yaliyosomwa yaweze kuhifadhiwa katika fahiwa za msomaji na yaweze kukumbukika.

Mawazo haya ndio ambayo Wamitila (2008) alisema kuwa mchanganuzi wa kazi za kifasihi anahitaji kutekeleza katika kazi yake kwa kuangazia viwango mbalimbali vya umitindo. Kwa hiyo, imebainika wazi kuwa aina na ukubwa na udogo wa fonti hutegemea kiwango cha umri wa msomaji anayelengwa katika usomaji wa makala hayo, huku wasomaji wachanga mno wakiyafurahia mandishi yaliyo makubuwa ilhali wale wa gredi ya zingine wakiendelea kufurahia mandishi madogo. Hii ni kusema ya kwamba dhima inayotekelezwa na fonti mbalimbali ni kutekeleza mawasiliano vyema kwa kumwezesha msomaji kusoma matini bila ugumu wowote na hivyo basi kuufasiri ipasavyo na hatimaye kupokea vyema ujumbe uliyolengwa na mwandishi na kuuhifadhi.

Vilevile nadharia ya mwitikio wa msomaji inaweka wazi ushahidi kuwa maana katika matini hutegemea utangamano dhidi ya matini na msomaji. Kama alivyosema Bliech (1978) kwamba, maana hihifadhiwa akilini mwa msomaji, maana hiyo inaweza kukumbukika vyema na kurejelewa kutegemea jinsi ilivyorekodiwa katika fahiwa ya msomaji. Ni kwa hali hii ndiposa wandishi na wachapishaji wa matini inayowalenga watoto wanahitaji kutumia vipengele vifaavyo kwa lengo la kukuza ufasiri wema unaoweza kukumbukika kwa urahisi na wasomaji wa umri mdogo.

#### 4.2.6.2 Ukubwa wa riwaya katika fasihi ya watoto

Riwaya tano zilizochunguzwa zilikuwa na ukubwa ufuatao kwa kipimo cha kurasa.


| RIWAYA | UKUBWA / IDADI YA KURASA |
|---|---|
| *Nyumba ya Sungura* (2012) | Kurasa 30 |
| *Hadithi za Mamba* (2009) | Kurasa 47 |
| *Harusi ya Mwanasungura* (2006) | Kurasa 22 |
| *Usicheze na Moto* (2003) | Kurasa 26 |
| *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) | Kurasa 18 |

Hizi kurasa zilijumlisha mandishi pamoja na picha. Dhima ya kuwa na kiwango cha riwaya zenye kurasa chache ni kumwezesha msomaji kuisoma kazi hiyo kwa kipindi kifupi. Makadirio ya kipindi kwa kumrejelea mtafiti ni muda usiozidi dakika sitini, ambayo ni saa moja. Kluck (1972) anahoji kwamba ukubwa wa vitabu vya wasomaji wachanga ni kipengele cha kimsingi katika uteuzi wa fasihi ya watoto kiasi kwamba, kwa wale walio na umri wa chini ya miaka sita, vitabu vyenye kurasa chache na vyepesi kimsamiati ambavyo wana uwezo wa kuvithibiti na kuvisoma kwa kipindi kifupi vitakuwa mwafaka kwao.

Kluck (1972) anaeleza kuwa muda wa kipindi kifupi utamwezesha msomaji mchanga, kwa kutegemea tajriba yake kuisoma aina hiyo ya kazi vyema bila makini yake kuathirika au kusumbuliwa. Hii ni kusema kuwa ikiwa msomaji ataisoma matini kwa muda mfupi kikamilifu, kuna uwezekano wa juu wa kuielewa vyema matini hiyo ambayo kutegemea maudhui, msomaji ataweza kuyakumbuka yale yaliyoangaziwa katika matini.

### 4.2.6.3 Mazoezi na maswali ya ufahamu

Mazoezi na maswali yaliyotumika katika riwaya zilizochunguzwa yamerejelewa katika mifano nambari **4.1.13.1** na **4.1.13.2.**


Zoezi
1. Hadithi hii inahusu wanyama
Taja wanne.
2. Panya na Paka walikuwa
kutembea katika mji fulan
uliitwaje?
3. Ni kwa nini Kaka Sung
kuwatembelea Paka na
kadhaa kabla ya sikukuu

Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Harusi ya Mwanasungura* (Waihiga, 2006) uk. 21.

Haya ni baadhi ya maswali ambayo mwandishi ameyaratibu mwishoni mwa matini. Dhima ya kuwepo kwa vipengele hivi katika fasihi ya watoto ni kuimarisha kiwango cha kumbukumbu za wasomaji. Hii ni kwa kuwa kila wanapoisoma riwaya na kuirejelea sehemu hiyo, uwezo wao wa kukumbuka huimarika na hivyo basi kuwafanya wasomaji kuwa wanafunzi na wanajamii wazuri kwa kuwa kumbukumbu ni upevu unaompa binadamu upekee.

Osborne na Chin (2008) wanaeleza kwamba kuwepo kwa maswali tamatini mwa matini huwa na dhima kuu katika usomaji wa kina, na kwamba ni tukio ambalo halijatafitiwakwa kina. Kwa mujibu wao, maswali humchochea msomaji kushiriki katika midahalo muhimu huku yakiendeleza na kudhihirisha kiwango cha utangamano baina ya mwandishi na msomaji. Hii ni kusema kwamba msomaji anapokumbana na maswali baada ya kuipitia matini, maswali hayo hutekeleza dhima ya kumwezesha msomaji kuyakumbuka aliyoyasoma kimantiki.

Dhima inayotekelezwa na maswali ndio vilevile inayotekelezwa na mazoezi ya ufahamu katika kazi za fasihi za wasomaji wachanga. Kwa vile ni shughuli inayohusu umitindo wa uwasilishwaji wa ujumbe kimaandishi, mhimili wa nadharia ya umitindo unaoafiki uandishi huu ni ule wa sarufi ambao Wamitila (2008) alisema kwamba unajumuisha viwango vya fonolojia na sintaksia. Hii ni kwa vile jinsi maswali na mazoezi hayo yanavyowasilishwa hutegemea kiwango cha msomaji na huchangia katika ufasiri mwema wa msomaji huyo.

Nappi (2018) amezungumzia umuhimu wa kuuliza maswali kama mkakati katika ukuzaji na unoaji wa fahiwa za msomaji. Hii ni kusema kwamba maswali yanayowekwa katika matini humpa msomaji fursa ya kuchochea ufasiri ufaao wa matini ambayo huwa inarejelewa. Kwa mujibu wa utafiti huu, kuwepo kwa sehemu ya maswali na mazoezi tamatini mwa riwaya zilizochunguzwa zilitekeleza dhima ya kumpa msomaji kumbukumbu bora.

### 4.2.7 Kujenga muwala na mshikamano

Fasihi yoyote andishi haiwezi kuwepo bila ya matumizi mema ya lugha. Hii ni kusema kwamba lugha ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa fasihi kimatini. Hata hivyo, lugha inahitaji kutumika kiufundi na mwandishi wa matini ili mwandishi aweze kuifikia azma yake na vilevile ile ya wasomaji kwa kuwa dhima ya mwandishi ni kuhakikisha ya kuwa ujumbe wake umewafikia walengwa. Matini yoyote ikiwemo ile ya kifasihi hujengeka kutokana na jinsi vipashio mbalimbali ambavyo hujumuisha sauti, silabi, virai, vishazi na sentensi hushirikiana.

Kulingana na Wamitila (2008:471), dhana ya muwala hurejelea njia au mbinu za kiisimu zinazofungamanisha au kushikamanisha matini pamoja na kuzifanya kuwa matini. Anaendelea kusema kuwa muwala unahusika moja kwa moja na uchunguzi wa elementi za matini ambazo hufungamanisha sehemu mbalimbali pamoja, jinsi maneno katika sentensi tofauti yanavyohusiana na kurejeleana. Wamitila (k.h.t) anahoji kuwa dhana ya mshikamano ni muhimu katika uchunguzi wa matini au kazi za kifasihi. Mshikamano unahusisha uhusiano kati ya maudhui ya kimatini, ulimwengu wa kimatini na uwasilishwaji au taswira za kiakili za msomaji za ulimwengu wa kimatini.


Dhana hizi zina uhusiano wa karibu sana kwa kuwa matini lazima itumie vipengele vya kiisimu huku mshikamano ukidhihirisha kuwa vipengele hivyo vya kiisimu vimehusishwa au kutumika kimantiki. Ni kwa hali hii ambapo vipengele vya kigrafolojia pia hutekeleza dhima ya kujenga muwala na mshikamano kwa kuhakikisha kwa mfano kuwa sentensi au nomino za pekee hutangulizwa kwa herufi kubwa huku vipengele vingine vikizingatia usarufi unaohitajika.

#### 4.2.7.1. Maumbo mbalimbali ya aya

Kipengele cha aya ni mojawapo ya vijenzi vya kimsingi katika uandishi wowote wenye maana. Kipengele hiki vilevile kilidhihirika katika riwaya tano teule zilizochunguzwa. Kilionekana kujitokeza kwa maumbo mbalimbali. Maumbo ya aya iliyoundwa kwa maneno mawili, aya iliyoundwa kwa sentensi moja miongoni mwa mengine mengi yalidhihirika kama ilivyo katika mifano nambari 4.1.8.1, 4.1.8.2, 4.1.8.3, 4.1.8.4, 4.1.8.5 na 4.1.8.6. Hata hivyo, licha ya maumbo haya tofauti ya aya, dhima iliyotekelezwa na aya katika riwaya tano teule zilizochunguzwa ni kuendeleza mshikamano na muwala katika matini.

**Simba. Simba.  Njoo hapa.**

Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (Bracey & Lieta, 2012) uk. 14.



Huyu ni Mamba.
Mamba huishi mtoni.
Hupenda kulala ukingoni mwa mto.
Anapenda kulala juani.

Mamba ni mnyama mlafi sana.
Anapenda kula nyama nyingi.
Huwala mbuzi na ng'ombe.
Waendapo mtoni kunywa maji,
Mamba huwashika na kuwala.

2

Mfano huu umetolewa katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (Bracey & Lieta, 2009) uk. 2.

Wamitila (2008) katika kuichanganua mihimili ya nadharia ya umitindo ameelezea mhimili wa sarufi. Kulingana naye, teneti hii hujumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia katika grafolojia. Kwa kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu katika kazi za kifasihi, basi sifa na matumizi yake huwa na athari kubwa katika uchanganuzi wa matini za kifasihi.

Hii ni kusema kuwa jinsi mwandishi anavyoyateua maneno katika matini hutekeleza dhima muhimu katika uwasilishwaji wa maudhui. Ni kwa hali hiyo ndiposa usahili, uambatani na uchangamani wa vijenzi vya aya vimerejelewa. Kulingana na mtafiti, msingi mwafaka wa kazi ya fasihi kwa msomaji mchanga ni usahili na anapoendelea kuimarika kitajriba, uambatani na kisha uchangamani wa matini unaweza kufasiriwa ipasavyo.

Le (2004) anadokeza kuwa aya katika matini inatekeleza dhima ya kuendeleza mshikamano katika matini. Wali na Madani (2020) wamesisitiza ya kwamba kilicho muhimu katika aya ni umoja, mshikamano na muwala katika aya nzima. Hata hivyo, kulingana na utafiti, aya sahili ni mwafaka kwa ufasiri wa msomaji wa gredi ya kwanza, na aya hiyo inaweza kuungwa vipengele vingine ikawa ambatani na kisha changamani kutegemea hali ya kuimarika kwa kiwango cha ufasiri na gredi ya msomaji kama ilivyojitokeza katika mifano mbalimbali ya aya zilizorejelewa.

Kwa mujibu wa Wali na Madani (2020), muundo wa aya ndicho kipengele kigumu mno kutafitiwa katika taaluma ya isimu kifasihi kwa kuwa sentensi kadhaa zinaunganishwa kwa njia ya kuleta mshikamano na muwala kuhusu tukio moja. Wamebainisha vijenzi kadha vya aya ambavyo vinajumulisha mwanzo, mwili na kisha hitimisho katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, ni wazi kuwa mtazamo wao umejikita katika hali ya uandishi wa

kawaida katika lugha ya Kiingereza. Aya zilizotolewa mifano katika riwaya teule zilizochunguzwa zilikiuka kaida zilizozoeleka kimaandishi kwa kuwa baadhi zina maneno machache huku zingine zikikamilika kwa sentensi moja tu. Urejeleo wa fasihi ya watoto kama alivyoeleza Cass (1967) ulitaja suala la usahili wa lugha na lengo la kumwezesha msomaji mchanga kung'amua ujumbe uliyomo. Wamitila (2008) anaongeza kuwa fasihi ya watoto iwe yenye msuko mwepesi na lugha nyepesi yenye maelezo mafupi.

Kulingana na nadharia ya umitindo, mwandishi wa kazi ya fasihi ameruhusiwa kukiuka kaida zilizozoeleka kama vile miundo ya aya hizi ilivyokiuka ukawaida. Kwa mujibu wa teneti ya nadharia ya umitindo ya uteuzi katika fasihi, mwandishi ana uhuru wa kuzikiuka kaida zilizopo kutokana na sababu nyingine za kiujumi au kiumbuji, kiitikadi, kimtazamo na kadhalika. Kwa hali hii, kuna uwezekano wa kuwepo kwa aya zenye maumbo tofauti kimatini kama inavyodhihirika katika mifano iliyorejelewa.

Vilevile katika nadharia ya mwitikio wa msomaji, mhimili wa usomaji kama tukio la kimapatano unampa msomaji uhuru wa kuibua ufasiri mbalimbali wa matini bila kushurutishwa. Hii ni kusema kwamba miundo hii ya aya inaafiki nadharia za utafiti. Kwa hiyo, usahili wa aya pamoja na ukiukaji wa miundo kama wanavyoangazia Wali na Madani (2020) ni mwafaka katika kuendeleza utanzu wa riwaya za fasihi ya watoto. Kwa mujibu wa maoni yao, utafiti huu umebaini kuwa muundo wa aya uliyo mwafaka ni aya sahili kama ilivyodhihirika katika mifano iliyowasilishwa.

#### 4.2.7.2 Usahili wa matini

Kati ya riwaya tano teule zilizochunguzwa, riwaya tatu za *Nyumba ya Sungura* (2012), *Hadithi za Mamba* (2009) na *Harusi ya Mwanasungura* (2006) zilidhihirisha usahili katika msamiati na pia katika sentensi zilizotumika kuziendeleza. Hii ni kusema ya kwamba katika riwaya hizo tatu, usahili ulidhihirika. Dhima ya kutumia usahili wa aina hii ilikuwa kumwezesha msomaji kujifahamisha na usomaji wa matini ya Kiswahili kwa kuwa ni safari inayoimarika hatua kwa hatua. Riwaya hizi ziliwalenga wanafunzi katika gredi za chini kama vile gredi ya kwanza, gredi ya pili na gredi ya tatu. Riwaya za *Usicheze na Moto* (2003) na *Dani na Wezi wa Toyota* (2015) zilionekana kuwa changamano kwa kuwa ziliwalenga wasomaji ambao kwa kiasi fulani walikuwa wameanza kupevuka akili kwa kuwa wanafahamu kusoma na pia kutamka maneno mbalimbali kutokana na tajriba walio nayo.

#### 4.2.7.3 Vielelezo na majedwali

Vielelezo au majedwali vilevile yalidhihirika katika badhi ya riwaya tano zilizochunguzwa kama ilivyo katika mifano nambari **4.1.12.1** na **4.1.12.2**. Matokeo ya utafiti yalibaini kwamba vielelezo au majedwali hutekeleza dhima ya kumpa msomaji uzoefu na vilevile kumfafanulia msamiati ambao mwandishi anakisia kuwa huenda unaweza kumpa msomaji changamoto. Miongoni mwa riwaya, sehemu hii imejitokeza kama zoezi ilhali kwingine imeangaziwa kama kamusi ama ufafanuzi wa maneno magumu. Hii imefanyika kwa matarajio kwamba wasomaji wanaolengwa huenda wakakosa ufahamu wa kutumia kamusi.

Matokeo haya yanashabihiana na maoni ya Ruthiiri (2012) anayesema kwamba ni vyema kwa mwandishi na mchoraji wa majedwali au vielelezo kuhakikisha ya kwamba vipengele hivi vinawasilishwa kwa namna ya kueleweka kwa haraka ili msomaji mchanga aweze kuufasiri ujumbe uliolengwa katika matini vyema kwa kutathmini hali ya vielelezo au majedwali na ujumbe unaolengwa kuwasilishwa. Hata hivyo, anasema kwamba vielelezo au majedwali hudhamiriwa kumwezesha msomaji kuutumia msamiati huo kwa njia fasaha anapokumbana nao katika matini nyingine.

Kulingana na nadharia ya umitindo, majedwali yana dhima inayoendana na mhimili wa kiwango cha grafolojia kinachohusu maandishi. Kwa kuwa fasihi haiwezi kumfikia msomaji kimatini bila kuandikwa, maelezo na ufafanuzi kuhusu msamiati uliotumika katika kuwasilisha ujumbe kama vifanyavyo vielelezo, vya kiisimu na visivyo vya kiisimu huchangia katika kuimarisha ufasiri wa ujumbe uliolengwa na mwandishi. Hii ni kusema kwamba ni vyema ikiwa fasihi ya wasomaji wachanga itajumuisha sehemu ya majedwali.

### 4.3 Muhtasari na athari ya vipengele mbalimbali vya grafolojia

Madhumuni ya tatu ya utafiti yalilenga kutathminia vipengele vya kigrafolojia katika uchimuzi wa maudhui. Utafiti ulibaini kuwa grafolojia na vipengele vyake huathiri msomaji kwa njia mbalimbali huku mojawapo ya athari hiyo ikiwa uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto.

#### 4.3.1.1 Grafolojia na uchimuzi wa maudhui miongoni mwa wasomaji


Mtafiti katika jitihada za kubaini athari ya vipengele vya kigrafolojia kwa wasomaji wachanga wa fasihi ya Kiswahili, aliiteua shule ya msingi ya Mumias Central

kidhamirifu miongoni mwa shule tatu alizozitafitia na vilevile akaiteua riwaya ya Kiswahili ya *Usicheze na Moto* (2003) kidhamirifu kwa kuwa alidhamiria kukusanya data ya kutosha ya kushughulikia madhumuni ya tatu. Kwa hivyo mtafiti aliweza kuyashughulikia madhumuni ya tatu kwa kutumia data iliyokusanywa na kuchanganuliwa kutoka riwaya asilia na riwaya mwigo. Ilikuwa riwaya mwigo kwa kuwa mtafiti alivichuna kwa kuviondoa vipengele vyote vya kigrafolojia ambavyo mwandishi alivitumia katika ujenzi wa riwaya asilia.

Pia mtafiti alitunga maswali matano ambayo alinuia kutumia kama kigezo cha kupimia athari ya vipengele vya kigrafolojia kwa uchimuzi wa maudhui miongoni mwa watafitiwa walioteuliwa. Jumla ya riwaya mwigo ishirini ziliundwa na kuwekewa msimbo wa nambari moja hadi ishirini ili kubana kutambuliwa kwa moja kwa moja kwa watafitiwa. Baadaye, mtafiti alizuru shule ya msingi ya Mumias Central kwa lengo la kukusanya data kulingana na madhumuni ya tatu ya utafiti. Shule iliyoteuliwa ilikuwa kiwakilisha cha shule teule tatu ambamo utafiti huu ulifanywa. Mtafiti alitangamana na wanafunzi waliokuwa watafitiwa walengwa ili kujifahamisha na zoezi la ukusanyaji wa data kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti.


Mtafiti alidhamiria kuwatathmini wanafunzi wa gredi ya nne katika shule teule kutokana na upevu na tajriba yao ya usomaji, na baada ya kushauriana na mwalimu mkuu, mtafiti alielekezwa kwa darasa la 4C lililokuwa na wanafunzi hamsini. Mtafiti aliitumia fursa hiyo kuvifanyia jaribio vifaa vyake vya ukusanyaji data ambavyo vilikuwa orodha ya maswali katika riwaya mwigo na vilevile katika riwaya asilia. Baadaye, mtafiti aliwateua wanafunzi ishirini kwa kutumia usampulishaji sahili kinasibu kutoka gredi ya 4C na kisha akampa kila mtafitiwa nakala mwigo na nakala asilia ya *Usicheze na Moto* (2003). Kila

mwanafunzi alihitajika kuisoma riwaya hiyo mwigo na riwaya asilia na kisha kujibu maswali matano yalioorodheshwa tamatini mwa kila nakala ya riwaya kama ilivyo katika kiambatisho nambari 45. Utathmini huo uliendelezwa vyema na ulichukua muda wa saa moja na dakika ishirini. Watafitiwa waliweza kuyashughulikia maswali yaliyolengwa kwa kutoa majibu mbalimbali, matokeo hayo yameonyeshwa katika jedwali linalofuata.




**Jedwali la 1: Matokeo ya utathmini wa wanafunzi kuhusu athari ya grafolojia kwa watafitiwa**

Hili jedwali la kwanza (1) linalowakilisha matokeo ya utathmini wa wanafunzi kuhusu athari ya grafolojia kwa watafitiwa, kwa kutumia riwaya mwigo ya *Usicheze na Moto* (2003).




**Jedwali la 2: Matokeo ya utathmini wa athari ya vipengele vya kigrafolojia kwa kutumia riwaya asilia ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003)**

Jedwali hili la pili (2) linawakilisha matokeo ya utathmini wa athari ya vipengele vya kigrafolojia kwa kutumia riwaya asilia ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003).

Katika swali la kwanza ambalo watafitiwa walihitajika kuipa riwaya mwigo na riwaya asilia anwani mwafaka, watafitiwa wanane (8) waliipa riwaya mwigo anwani ya **Leo ni siku ya Jumamosi / siku ya kupumzika,** ambalo lilikuwa jibu sahihi ilihali watafitiwa kumi na wawili (12) walipotoka. Watafitiwa ishirini (20) waliotathminiwa katika riwaya asilia waliipa riwaya hiyo anwani sahihi vilevile.

Katika swali la pili ambalo watafitiwa ishirini (20) waliulizwa kwa nini watoto hawakwenda shuleni siku hiyo, watafitiwa ishirini wote (20) walijibu ya kwamba **Ilikuwa siku ya Jumamosi / kupumzika** katika riwaya mwigo na vile vile katika riwaya asilia. Kwa hivyo watafitiwa wote walikuwa na jibu sahihi. Katika swali la tatu, watafitiwa walihitajika kueleza chochote kilichowavutia katika riwaya waliyoisoma.

Watafitiwa wanane (8) waliotoa majibu yao katika riwaya mwigo walijibu **michezo mbalimbali** huku watafitiwa kumi na wawili (12) wakipotoka ilihali watafitiwa wote ishirini walijibu michezo mbalimbali katika riwaya asilia, ambalo lilikuwa jibu sahihi. Swali la nne liliwahitaji watafitiwa kutaja michezo mitano iliyochezwa na watoto. Watafitiwa wote ishirini (20) walitaja michezo ya kibe, gololi, kubahatisha shilingi, nijifiche unifichue, kuruka kamba na kupika katika riwaya mwigo na pia katika riwaya asilia.

Katika swali la tano, watafitiwa walihitajika kueleza maudhui yaliyodhihirika katika riwaya. Watafitiwa kumi na watatu (13) walijibu kuwa si vizuri kuchezea moto katika riwaya mwigo, ambalo lilikuwa jibu sahihi huku watafitiwa saba (7) wakapotoka ilhali watafitiwa kumi na saba (17) walijibu usicheze na moto huku watafitiwa watatu (3) wakipotoka katika riwaya asilia. Kufuatia majibu yaliyodhihirika katika tathmini ya riwaya mwigo na riwaya asilia ya *Usicheze na Moto* (2003), inabainika kuwa vipengele

vya kigrafolojia huathiri uchimuzi wa maudhui katika fasihi, hususan fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Majibu yaliyotolewa na watafitiwa katika tathmini ya riwaya asilia na tathmini ya riwaya mwigo yalilinganishwa, na matokeo yalionyesha kuwa vipengele vya kigrafolojia vilikuwa kama mwangwi wa maudhui ambayo mwandishi alilenga kuyawasilisha kwa kuwa, vilimpa mtafitiwa mwanga kuhusu ujumbe ambao ulirejelewa na mwandishi katika riwaya asilia. Vilevile, iliweza kubainika kuwa mtafitiwa alichukua muda mfupi wa takriban dakika arobaini kuishughulikia riwaya asilia kwa kuisoma na kujibu maswali yaliyoambatishwa katika riwaya hiyo kufuatia kuwepo kwa vipengele mbalimbali vya kigrafoloji, ikilinganishwa na muda mrefu wa zaidi ya saa moja na dakika ishirini uliotumika kusoma na kujibu maswali katika riwaya mwigo. Hii inaonyesha kuwa vipengele vya kigrafolojia huimarisha uchimuzi na kisha ufasiri wa maudhui katika matini.

Matokeo haya yanatuchochea kukiri ya kwamba riwaya ambayo imejengeka kwa vipengele vya kigrafolojia, na msomaji ana ujuzi wa kuweza kuvifasiri vipengele hivyo, huweza kueleweka vyema na kwa haraka ikilinganishwa na ile isiyo na vipengele hivyo. Matokeo haya yanashadidiana na matokeo ya utafiti wa Aggleton (2017). Aggleton (k.h.t) alifanya utafiti kuhusu athari ya vipengele vya grafolojia katika kazi ya Jim Kay kuhusu usomaji wa *A Monster Calls*. Katika utafiti wake, wasomaji wachanga sita (6) wa kati ya umri wa miaka kumi na moja (11) na kumi na minne (14) waliteuliwa. Miongoni mwao, wasomaji watatu walipewa kitabu kilichojumuisha mseto wa matini na michoro ilhali watatu walipewa kitabu kilichojumuisha matini pekee.

Matokeo ya utafiti huo yalibaini kwamba wasomaji wachanga waliopewa kitabu kilichojumuisha matini na picha walidhihirisha ufahamu wa kina wa ujumbe uliokuwa katika kitabu hicho, huku wakivutiwa na kitabu hicho, wakilinganishwa na wale ambao kitabu chao kilikuwa na maandishi pekee bila picha na michoro. Hii inaashiria kuwa bila shaka vitabu vinavyojumuisha matini na picha vinapendwa na wasomaji wachanga, na kuwa raslimali za picha na michoro huwa na athari ya kuimarisha ufasiri wa ujumbe katika matini. Kwa hali hiyo, hii huchimuza maudhui ambayo huwa yamebebwa katika matini.

Akichangia kuhusu athari ya vipengele vya kigrafolojia katika matini za fasihi ya watoto, Abaci (2014) alisema kuwa vitabu vizuri vya watoto ni vile ambavyo vinajumuisha maneno na picha au michoro kwa njia iliyo ya kipekee ambavyo ni vyema kwa ufasiri, mvuto wa kihisia, mawazo pamoja na ulimwengu mzima wa ubunifu na ambavyo vilevile huwa na maudhui yanayoafiki mahitaji ya watoto na usomaji wao. Hii ni kwa kuwa michoro na picha miongoni mwa raslimali zingine katika matini, huwa na athari kuhusu ufasiri wa maudhui. Utafiti huu uliangazia moja kwa moja athari ambayo inatokana na baadhi ya vipengele vilivyodhihirika katika riwaya zilizotafitiwa na ukabaini kuwa vipengele hivi huchimuza maudhui kifasihi.

Katika hali ya kawaida, ufasiri wa ujumbe unaobebwa na matini ni miongoni mwa changamoto zinazowakumba wasomaji katika viwango mbalimbali vya ujifunzaji. Hii ni kwa sababu ni nadra katika hali ya kawaida kwa msomaji yeyote wa kazi ya kifasihi kumwandama mwandishi wa kazi fulani kwa lengo la kumsaili ili apata mwanga kuhusu ujumbe ambao mwandishi huyo huwa amenuia kuuwasilisha kupitia kwa kazi yake anavyoifinyanga hivyo. Kwa hivyo msomaji anasalia tu na njia ya kutumia ujuzi na

tajriba aliyonayo katika kumwelekeza kwa ufasiri mwema wa ujumbe au maudhui katika matini. Hata hivyo hii huwawia vigumu wasomaji wachanga kwa kuwa hawana tajriba ya kuwawezesha kuufasiri vyema ujumbe uliolengwa na mwandishi wa matini. Kwa hivyo ufasiri wa matini ni shughuli ambayo inahitaji umakinifu na ujuzi mpana kwa kuwa waandishi mbalimbali hudhihirisha upekee katika kazi zao kimaandishi.

Kupitia utafiti huu, ilibainika kwamba vipengele mbalimbali vya kigrafolojia huwa na athari ya kuyachimuza maudhui kwa njia mbalimbali katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Kwanza, vipengele hivi humvutia msomaji katika usomaji na anapovutiwa, makini yake huwa imedhibitika na mnato huwa katika matini. Kisha mnato huo humchochea msomaji kusoma matini na hata kulinganisha anachosoma na picha zinazodhihirika katika matini hiyo. Kwa hali hiyo, msomaji huitalii matini kwa jicho pekuzi, akiuandama msamiati na ufundi wote ambao mwandishi huwa ameufungamanisha katika jitihada zake za kuiandika kazi yake. Matokeo ya shughuli za msomaji ni ufasiri unaofaa wa ujumbe ambao mwandishi wa kazi ya matini huwa amelenga kuuwasilisha.

Kutokana na uchanganuzi wa data iliyokusanywa kupitia usaili usio rasmi wa walimu, ilibainika kuwa wengi wa walimu walifahamu tu picha mbalimbali pamoja na rangi kama vijenzi vikuu katika taaluma ya fasihi ya watoto, kuashiria kuwa hawakuwa na ujuzi au ufahamu wa kina kuhusu grafolojia na vijenzi vyake. Vilevile wengi wa walimu walifahamu ya kwamba dhima ya kimsingi iliyotekelezwa na vipengele hivyo ilikuwa ya kiujumi tu kutokana na jinsi walivyojibu maswali kwa kushikilia kuwa kazi za kifasihi zinazowalenga watoto lazima ziwe za kuvutia. Kwa hivyo ilibainika kuwa idadi kubwa

ya walimu hawakuelewa athari inayotekelezwa na vipengele vingine vya kigrafolojia katika uchimuzi wa maudhui.

Hata hivyo usaili huo usio rasmi ulichangia pakubwa katika ukusanyaji wa data ya kimsingi. Usaili usio rasmi unahusu kutozingatia mfululizo wa maswali kama yalivyoorodheshwa katika orodha ya maswali kwa kuwa mtafiti analazimika kuelezea zaidi au kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu anachokitafitia kwa watafitiwa, na hata wakati mwingine kuepuka kuuliza baadhi ya maswali ambayo mtafiti huwa amelenga kuangazia kama ilivyodhihirika katika usaili usio rasmi wa mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya kwanza katika shule ya msingi ya Mtakatifu Anna ya Mumias. Mtindo huu wa usaili usio rasmi unamwezesha mtafiti kumwelekeza mtafitiwa kwa lengo la kupata data toshelevu. Usaili usio rasmi uliunufaisha utafiti huu kwa kuwa uliwachochea watafiti kujieleza kikamilifu kuhusu walichofahamu na wasichofahamu kulingana na vijenzi vya kimsingi vya fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Kando na usaili usio rasmi wa walimu wanne, mmoja katika kila gredi, wanafunzi wanne kutoka katika kila gredi vilevile waliweza kushirikishwa katika usaili usio rasmi kama inavyodhihirika katika kiambatisho nambari tisa (9). Majibu hayo yaliyotokana na usaili usio rasmi wa wanafunzi, mmoja mmoja kutoka katika gredi ya kwanza, gredi ya pili, gredi ya tatu na gredi ya nne, na unatupa mwanga kuhusu athari inayotokana na vipengele vya kigrafolojia katika ufasiri wa maudhui. Hata hivyo, kutegemea utofauti wa viwango vya wasomaji, ilibainika kuwa vipengele vya kigrafolojia ni vijenzi vya kimsing katika fasihi ya watoto ya Kiswahili, hususan picha na rangi. Kwa mfano msailiwa wa gredi ya nne (4E) alikiri kufurahishwa na kurasa chache za riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (Ngugi, 2015) ambayo aliweza kusoma kwa muda mfupi huku picha zenye rangi

nzuri, maelezo ya maneno magumu na maswali yakimwezesha kuelewa ujumbe ambao mwandishi alilenga kuuwasilisha.

Msailiwa mmoja wa darasa la tatu Magharibi aliweza kuelewa umuhimu wa urafiki wa dhati na maadili mema kutokana na uhaini wa Panya na mkewe kupitia kwa picha za wanyama Paka, Panya na Sungura pamoja na familia zao katika riwaya ya *Harusi ya Mawanasungura* (2006). Msailiwa mmoja wa wa gredi ya 2W alionekana kufurahia miondoka ya Mamba kama afanyavyo binadamu, na vipengele vya kigrafolojia vikamwezesha kuelewa tabia ya Mamba, mojawapo ya tabia ikiwa ulafi au kukuwa na mate mengi kwa Mamba, huku Sungura akionekana mwenye mikakati maarufu miongoni mwa wanyama wa porini katika riwaya ya *Hadithi za Mamba* (2009). Msailiwa wa kwanza wa gredi ya 1E ameonekana kuathirika na rangi mbalimbali, huku akitambua kuwa Sungura alikuwa amevalia nguo ya rangi ya *'red'* katika riwaya ya *Nyumba ya Sungura* (2012).

Hii ina maana kuwa vipengele vya kigrafolojia huchangia pakubwa katika uchimuzaji wa maudhui na ufasiri wa ujumbe ambao wandishi hulenga kuuwasilisha kupitia matini zao. Matokeo haya yanashadidia maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu namna vipengele vya grafolojia vinavyoathiri uchimuzi wa maudhui katika tanzu mbalimbali za kifasihi, ikiwemo riwaya za watoto katika Kiswahili.

Utafiti huu uliibua matokeo tofauti tofauti ambayo yanahusiana moja kwa moja na shabaha na madhumuni ya utafiti. Aidha vipengele mbalimbali vya kigrafolojia viliweza kuibuliwa huku athari ya vipengele hivyo ikielezwa waziwazi. Matokeo ya utafiti yaliweza kuongezea kwa orodha ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo havikutajwa awali na watalaam ambavyo ni maswali, mazoezi, faharasa na majedwali  miongoni mwa

vipengele vingine ambavyo hutekeleza dhima mahususi na huwa na athari mbalimbali katika ujenzi wa kazi za kifasihi, hususan riwaya ya watoto ya Kiswahili.

Utafiti ulibaini kuwa viakifishi huwa na athari kubwa katika maandishi yoyote, yawe ya kifasihi au ya kiisimu na kwa hivyo huathiri ufasiri wa ujumbe uliobebwa na mandishi hayo. Kama anavyosema Nordquist (2016), matumizi ya viakifishi kwa njia ya kawaida na hata kwa njia isiyo ya kawaida, au hata upachikaji kiakifishi pasivyo katika mandishi huathiri maana ya matini. Lauchman (2010) aliviita viakifishi msimbo, na akasema ya kuwa msimbo huu hutenganisha sehemu za sentensi na kwa hali hiyo huathiri ufasiri unaobebwa na vipashio vyovyote vya lugha kimaana.

Ujumbe unaolengwa kuwasilishwa na matini ndio maudhui yanayoendelezwa na mwandishi wa kazi ya fasihi. Hii ni kusema ya kwamba viakifishi huathiri matini, kwa kuipa matini hiyo maana, na kwamba, mandishi yoyote yasiozingatia matumizi mema ya viakifishi huwa hayawezi kufasiriwa vyema. Kama vile mhimili wa nadharia ya mwitikio wa msomaji wa usomaji kama tukio la kimapatano unavyoshikilia ya kwamba maana kimatini huibuliwa kufuatia kutangamana kwa msomaji na matini, usomaji mwema na uibuliwaji wa maana vyema hutegemea matumizi mema ya viakifishi, kiasi kwamba bila viakifishi, matini huwa haina maana. Kwa hivyo viakifishi vina athari ya kumdhibiti msomaji katika kuufasiri vyema maudhui kifasihi.

Herufi kubwa inatumika kimatini kuyapa maneno mengine hadhi ya juu dhidi ya maneno mengine ambayo huenda yakatumika kikawaida katika matini. Hii hadhi ya juu kwa hivyo huyafanya maneno hayo kupandishwa ngazi kwa kuonekana tofauti na yale maneno ya kawaida na huko ni kuyachimuza maneno hayo. Athari inayomjia msomaji ni kumakinikia msamiati ambamo herufi kubwa huwa imetumika.

Treimen na Kessler (2004) katika utafiti wao wa kubaini athari ya herufi kubwa kwa wasomaji wachanga walitambua kuwa matumizi ya herufi kubwa huathiriwa na tawi la isimu la fonolojia, na kuwa msomaji mchanga ambaye alidhihirisha uzoefu wa kuitwa jina fulani aliweza kuandika neno lililoendana na sauti hiyo kwa kuchanganya herufi kubwa huku akiashiria upekee. Hii ni kusema kuwa herufi kubwa inatumika katika miktadha ya kipekee na inapofanyika hivyo, huashiria umuhimu wa ujumbe ambao huwa umelengwa ambao huwa umechimuzwa.

Picha na michoro katika matini huwa na athari nzito. Kando na kuleta uhalisia katika matini, hususan ikiwa mifano ya picha au michoro inayorejelewa ni ya viumbe wanaopatikana katika ulimwengu halisi wa msomaji kama anavyosema Heinsbergen (2013), picha huimarisha ufasriri wa maudhui katika matini za kifasihi na hususan fasihi za watoto katika Kiswahili. Anasema kuwa vitabu vyenye picha humpa msomaji fursa ya kujifahamisha na fasihi kiupeo ulimwenguni. Hi ni kwa sababu msomaji hunufaika kwa kuelekezwa na maneno, kuelekezwa na picha au michoro na ujumbe kamilifu unaoendelezwa na vipengele hivi vyote. Ujumbe unaoangaziwa na vipengele hivyo hauwezi kukinzana na maudhui yaliyolengwa kuwasilishwa na mwandishi.

Hata hivyo, matokeo haya yanakinzana na walivyopendekeza akina MacCann na mwenzake (1973), Peeck (1974), Beck (1984) na wengine walioonelea ya kwamba picha katika matini huathiri wasomaji visivyo huku wakipendekeza utungaji wa riwaya zisizo na picha kwa madai kwamba picha huhitilafiana na usomaji na ufasiri wa matini. Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yanaunga mkono mawazo ya watafiti wengi wa fasihi ya watoto wanaoshikilia kwamba, fasihi ya watoto haikamiliki bila kuwepo kwa picha wala mchoro. Katika maandalizi na ujenzi wa kazi zao, wandishi wa riwaya hizi walihakikisha

ya kwamba picha na matini zinatumika vyema katika matini zao kulingana na mawazo ya Wamitila (2008) na watalaam mbalimbali wa fasihi ya watoto.

Wamitila (2008) katika kueleza kuhusu mhimili wa nadharia ya umitindo wa miundo ya lugha alitaja picha. Alisema ya kwamba picha zinatumika katika fasihi kijazanda ambako zinaweza kuwa jazanda za kimaelezi zinazotumia maneno au jazanda za kiishara ambazo zitawakilishwa kupitia kwa picha au michoro. Linalobainika katika mchakato huu ni kwamba kwa kweli, fasihi ya Kiswahili ya watoto haikamiliki bila kazi hiyo kuhusishwa moja kwa moja na picha au moja kwa moja na michoro ambayo athari yake kwa msomaji ni kuimarisha uchimuzi wa maudhui.

Kama anavyosema Rosenblatt (1988), kupitia mhimili wa nadharia ya mwitikio wa msomaji wa usomaji kama tukio la kimapatano, kwamba maana katika shughuli za usomaji ni mapatano, mapatano hayo vilevile huathiriwa na mazingira yanayoizunguka matini. Hii ni kusema ya kwamba ikiwa matini yameandamana na picha au michoro, msomaji ana uwezo wa kuibua ufasiri mwema kwa vile ule ufasiri utategemea moja kwa moja picha au michoro na matini katika muktadha huo. Kwa ufupi, matini iliyo na picha au mchoro inaibua ufasiri mwema wa msomaji na hivyo basi ujumbe aliyolenga kuwasilisha mwandishi humfikia msomaji kwa njia iliyo rahisi.

Jicho la mwanadamu lina uwezo wa kuzitambulisha aina nyingi za rangi. Kila mojawapo ya riwaya tano teule zilizochunguzwa zilidhihirisha matumizi ya aina mbalimbali za rangi ambapo kulibainika kuwepo kwa rangi ng’avu na zisizo ng’avu. Rangi hizi zilitumika kuimarisha uchimuzi wa maudhui. Kwa mfano katika riwaya ya *Dani na Wezi wa Toyota* (2015), gari aina ya Toyota lililoripotiwa kuibwa lilikuwa la rangi nyekundu na mwandishi aliitumia rangi nyekundu katika picha ya gari linalorejelewa. Kwa hali

hiyo, ule ujumbe unaorejelewa riwayani humo humfikia msomaji moja kwa moja huku taswira ya gari lililoripotiwa kuibiwa ikijitokeza waziwazi akilini mwake.

Fetic (2014) anasema ya kwamba rangi katika matini hutumika kuleta athari ya hisia ili kuwasilisha toni na uhalisia wa tukio fulani. Nao Olurinola na Tayo (2015) wanasema ya kwamba rangi ina athari kuu katika uhifadhi wa kumbukumbu miongoni mwa wasomaji. Wamebainisha kuwa aina mbalimbali za rangi zina athari ya kuchochea uwezo wa msomaji wa matini wa kuyakumbuka yale aliyoyasoma katika matini na kwamba, rangi mbalimbali zinahitaji kutumika katika kuvitambulisha vipengele vya uandishi ikiwemo hoja muhimu inayostahili kumfikia msomaji.

Rosenblatt (1988) katika mchango wake wa nadharia ya mwitikio wa msomaji anazungumzia mhimili wa usomaji kama tukio la kiwakati. Anataja mchango wa dhima ya kiujumi katika matini ambayo athari yake huwa ni kumpa msomaji kumbukumbu. Bila shaka kumbukumbu njema huibuliwa na ufasiri mwema wa matini ambao huiweka picha fulani akilini mwake. Kwa hali hiyo rangi mbalimbali katika matini na hata katika picha huwa na athari ya kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu ya msomaji, tukio ambalo moja kwa moja linawiana na uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Matini ni mkusanyiko wa herufi zilizochapishwa kwa mtindo na kwa kipimo fulani. Matini iliyoandikwa vyema humwezesha msomaji kuisoma kwa kasi inayofaa bila ugumu wowote na hatimaye humuathiri kwa kuimarisha ufasiri wa maudhui na pia humwekea kumbukumbu mwafaka kama wanavyoeleza Hojjati na Muniandy (2014). Hii ni kwa sababu matini ni kipengele cha kimsingi katika uwasilianaji. Matokeo ya utafiti huu yalibaini ya kwamba taipografia kwa ujumla huimarisha ufasiri wa maudhui katika riwaya teule zilizochunguzwa. Ifahamike kuwa kama wanavyosema Hojjati na Muniandy

(w.h.t) usomaji wa matini wazi ni njia mojawapo ya kuashiria mawasiliano na usomaji mwema unahusu moja kwa moja jinsi matini ilivyowasilishwa, suala ambalo pia hutupa mwanga kuhusu mwandishi na tajriba yake pamoja na ujumbe alionuia kuwasilisha.

Fetic (2014) amesema ya kwamba matini ni zao la kimsingi la sayansi ya taipografia na ufundi, na kwamba matini nzuri lazima idhihirishe uwezo wa kusomeka dhahiri. Hata hivyo kusomeka kwa matini kunaweza kutazamwa kwa njia mbili: jinsi matini ilivyopangika vizuri na pia jinsi matini inavyoweza kufasiriwa kwa njia iliyo sahili. Matini bora lazima idhihirishe uwazi mwafaka ili iweze kufasiriwa vyema na wasomaji wa viwango tofauti. Hii ni kumaanisha ya kwamba ukubwa wa fonti na nafasi pana kati ya maneno na mistari huathiri usomaji na ufasiri mwema wa maudhui kutegemea kiwango cha umri wa msomaji.

Utafiti huu ulibaini ya kwamba msomaji mchanga wa gredi ya kwanza na gredi ya pili anasoma na kufasiri vyema matini iliyoandikwa kwa fonti kubwa na ambayo vilevile hudhihirisha upana mkubwa kati ya maneno na mistari ilhali msomaji wa gredi ya tatu na gredi ya nne hupendelea mandishi yenye fonti ndogo na pia nafasi iliyobanwa kati ya maneno na mistari. Hii ni kutokana na tofauti ya tajriba ya wasomaji wa viwango hivi. Kwa hivyo nafasi iliyodhihirika katika riwaya tano zilizochunguzwa ilikuwa ya mara mbili, ambayo ni mwafaka katika usomaji kama alivyodokeza Dyson, katika Hojjati na Muniandy (2014).

Watafiti Tinker (1963), Watts na Nisbett (1974), Walker (1992) na Wilkins (1995) katika Hughes na Wilkins (2000) wanasema kwamba mifano mbalimbali ya taipografia na aina ya fonti na ukubwa wa fonti, nfasi kati ya mistari na pia nafasi kati ya maneno na herufi, mkinzano kati ya chapisho na aina ya karatasi huathiri usomaji na hivyo basi ufasiri wa

ujumbe uliobebwa na matini. Katzir, Hershko na Halamish (2013) walifanya utafiti kuhusu athari ya kiwango cha ukubwa na udogo wa fonti katika ufasiri wa maudhui miongoni mwa wasomaji wachanga mia moja (100) ambao walikuwa katika gredi ya pili (2) na ya tano (5) ya usomaji.

Matokeo ya utafiti wao yalibaini kwamba wasomaji wa gredi ya pili (2) walikuwa na ugumu katika kusoma na kufasiri mandishi yaliyokuwa na fonti ndogo ilhali wale wasomaji wachanga wa gredi ya tano (5) walionekana kusoma na kufasiri vyema mandishi yaliokuwa na fonti ndogo. Kwa hiyo, walisema ya kwamba si kila wakati mandishi makubwa huwa mema kwa msomaji. Hawa wataalamu kwa kutotarajia walizua suala kuhusu kiwango au umri wa msomaji na upokezi wa ujumbe ulio katika matini kutegemea taipografia ya mandishi.

Wolfgang (1978) akichangia kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji, alizungumzia kuhusu jinsi maana katika matini inavyoibuliwa. Alizungumzia jinsi maana inavyojitokeza baina ya nguzo mbili za kisanaa na kiujumi. Ni nguzo hizi ambazo ziliumba mhimili wa usomaji kama tukio la kiwakati za nadharia ya mwitikio wa msomaji. Hii ni kusema ya kwamba msomaji huanza kwa kusoma mandishi yenye taipografia kubwa na pana kwa kuwa hana umilisi na tajriba inayohitajika katika usomaji. Hali hii hujengeka kwa wakati msomaji anapoendelea kutangamana na mandishi na hatimaye kukuza tajriba yake ya usomaji. Ukuzaji tajriba huo vilevile huenda moja kwa moja na upanuzi wake wa ufasiri kwa kuwa msomaji pia huwa amepata maana ya matumizi ya maneno mbalimbali kutegemea miktadha ambamo maneno hayo hutumika. Ni kwa hali hii ndiposa athari ya taipografia katika uimarishaji wa ufasiri wa maudhui hudhihirika kama ilivyojitokeza katika riwaya tano teule zilizotafitiwa.

Utafiti huu ulibaini ya kwamba mkolezo una athari ya kuimarisha uchimuzi wa maudhui katika fasihi. Kama wanavyosema Macaya na Perea (2014), neno linaweza kuendelezwa kwa mkolezo na dhima ya kuyavuta makini ya msomaji katika neno hilo ili msomaji aweze kulipa neno hilo ufasiri unaohitajika na hivyo basi kumwezesha kuelewa ujumbe ambao mwandishi huwa amelenga kuuwasilisha. Perea na Acha (2009)katika Macaya na Perea (w.h.t) wanasema kuwa mlazo vilevile unaweza kutumika kwa dhima hiyo ambayo ni kuweka msisitizo na huwa na athari ya kuimarisha uchumuzi wa maudhui. Yehudah & Alkalai (2017) wanaielezea hali ya kulifanya neno au kipashio cha kisarufi kuonekane zaidi ya kingine kama uchimuzi, ambayo athari yake wanasema ni kuimarisha ufasiri na uelelwa wa matini au ujumbe uliolengwa kuwasilishwa na mwandishi. Kutokana na utathmini wa baadhi ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo vimeshughulikiwa katika utafiti huu, imebainika kuwa grafolojia ina athari ya kuimarisha uchimuzi wa maudhui katika fasihi na hususan fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 4.4 Changamoto za utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadhaa; kwanza baadhi ya wasailiwa (wanafunzi na walimu) hawakufahamu vipengele vya kigrafolojia vilivyokuwa vikitafitiwa kwa kina, hali iliyomlazimu mtafiti kutumia muda mwingi akitoa ufafanuzi na maelezo kuvihusu. Vilevile tafiti zilizofanywa awali kuhusu grafolojia na uchimuzi zilifanywa na kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza, hali hii ilimlazimu mtafiti kukuza na kudhihirisha uwezo wa kusoma vitabu, makala na tasnifu kwa lugha ya Kiingereza na kisha kutafsiri ujumbe uliyomo katika matini hizo kwa lugha ya Kiswahili, tukio ambalo lilihitaji muda mwingi na umakinifu wa kina.

Matumizi ya lugha ya kwanza katika ufundishaji wa masomo katika viwango vya usomaji katika gredi ya kwanza na ya pili katika shule za Msingi za Umma, kama ilivyopendekezwa na tume ya utekelezaji elimu pia ulionekana kuwa changamoto kubwa wakati wa utafiti. Hii ni kwa kuwa baadhi ya wanafunzi walizisoma riwaya hizo kwa kusitasita na kutamka silabi zilizotumika katika ujenzi wa maneno katika vitabu hivyo badala ya kuyasoma maneno kama yalivyoandikwa kufuatia ukosefu wa umilisi ufaao. Hali hii ilionekana kuchangia katika kuhitilafiana na ufasiri wema wa maudhui katika matini.

Kwa hivyo ilidhihirika kwamba kuidhinishwa kwa matumizi ya lugha ya kwanza katika shughuli za elimu katika shule za msingi za umma kungelemaza manufaa yanayohusishwa na matumizi ya lugha ya Kiswahili, na mtafiti aliazimia kupendekeza kubatilishwa kwa hali hiyo nchini ili lugha ya Kiswahili iendelee kutumika katika ufundishaji shuleni kama ilivyokuwa awali. Hii italenga kuwatangamanisha wasomaji kutoka kwa misingi na mazingira mbalimbali nchini. Aidha, baadhi ya wanafunzi walionekana kukosa ujasiri kwa hivyo usaili wa kibinafsi wa wasomaji hawa ulichukua muda mrefu.

Tatizo lingine lilikuwa kuzuka kwa janga la ugonjwa wa Korona, hii ilikuwa mwanzoni mwa mwaka wa 2020. Kufikia katikati mwa mwezi wa Machi 2020, shule zote nchini Kenya zilishurutishwa kufungwa, kwa hivyo mtafiti alilazimishwa kuibadilisha ratiba yake kinyume na alivyoazimia kuizingatia hapo awali. Kwa hivyo janga hili liliuchelewesha utafiti huu kwa kuwa mtafiti hakuweza kwenda nyanjani kama ilivyotarajiwa katika jitihada za kukusanya data ya kimsingi kwa wakati.

### 4.5 Hitimisho

Sura hii imejishughulisha na uchanganuzi na uwasilishwaji wa matokeo kwa kurejelea vipengele mbalimbali vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto ambavyo ni viakifishi, herufi kubwa, picha na michoro, mandishi yenye rangi tofauti tofauti, taipografia na aina mbalimbali za fonti, nafasi kati ya maneno na mistari, mkolezo, mlazo, miundo mbalimbali ya aya na kipimo cha ukubwa wa riwaya. Aidha umehitimisha kuwa, kando na vipengele hivi ambavyo vimetajwa na kujadiliwa kwa kina na wataalamu mbalimbali, kunavyo vipengele vingine kama vile vielelezo, majedwali, faharasa, maswali na mazoezi ambavyo vinatekeleza dhima mahususi katika ujenzi wa fasihi ya watoto ya Kiswahili na ambavyo vinahitaji kujumuishwa miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia.

Vipengele hivi vya kigrafolojia hutekeleza dhima ya kuimarisha mawasiliano, kuendeleza uhalisia, kuendeleza ujumi, kumsisimua msomaji, kuchimuza maudhui, kuweka msisitizo, kumwekea msomaji kumbukumbu pamoja na kujenga muwala na mshikamano. Vipengele hivi huwa na athari ya kuimarisha uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto. Sura inayofuatia inaangazia muhtasari, mahitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu, mahitimisho na mapendekezo. Maelezo haya yametokana na uchunguzi na uchanganuzi wa grafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto, kwa kurejelea mifano ya riwaya tano teule za fasihi ya watoto katika Kiswahili.

## 5.1 Muhtasari wa tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imeanza kwa kushughulikia usuli wa mada. Katika usuli huo, ufafanuzi ulitolewa kuhusu grafolojia, fasihi ya watoto na uchimuzi kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali. Hata hivyo, utafiti huu uliegemea katika mkondo wa grafolojia kifasihi na ndio ambao ulioudhibiti utafiti. Kuhusu fasihi ya watoto, ingawa wengi wa wataalamu waliorejelewa waliiangazia dhana hii kama vitabu vinavyowalenga watoto, utafiti huu ulibaini kwamba kando na vitabu, kuna nyenzo nyingine ambayo fasihi ya watoto inaweza kuwafikia watoto kama hadhira kuu, kama vile kupitia kwa masimulizi. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, fasihi ya watoto ililenga riwaya teule za watoto zilizoandikwa kwa Kiswahili. Uchimuzi ulitumika katika mkabala wa kijumla wa ukiukaji na ujitokezeaji. Katika msingi huo, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti, mtajo wa

nadharia za utafiti, tahadhania za utafiti, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti na mahitimisho pia zilishugulikiwa kikamilifu.

Katika sura ya pili inayoshughulikia uhakiki wa mandishi, nadharia mseto za Umitindo na Mwitikio wa msomaji pamoja na mihimili na ufaafu wa nadharia ambazo zilitumika katika utafiti zimeangaziwa kwa kina. Sura hii pia imeshughulikia dhana za grafolojia ambapo mawazo mbalimbali ya wataalamu yalirejelewa huku utafiti ukiegemea katika ujumla wa dhana hii. Dhana ya fasihi ya watoto pia iliwezakuangaziwa huku baadhi ya watalaam wakishikilia kuwa inahusu matini inayowalenga watoto. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa, fasihi simulizi inaweza kuhusisha nyenzo zingine kama vile masimulizi yanayowalenga watoto. Aidha vipengele vya kigrafolojia katika fasihi viliweza kuwekwa wazi, utafiti huu ukibaini kwamba kuna vipengele vingine kama vile mazoezi, maswali, majedwali na faharasa ambavyo hutukia tamatini mwa matini ya kazi zinzowalenga watoto ilhali havitajwi wala kutambulika rasmi kama miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia.

Dhima ya grafolojia katika fasihi ya watoto iliweza kuchanganuliwa ikajitokeza wazi kwamba vipengele hivi hutekeleza dhima mbalimbali zikiwemo kumsisimua msomaji. Dhana ya uchimuzi kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali pia iliweza kuangaziwa na kubainika kuwa vipengele vya kigrafolojia huwa na athari ya kuchimuza maudhui miongoni mwa athari zingine katika matini. Vilevile muhtasari wa riwaya teule zilizochunguzwa ulishughulikiwa.

Sura ya tatu imejihusisha na mbinu za utafiti kwa kurejelea muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, usampulishaji na sampuli, mbinu za ukusanyaji data na vifaa vya kukusanyia data, mbinu za uchanganuzi na uwasilishwaji wa data, uhalali na utegemezi,

maadili ya utafiti pamoja na hitimisho. Aidha sura ya nne imeshughulikia matokeo na mjadala katika utafiti. Iliweza kuvibainisha vipengele mbalimbali vya kigrafolojia ambavyo vilidhihirika katika riwaya teule zilizochunguzwa. Vilevile iliweza kuchanganua dhima inayotekelezwa na vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto katika Kiswahili kwa mujibu wa wataalam mbalimbali pamoja na mihimili ya nadharia zilizotumika. Pia athari ya matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto katika Kiswahili iliweza kuwekwa wazi, ambayo ni uimarishaji au uchimuzi wa maudhui kimatini. Sura ya tano ililenga muhtasari, mahitimisho na mapendekezo.

### 5.1.1 Vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto

Utafiti huu ulibaini kuwa katika fasihi ya watoto na hasa riwaya zilizorejelewa, kuna vipengele mbalimbali vya kigrafolojia kama vile herufi kubwa, picha au michoro, maandishi yenye rangi tofauti na usimulizi, mlazo, mkolezo, aina za fonti, aya, viakifishi, nafasi baina ya mistari, faharasa, vielelezo au majedwali, maswali na mazoezi ya ufahamu, kiwango cha udogo na ukubwa wa matini au riwaya na hatimaye umbo la matini. Baadhi ya vipengele hivi kama vile faharasa, maswali, mazoezi na majedwali havijatajwa na watalaam kama vyenye kujumuishwa katika orodha ya vipengele vya kigrafolojia ingawa utafiti huu ulivitambua na kuvijumuisha kama vipengele mahususi ambavyo hutekeleza dhima kuu na huwa na athari mbalimbali katika ufasiri wa maudhui miongoni mwa wasomaji wa matini. Vipengele hivi hutekeleza dhima tofauti katika matini na vilevile kuathiri ufasiri wa msomaji kutegemea kiwango chake cha usomaji au kitajriba.

### 5.1.2 Dhima ya grafolojia katika fasihi ya watoto

Utafiti huu umethibitisha ya kwamba matini ya fasihi ya watoto ya Kiswahili haijengeki kwa masimulizi tu bali vilevile hupokea mchango wa vipengele vingine, vya kiisimu na visivyo vya kiisimu ambavyo huchangia pakubwa katika kuimarisha matini hizo kwa njia mbalimbali. Aidha, vipengele vya kigrafolojia ni vingi na vinatekeleza dhima kadhaa katika fasihi ya watoto. Herufi kubwa kama ilivyobainika hutekeleza dhima kuu mbili: ya kawaida na isiyo ya kawaida. Ikiwa herufi kubwa itatumika visivyo, dhima yake itakuwa kuchimuza kwa kusisitiza.

Picha na michoro hutekeleza dhima ya kuifafanua matini, kujenga ploti, kuwafafanua wahusika na matini na pia kuwavutia wasomaji wachanga kando na kuendeleza uhalisia katika matini. Mlazo na mkolezo hutekeleza dhima ya kusisitiza huku fonti na uwazi kati ya maneno na mistari zikirahisisha usomaji na vilevile kutekeleza dhima ya kiujumi. Aidha, viakifishi hudhibiti matini huku faharasa ikifafanua msamiati kimuktadha. Vielelezo hukuza tajriba huku maswali na mazoezi yakimchochea msomaji kujenga kumbukumbu bora. Viakifishi hudhibiti matini huku aya zikitekeleza dhima ya kuleta mshikamano na muwala katika matini.

### 5.1.3 Athari ya grafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto

Utafiti ulibaini kuwa vipengele vya grafolojia huathiri uchimuzaji wa maudhui. Vipengele vya kigrafolojia huathiri mwandishi na vilevile msomaji kwa vile vinaibua nguvu zakiuamilifu zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kimtindo na kidhana, na hivyo basi kuimarisha mvuto wa matini kwa wasomaji wachanga. Wasomaji wachanga hunufaika kupitia uimarishaji wa upokezi na ufasiri ufaao wa maudhui na

itikadi zinazowasilishwa katika matini. Hii ni kusema kwamba vipengele vya kigrafolojia huchimuza elementi muhimu katika matini ambazo huchangia katika kurahisisha ufasiri wa ujumbe uliolengwa kuwasilishwa kwa msomajina mwandishi.

## 5.2 Mahitimisho

Utafiti umehitimisha kuwa vipengele vya kigrafolojia vinavyotumika katika ujenzi wa kazi za kifasihi katika Kiswahili ni vingi. Aidha, vinajumuisha vile ambavyo watalaam mbalimbali wamevitaja kama vile viakifishi, picha na michoro, herufi kubwa, maumbo mbalimbali ya aya, mlazo, mkolezo, rangi, taipografia na fonti, kiwango cha ukubwa wamatini, ukawaida wa mandishi, mgawanyo wa kurasa, matumizi ya kigothi, vifupisho, udondoshaji, upembe wa maandishi pamoja na muhtasari kuja chini. Vipengele ambavyo vinahitaji kujumishwa miongoni mwa vilivyotajwa kutokana na utafiti ni pamoja na faharasa, mazoezi, majedwali pamoja na maswali tamatini mwa riwaya.

Vipengele hivi vya kigrafolojia vina dhima muhimu katika matini za fasihi ya watoto katika Kiswahili ambazo ni pamoja na kuimarisha mawasiliano, kuendeleza uhalisia, ujumi na kumsisimua msomaji, kuchimuza maudhui, kuweka msisitizo, kumwekea msomaji kumbukumbu na kujenga muwala na mshikamano. Grafolojia huwa na athari ya kuchimuza maudhui ambayo husaidia katika ufasiri wa maudhui.

## 5.3 Mapendekezo

### 5.3.1 Mapendekezo ya utafiti

Kufuatia matokeo ya utafiti, inapendekezwa kuwa vipengele vya faharasa, mazoezi, maswali na majedwali vijumuishwe rasmi miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia kwa

kuwa vinatekeleza dhima muhimu na huathiri wasomaji wachanga katika ufasiri wa maudhui na pia katika ujenzi wa kazi za kifasihi, hususan fasihi ya watoto ya Kiswahili. Vilevile walimu wahamasishwe kuhusu vipengele vyote vya kigrafolojia, dhima na athari yavyo katika uchimuzaji wa maudhui kifasihi. Aidha, wasomaji wachanga waelekezwe na walimu kwa kushirikishwa katika utungaji wa fasihi yao ya Kiswahili wenyewe kwa lengo la kuibua na kukuza vipaji vya uandishi bunifu miongoni mwa baadhi yao. Inapendekezwa kwamba waandishi wa fasihi ya watoto na mashirika ya uchapishaji yazingatie viwango tofautitofauti vya wasomaji ili wanapovitumia vipengele vya kigrafolojia, vipengele hivyo viweze kufasiriwa vyema bila kuwapa wasomaji hao changamoto.

### 5.3.2 Mapendelezo kwa ajili ya tafiti za baadaye

Utafiti huu ulichanganua vipengele kadhaa vya kigrafolojia katika fasihi ya watoto kwa kuvibainisha na kutathmini dhima na athari yavyo katika uchimuzi wa maudhui katika riwaya tano teule. Hata hivyo, idadi kubwa ya wasailiwa walionyesha ukosefu wa ufahamu wa vipengele hivyo. Kwa hivyo inapendekezwa kuwa utafiti mwingine ufanywe kwa lengo la kuwahamasisha walimu na wanafunzi kuhusu dhana hizi na umuhimu wake katika fasihi. Vilevile, utafiti mwingine unaweza kufanywa ili kuchanganua, kubainisha, na kutathmini athari ya vipengele vya kigrafolojia katika tanzu zingine za kifasihi za Kiswahili kama vile ushairi, tamthilia na hata hadithi fupi. Isitoshe, tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu fasihi ya watoto ya Kiswahili kama taaluma huru inayoweza kutafitika kinadharia kwa misingi ya nadharia zingine, kando na nadharia za umitindo na mwitikio wa msomaji ambazo zilitumika katika utafiti. Aidha, wasailiwa wengine hasa

wanafunzi wa viwango vya juu kama vile darasa la tano na sita pia wanaweza kuteuliwa na kushirikishwa kama watafitiwa kwa lengo la kupima ufasiri wao wa kazi zingine za fasihi ambazo zimetawaliwa na vipengele vya kigrafolojia. Pia, tafiti zingine zifanywe kwa lengo la kutathmini athari zingine zinazotokana na matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika fasihi ya Kiswahili ya watoto, kando na kuchimuza maudhui na vilevile kutekeleza dhima ya kiujumi.

## MAREJELEO

### MAKALA

Abdulmughni, S. A. S. (2016). "Teaching skills through literature." International Journal

Abdul-Zahra, S. (2013). *The Deviated Use of Punctuation Marks in Poetry:* A Stylistic Study. University of Al-Qadissiya.

Achar, D. (1997). "Adult Talk: On Defining Children's Literature." Critical Theory: Western and Indian. Ed. Prafulla, C. Kar. New Delhi: Pencraft.

Adegoju, A. (2008). "Graphology as a signifying system in the University of Ibadan Official Bulletin". In Atoye, R.O (Ed.) Papers in English and Linguistics, Vol. 9.

Adeniyi, E. (2017). *Indexicality and Graphetics as Linguistic Tools for Meaning Creation and Negotiation in the Poem* [Published in Leeds African Studies Bulletin 79] (Winter 2017/18), pp. 55-83).

Adeyanju, D. (2008). "Season's Greetings from a Cleric: A stylo-Semantic Analysis of Pastor Adeboye's New Year Compliments". In Atoye, R. O. (Ed). Papers in English and Linguistics. Vol. 9.

Aggleton, J. (2016). *What is the Use of a Book Without Pictures?'' An Exploration of the Impact of Illustrations on Reading Experience in A Monster Calls.* Published Open Access at Springerlink.com.

Akanwa, P. C. (2017). *Children's Literature in the School Library as a Correlate of Child Development.* Department of Library and Information Science, Imo State University, Owerri Journal of Nigerian Languages and Culture Vol. 17

Alexandra, N. M. , Howison, M. A., Bazzi, S. D. M. & Darmon, A. N.M. (2020). *Pull out all the stops*: *Textual analysis via punctuation sequences*. Oxford OX2 6GG. United Kingdom.

Alotaibi, A. Z. (2017). *Effects of Line Spacing on Reading Performance of Normally Sighted and Simulated Visually-Impaired Subjects:* A Pilot Study Using Arabic Words. King Saud University. Published by Canadian Center of Science and Education 1916-9744.

Alowonle, F. K. (2016). "Resourcefulness of Graphology: A stylistic study of three African Poems". Department of English Language and Literature, Alvan Ikoku University of Education, Owerri. khabyrfasasi@yahoo.com

Amelsvoort, M. V. (2013). *Images and Memory: A literature Review of issues in the use of images to Aid Vocabulary Acquisition and Reading Comprehension and Recall*. Bulletin of Kanagawa Prefectual Institute of Language and Culture Studies.

Anantha, A. D. (2014). *A graphological Deviation of Andre Raditya's life signs ( A stylistic approach).* Semarang: Faculty of Humanities Diponegoro University. Poems –Published in Leeds African Studies Bulletin 79 (Winter 2017/18), pp.55-83].

Ayeomoni, M. O. (2012). *A Graphostylistic Analysis of Selected Poems in Remi Raji's Web of Rememberance.* Published by Canadian Center of Science and Education. 101 International Journal of English Linguistics; Vol. 2, No. 5; 2012 ISSN 1923-869X E-ISSN 1923-8703.

Aygün, A. & Abaci, O. (2014). *Examination of illustrated story books published between the* Organizing Committee of the ERPA Congress. Elsevier Ltd. Procedia – Social and Behavioral Sciences 152 ( 2014 ) 94 – 99.

Azizović, E. & Fetić, S. (2014). *The basis of Typography and Classification of Scriptures*. University of Novi Pazar. University journal of Information Technology and Economics Available online: http://unite.edu.rs/

Babajide, A. O. (2000). "Of Style and Stylistics". In Babajide, A.O. (Ed.). Studies in English Language. Ibadan: Enicrownfit.

Bakize, L. H., Ngugi, P. M. Y. & Lyimo, E. B. (2018). *Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto nchini Tanzania na Kenya:* Mkabala Linganishi.

Bakuuro, J., Tuurosong, D. & Pelpuo, R. H. (2018). *Linguistic Analysis of Literary Texts- A Necessity or a Mere Aberration?* British Journal of 2018, Published by European Centre for Research Training and Development UK. (www.eajournals.org) Print ISSN: 2055-6063(Print), Online ISSN:2055-6071(Online).

Baratz, L. & Hazeira, H. A. (2012). *Children's Literature as an Important Tool for Education of Sustainability and the Environment*. Israel: Achva-College of Education. International Electronic Journal of Environmental Electronic Journal of Environmental Education www.iejeegreen.com.

Beck, I. (1984). "Developing Comprehension: The impact of the directed reading lesson". In R. C. Anderson, J. Osborn, & R. J. Tierney (Eds.). Learning to read in American Erlbaum Associates.

Carter, R. (1996). *Look both ways before crossing: Developments in the language and Literature classroom.* In R. Carter and J. McRae (Eds.), *Language, literature*

Castillo, A. D & Mongui, Y. B. (2011). *Types of paragraphs*. http://www.writersonlineworkshops.com

Çer, E. (2016). *Preparing Books for Children from Birth to Age Six: The Approach of Appropriateness for the Child.* Faculty of Education, Department of Turkish Education, Amasya University, Turkey. Journal of Education and Practice www.iiste.org.ISSN 2222-1735 (Paper) ISSN 2222-288X (Online), Vol.7, No.6, 2016.

Chukwu, E. (2010). *Graphological Elegance of English Punctuation Notations in the* Clark, U. & Sonia, Z. (2003). *Towards a Pedagogical Stylistics. Language and Literatur*e, Vol. 12, No. 4, 339-351 (2003) Martin's.

Colorado State University Writing Centre. (2004). Retrieved October 18, 2004, from http://writing.colostate.edu/references/research/contentpop2a.cfm.

Dressler, E. R. (2019). *Understanding the Effect of Font Type on Reading Comprehension / Memory under Time Constraints*. University of Nebraska at Omaha.

Elster, C., & Simons, H. D. (1985). *How important are illustrations in children's readers?* The Reading Teacher, 148-152.

Fang, Z. (1996). *Illustrations, text, and the child reader: what are pictures in children's storybooks for?* Reading Horizons, 37, 130-142.

Farkas, D. K. (1983) *The use of Quotation Marks and Italics to Introduce Unfamiliar Terms*. J. Technical Writing and Communication, Vo. 13 (4), 1983. University of Washington.

Farrell, J. (2010). *Literary Criticism*. Oxford: University of Pennsylvania, jfarrell@sas.upenn.edu.

Fetić, S. & Azizović, E. (2014). The Basis of Typography and Classification of Scriptures Department of technical science, UNITE JOURNAL: VOL.1 (NO.1) / June 2014 / ISSN: 2335-0628University of Novi Pazar, Dimitrija Tucovića bb, 36300 Novi Pazar, Serbia, azizovic.emrus@gmail.com

Frye, J. M. (2017). *Lifelong Learning: Five Ways To Excite Kids about Reading this Summer.* New York Public Library Summer Reading Challenge.

Fordonski, K. (1996). "Literary Graphology or the Meaning of Font in the Novels of William Wharton". Edelson, Maria, Adam Sumera and Jadwiga Uchman eds. *PASE Papers in Literature and Culture*. Proceedings of the Fifth Annual Conference of the PASE Łódź 1996, Łódź: Wydawnictwo Uniwersytetu Łódzkiego, 1999 pp. 23-28.

Greene, M. (2001). *Variations on a blue guitar: The Lincoln Center Institute lectures onaesthetic education:* New York: Lincoln Center Institute.

Hartono, R., Sofwan, A., Saleh, M. & Iskhak (2017). "Investigating the Effects of Reader Response Journals on the Quality of Teacher Trainees' Responses to Literary Works" ISSN 1799-2591 Theory and Practice in Language Studies, Vol. 7, No. 10, pp. 831-840, October 2017DOI:

Helmly, M. P. (2010). *The Power of the Picturebook: Examining Aesthetics and Critical Literacy for Imagination.* Electronic Theses and Dissertations Graduate Studies, Jack, N. Averitt College of Summer 2010. Georgia Southern University Digital Commons@Georgia Southern.

Hojjati, N. & Muniandy, B. (2014). *The Effects of Font Type and Spacing of Text for Online Readability and Performance.* Universiti Sains Malaysia, Malaysia.

Hughes, L. E. & Wilkins, A. J. (2000). *Typography in children's reading schemes may be suboptimal: Evidence from measures of reading rate.* Visual Perception Unit, Department of Psychology, University of Essex. Journal of Research in Reading, ISSN 0141-

Hunt, P. (1999). (Editor). *Understanding Children's Literature: Key essays from the International Companion Encyclopedia of Children's Literature*. London: Routledge.

Jakobson, R. (1961). 'Closing statement: linguistics and poetics'in Sebeok, T. A. (1961), 350-77, Cambridge, Mass, MIT Press.

Jimenez, E. M. G. (2015). *An Introduction to Graphology: definition, theoretical background and levels of analysis.* miscelánea: a journal of English and American studies 51 (2015): pp. 71-85 ISSN: 1137-6368.

Jiménez, E. M. G. (2017). *Foregrounding effects of the unconventional capitalization in the experimental poetry of* E. E. Cummings. University of Birminghame.m.gomez-jimenez@bham.ac.uk

Junaid, S. (2013). *The Basic Concept of Children Literature*. Alauddin State Islamic University syahruni.junaid@gmail.com.

Kaburi, C. & Wanjiru, M. W. M. (2014). *A Historical Overview of the Representation of Female Characters in Children's Fiction in Kenya.* International Journal of Liberal Arts and Social Science ISSN: 2307-924X www.ijlass.org 168.

Kang, C. (2018). *Stylistics and the Teaching of Advanced English for Senior English Majors.* Chongqing Institute of Humanity and Science: China. ISSN 1799-2591 Theory and Practice in Language Studies, Vol. 8, No. 10, pp. 1346-1350.

Katzir, T., Hershko, S. & Halamish, V. (2013). *The Effect of Font Size on Reading* Comprehension on Second and Fifth Grade Children: Bigger Is Not Always Better. University of Haifa, Haifa, Israel. PLOS ONE | www.plosone.org.

King'ei, K. (1999). "Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili".Chemichemi Vol.1 1999.

Kluck, S. (1972). *Selecting Literature for the Pre-school Child*. Ouachita Baptist University. Scholarly Commons @ Ouachita.

Le, E. (2004). *The role of paragraghs in the construction of coherence text linguistics and translation studies.* Article in IRAL - International Review of Applied Linguistics.

Macaya, M. & Perea, M. (2014). *Does Bold Emphasis Facilitate The Process of Visual-Word Recognition.* Universidal de Buenos Aires (Argentina), Universitat de Valencia (Spain). Spanish journal of Psychology.

Madhavan, I., Kaur, S., Hairol, M. I. & Mohammed, H. (2016). *Spacing improves reading in* Differences. Optometry and Vision Science Programme, Faculty of Health Sciences, Universiti Kebangsaan, Malaysia.

Matthews, G. & Amy, M. (2015). “The Philosophy of Childhood.” The Stanford Encyclopedia of Philosophy. Ed. Edward N. Zalta. Spring 2015 Edition.

Mbuthia, M. E. (2008). “The Role of Kiswahili Children’s Literature in formulating their World view”. International Journal of Education and Research Vol. 6. No.

Miall, D. S. & Kuiken, D. (1994). *Foregrounding, defamiliarization, and effect: Response to literary stories.* Edmonton: Department of English, University of Alberta.

Mirhosseini, S. A. (2017). (Editor). *Reflections on Qualitative Research in Language and Literacy Education.* Tehran: Springer International Publishing.

Mitchell, W. J. T. (2005). *What do pictures want?: The lives and loves of images.* Chicago: The University of Chicago Press.

Moeller, R. A. & Beenel, K. (2018). *Drawing Diversity: Representation of Race in Graphic Novels for Young Adults.* School Library Research. Research Journal of the American Association of School Librarians, Vol.21.

Mohr, K. A. J. (2006). *Children’s Choices for Recreational Reading: A Three-Part Investigation of Selection Preferences, Rationales, and Processes.* Department of Teacher Education and Administration University of North Texas Journal of Literacy Research, 38(1), 81–104 Copyright © 2006, Lawrence Erlbaum Associates, Inc.

Moore, N. (2016). *What’s the point? The role of punctuation in realising information structure* 016-0029-x.

Mutahi, M. & Mbuthia, E. M. (2017). *The impact of the depiction of children in selected Swahili Children’s stories.* International Journal of Contemporary Applied

Nappi, J. S. (2018). *The Importance of Questioning in Developing Critical Thinking Skills* The Delta Kappa Gamma Bulletin: International Journal for Professional Educators.

Ngozi, E. O. (2014). *The present state of children's literature in indigenous African languages: The Igbo.* Department of English Language and Literature Nnamdi Azikiwe University, Awka Anambra State, Ngeria, An International Journal of Arts and Humanities Bahir Dar, Ethiopia (IJAH)

Ngugi, Y. P. (2012). Children's Literature Research in Kenyan Universities: Where are we *now?* Kenyatta University. muhadiap@yahoo.com International Journal of Arts and Commerce Vol. 1. No. 2.

Ngugi, Y. P. (2017) "Fasihi ya Wototo katika kutekeleza Mahitaji ya Mtoto Kisaikolojia". Kiswahili Juzuu. 77.

Nordquist, R. J. (2019). *Bridges in a letter to Thomas Hearne, May 25, 1723*. Oxford Historical Society: Publications Vol. 50.

Olurinola, O. & Tayo, O. (2015). *Colour in Learning: It's Effect on the Retention Rate of Graduate Students*. Department of Science and Technology Education,

Ononye, C. F. (2017). *Lexico-stylistic choices and Media Ideology in Newspaper reports on Niger Delta Conflicts.* University of Nigeria, Nsukka, Nigeria. chuka.ononye@unn.edu.ng.

Onyango, O. J. (2007). *Masculinities in Kiswahili Children's Literature in Kenya*. Swahili Forum 14. International Journal of Arts and Commerce Vol. 2 No. 5 May 2013.

Opara, S. (2013). *A Phono-Graphological Study of Selected Narrative Discourse.* Department of English and Literary Studies, Faculty of Humanities, Imo State University, P.M.B 2000 Owerri, Nigeria susancopara@yahoo.com 2348034350486.

Osborne, J. & Chih, C. (2008). *Students' questions: a potential resource for teaching and learning science*. Routledge, London. ISSN: 0305-7267 (Print) 1940-8412. (Online) Journal homepage: https://www.tandfonline.com/loi/rsse20.

Osunuuga, O. (2016). *Graphological Foregrounding in Contemporary Yoruba Newspapers.*

Ouameur, M. D. (2013). *Linguistic Deviation in Dickens's*" Hard Times" Letters and Foreign Languages. Specialty: Anglo-Saxon Literature. University of Ouargla.

Pan, Y. (2012.) *Attentional capture by working memory contents.* Canadian Journal of Experimental Psychology. 64 (2), 124–128. Retrieved from http://www.ncbi.nlm.nih.gov/pubmed/20565178.

Parikh, K. (2022). *Colour Symbolism: Emotional Values of Colour*. Department of Applied Arts. Universty of Baroda.

Peeck, J. (1974). *Retention of pictorial and verbal content of a text with illustrations.* Journal of Educational Psychology, 66, 880-888.

Petzold, D. (2012). “Wish-fulfilment and Subversion: Roald Dahl’s Dickensian Fantasy.

Pierson, A. (2008). ‘ Colour: the influence in visual commucation’. Bemidji State University under consideration for publication in Euro. Journal of Applied Mathematics 1.

Purbani, W. (2018). *The Role of Children's Literature in Developing Multicultural Literacy*.

Radita, A. (2017. *Error Analysis Using Punctuation in Abstract of Final Report* at English Department of State Polytechnic of Sriwijaya.

Raj, J. (2015). "Linguistic Analysis of Advertising Communication: Phonological & Graphological Deviations". International Journal of Enhanced Research in Educational Development (IJERED), ISSN: 2320-8708Vol. 3, Issue 1, Jan.-Feb., 2015, pp: (40-42), Impact Factor: 1.267, Available online at: www.erpublications.com.

Rosenblatt, L. M. (1978*). The reader, the text, the poem: The transactional theory of the literary work.* Carbondale: Southern Illinois University Press.

Rosenblatt, L. M. (1988). A reading Research and Education Center Report: "The Transactional Theory: Technical Report No. 416", Center for the Study of Writing and Reading.

Rosenblatt, L. M. (2007). *Literature: The Reader's Role*: The English Journal, Vol. 49, No. 5. 2007.

Saleem, M. (2012). *Language in India: Strength for Today and Bright Hope for Tomorrow*. *Analysing Graphological Deviations in T. S. Eliot's Poem*. Volume 12 : 3 March 2012 ISSN 1930-2940 Ash-Wednesday.

Sakti, R. B. (2014). *A Thematic Structure Analysis of the English - Bahasa Indonesia Tanslational 2012 Film Texts.* A Thesis Presented as Partial Fulfillment of the Requirements for the Attainment of A Sarjana Sastra Degree in English Language and Literature. Yogyakarta State University.

Sanders, J. (1967). “Psychological Significance of Children’s Literature” Katika The Library Quartely. The University of Chicago Press.

Schallert, D. L. (1980). *The role of illustrations in reading comprehension*. In R. J. Spiro, B. C. Bruce, & W. F. Brewer (Eds.),

Schneider, J. J. (2016). “The Inside, Outside, and Upside Downs of Children’s Literature: From Poets and Pop-ups to Princesses and Porridge”. University of South Florida.

Short, K. G. (2018). *What’s Trending in Children’s Literature and Why It Matters.*

Stakić, M. (2014). *The Specifics of Children’s Literature in the Context of Genre Classification*. Rome-Italy MCSER Publishing. Mediterranean Journal of Social Sciences. ISSN

Stephano, R. (2015). *Ukiukwaji wa Nadharia Tumizi ya Uakifishaji katika Kazi za Kitaaluma za Wanafunzi wa Shule za Msingi Tanzania*. 153 MULIKA NA. 37.

Suliman, F., Ahmeida, M. B. & Mahalla, S. (2019). *Importance of Punctuation Marks for Writing and Reading Comprehension Skills.* Faculty of Arts - Misurata

Toboso, M. B. (2018). *Graphological Foregrounding in S. A. Mohamed’s Babu Alipofufuka.* Alupe University. www.ijird.com Vol. 7 Issue 8.

Traore, F. A. (2010). *African children’s literature and the promotion of readership: Swahili books for children in Tanzania*. 7 CONGRESSO IBÉRICO DE ESTUDOS AFRICANOS | 7.º CONGRESO DE ESTUDIOS FRICANOS 7TH CONGRESS OF AFRICAN STUDIES LISBOA 2010.

Treiman, R. & Kessler, B. (2004). *The case of case: Children's knowledge and use of upper and lower case letters.* Washington University in St. Louis, Applied Psycholinguistics 25(2004), 413–428 Printed in the United States of America.

Ufot, B. (2017). *Stylistic Foregrounding in the Language of Advertising.* Uyo: Department of English, University of Uyo.

Ul Huda, A. R., Ali, S. A., & Mahmood, S. (2014). *Stylistic Analysis of William Blake's Poem* "A poison Tree" University of Sargodha. International Journal of Linguistics,

Viera, R. T. ( 2017). *Vocabulary knowledge in the production of written texts: a case study on EFL language learners.* Language Cultural Center, Technical University of Cotopaxi Simón Rodríguez Av., El Ejido Town, San Felipe Sector. Latacunga, Ecuador. rodrigo.tovar@utc.edu.ec / victov912@hotmail.com

Wali, O. & Madani, A. Q. (2020). *The Importance of Paragraph Writing: An Introduction.* International Journal of Latest Research in Humanities and Social PP. 44-504 | Page www.ijlrhss.com. Nangarhar University, Jalalabad, Afghanistan.

Wehrmeyer, E. (2010). *Animal Characteristics in Children's Literature: Friends or scoundrels?* Unisa Press ISSN 0027-2639 Mousaion 28 (2) Spes 2010 pp. 85–100.

Wolfenbarger, C. D. & Sipe, L. R. (2007). *A Unique Visual and Literary Art Form: Recent Research on Picturebooks*. Review Resaerch.

Yadav, P., Chakrabarti, D. & Bisoyi, D. (2017). *Typography as a statement of Design*. Dept of Design, Indian Institute of Technology, Guwahati, India.

Yaping, G. & Yuying, L. (2017). *Foregrounding Theory in Novel Translation: A Case Study of the Translation of The Journey to the West*. Studies in Literature www.cscanada.org.

Yehudah, G. B. & Alkalai, Y. E. (2017). *The contribution of text-highlighting to comprehension: A comparison of print and digital reading.* Department of Education and Psychology. The Open University of Israel Paper in press, Journal of Educational Multimedia and Hypermedia.

Yeibo, E. & Akerele, C. (2014). *Graphological Foregrounding in Chimamanda Adichie's Purple Hibiscus.* Niger Delta University Faculty of Arts Department of English and LiteraryStudies Wilberforce Island Bayelsa State. International Journal of Language and Linguistics ISSN 2374-8850 (Print), 2374-8869 (Online)

Yemets, A. (2019). *Types and Functions of Foregrounding in the Contemporary Flash Fiction Stories*. Khmelnytsky National University. In SKASE Journal of Theoretical http://www.skase.sk/Volumes/JTL42/pdf_doc/06.pdf. ISSN 1336-782X.

Yu, H. C. (2014). *A Cross-Cultural Analysis of Symbolic Meanings of Color*. Chang Gung

Yuliya, K. & Yuliya, D. (2017). *From Defamiliarization to Foregrounding and Defeated Expectancy: Linguo-Stylistic and Cognitive Sketch.* Lege Artis.

Zaheer, A. (2016). A graphostylistic analysis of Rafat's meditation and prayer in arrival of the *Monsoon*, katika Buitems Journal of Social Sciences and Humanities, Vol. 2.ISSN 2308-3824 Issue 1.

Zahra, S. A. (2013). *The Deviated Use of Punctuation Marks in Poetry: A Stylistic Study*. University of Al-Qadissiya

**TASNIFU**

Adam, H. J. (2019). *Cultural diversity and children's literature*: "Kindergarten educators'practices to support principles of cultural diversity through book sharing". Edith Cowan University. Research Online. Doctorates & Masters Theses.

Angelidou, K. (2013*). The Invention of Children's Literature: The Case of the Mischievous Roald Dahl.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Aristotle, Thessaloniki.

Baazizi, N. (2015). *A Relevance-theoretical Approach to Italicization in Edgar Allan Poe's The Tell-Tale Heart and The Black Cat.* Kasdi Merbah University-Ouargla. M.A. Thesis.

Chapleau, S. (2009). *Work in Progress: Children's Literature and Childist Criticism-Towards an Institutional Re-Consideration.* A Thesis Submitted in Candidature for the Degree of Doctor of Philosophy, University of Wales, Cardiff.

Coetzee, L. (2003). *Beyond the Horizon: An Enquiry into the Production and Reception of the Writing of Enid Blyton.* Submitted in fulfilment of the requirements for the degree of M. A. at the University of Pretoria Department of English Pretoria.

Cronje, P. E. (2009). *The Viability of Graphology in Psycho-Educational Assessment.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Afrika Kusini.

Gallagher, L. (2018). *Typography and Narrative Voice in Children's Literature: Relationships, Interactions, and Symbiosis.* University of Dublin, Trinity College. Ph.d Thesis.

Grindlay, B. J. W. (2002). *Missing the Point: The effect of punctuation on reading performance*. Ph.D Thesis. Adelaide University.

Kawira, N. L. (2013). *Young Adults' Literature as a Tool of Change in the lives of Young Kenyans: A Case study of Never Say Never*, by Anthony Mugo and The *Delegate* by Edward Mwangi. Chuo Kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya Uzamili.

Kazungu, K. (1982). *Deviation and Foregrounding in chosen Swahili Literary Texts.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili (Imechapishwa) Maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Liberto, J. K. (2012). *Student and the Graphic Novels: How Visuals Aid in Literary Term Recall and Students' Perceptions of the Tools*. M.S Literacy Education. School of Arts and Sciences. St. John Fisher College.

Mascarenhas, L. M. (2015). *Different Worldviews in Children's Literature*. University of Goa, Ph.d Thesis.

Matundura, B. (2007). *Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto*. Nairobi: Chuo kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili.

Mpesha, N. (1996). *Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth And Development.* Ph.D Thesis. Kenyatta University.

Murunga, G. R. (1998). *The Evolution of Mumias Settlement into an Urban Centre to Circa 1940*. M.A Thesis, Nairobi. Kenyatta University.

Musotsi, T. E. (2017). *Grafolojia Katika Uchapaji wa Riwaya ya Mkamandume*. Nairobi: Chuo kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili.

Mwanaika, M. M. (2015*). Kuchambua Maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba.* Chuo kikuu Huria cha Tanzania. Tasnifu ya Uzamili.

Ngugi, Y. P. (2009). *Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya* . Ph.D Thesis. University of Vienna.

Ruthiiri, M. K. (2012). *Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya Waandishi Wanne*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta.

Soile, J. (2008). *The Captalization of Abbreviated Terms and Their Full Forms, with Special Reference to VoLP, WiMAX, and FLASH-OFDM*. University of Tampere. Post Graduate Thesis.

Steenkamp. N. (2007). *Interlectual Capital Reporting in New Zealand: Refining Content Analysis as a research method*. Tasnifu ya Uzamili iliyowasilishwa ili kukidhi mahitaji ya shahada ya uzamifu katika chuo kikuu cha Teknolojia cha Aukland.

Yu Chang, J. F. (2007). *The Role of Children's Literature in the Teaching of English to Young Learners* in Taiwan Ph.D Thesis. University of Waikato.

## VITABU


Ang, S. (2000). *The Widening World of Children's Literature*. New York: MacMillan Press Ltd.

Bleich, D. (1978). *Subjective Criticism.* Baltimore: Johns Hopkins University Press.

Bracey. D. & Lieta, P. (2008). *Nyumba ya Sungura*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Bracey. D. & Lieta, P. (2009). *Hadithi za Mamba*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Bray, J., Handley, M. & Henry, A. C. (2000). *Ma(r)king the Text: The Presentation of Meaning on the Literary Page.* Aldershot: Aldergate.

Brown, C. L. & Tomlinson, C. M. (1999). *Essentials of Children's Literature*. Third Edition. London: Allyn & Bacon.

Burke, M. (2014). *The Routledge Handbook of Stylistics.* London: Routledge.

Burke, C. L. & Copenhaver, J. G. (2004). *Animals as People in Children's Literature.* National Council of Teachers of English.

Burke, M. (2011). *Handbook of Stylistics*. London: The Routledge.

Carle, E. (1981). *The Very Hungry Caterpillar*. Hamilton: World Publishing Company.

Carroll, L. (1865). *Alice's Adventures in Wonderland*. Harmondsworth: Penguin.

Cass, J. E. (1967). *Literature and the Young Child.* London: Longman Group Ltd.

Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Programme.* Cambridge: Massachuessette Institute of Technology Press.

Cianciolo, P. (1970). *Illustrations in children's books (2nd ed.)*. Dubuque, IA: William C. Brown Company Publishers.

Creswell, J. W. (2007). *Qualitative Inquiry & Research Design: Choosing among Five Approaches.* Second Edition. London: SAGE Publications.

Creswell, J. W. & Creswell, J. D. (2018). *Research Design: Qualitative, Quantitative & Mixed Approaches.* Fifth Edition. California : SAGE Publications Inc.

Crystal, D. (1995). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Great Britain: Cambridge University Press.

Cuddon, J. A. (1991). *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Cambridge: Blackwell.

Dickens, C. (1995). *Hard Times.* Britain: Wordsworth.

Dominic, P. (2004). *Majivuno yamuua Samaki*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Emmott, C. & Marc, A. (2014). " Foregrounding, burying, and plot construction"*: The* Cambridge Handbook of Stylistics. Series: Cambridge Handbooks in Language and Linguistics Cambridge University Press.

Finch, G. *Linguistic Terms and Concepts*. London: Macmillan, 2000.

Fish, S. (1980). *Is there a text in this class?* Cambridge: Harvard University Press.

Grenby, M. O. (2008). *Children's Literature.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Grenby, M. O. & Immel, A. (2009). *Children's Literature*. Cambridge: Cambridge University Press.

Halliday, M., Mcintosh, A. & Strevens, P. (1964). *The Linguistic Sciences and Language* Teaching. London: Longman.

Halliday, M. A. K. (1994). *An Introduction To Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

Heinsbergen, N. A. (2013). *The Positive Effects of Picture Books Providing Acceptance of Diversity in Social Studies and Increase Literacy in Early Childhood Education.* The College at Brockport.

Hugo, J. V. H. (1919). *A text-book of Graphology for Expert & Students and Laymen*. New York: Robert R. Ross, Publisher. "American Graphological Society " and member of " Societe Graphologique".

Hunt, P. (1991). *Criticism, Theory and Children's Literature.* Oxford: Blackwell.

Jacobs, J. S. & Michael, O. T. (1996). *Children's Literature Briefly*. Upper Saddle River: Prentice-Hall.

Johnson, R. B. & Christensen, L. (2014). *Educational Research: Quantitative, Qualitative and Mixed Approaches 5$^{th}$ Edition.* California: SAGE Publications.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods & Techniques.* (Second Revised Edition). New Dehli: New Age International Publications Ltd.

Kress, G. (2003). *Interpretation or Design: From the World Told to the World Shown*. In Morag Styles & Eve Bearne (Eds.), Art, Narrative and Childhood (pp. 137–153). Staffordshire: Trentham Books Limited.

Krippendorff, K. (2004). *Content Analysis: An Introduction to its Methodology*. Second Edition. London: Sage Publications Ltd.

Kumar, R. (2011). *Research Methodology. a step- by- step guide to beginners.* Third Edition. London: Sage Publications Ltd.

Lauchman, R. (2010). Punctuation at Work: Simple Principles for Achieving Clarity and Good Style: Paperback

Leech, G. N. & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. New York: Longman Group Limited.

Leech, G. N. & Short, M. H. (2007). *Style in Fiction* (2nd Ed.). London: Pearson Education Ltd.

Lennard, J. (2005). *The Poetry Handbook*. Oxford: Oxford University Press.

Levenston, E. (1992). *The Stuff of Literature: Physical Aspects of Texts and Their Relation to Literary Meaning.* Albany: State University of New York Press.

Lynch, C. B. & Tomlinson, C. (1999). *Essentials of Children's Literature.* Boston: Allyn & Bacon.

Mahimbali, R. (2005). *Bibi Mwenye Macho Mekundu*. Dar es Salaam: Ruvu Publishers.

Matemu, E. L. (2005). *Nyuki na Vipepeo*. Dar es Salaam: Ruvu Publishers.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mem, F. (2004). *Where is the green sheep?* Camberwell, Victoria: Penguin Group.

Mganga, D. P. (2004). *Chui Wadogo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: E.A.E.P.

Mohamed, N. (2015). *Children's Literature*. Aukland: University of Aukland Press.naasha@hotmail.com

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2013). *Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mtobwa, B. R. (1998). *Kipofu Mmwenye Miwani Myeusi*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (2001). *Ngome ya Mianzi.* London: Cambridge University Press

Mulokozi, M. M. (2001). *Moto wa Mianzi.* London: Cambridge University Press.

Murray, K. & Kirsten, M. (2003). *Language and Control in Children's Literature.* London: Routledge.

Neuman, W. L. (2014). *Social Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Edinburgh Gate, Harlow: Pearson Education Limited. Seventh Edition.

Ngugi, Y. P. (2003). *Usicheze na Moto*. Nairobi: Oxford University Press.

Ngugi, Y. P. (2015). *Dani na Wezi wa Toyota*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Nikolajeva, M. (1995). *Aspects and Issues in the History of Children's Literature.* London: Greenwood Press.

Nodelman, P. (2008). *The Hidden Adult: Defining Children's Literature*. Baltimore: Johns Hopkins University Press.

Potter, B. (2002). *The Tale of Peter Rabbit*. Warne.

Seuss, Dr. (1957). *The Cat in the Hat*. Random House.

Shaali, A. K. (2004). *Mfalme Chura*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Shafi, A. (2012). *Mbali na Nyumbani*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Shaw, H. (1986). MeGrawn- *Hill Handbook of English*. New York: New York University Press.

Sheria za Kenya. *CHILDREN ACT NO. 8 OF 2001*. Nairobi: Revised Edition 2018.

Short, M. (1997). *Exploring the Language of Poems, Plays and Prose. Harlow:* Addison Wesley Longman Limited.

Simpson, P. (2004). *Stylistics.* London: Routledge.

Singer, E. (1949). *Graphology for Every Man*. London: Gerald Duckworth & Co. Ltd.

The Oxford English Dictionary. (2013). Oxford: Oxford University Press. On-line. 20th

Toolan, M. (2013). *Language in Literature: An Introduction to Stylistics*. London: Routledge.

Trask, L. (1997). *The Penguin Guide to Punctuation.* Harmondsworth: Penguin.

Vanderstoep, S. W. & Johnston, D. D. (2009). *Research Methods For Everyday Life: Blending Qualitative and Quantitative Approaches*. San Francisco: Jossey-Bass A Wiley Imprint.

Waihiga, G. (2006). *Harusi ya Mwanasungura*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics*. London: Longman.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2002). *Zimwi la Leo.* Nairobi: Sasasema Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2006). *Yatima.* Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Weinreich, T. & Bartlett, D. (2000). *Children's Literature: Art or Pedagogy.* Rosttilde: Rosttilde University Press.

Widdowson, H. G. (1975). *Stylistics and the Teaching of Literature*. London: Longman Publishers.

Zito, J. (2018). *Animal Protagonists in Children's Literature*. New York: Suny New Paltz. http://dx.doi.org/10.17507/tpls.0710.02. Global Journal of Health Science; Vol. 9, No. 8; 2017 ISSN 1916-9736 E-ISSN Journal of Humanities and Social Sciences 7:1 (April 2014), 49-74. English Linguistics Vol.6, No.2, pp.34-55, March Reading: New York University, January 1988. 0423 Volume 23, Issue 3, 2000, pp. 314 -324. Language Teaching· January 2004. University of Alberta. elisabeth.le@ualberta.caEducation Vol. 2, Issue 1, Jan 2012 Copyright © International Web. 19 February 2012.

**Kiambatisho1: Ratiba ya utafiti**

| **Shughuli** | **Muda** | **Mlengwa** | **Matarajio kwa mtafiti** | **Matarajio kwa Idara na Kurugenzi ya masomo ya upeo** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mahudhurio ya masomo | Mwaka mmoja **(2018)** | Mtafiti | Kusoma na kutahiniwa kuhusiana na kozi hii | Mtafiti kuzingatia masharti ya masomo ya upeo chuoni MMUST | Mtafiti aliyazingatia masharti ya kimsingi chuoni |
| Maandalizi na utetezi wa pendekezo | Agosti 2019 | Mtafiti kwa ushirikiano na wasimamizi wake | Marekebisho kuhusiana na pendekezo la utafiti na kuidhinishwa kwa utafiti | Pendekezo liwasilishwe na kutetewa na mtafiti ipasavyo | Pendekezo liliwasilishwa na likakumbwa na changamoto za ufahamu wa eneo la utafiti |
| Marekebisho ya kwanza | Agosti 2019 | Mtafiti kwa uelekezi wa | Kuyazingatia marekebisho na | Kazi iliyoboreshwa | Mtafiti aliyazingatia |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kwa pendekezo la utafiti | | Dkt. Miruka na Dkt.Okal | kuyashughulikia kwa muda ufaao | ya kukidhi kiwango cha mtafiti | marekebisho na kuyashughulikia kwa muda mfupi |
| Marekebisho ya pili ya pendekezo | Septemba 2019 | Mtafiti kwa uelekezi wa Dkt. Miruka na Dkt. Okal | Kazi iliyoboreshwa | Kazi iliyoboreshwa | Kazi ilikuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa awali |
| Uwasilishaji wa pendekezo / utetezi | Novemba 2019 | Mtafiti kutetea pendekezo mbele ya wasimazi wake na wanajopo | Utetezi kamilifu kisimulizi uliendelezwa na mtafiti | Mtafiti kudhihirisha uwezo wa kulitetea pendekezo lake | Utetezi uliendelezwa vyema na mtafiti akapewa idhini ya kuendelea na utafiti |
| Ukusanyaji data | Januari na Februari 2020 | Wasimamizi wa mtafiti: Daktari Miruka na Daktari Okal | Ukusanyaji data kamilifu | Ukusanyaji data kamilifu | Data haikukusanywa kama ilivyodhamiriwa kufuatia kuzuka kwa janga la |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Korona |
| Upangaji, uchanganuzi na ufasiri wa data | Mei na Juni 2020 | Mtafiti kupanga na kuchanganua data | Kuchanganua na kuipanga data | Kuipiga msasa kazi ya mtafiti | |
| Uwasishwaji wa data | Juni 2020 | Wakuu wa shule ya fani na sayansi za kijamii pamoja wahadhiri katika Idara ya Lugha, Elimu na Fasihi | kuwasilisha data kamilifu | kuwasilishiwa data kamilifu ya utafiti | |
| Kufuzu na shahada ya uzamifu | Desemba 2020 | Mtafiti | Kufuzu | Kushiriki katika kufuzu kwa mtafiti | |

ZINGATIA:

Mtafiti alidhamiria kuzingatia ratiba hii. Hata hivyo, kwa muda mrefu (kati ya miezi tisa na mwaka mmoja), utafiti uliyumbishwa kufuatia kuzuka kwa janga la ugonjwa wa Korona. Hivyo basi, mtafiti alilazimishwa kuipangua ratiba yake na kuibua mikakati mipya ya kuhakikisha ya kwamba utafiti wake unatekelezeka kikamilifu.

## Kiambatisho 2: Bajeti ya utafiti

Hii ndio iliyokuwa bajeti ya utafiti

| Orodha ya kipengele | Jumla ya senti kwa sarafu ya Kenya (Kshs) |
|---|---|
| Karo chuoni | 544,500/= |
| Ununuzi wa vitabu | 50,000/= |
| Ununuzi wa kipakatalishi | 100,000/= |
| Mahudhurio ya makongamano | 50,000/= |
| Usafiri na ukusanyaji data nyanjani | 50,000/= |
| Mawasiliano | 20,000/= |
| Mashauriano | 30,000/= |
| Matumizi anuwai | 50,000/= |
| Jumla ya Gharama | 894,500/= |

**Kiambatisho 3: Orodha ya watafitiwa kwa ujumla**

1. Shule ya msingi ya St. Peters, Mumias (ya wanafunzi wa kiume)

   Gredi ya kwanza Mashariki, Kusini na Magharibi

   Gredi ya pili Mashariki na Magharibi

   Gredi ya tatu Mashariki na Magharibi

   Gredi ya nne Mashariki na Magharibi

   Pamoja na walimu

2. Shule ya msingi ya St. Annes, Mumias (ya wanafunzi wa kike)

   Daraja la 1B na 1W

   Daraja la 2B na 2W

   Daraja la 3B na 3W

   Daraja la 4B, 4W na 4R

   Pamoja na walimu

3. Shule ya msingi ya Mumias Central (ya wanafunzi mseto)

   Daraja la 1C, 1E, 1N na 1P

   Daraja la 2C, 2E, 2N na 2P

   Daraja la 3C, 3E, 3N na 3P na Daraja la 4C, 4E, 4N na 4P

**Kiambatisho 4: Orodha ya vipengele vya kuthibiti grafolojia**

1. Herufi kubwa
2. Maandishi yenye mlazo
3. Maandishi yenye wino au rangi tofauti
4. Mtindo wa michoro au picha
5. Maneno yaliyokolezwa
6. Aina na ukubwa wa fonti
7. Muundo wa aya
8. Viakifishi
9. Nafasi kati ya maneno na mistari
10. Matumizi ya vielelezo / majedwali
11. Kistariungio
12. Ukubwa wa kurasa
13. Umbo la matini (sura)
14. Upigaji mstari chini ya maneno
15. Ukawaida wa maandishi
16. Matumizi ya herufi ndogo
17. Udondoshaji wa maneno
18. Matumizi ya kigothi
19. Matumizi ya akronimu au vifupisho
20. Muhtasari kuja chini
21. Upembe wa maandishi
22. Mgawanyo wa ukurasa

23. Tahajia au taipografia.

**Kiambatisho 5: Orodha ya vipengele kutokana na upekuzi wa yaliyomo**

**Anwani ya Riwaya**

| **Aina ya kipengele cha kigrafolojia** | ***Nyumba ya Sungura*** | ***Hadithi za Mamba*** | ***Harusi ya Mwanasungura*** | ***Usicheze na Moto*** | ***Dani na Wezi wa Toyota*** |
|---|---|---|---|---|---|
| herufi kubwa | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Picha | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| mandishi ya mlazo | X | X | X | X | X |
| mandishi yenye rangi tofauti | X | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| maneno yaliyokolezwa | ✓ | ✓ | X | ✓ | ✓ |
| matumizi ya vifupisho au akronimu | X | X | X | ✓ | X |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ving'ong'o | X | ✓ | X | X | X |
| Koloni | X | X | X | ✓ | ✓ |
| semi koloni | X | ✓ | X | X | X |
| alama za kunukuu | X | X | ✓ | ✓ | ✓ |
| udondoshaji | X | X | X | X | ✓ |
| Kistariungio | X | X | X | X | ✓ |
| Viulizi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| idadi ya kurasa | 30 | 47 | 22 | 26 | 17 |
| umbo la matini (sura) | michoro inayofafanuliwa na maelezo katika kila ukurasa | michoro inayofafanuliwa na maelezo katika kila ukurasa | mandishi mengi huku michoro kadha ikidhihirika | changamano : kuna wimbo, masimulizi ya nafsi ya tatu pamoja na michoro | Kawaida |
| matumizi ya | kawaida | kawaida | kawaida | kawaida | kawaida |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| herufi ndogo | | | | | |
| ukawaida wa maandishi | usio kawaida | usio kawaida | usio kawaida | kawaida | Kawaida |
| upembe wa maandishi | mandishi yako wima katika matini yote | mseto wa mandishi ulidhihirika | kawaida | kawaida | Kawaida |
| mgawanyo wa ukurasa | michoro imechukua nafasi kubwa na mandishi nafasi ndogo | wastani katika matumizi ya michoro na maneno | mandishi mengi huku michoro michache ikijitokeza | michoro imetawala riwaya huku mandishi yakichukua asili mia kidogo | mandishi mengi huku michoro michache ikijiri |
| taipografia / aina ya fonti | fonti aina ya Futura Md BT 24. | fonti aina ya Futura Md BT24. | fonti aina ya Futura Md BT24. | fonti ya kawaida ya *Times Roman 12* | fonti ya kawaida ya *Times Roman 12* |
| nafasi kati ya mistari | pana | banifu | kawaida | kawaida | Kawaida |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| muundo wa aya | sahili | changamano | changamano | changamano | Changamano |

## Kiambatisho 6: Mwongozo wa usaili usio rasmi wa kuwasaili walimu

Wakati wa usaili:

Tarehe ya usaili:

Mahali pa usaili:

Msaili:

Msailiwa:

Nafasi ya msailiwa (Mwalimu mkuu / Naibu / kawaida):

Kiwango cha elimu (cheti, stashahada, digri, Uzamili, Uzamifu):

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?
2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani?
3. Je, kuna vipengele vyovyote visivyo vya kifasihi ambavyo umevitambua kuwepo katika riwaya hii?
4. Je, hivyo vipengele ni vipi? Vitaje.
5. Je, unafikiri vipengele hivyo vina mchango wowote kwa ujumbe unaowasilishwa na Wandishi kimatini?
6. Je, unafikiri mchango huo ni upi?
7. Je, kwa maoni yako, unafikiri vipengele hivyo vinaweza kuondolewa katika fasihi ya watoto?
8. Toa sababu za jibu lako katika nambari ya 7.

**Kiambatisho 7: Dodoso za kuwasaili wanafunzi (usaili wa kibinafsi)**

**1**. Je, kuna kitu chochote kinachokuvutia katika kitabu hiki?

2. Kitaje / Vitaje vitu hivyo

3. Kwa mawazo yako, unafikiria vitu ulivyovitaja katika sehemu ya (2) vina umuhimu wowote katika kitabu hiki?

4. Toa maelezo kuhusu jibu la swali la 3.

5. Je, unafikiri kitabu hiki kinaweza kukuvutia iwapo vitu hivyo vitaondolewa?

**Kiambatisho 8: Usaili usio rasmi wa mwalimu**

**A. Usaili wa mwalimu**

**Wakati wa usaili**: Saa nne unusu asubuhi

**Tarehe ya usaili**: 25/01/2021

**Mahali pa usaili**: Darasani

**Msaili:** Eliud Musotsi

**Msailiwa:** Mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya nne (4C) katika shule ya Msingi ya Mumias Central

**Nafasi ya msailiwa** (Mwalimu mkuu / Naibu / **kawaida):**✓

**Kiwango cha elimu** (**cheti**✓, stashahada, digri):

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

   **Huu ndio mwaka wangu wa tano.**

2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani?

   **Huu ndio mwaka wa pili nikiwashughulikia katika somo la Kiswahili.**

3. Je, kuna vipengele vyovyote visivyo vya kifasihi ambavyo umevitambua kuwepo katika hii riwaya? **Ndivyo, labda picha na rangi mbalimbali ilizotumika katika kitabu.**

4. Je, hivyo vipengele ni vipi? Vitaje. **Kama nilivyotaja hapo awali**

5. Je, unafikiri vipengele hivyo vina mchango wowote katika kuimarishwa kwa ujumbe unaolengwa kuwasilishwa na mwandishi? **Naam, vinaifanya kazi hiyo ya kuwavutia wasomaji**.

6. Je, unafikiri mchango huo wa kuwavutia wasomaji unahusika kwa njia gani na ufasiri wa ujumbe ambao mwandishi analenga kuuwasilisha? **Kuwavutia wasomaji**

**na kwa hiyo kuchangia katika kuwamakifisha na hivyo basi kuwawezesha kuelewa maudhui katika kazi hiyo.**

7. Je, kwa maoni yako, unafikiri nini kitakachofanyika iwapo vipengele hivyo vinaweza kuondolewa katika fasihi ya watoto? **Naona ni kama vikiondolewa katika kazi hiyo, vitabu hivyo havitawavutia wasomaji ambao ni watoto, na kwa hivyo labda havitasomwa kwa wingi**.

8. Toa sababu za jibu lako katika nambari ya 7. **Kazi yoyote ambayo inawalenga wasomaji wachanga lazima itilie maanani mahitaji ya wasomaji hao. Wengi wanavutiwa na picha za wanyama na rangi mbalimbali na bila raslimali hizo, kazi hiyo haitawapendeza wasomaji, hususan hawa wachanga.**

**9.** Je, vipengele hivyo vina athari gani katika uimarishaji wa ufasiri wa maudhui katika hii riwaya? **Sina uhakika.**

Ahsante kwa muda ushirikiano wako na Mungu akubariki.

**B**. **Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Wakati wa usaili: **Saa mbili asubuhi**

Tarehe ya usaili: **3/2/2021**

Mahali pa usaili: **Nje ya ofisi, shuleni**

Msaili: **Eliud Musotsi**

Msailiwa: **Mwalimu wa gredi ya tatu (3W) wa somo la Kiswahili katika shule ya msingi ya St. Peters, Mumias.**

Nafasi ya msailiwa (Mwalimu mkuu / Naibu / **kawaida)** ✓

Kiwango cha elimu (cheti, **stashahada**✓, digri):

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani? **Huu ni mwaka wangu wa tatu.**
2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani? **Tangu nilipoajiriwa miaka mitatu iliyopita na tume ya kuajiri walimunya TSC.**
3. Je, kuna vipengele vyovyote visivyo vya kifasihi ambavyo umevitambua kuwepo katika riwaya hii? **Eeeh, kwa hakika hiki kitabu kina picha mbalimbali za wanyama na za binadamu ambazo pia zimeng'arishwa kwa rangi mbalimbali, kando na mandishi makubwa yanayosomeka vizuri.**
4. Je, hivyo vipengele ni vipi? Vitaje. **Ni kama nilivyoeleza hapo awali.**
5. Je, unafikiri vipengele hivyo vina mchango wowote kwa ujumbe unaowasilishwa na wandishi? **Ndio, kwa kuwa vinakifanya kitabu kuwa na uhai fulani**.
6. Je, unafikiri mchango huo ni upi? Au uhai kwa maana gani? **Nimemaanisha ya Kwambavinakifanya hiki kitabu kuwa na mvuto na pia mwanafunzi anayasoma matu kio ambayo pia anayashuhudia na kwa hali hiyo kumwezesha**

**kuelewa kwa haraka.**

7. Je, kwa maoni yako unafikiri vipengele hivyo vinaweza kuepukika katika fasihi ya watoto? **La.**

8. Toa sababu za jibu lako katika nambari ya 7.**Ni kwa sababu vinakifanya hiki kitabu kupendwa na watoto.**

Ahsante san kwa muda na ushirikiano wako. Ubarikiwe sana.

**C. Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Wakati wa usaili: Saa nane mchana

Tarehe ya usaili: 04/02/2021

Mahali pa usaili: **Chini ya mti, shuleni**

Msaili: **Eliud Musotsi**

Msailiwa: **Mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi yapili (2W) katika shule ya St. Annes, Mumias**

Nafasi ya msailiwa (Mwalimu mkuu / Naibu / **kawaida)**:**)** ✓

Kiwango cha elimu (**cheti, )** ✓stashahada, digri):

1.Je, mwalimu, umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

**Kwa hakika, huu ni mwaka wangu wa kumi na mbili humu shuleni.**

2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani? **Kwa takriban miaka mitano hivi.**

3. Je, ukikitazama hiki kitabu wanachokitumia katika somo la Kiswahili cha *Hadithi za Mamba*, kina chochote ambacho kinawavutia watoto? **Ndio.**

4. Je, ni nini? **Kitabu hiki ndicho tunachokitumia na wanafunzi wanakipenda kwa sababu kina picha za wanyama mbalimbali**

5. Je, unafikiri hizo picha zina mchango gani? **Watoto wa umri huu wanapenda picha za wanyama mbalimbali ambazo zinawafanya wakipende kitabu hiki.**

6. Je, kwa maoni yako unafikiri vipengele hivyo vinaweza kuondolewa katika kitabu hiki na wanafunzi waendelee kukipenda? **Sidhani**

7. Toa sababu za jibu lako katika nambari ya 6. **Ni kwa sababu hawa wanafunzi**

**Wanapenda picha miongoni mwa vitu vingine vya kuwavutia.**

**D. Usaili usio rasmi wa mwalimu.**

Wakati wa usaili: **Saa nne unusu asubuhi**

Tarehe ya usaili: **04/02/2021**

Mahali pa usaili: **Ofisini mwake**

Msaili: **Eliud Musotsi**

Msailiwa: **Mwalimu wa somola Kiswahili wa gredi ya kwanza (1B) katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias**

Nafasi ya msailiwa (Mwalimu mkuu / Naibu / **kawaida)** ✓:

Kiwango cha elimu (**cheti**,✓stashahada, digri):

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani? **Sasa huu ndio mwaka wangu wa pili tangu nihamishiwe hapa**
2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani? **Huu ndio mwaka wa pili sasa**
3. Je, unaweza kusema nini kuhusiana na kitabu cha Nyumba ya Sungura kinachotumika katika somo la Kiswahili? **Kwa kweli ni kitabu kizuri kulingana na maelezo mepesi na pia picha nyingi.**
4. Je, kuna changamoto zozote unazopata katika matumizi ya kitabu hicho**? Naana changamoto ni nyingi, kwa kuwa si kila mwanafunzi anayo nakala hiyo, na pia kuna athari inayotokana na matumizi ya lugha ya kwanza, hivyo basi wanafunzi wengi wanapata shida katikamatumizi ya lugha ya Kiswahili..**

**Kiambatisho 9: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Huyu alikuwa mwanafunzi wa gredi ya Kwanza (1E) katika shule ya msingi ya St. Peters Mumias

**Swali:** 1. Je, kuna vitu vyovyote vinavyokuvutia katika kitabu hiki?

**Jibu:** **Ndio.**

**Swali:** 2. Vitaje vitu hivyo.

**Jibu:** Sungura, Nyumba na Simba.

**Swali:** 3. Sungura amevalia nguo ya rangi gani?

**Jibu:** **Red.**

**Swali:** 4. Red kwa Kiswahili ni rangi gani?

**Jibu:** N**yekundu.**

**Swali:** 5. Kwa maoni yako, unafikiria vitu ulivyovitaja katika sehemu ya 2, na 3 vina umuhimu wowote katika kitabu hiki?

**Jibu:** **Vinafanya kitabu kupendeza.**

**Swali:** 6. Toa maelezo kuhusu jibu la swali la 5.

**Jibu:** **Sijui.**

**Swali:** 7. Je, unafikiri kitabu hiki kingeweza kukuvutia ikiwa vitu ulivyovitaja vingeondolewa?

**Jibu:** **Hapana.**

**Swali:** 8. Kwa nini unasema hapana?

**Jibu:** **Ninapenda vitabu vya picha.**

Ahsante kwa ushirikiano wako.

**B. Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili usio rasmi wa wanafunzi wa gredi ya pili (2W) katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.

**Swali:**1. Hebu isome anwani ya kitabu hiki.

**Jibu:** *Hadithi za Mamba.*

**Swali:** 2. Je, unaona nini kwenye sehemu ya juu ya kitabu hiki?

**Jibu:** Mamba akitembea.

**Swali:** 3. Je, Mamba huyo anatembeaje?

**Jibu:** Anatembea kama mtu.

**Swali:** 4. Kuna vitu vyovyote vinavyokuvutia katika kitabu hiki kando na Mamba?

**Jibu:** Ndio.

**Swali:** 5. Unaweza kuvitaja vitu hivyo?

**Jibu:** Ni Mamba, Ng'ombe, Mbuzi, Ndege, Mbuni, Sungura, Miti Mmaembe, na Nyani.

**Swali:** 6. Miti ambayo umetaja ni ya rangi gani?

**Jibu:** Green

**Swali:** 7. Green kwa Kiswahili ndio rangi gani?

**Jibu:** Sijui.

**Swali:** 8. Kitabu hiki kinahusu nini?

**Jibu:** Mamba alitaka kukula Mbuni lakini Mbuni akakimbia.

**Swali:** 9. Je, unafikiri kitabu hiki kinaweza kuendelea kukuvutia ikiwa picha zilizomo zitaondolewa?

**Jibu:** Hapana.

**Swali:** 10. Kwa nini unasema hivyo?

**Swali:** Kwa sababu vitabu vikiwa na picha vinafurahisha.

**C. Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya tatu (3W) katika shule ya msingi ya St Annes, Mumias.

**Swali:** 1. Hebu soma anwani ya kitabu hiki.

**Jibu:** *Harusi ya Mwanasungura.*

**Swali:** 2. Je, kuna chochote kinachokufanya ukipende katika kitabu hiki?

**Jibu:** Ndio. Hiki kitabu kina picha za wanyama kama vile Paka, Sungura na Panya pamoja na familia zao, na wamejivalia nguo nzuri.

**Swali:** 3. Nini kinachokuvutia kwa wanyama hao? Wanyama hawa wanapendeza kwa vile wanashirikiana kwa kila jambo.

**Swali:** 4. Kwa maoni yako, nguo nzuri ndio ipi?

**Jibu:** Ya rangi ya mbalimbali.

**Swali:** 5. Kwa wanyama hao, ni yupi unayempenda?

**Jibu:** Sungura.

**Swali**: 6. Kwa nini unampenda Sungura?

**Jibu:** Kwa sababu ni mzuri na tena mtoto wake alifanya harusi.

**Swali:** 7. Kisa cha Paka na Panya kinatufunza nini?

**Jibu**: Tuwe marafiki wazuri.

**D: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili usio rasmi wa wanafunzi wa gredi ya nne (4E) wa shule ya msingi ya Mumias Central.

Wanafunzi hawa kwa sababu ya tajriba yao ya usomaji, walisailiwa kwa riwaya mbili ya *Usicheze na moto* (2003) na *Dani na Wezi wa Toyota* (2015)

**Swali:** 1. Je, umevisoma vitabu hivi kikamilifu?

**Jibu:** Ndivyo.

**Swali:** 2. Kuna nini kinachokuvutia katika kitabu cha *Usicheze na moto*?

**Jibu:** Kitabu hiki kina picha za watoto wakicheza michezo mbalimbali, na pia kamusi ya maneno magumu na maswali.

**Swali:** 3. Nini unachojifunza kutokana na kisa cha moto kilichotokea katika hiki kitabu?

**Jibu:** Tuepuke kushiriki michezo ambayo inaweza tutia matatani kama walivyofanya watoto.

**Swali:** 4. Nini kinachokufurahisha katika kitabu cha *Dani na Wezi wa Toyota* (2015)?

**Jibu:** Kitabu hicho kina kurasa chache, kwa hivyo mtu anaweza kusoma na kumaliza haraka. Pia kina picha za rangi nzuri, kina maswali na pia maneno magumu yameelezwa mwisoni mwa kitabu.

**Kiambatisho 10: Idhini ya Kurugenzi ya masomo ya upeo chuoni MMUST**

MASINDE MULffiO UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY (MMUST)

Tel: 056-30870
Fax: 056-30153
E-mail: directordps@mmust.ac.ke
Website: www.mmust.ac.ke

P.O Box 190
Kakamega- 50100
Kenya

Directorate of Postgraduate Studies

---

Ref: MMU/COR: 509099

Date: 9th December, 2019

Eliud Teyie Musotsi,
EDKJH/01-53095/2018
P.O. Box 190-50100
KAKAMEGA

Dear Mr. Musotsi,

RE: APPROVAL OF PROPOSAL

I am pleased to inform you that the Directorate of Postgraduate Studies has considered and approved your Ph.D proposal entitled: *"Matumizi ya Grafolojia katika Uchimuzi wa Maudhui Katika Fasihi ya Watoto: Uchanganuzi wa Riwaya Teule za Watoto"* and appointed the following as supervisors:

1. Dr. Fridah Miruka - Department of Languages- MMUST
2. Dr Benard O. okal - Department of Languages- Maseno University

You are required to submit through your supervisor(s) progress reports every three months to the Director of Postgraduate Studies. Such reports should be copied to the following: Chairman, School of Arts & Social Sciences Graduate Studies Committee and Chairman, Department of Languages. Kindly adhere to research ethics consideration in conducting research.

It is the policy and regulations of the University that you observe a deadline of three years from the date of registration to complete your Ph.D thesis. Do not hesitate to consult this office in case of any problem encountered in the course of your work.

We wish you the best in your research and hope the study will make original contribution to knowledge.

Yours Sincerely,

DEAN
SCHOOL OF GRADUATE STUDIES
MASINDE MULIRO UNIVERSITY
OF SCIENCE & TECHNOLOGY
Date.............Sign.............

Pro . John Obiri
DIRECTOR, DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES

**Kiambatisho 11: Idhini kutoka kwa Kamishna wa Kaunti ya Kakamega**

**REPUBLIC OF KENYA**

**THE PRESIDENCY**

**MINISTRY OF INTERIOR & CO-ORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT**

Office Mobile No: 0707 085260
Email-cckakamega12@yahoo.com

When replying please quote

**Ref No: ED/12/1/VOL.V/63**

**COUNTY COMMISSIONER**
**KAKAMEGA COUNTY**
**P O BOX 43-50100**
**KAKAMEGA.**

**Date:** 10th Feb, 2020

ELIUD TEYIE MUSOTSI
MASINDE MULIRO UNIVERSITY &
TECHONOLOGY
**KAKAMEGA**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your authorization vide letter Ref: NACOSTI/P/20/3679/649985 dated 3rd February, 2020 by NACOSTI to undertake research on ***"Matumizi ya grafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto: uchanganuzi wa riwaya za watoto Kakamega County, Kenya."*** I am pleased to inform you that you have been authorized to carry out the research on the same.

COUNTY COMMISSIONER
KAKAMEGA COUNTY

**V. CHERONO**
**FOR: COUNTY COMMISSIONER**
**KAKAMEGA COUNTY**

**Kiambatisho 12: Idhini ya Mkurugenzi wa Elimu, Kaunti ya Kakamega**

**MINISTRY OF EDUCATION**
**STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION**

Telephone: 056 – 30411
Fax : 056 – 31307
E-mail : wespropde@yahoo.com
When replying please quote

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KAKAMEGA COUNTY
P. O. BOX 137 - 50100
KAKAMEGA

**REF: KAK/C/GA/29/17 IV/70**

**12th February, 2020**

Eliud Teyie Musotsi
Masinde Muliro University of Science & Technology
P. O. Box 190 - 50100
**KAKAMEGA**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

The above has been granted permission by National Commission for Science, Technology and Innovation vide their letter Ref: NACOSTI/P/20/3679/649985 dated 3rd February, 2020 to carry out research on "**MATUMIZI YA GRAFOLOJIA KATIKA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO : UCHANGUNUZI WA RIWAYA ZA WATOTO , Kakamega County Kenya**, for a period ending **3rd February, 2021.**

Please accord him any necessary assistance he may require.

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KAKAMEGA COUNTY

**DICKSON O. OGONYA**
CDE/CEB – SECRETARY
**KAKAMEGA COUNTY**

CC:

The Regional Director of Education
**WESTERN REGION**

**Kiambatisho 13: Ombi kwa Katibu wa Kaunti ya Kakamega.**

ELIUD TEYIE MUSOTSI

P.O BOX 1119-50102

MUMIAS

+254720614662

10TH FEBRUARY

musotsi23@gmail.com

THE COUNTY SECRETARY,

THE COUNTY GOVERNMENT OF KAKAMEGA

P. O BOX 36-50100

KAKAMEGA.

Dear Sir,

REF: **AUTHORITY TO CONDUCT RESEARCH IN SCHOOLS.**

I am the above mentioned PhD student at Masinde Muliro University of Science & Technology, License number **NACOSTI /P/20/3679.** I wish to request for your authority to allow me conduct an academic research in three selected schools of **St. Peters Boys Primary School, St. Annes Girls Primary School** and **Mumias Central Primary** within the Sub County of Mumias West, of Kakamega County in the course of term one. I wish to reiterate that the research will be purely academic and that I will stick to the ethical requirements in the course of my research as well as in the mentioned institutions.

Yours Faithfully

ELIUD TEYIE MUSOTSI

**Kiambatisho14: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.**

ELIUD TEYIE MUSOTSI
P.O BOX 1119-50102
MUMIAS
+254720614662
9TH JANUARY 2021
musotsi23@gmail.com

THE HEADTEACHER,
ST. ANNES GIRLS PRIMARY SCHOOL
P. O BOX 237-50102
MUMIAS.

Dear Madam,

REF: REQUEST TO CONDUCT RESEARCH IN YOUR SCHOOL.

I am the above mentioned Ph.D student at Masinde Muliro University of Science & Technology undertaking studies in Kiswahili Literature, License number **NACOSTI /P/20/3679.** I wish to request for your authority to allow me conduct an academic research in your school, namely **St. Annes Girls Primary School** within the Sub-County of Mumias West, of Kakamega County in the course of term one. I am carrying out research on a topic ***MATUMIZI YA GRAFOLOJIA KATIKA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO: UCHANGANUZI WA RIWAYA TEULE ZA WATOTO.*** The research will be conducted through informal interviews of learners and teachers as well as participatory observation of learners in class one, two, three and four. I wish to reiterate that the research will be purely academic andthat I will stick to the ethical requirements in the course of my research.

Yours Faithfully

ELIUD TEYIE MUSOTSI

**Kiambatisho 15: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya St. Peters Mumias**

ELIUD TEYIE MUSOTSI
P.O BOX 1119-50102
MUMIAS
+254720614662
9TH JANUARY 2021
musotsi23@gmail.com

THE HEADTEACHER,
ST. PETERS BOYS PRIMARY SCHOOL
P. O BOX 15-50102
MUMIAS.

Dear Madam,

REF: REQUEST TO CONDUCT RESEARCH IN YOUR SCHOOL.

I am the above mentioned Ph.D student at Masinde Muliro University of Science & Technology undertaking studies in Kiswahili literature, License number **NACOSTI /P/20/3679.** I wish to request for your authority to allow me conduct an academic research in your school, namely **ST. PETERS BOYS PRIMARY SCHOOL** within the Sub-County of Mumias West, of Kakamega County in the course of term one.I am carrying out research on a topic ***MATUMIZI YA GRAFOLOJIA KATIKA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO: UCHANGANUZI WA RIWAYA TEULE ZA WATOTO.*** The research will be conducted through informal interviews of learners and teachers as well as participatory observation of learners in class one, two, three and four. I wish to reiterate that the research will be purely academic andthat I will stick to the ethical requirements in the course of my research.

Yours Faithfully

ELIUD TEYIE MUSOTSI

**Kiambatisho 16: Ombi la utafiti katika shule ya msingi ya Mumias Central**

ELIUD TEYIE MUSOTSI
P.O BOX 1119-50102
MUMIAS
+254720614662
9th JANUARY 2021
musotsi23@gmail.com

THE HEADTEACHER,
MUMIAS CENTRAL PRIMARY SCHOOL
P. O BOX 892-50102
MUMIAS.

Dear Madam,

REF: REQUEST TO CONDUCT RESEARCH IN YOUR SCHOOL.

I am the above mentioned Ph.D student at Masinde Muliro University of Science & Technology studying Kiswahili literature, License number **NACOSTI /P/20/3679.** I wish to request for your authority to allow me conduct an academic research in your school, namely **MUMIAS CENTRAL PRIMARY SCHOOL** within the Sub-County of Mumias West, of Kakamega County in the course of term one.I am carrying out research on a topic ***MATUMIZI YA GRAFOLOJIA KATIKA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO: UCHANGANUZI WA RIWAYA TEULE ZA WATOTO.*** The research will be conducted through informal interviews of learners and teachers as well as participatory observation of learners in class one, two, three and four. I wish to reiterate that the research will be purely academic andthat I will stick to the ethical requirements in the course of my research.

Yours Faithfully

ELIUD TEYIE MUSOTSI

**Kiambatisho 17: Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa na KICD**

LONGHORN PUBLISHERS PLC | PRICE LIST 2019

PRIMARY READERS [English & Kiswahili]...*Continued*

Price inclusive of VAT

**HADITHI ZA KUSISIMUA**

| ISBN | TITLE E&OE | AUTHORS | KSHS |
|---|---|---|---|
| 49 721 8 | Vituko Duniani | Mtegwa n.w | 279 |
| 49 769 2 | Visa vya Ali | Musa | 279 |
| 49 700 5 | Mashimo ya Mfalme Suleiman [Kimeidhinishwa] | Haggard | 412 |
| 49 759 5 | Mtaka yote Hukosa yote [Kimeidhinishwa] | Omolo | 256 |
| 49 701 3 | Kisiwa chenya Hazina [Kimeidhinishwa] | Stevenson | 360 |
| 49 718 8 | Hadithi za Kale [Kimeidhinishwa] | Saidi | 244 |
| 49 765 X | Kichaa cha Pesa [Kimeidhinishwa] | Muthusi | 180 |
| 49 731 5 | Mwisho wa Mapenzi [Kimeidhinishwa] | Simbamwene | 203 |
| 49 762 5 | Nyayo za Mewendo wa Binadamu BK 1 [Kimeidhinishwa] | Higham | 203 |
| 49 727 7 | Uhalifu Haulipi [Kimeidhinishwa] | L O Omolo | 203 |
| 49 725 0 | Ng'ombe Akivunjika Mguu [Kimeidhinishwa] | Matunga Girls | 203 |
| 49 724 2 | Bahati Nasibu [Kimeidhinishwa] | M Thomas | 203 |
| 49 719 6 | Tabibu Kalulu [Kimeidhinishwa] | Wingate | 244 |
| 49 715 3 | Usininyonye [Kimeidhinishwa] | Komora | 203 |

**USENA SERIES**

| ISBN | TITLE | AUTHORS | KSHS |
|---|---|---|---|
| 36 215 0 | Makumbi Hodari [Kimeidhinishwa] | C. Momanyi | 290 |
| 49 882 0 | Dani na Wezi wa Toyota [Kimeidhinishwa] | P. Ngugi | 209 |
| 36 210 X | Paka na Bibi [Kimeidhinishwa] | Said A Mohamed | 383 |
| 36 124 3 | Gharama ya Amani | Said A Mohamed | 406 |
| 36 143X | Nguvu za Ukweli: Kitabu cha 1 | Said A Mohamed | 406 |
| 31 146 7 | Nguvu za Ukweli: Kitabu cha 2 | Said A Mohamed | 406 |
| 36 213 4 | Adhabu ya Joka | E. Matundura | 406 |
| 36 212 6 | Adha ya Kisauni | E. Matundura | 406 |
| 36 126 X | Dawa ya Kikojozi [Kimeidhinishwa]i | Ali Abdula Ali | 360 |
| 36 214 2 | Ushindi wa Nakate [Kimeidhinishwa] | Clara Momanyi | 360 |
| 36 142 1 | Tofauti: Kitabu cha 1 [Kimeidhinishwa] | Said A Mohamed | 360 |

33 KENYA ECDE & PRIMARY

## PRIMARY READERS [English & Kiswahili]...*Continued*

Prices inclusive of VAT

### HADITHI ZA KUSISIMUA

| ISBN | TITLE E&OE | AUTHORS | KSHS |
|---|---|---|---|
| 49 721 8 | Vituko Duniani | Mtegwa n.w | 279 |
| 49 769 2 | Visa vya Ali | Musa | 279 |
| 49 700 5 | Mashimo ya Mfalme Suleiman [Kimeidhinishwa] | Haggard | 412 |
| 49 759 5 | Mtaka yote Hukosa yote [Kimeidhinishwa] | Omolo | 256 |
| 49 701 3 | Kisiwa chenya Hazina [Kimeidhinishwa] | Stevenson | 360 |
| 49 718 8 | Hadithi za Kale [Kimeidhinishwa] | Saidi | 244 |
| 49 765 X | Kichaa cha Pesa [Kimeidhinishwa] | Muthusi | 180 |
| 49 731 5 | Mwisho wa Mapenzi [Kimeidhinishwa] | Simbamwene | 203 |
| 49 762 5 | Nyayo za Mewendo wa Binadamu BK 1 [Kimeidhinishwa] | Higham | 203 |
| 49 727 7 | Uhalifu Haulipi [Kimeidhinishwa] | L O Omolo | 203 |
| 49 725 0 | Ng'ombe Akivunjika Mguu [Kimeidhinishwa] | Matunga Girls | 203 |
| 49 724 2 | Bahati Nasibu [Kimeidhinishwa] | M Thomas | 203 |
| 49 719 6 | Tabibu Kalulu [Kimeidhinishwa] | Wingate | 244 |
| 49 715 3 | Usininyonye [Kimeidhinishwa] | Komora | 203 |

### USENA SERIES

| ISBN | TITLE | AUTHORS | KSHS |
|---|---|---|---|
| 36 215 0 | Makumbi Hodari [Kimeidhinishwa] | C. Momanyi | 290 |
| 49 882 0 | Dani na Wezi wa Toyota [Kimeidhinishwa] | P. Ngugi | 209 |
| 36 210 X | Paka na Bibi [Kimeidhinishwa] | Said A Mohamed | 383 |
| 36 124 3 | Gharama ya Amani | Said A Mohamed | 406 |
| 36 143X | Nguvu za Ukweli: Kitabu cha 1 | Said A Mohamed | 406 |
| 31 146 7 | Nguvu za Ukweli: Kitabu cha 2 | Said A Mohamed | 406 |
| 36 213 4 | Adhabu ya Joka | E. Matundura | 406 |
| 36 212 6 | Adha ya Kisauni | E. Matundura | 406 |
| 36 126 X | Dawa ya Kikojozi [Kimeidhinishwa]i | Ali Abdula Ali | 360 |
| 36 214 2 | Ushindi wa Nakate [Kimeidhinishwa] | Clara Momanyi | 360 |
| 36 142 1 | Tofauti: Kitabu cha 1 [Kimeidhinishwa] | Said A Mohamed | 360 |

**Kiambatisho 18: Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa na KICD.**

# MUMIAS CENTRAL PRIMARY SCHOOL

P.O. BOX 892

MUMIAS

f:..........................................................  Date:...........................20..........

ef:..........................................................


Parent/ Guardian,

buy the following class readers to help your child develop language efficiency, mastery and tency in comprehension skills. Buy any two (2) English and two (2) Kiswahili readers at the ncement of term 1 next year.

- 6: BOOK LIST FOR 2013

| | ENGLISH | KISWAHILI |
|---|---|---|
| | . Oxford Primary English Dictionary<br>1. Home at Last<br>2. Moses (OUP)<br>3. Give her a Chance<br>4. Caught in the Wax<br>5. No Escape<br>. Effective Composition Writing | . Kamusi ya Shule za Msingi<br>1. Vituko vya Sungura<br>2. Kifimbo Cheza<br>3. Usicheze na Moto<br>4. Hapo kale<br>. Insha Hatua kwa Hatua |
| | . Oxford Primary English Dictionary<br>1. The Boy Next door<br>2. The Turning Point<br>3. Moses and the Ghost<br>4. The Knife<br>5. The courage to dream<br>. Effective Composition Writing | . Kamusi ya Shule za Msingi<br>1. Ndoto ya Riziki<br>2. Hapo Kale<br>3. Hadithi kwa Methali<br>4. Embe Tamu<br>. Insha Hatua kwa hatua |
| | **. Oxford Primary English Dictionary**<br>1. Moses and the Kidnappers<br>2. The Shy Girl<br>3. Hope restored<br>4. Change of Heart<br>5. That's a Deal<br>. Effective Comprehension Skills | **. Kamusi ya Shule za Msingi**<br>1. Ahsante ya Punda<br>2. Mwanamke aliyabeba Chatu<br>3. Maskini Bibi Yangu<br>4. Kapotei na Lulu<br>. Sarufi hatua kwa hatua |

**Kiambatisho 19: Vitabu vilivyoidhinishwa na KICD**



ST. ANNES GIRLS PRIMARY SCHOOL

P.O. BOX 237

MUMIAS

BOOKLIST 2019

STD 4

| UBJECT | COURSE BOOK | PUBLISHER |
| --- | --- | --- |
| Story books | English: 1. If only I had Wings | JKF |
| | 2. The miracle twins | JKF |
| | 3. The free film | JKF |
| | 4. The crown is mine | JKF |
| | 5. The party is over for baboons | JKF |
| | | |
| | Kiswahili: 1. Juhudi za Bahati | JKF |
| | 2. Kisa cha Peremende | Moran |
| | 3. Usicheze na Moto | Oxford |
| | 4. Pwagu na pwaguzi | JKF |
| | 5. Asante ya punda | JKF |
| ctionary | Oxford primary Dictionary for East Africa | Oxford |
| ble | Good News bible | Biblica |
| musi | Kamusi ya Msingi | Oxford |
| las | Foundation primary atlas (Counties) | JKF |

**Kiambatisho 20: Uchunzaji wa kushiriki, shule ya msingi ya Mumias Central**




Ukusanyaji data ya kimsingi kutoka kwa wanafunzi wa gredi ya nne (4W) katika shule ya msingi ya Mumias Central mnamo tarehe 25/01/2021 kupitia uchunzaji wa kushiriki.

**Kiambatisho 21: Usaili usio rasmi wa mwalimu darasani**




Usaili usio rasmi wa mwalimu wa gredi ya nne (4 W) katika shule ya msingi ya Mumias Central, mnamo tarehe 25/01/2021.

**Kiambatisho 22: Usaili usio rasmi wa mwalimu**



Usaili usio rasmi wa mwalimu wa gredi ya tatu (3) katika shule ya msingi ya Mumias Central tarehe 25/1/2021.

**Kiambatisho 23: Nikiwasili katika shule ya msingi ya Mumias Central**




Siku ya pili ya utafiti. Nikiwa katika lango kuu la shule ya msingi Mumias Central nilipokuwa nikielekea kukusanya data ya kimsingi shuleni humo mnamo tarehe ishirini na sita Januari mwaka elfu mbili na ishirini na moja (26/01/2021).

**Kiambatisho 24: Usaili wa mwanafunzi darasani**



Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa darasa la tatu (3N), shuke ya msingi ya Kati, Mumias mnamo tarehe 26/1/2021.

**Kiambatisho 25: Usaili wa mwanafunzi darasani**



Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya pili (2E) katika shule ya msingi ya Kati, Mumias tarehe 26/01/2021.

**Kiambatisho 26: Uchunzaji wa kushiriki darasani**



Uchunzaji wa kushiriki wa wanafunzi wa gredi ya pili (2 E) katika shule ya msingi ya Mumias Central.

**Kiambatisho 27: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi darasani**



Usaili usio wa rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya tatu (3 W) katika shule ya msingi ya St.Peters, Mumias mnamo tarehe 3/2/2021.

**Kiambatisho 28: Usaili usio rasmi wa mwalimu**



Usaili wa mwalimu wa gredi ya pili (2 E ) katika shule ya msingi ya St.Peters, Mumias tarehe 3/2/2021.

**Kiambatisho 29: Nikiwasili katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.**




Nikiwa langoni mwa shule ya msingi ya St. Annes, Mumias  kwa shughuli ya kukusanya data ya kimsingi mnamo tarehe 4/02/2021.

**Kiambatisho 30: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**



Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya Pili (2 W) katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.

**Kiambatisho 31: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia.**





Utathmini huo ulifanywa tarehe 6/9/2021 katika shule ya msingi ya Mumias Central katika darasa la gredi ya 4C

**Kiambatisho 32: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia.**



Mwanafunzi huyu alikuwa miongoni mwa wengine ambao walikuwa wakitathminiwa kuhusu athari ya vipengele vya kigrafolojia katika uchimuzi wa maudhui katika fasihi ya watoto. Alipewa mfano wa riwaya iliyochunwa kwa kuondolewa vipengele vyote vya kigrafolojia ili aisome na kubaini athari hiyo. Ilikuwa mnamo tarehe 6/9/2021 katika ukumbi wa gredi ya 4C katika shule ya msingi ya Mumias Central.

**Kiambatisho 33: Tathmini ya athari ya vipengele vya kigrafolojia.**




Utathmini huu ulihusu riwaya mwigo na ulifanyika tarehe 6/9/2021 katika darasa la gredi ya 4C katika shule ya msingi ya Mumias Central.

**Kiambatisho 34: Uchunzaji wa kushiriki**




Utathmini huu ulifanyika tarehe 7/9/2021 katika darasa la gredi ya 4C katika shule ya msingi ya Mumias Central na ulihusu riwaya asilia ya *Usicheze na Moto* (2003).

**Kiambatisho 35: Uchunzaji wa kushiriki**




Watafitiwa wa gredi ya 4C katika shule ya msingi ya Mumias Central mnamo tarehe 7/9/2021

**Kiambatisho 36: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya Kwanza katika shule ya msingi ya St.Peters, Mumias

Fomu za usaili kama zilivyojaza

Usaili 1.

Usaili usio rasmi wa wanafunzi wa gredi ya kwanza (1)

**Swali:** 1. Je, kuna vitu vyovyote vinavyokuvutia katika kitabu hiki?

**Jibu:** Ndio.

**Swali:** 2. Vitaje vitu hivyo.

**Jibu:** Sungura, Nyumba na Simba.

**Swali:** 3. Sungura amejivalia nguo ya rangi gani?

**Jibu:** Red.

**Swali:** 4. Red kwa Kiswahili ni rangi gani?

**Jibu:** White. Hapana, sema nyekundu.

**Swali:** 5. Kwa maoni yako, unafikiria vitu ulivyovitaja katika sehemu ya 2, na 3 vina umuhimu wowote katika kitabu hiki?

**Jibu:** Hapana.

**Swali:** 6. Toa maelezo kuhusu jibu la swali la 5.

**Jibu:** Sijui.

**Swali:** 7. Je, unafikiri kitabu hiki kingeweza kukuvutia ikiwa vitu ulivyovitaja vingeondolewa?

**Jibu:** Hapana.

**Swali:** 8. Kwa nini unasema hapana?

**Jibu:** Ninapenda vitabu vya picha.

**Kiambatisho 37: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili 3.

Usaili usio rasmi wa mwanafunzi wa gredi ya tatu (3) katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.

**Swali:** 1. Hebu soma anwani ya kitabu hiki.

**Jibu:** Harusi ya Mwanasungura.

**Swali:** 2. Je, kuna chochote kinachokuvutia katika kitabu hiki?

**Jibu:** Ndio. Hiki kitabu kina picha zawanyama kama vile Paka, Sungura na Panya pamoja na familia zao na wamejivalia nguo nzuri.

**Swali:** 3. Nini kinachokuvutia kwa wanyama hao? Wanyama hawa wanapendeza kwa vile wanapendana sana na wana nguo nzuri.

**Swali:** 4. Kwa maoni yako, nguo nzuri ndio ipi?

**Jibu:** Ya rangi ya nyekundu.

**Swali:** 5. Kwa wanyama hao, ni yupi unayempenda?

**Jibu:** Sungura.

**Swali**: 6. Kwa nini unampenda Sungura?

**Jibu:** Kwa sababu ni mzuri na tena mtoto wake alifanya harusi.

**Swali:** 7. Kisa cha Paka na Panya kinatufunza nini?

**Jibu**: Tuwe marafiki wazuri.

**Kiambatisho 38: Usaili usio rasmi wa mwanafunzi**

Usaili usio rasmi wa wanafunzi wa gredi ya nne (4) wa shule ya msingi ya Mumias Central.

Wanafunzi hawa kwa sababu ya tajriba yao ya usomaji, walisailiwa kwa riwaya mbili ya Usicheze na moto (2003) na Dani na Wezi wa Toyota (2015)

**Swali:** 1. Je, umevisoma vitabu hivi kikamilifu?

**Jibu:** Ndivyo.

**Swali:** 2. Kuna nini kinachokuvutia katika kitabu cha Usicheze na moto?

**Jibu:** Kitabu hiki kina picha za watoto wakicheza michezo mbalimbali na pia kamusi ya maneno magumu na maswali.

**Swali**: 3. Nini unachojifunza kutokana na kisa cha moto kilichotokea katika hiki kitabu?

**Jibu:** Tuepuke kushiriki michezo ambayo inaweza tutia matatani kama walivyofanya watoto.

**Swali**: 4. Nini kinachokufurahisha katika kitabu cha Dani na Wezi wa Toyota (2015)?

**Jibu**: Kitabu hicho kina kurasa chache, kwa hivyo mtu anaweza kusoma na kumaliza haraka. Pia kina picha za rangi nzuri, kina maswali na pia maneno magumu yameelezwa tamatini mwa kitabu.

**Kiambatisho 39: Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Usaili wa mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya kwanza (1) katika shule ya msingi ya Mumias Central.

**Wakati wa usaili:** saa nne asubuhi hadi saa nne unusu asubuhi.

Tarehe ya usaili: 4/02/2021

**Mahali pa usaili:** Chini ya mti shuleni

**Msaili:** Musotsi Teyie Eliud

**Msailiwa:** Mwalimu

**Nafasi ya msailiwa** (Mwalimu mkuu / Naibu / kawaida)

Mwalimu wa kawaida wa somo la Kiswahili aliye pia mwalimu wa darasa hilo.

**Kiwango cha elimu** (cheti, stashahada, digri):

cheti

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

   **Naam, huu ndio mwaka wangu wa saba katika shule hii.**

2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani?

   **Ni miaka mitatu sasa tangu nianze kuwafunza wanafunzi wa gredi ya kwanza.**

3. Je, mwalimu, kando na kitabu hiki cha *Nyumba ya Sungura* (2012), ni kitabu kipi kingine unachokitumia katika ufunzaji wa somo la Kiswahili?

   **Tunasisitiza kila mwanafunzi awe na nakala hii ili tuwe na ulinganifu katika usomaji. Ila kwa sababu ya mfumo wa elimu bila malipo, hatuwalazimishi wazazi kuwanunulia watoto wao vitabu. Hi ndio sababu si kila mwanafunzi anayo nakala ya kitabu hiki.**

4. Naam mwalimu, umesema kwamba nyinyi kama shule mnasisitiza kitabu cha *Nyumba*

*ya Sungura* (2012). Naomba labda kama mtaalamu, unieleze baadhi ya sababu zilizowachochea kusisitiza kuwa kila mwanafunzi awe na nakala ya kitabu hiki.

**Naam, kwanza kitabu hicho kimo katika *Orange Book*, kumaanisha kuwa kimeidhinishwa na KICD. Pia kina michoro mingi za rangi mbalimbali ambazo ni kivutio kikubwa kwa wanafunzi wa kiwango hiki kwa kuwa wanafunzi wa kiwango hiki wanapenda vitabu vilivyo na michoro. Pia kimetumia lugha nyepesi.**

5. Je, unafikiri kuwa picha zina mchango upi katika kitabu hiki?

**Nafikiri watoto katika kiwango hiki wanapenda tu picha katika vitabu vyao.**

6. Je, kwa maoni yako unafikiri picha hizo zinaweza kuepukika katika fasihi ya watoto?

**Sidhani ya kwamba hizo picha zikiondolewa katika hivyo vitabu hata wanafunzi wataviangazia.**

**Kiambatisho 40: Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Usaili wa mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya pili katika shule ya msingi ya St. Peters, Mumias.

**Wakati wa usaili:** saa tisa hadi saa kumi kasorobo alasiri

Tarehe ya usaili:5/02/2021

Mahali pa usaili: Darasani

**Msaili:** Musotsi Teyie Eliud

**Msailiwa:** Mwalimu

**Nafasi ya msailiwa** (Mwalimu mkuu / Naibu / kawaida)

Mwalimu wa kawaida wa somo la Kiswahili aliye pia mwalimu wa darasa hilo.

**Kiwango cha elimu** (cheti, stashahada, digri):

cheti

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

   **Naam, huu ndio mwaka wangu wa tano tangu nipate uhamisho wa kukuja humu shuleni**.

2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani?

   **Huu ni mwaka wangu wa pili tangu nianze kufundisha wanafunzi wa gredi ya pili.**

3. Je, mwalimu, kando na kitabu hiki cha *Hadithi za Mamba* (2009), ni kitabu kipi kingine unachokitumia katika ufunzaji wa somo la Kiswahili?

   **Tunakitumia tu hicho**.

4. Je, kuna sababu zozote za kusisitiza kuwa lazima wanafunzi wawe na kitabu hicho?

   **Naam, tunafanya hivyo kwa kuwa ni kitabu ambacho kimeidhinishwa na**

**KICD. Pia kina vitu ambavyo huwavutia watoto kama picha.**

5. Je, unafikiri kuwa picha zina mchango upi katika kitabu hiki?

   **Picha zinawavutia watoto ili wapende vitabu.**

6. Je, ipi ndio athari inayotokana na kuwepo kwa vipengele kama vile picha kwa msomaji wa gredi ya pili? **Hii inamfanya mtoto kuhisi kuwa yeye anaviona vitu asili**

**Kiambatisho 41: Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Usaili wa mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya tatu katika shule ya msingi ya St. Annes, Mumias.

**Wakati wa usaili:** saa nane hadi saa tisa alasiri

Tarehe ya usaili: 5/02/2021

Mahali pa usaili: Darasani

**Msaili:** Musotsi Teyie Eliud

**Msailiwa:** Mwalimu

**Nafasi ya msailiwa** (Mwalimu mkuu / Naibu / kawaida)

**Mwalimu wa kawaida wa somo la Kiswahili aliye pia mwalimu wa darasa hilo.**

**Kiwango cha elimu** (cheti, stashahada, digri):

**cheti**

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

   **Naam, naweza kusema kuwa huu ndio mwaka wangu saba katika shule hii na nimefunza hili darasa sasa kwa miaka minne.**

2. Je, mwalimu, kando na kitabu hiki cha *Harusi ya Mwanasungura*(2006), ni kitabu kipi kingine unachokitumia katika ufunzaji wa somo la fasihi ya Kiswahili?

   **Tumekiteua tu hicho kwa kuwa kimeidhinishwa na taasisi ya KICD.**

4. Je, kuna sababu zozote za kusisitiza kuwa lazima wanafunzi wawe na kitabu hicho?

   **Ndio, kwa kuwa kimefurahiwa sana na wanafunzi wanapowaona wanyama mbalimbali wakitangamana.**

5. Je, ipi ndio athari inayotokana na kuwepo kwa vipengele kama vile picha kwa msomaji wa gredi ya tatu? **Vinaifanya riwaya hiyo kuwa na uhai wa kipekee.**

**Kiambatisho 42: Usaili usio rasmi wa mwalimu**

Usaili wa mwalimu wa somo la Kiswahili wa gredi ya nne katika shule ya msingi ya Mumias Central.

**Wakati wa usaili:** saa sita na nusu hadi saa saba na robo Alasiri.

Tarehe ya usaili:5/02/2021

**Mahali pa usaili:** Darasani wakati wa chamcha

**Msaili:** Musotsi Teyie Eliud

**Msailiwa:** Mwalimu

**Nafasi ya msailiwa** (Mwalimu mkuu / Naibu / kawaida)

Mwalimu wa kawaida wa somo la Kiswahili aliye pia mwalimu wa darasa hilo.

**Kiwango cha elimu** (cheti, stashahada, digri):

stashahada

1. Je, mwalimu umekuwa ukifundisha somo la Kiswahili shuleni humu kwa muda gani?

   **Naam, huu ndio mwaka wangu wa tano tangu niajiriwe na tume ya kuajiri walimu ya T.S.C**

2. Je, umekuwa ukifunza wanafunzi wa gredi hii kwa muda gani?

   **Huu ni mwaka wangu wanne wa kufundisha wanafunzi wa gredi ya nne.**

3. Je, mwalimu, kando na kitabu hiki cha *Dani na Wezi wa Toyota* (2015), ni kitabu kipi kingine unachokitumia katika ufunzaji wa somo la Kiswahili?

   **Vilevile tunatumia kitabu cha *Usicheze na Moto* (2003), ingawa wazazi wengi wana ulegevu katika kuhakikisha ya kwamba watoto wao wana nakala hizi mbili. Wengi wameathirika na tangazo la serikali kuwa Elimu ya msingi haina gharama kwa hivyo ni vigumu kuwasukuma wote wawe na nakala hizi kwa kuwa**

**tunaweza kushtakiwa kwa Mkurugenzi wa Elimu katika Kaunti ndogo, na hilo tunajarubu kuliepuka.**

4. Je, mwalimu unafikiri kuwa vitabu hivyo vinawafaa wanafunzi wa gredi ya nne katika shule zetu? **Eeeh, ninaona kuwa ni vitabu vizuri kwa kuwa wanafunzi wamevichangamkia na kuvipenda kwa sababu ya picha zilizomo.**
5. Je, unafikiri kuwa picha zina mchango upi katika kitabu hiki?

   **Nafikiri picha inarahisisha kuwasilisha ujumbe wa mwandishi katika kitabu kwa sababu ninaamini kuwa fasihi kwa wanafunzi kama hawa ni lazima iwe na picha.**

**Kiambatisho 43: Riwaya mwigo ya *Usicheze na Moto* (2003)**

Leo ni Jumamosi. Aliya, Aida, Dodo na marafiki zao wako nyumbani. Wao hawaendi shuleni. Leo ni siku ya kupumzika. Watoto hawa wanacheza mchezo wa **kibe.**

Watoto wanaimba.

Wanamwimbia Dodo:

Kibe! Bado!

Kibe! Bado!

Fungua macho yako.

Baki peke yako.

Haya tujifiche watoto.

Tucheze mchedzo wa kitoto.

Hesabu moja sio ziro.

Kwa sauti yako nyororo.

Hesabu hadi ishirini.

Harakatuingie mitini.

Fungua macho yako!

Tutafute wapi tuko!

Sasa ndio tuko.

Sasa la hatuko.

Kibe! Bado!

Kibe! Bado!

Watoto waliendelea kucheza. Walicheza kwa muda mrefu. Naam walichoka kucheza kibe. Wanataka kucheza mchezo mwingine sasa. Watoto wengine wanaamua kucheza mchezo wa kupika.

“ Leo tupikeni viazi”, Aliya alisema. “Ah, kwani mnahisi njaa?” Dodo aliruka.

“La. Huu ni mchezo tu,” Aliya akamjibu. Aida akamwambia, “Lakini mama alitukataza kuwasha moto. Alisema watoto hawafai kucheza na moto.”

“Ikiwa hutaki, tuwashe sisi tupike,” Aliya akamwambia. Aida aliondoka. Aliwaacha. Alienda zake.

Aliya na wenzake walikusanya kuni. walizipanga katikati ya mawe matatu makubwa. Haya yanaitwa mafiga. Hilini aina ya jiko.

Walichukua mkebe mtupu wa mafuta ya kupikia.Wakaufanya ni sufuria. Walichukua viazi. Wakavikata vipande vidogovidogo. Kisha wakavitia ndani ya mkebe. Wakawasha moto kwa kiberiti. Wakauweka ule mkebe juu ya mafiga. Wakaongeza maji kwenya mkebe. Halafu wakaviacha viazi viive.

Wakati wanasubiri viazi viive viwe tayari, watoto walicheza michezo mingine. Wengine wao waliruka kamba. Wengine wanacheza gololi. Wengine wanacheza mchezo wa kubahatisha shilingi imefichwa mkono upi. Watoto wote walifurahia michezo hii yao.

Karibu na yale mafiga, kulikuwa na ghala. Ghala la nyasi kavu, miti na makuti. Ghala lilikuwa limejaa. Lilikuwa lina magunia. Magunia ya mahindi, wimbi na maharagwe. Mazao haya yalivunwa kutoka shambani. Wazazi wa Aliya walifanya kazi nyingi kuvuna mazao hayo.

Mbali na lile ghala, kulikuwa na wanyama. Walikuwa mbuzi sita na kondoo tisa. Wanyama hawa walikuwa wanakula nyasi. Eh! Wao walikuwa hawana habari kama viazi

vinapikwa. Lakini waliwaona watoto hao wanacheza michezo yao. Wakati mbuzi na kondoo wanakula nyasi na watoto wale wanacheza, jambo lilitokea. Jambo hili lilileta hasara kubwa.

Upepo mkali ulivuma. Ulielekea upande wa chakula kilichokuwa kikipikwa. Upepo huo ulisababisha cheche za moto wa kuni kuruka. Cheche zile ziliruka mpaka kwenye ghala. Ghala lilianza kushika moto. Watoto hawakuona kamwe moto ulioanza.

Aida alirudi. Kwa mbali aliona moshi. Moshi ulitokeza upande wa ghala. Ghala lilikuwa limeanza kuteketea. Mbuzi na kondoo walianza kulia. Walitoa sauti nyingi. Sauti za kusikitisha. Aida alipiga ukulele, ‘Moto! Woi! Moto! Jameni moto!

Watoto wale wengine walishtuka. Sasa ghala lote lilikuwa linachomeka. Moto ulikuwa mkubwa mno!

Watoto wakasahauo michezo yao na chakula chao. Aliya na wenzake wakaanza kukimbia.

Kila mmoja alikimbia upande wake. Wote walikuwa wanatafuta kitu. Walitafuta kitu cha kuzimia moto. Kila mmoja alikuwa anapiga kelele pia. Wanapiga keleleza kutaka usaidizi. “Jamenimoto! Moto! Njooni mtusaidie!”

Majirani walisikia kelele. Walitoka nje. Wakaona ghala linachomeka na watoto wanajaribukuzima moto. Majirani wakaenda kuwasaidia watoto kuuzima moto ule. Kila mmoja alibeba chombo cha kuzimia moto. Wengine walibeba ndoo za maji. Baadhi yao walibeba mchanga.

Fujo lile na moshi uliwatoa shambani wazazi wake Aliya. Wazazi wa Aliya walishangaa. Wao pia walitimua mbio. Walienda kusaidia kuzima moto. Moto ulianza kupungua. Halafu ghafla ukazimika wote. Lakini hasara ilikuwa kubwa.

Magunia yote yaliungua. Hakukubakia kitu. Hata ghala pia. Yaliyobaki yakawa ni matope na majivu.

Baada ya muda, Aliya alimwendea baba yake. " Tafadhali baba, tusamehe," Aliya alimwomba msamaha baba yake, huku anatokwa na machozi.

Baba yake Aliya alikuwa na hasira tele. Alikuwa anafikira vipi atakavyopata pesa za kununua chakula. Au namna atakavyopata pesa za kununua mavazi ya familia yake. Alikuwa pia anafikiria wapi atapata karo za kulipia masomo ya watoto wake. Mkasa ule ulimfanya ahuzunike sana. Hasira zilimfanya akatae kusema na motto wake. Baba yake Aliya aliingia nyumbani kwake.

Familia ya Aliya iko ndani ya nyumba. Hasira zilimshuka baba yake Aliya. Alianza kuzungumza na mwanawe kwa upole.

"Ewe mwanangu Aliya! Mara ngapi nimewakataza kuwasha au kucheza na moto? Je, kama mngechomeka? Balaa ngapi mngetuletea? Sasa angalia hasara tuliyoipata!"

Mama yake Aliya akasema, "Basi yaishe baba yake Aliya. Wasamehe. Watoto hawakulichoma ghala makusudi! Umesikia watu wakisema kulikuwa na upepo mkali. Na wewe Aliya sikiliza kwa makini. Ni lazima uwe mwangalifu siku nyingine. Usicheze na moto tena!"

Aliya alisikitishwa na msiba uliowapata. Pia aliwahurumia wazazi wake. Alitambua kosa lake. Aliamua kuwasikiliza na kuwatii wazazi wake.

Tangu mkasa huo wa moto utokee, Aliya alikuwa mwangalifu sana. Aliamua kuwa hatawasha wala kucheza na moto tena. Aliyakumbuka maneno aliyoambiwa na wazazi wake. Alijifunza kuwa moto si dhihaka. Si kitu cha kucheza nacho. Moto huteketeza,

huchoma na huunguza vitu na watu. Moto huua. Moto haujui rafiki au adui. Moto ni hatari.

Maswali

1. Taja kichwa / anwani nzuri ya hadithi uliyoisoma.


2. Kwa nini watoto hawakwenda shuleni?

3. Ni nini kinachokuvutia katika hadithi hii?

4. Taja michezo mitano waliocheza watoto?


5. Eleza ujumbe ambao umeangaziwa na hadithi hii.

**Kiambatisho 44: Riwaya asilia iliyochunguzwa**



**Kiambatisho 45: Mfano wa majibu ya mtafitiwa**

Haya yalikuwa majibu ya makala mwigo ya riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi, 2003) aliyepewa msimbo wa nambari 8



2. Kwa nini watoto hawakwenda shuleni? Ilikuwa siku ya Jumamosi


3. Ni nini kinachokuvutia katika hadithi hii? Watoto walikuwawara. Chezea moto

4. Taja michezo mitano waliocheza watoto? Kibe, Mchezo wa kupika, kujificha, kukimbia, kurukakamb

Eleza ujumbe ambao umeangaziwa na hadithi hii. Usichezee moto ni mbaya

**Kiambatisho 46: Majibu ya mtafitiwa aliyepewa msimbo wa nambari 8**

Haya yalikuwa majibu ya makala asilia ya riwaya ya *Usicheze na Moto* (Ngugi,2003)




**Maswali**

1. Taja kichwa / anwani nzuri ya hadithi uliyoisoma.
   Usicheze na moto
2. Kwa nini watoto hawakwenda shuleni?
   Ilikuwa siku ya kupumzika
3. Ni nini kinachokuvutia katika hadithi hii?
   Mtoto alie kosa kuchezea moto
4. Taja michezo mitano waliocheza watoto?
   Gololi, kurukakamamba, kupika
5. Eleza ujumbe ambao umeangaziwa na hadithi hii.
   Usicheze na moto ni hatari


8

**Kiambatisho 47: Ramani ya Kaunti ya Kakamega**

Katika ramani hii, eneo la utafiti kijiografia la Mumias Magharibi limeonyeswa.



**Kiambatisho 48: Kaunti Ndogo ya Mumias Magharibi**



**Kiambatisho 49: Cheti / idhini ya kufanya utafiti (NACOSTI)**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 649985

Date of Issue: 03/February/2020

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Eliud Musotsi of Masinde Muliro University of Science and Technology, has been licensed to conduct research in Kakamega on the topic: MATUMIZI YA GRAFOLOJIA KATIKA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO:UCHANGANUZI WA RIWAYA ZA WATOTO. for the period ending : 03/February/2021.**

License No: **NACOSTI/P/20/3679**

**649985**

**Applicant Identification Number**

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.